Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 22 Mei, 2014**

*(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe.Mussa A. Zungu ) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. SELEMANI SAID JAFO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, NA UHUSIANO WA KIMATAIFA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mmbo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. NAMNELOK EDWARD MORINGE SOKOINE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. ROSE KAMILI SUKUM - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali letu la kwanza leo ni Ofisi ya Waziri Mkuu na litaulizwa na Mheshimiwa Christina Lissu Munghwai.

Na. 105

**Kuwawezesha Wazalishaji wa Chumvi**

**MHE. CHRISTINA L. MUNGHWAI** aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Kikio katika Wilaya ya Ikungi hujishughulisha na uzalishaji wa chumvi katika ukanda wa Bonde la Ufa;

Je, ni lini Serikali itawawezesha wanakijiji hao kwa kuwapatia teknolojia inayofaa ili wazalishe chumvi bora kwa chakula?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Christina Lissu Munghwai, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ina vikundi viwili vya uzalishaji chumvi ambavyo ni *NGAA Group* na *ISANJA Group* ambavyo vina jumla ya wanachama 100 na 65 kwa pamoja. Vikundi hivi vilianzishwa mwaka 2007 vikiwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida kwa kipindi hicho.

Serikali kwa kutambua umuhimu wa vikundi hivi, ilivipatia mabomba thelathini (30) kupitia uhisani wa *UNICEF* kwa ajili ya kuchangia madini joto katika chumvi.
Aidha, vikundi hivi vilipatiwa pia Madini Joto na vifaa vya kupimia Madini Joto *(Iodine Test Kits)* kutoka *Tanzania Food & Nutrition Center (TFNC)* pamoja na mafunzo ya jinsi ya kuchanganya chumvi na Madini Joto jinsi ya kuhifadhi chumvi ili isipoteze ubora wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu Halmashauri ya Wilaya ya Singida kabla ya kugawanywa kuwa Halmashauri mbili ilitoa 16,000,000/= kutokana na makusanyo ya ndani kwa vikundi 33 vilivyosajiliwa na vilivyoomba mikopo. Mwaka 2011/2012 vikundi 14 vya akina Mama wajasiriamali vilikopeshwa shs. 7,000,000/=, mwaka 2013/2014 vikundi 19 vya akina Mama wajasiriamali vilikopeshwa Shs.9,000,000/=.

Aidha, kwa mwaka 2014/2015 Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi imetenga shs.62,800,000/= kwa ajili ya mikopo ya masharti nafuu kwa vikundi vya akinamama na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuvikumbusha vikundi hivi vijisajili ili viweze kupata mkopo wa masharti nafuu na pia viweze kujiunga na Chama cha Wazalishaji Chumvi Tanzania (*Tanzania Salt Producer Association* – TASPA) kwa lengo la kuzalisha chumvi inayokidhi viwango kwa kutumia Teknolojia ya kisasa. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTINA L. MUNGHWAI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, wananchi walio wengi katika Wilaya ya Ikungi hawana uelewa wa kutosha wa umuhimu wa Madini Joto mwilini na wamekuwa hawatumii chumvi yenye Madini Joto kwa madai kwamba inaharibu mfumo wa uzazi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea elimu juu ya umuhimu wa kutumia chumvi yenye Madini Joto?

Pamoja na jitihada za wananchi wa Mkoa wa Singida ya kuzalisha chumvi wananchi hawa hawana uhakika na soko la bidhaa yao.
Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia wananchi wa Mkoa wa Singida soko la chumvi ili waache kutegemea walaji wa ndani ya Mkoa tu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili la kwanza analolisema Mbunge ana *address* jambo la msingi hapa kwa sababu chumvi hii inayopatikana eneo hili la Ikungi haina *iodine*.

Kwa hiyo, wakitumia hivi hivi ndiyo unasikia watu wanapata *goiter* na matatizo mengine ya namna hiyo nimezungumza na Kaimu Mkurugenzi anaitwa Ayubu Sengo, asubuhi hii nikamwuliza tatizo hili lina kwenda je, wananchi wa pale wanahitaji elimu kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema kwasababu wanasema kwamba udongo wa kwao wao wenyewe una *iodine*.

Kwa hiyo, hii *element* ya elimu anayoizungumza hapa ni muhimu kwasababu chumvi haitumiki pale Ikungi tu inatoka nje inakwenda Mwanza, inakwenda Dar es salaam na inakwenda sehemu mbalimbali. Halmashauri katika haya mambo ambayo yamezungumzwa hapa inachofanya ni kujaribu kutoa elimu.

Sasa nikiri hapa kuwa Ikungi ni Wilaya mpya, hata hizi *data* nilizochukua hapa ni *data* ambazo nilipata zamani wakiwa katika Halmashauri ya Singida. Ni jambo la msingi na ninakubaliana na wewe Mheshimiwa Mbunge na tutahakikisha kuwa tunakuwa na watu wa *extension services* ambao wataenda kutoa elimu hii ambayo inazungumzwa hapa.

Hili linakwenda sambamba na hili la soko analolizungumza hapa. Ni kweli, hata mimi mwenyewe kabla sijajibu nilikuwa sijui hivi kumbe Singida kuna chumvi. Mimi nilikuwa ninajua ni uvinza tu ndiko kuna chumvi.

Sasa kumbe na wao wanayo na wana huu utaratibu wa kuhakikisha kuwa wanaweka *iodine*. Nadhani tumetenga fedha hapa shilingi 67,000,0000 zitakazotoka katika *own source* na sehemu kubwa ya hiyo ni pamoja na ku- *advertise*. Kuweza kufanya watiu wengi kujua kuwa kumbe hata chumvi pia inapatikana kule Singida. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kuwa chumvi inayopatika Singida Uvinza na maeneo mengine ni sehemu ya Madini tuliyonayo hapa Tanzania na chumvi ya Singida inaoekana inakosekana madini ya *iodine*ili kuwa na ubora wa chumvi nini Sera ya Serikali kuwa na teknolojia iliyo bora ambapo watatafuta watu wenye uwezo wa technolojia wasaidie hawa wawekezaji wadogo wadogo ili wawe na Ubia wa pamoja kuwawezesha wazawa wa nchi hii nao waweze kufaidi madini tuliyo nayo pamoja na sekta nyingine?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani hili suala tumeliongea sana na suala la uzawa kuna watu baadhi yetu Watanzania kama yeye hakusaidiwa na basi wazawa wengine hawajasaidiwa ninadhani hii dhana tuachane nayo hii. Ni kwamba katika migodi, umesema ni madini sasa usikilize jinsi wazawa wanavyosaidiwa kwenye madini ah! Ndiyo umeongea madini tulia sasa. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nimempa nafasi Waziri wa Nishati na Madini.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo niliwaeleza hivi juzi kwamba tumetoa ruzuku kwa vikundi kumi vya uchimbaji wa madini na kati ya hivyo vikundi kumi kimoja kinachimba chumvi. Tumetoa dola 50,000 na mwisho wa mwezi huu tutatoa tena Dola 50,000 kwa kila kikundi na fedha tumeweka *Tanzania Investment Bank* shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hili suala kwa sababu kuna mtu fulani yeye hajapendelewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ninakushukuru tunaendelea. Waheshimiwa tunaendelea swali 106 Dkt. Haji Mponda.

Na. 106

**Zoezi la Kupunguza Mifugo Katika Wilaya Ulanga**

**MHE. DKT. HAJI HUSSEIN MPONDA** aliuliza:-

Katika msimu wa kiangazi wa mwaka 2012, Halmashauri ya Wilaya Ulanga kwa msaada wa Wizara ya Maliasili na Utalii walitekeleza zoezi la kupunguza mifugo (Ng'ombe)ambao tayari waliishaanza kutishia kwa kutoweka kwa uendelevu wa ardhi yenye rutuba kwa kilimo na ufugaji wenye tija.

(a) Je, zoezi hilo limegharimu fedha kiasi gani, na nini vyanzo vyake?

(b) Je, zoezi hilo limefanikiwa kwa kiasi gani kulingana na malengo yaliyopangwa?

(c) Je, ni lini Serikali itawajengea miundombinu ikiwamo malambo na majosho kwa ajili ya mifugo katika maeneo yaliyotengwa rasmi kwa ajili ya malisho ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Haji Hussein Mponda, Mbunge wa Jimbo la Ulanga, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili liligharimu kiasi cha shilingi 481,731,510/= kiasi kilichokuwa kimepangwa na zoezi hilo kilikuwa Tshs 85,000,000 ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii ilitoa Tshs. 75,000,000/= na Halmashauri ya Ulanga Tshs. 10,000,000/= Aidha, jumla ya Tshs.396,731,510/= ziliongezeka kwani muda uliokusudiwa mwanzo wa operesheni hii ambazo zilikuwa siku nne haukutosha na hivyo kuchukua muda wea miezi mitatu (30/10/2012) hadi (3/1/2013).

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho ng'ombe waliokuwepo ni takribani 350,000. Jumla ya ng'ombe 285,000 walipunguzwa na kufikia kiasi cha ng'ombe waliopunguzwa na kufikia kiasi cha ng'ombe 65,700 ambao ndiyo ilikuwa lengo la operesheni hiyo kulingana na uwezo wa eneo hilo *(carrying capacity)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza azma ya ujenzi wa miundombinu ya malambo na majosho katika maeneo ya wafugaji Wilayani Ulanga, Mwezi Oktoba, 2013 Halmashauri ilipitisha mpango wa muda mrefu kuanzia 2013/2014 hadi 2017/2018 unaohusu ujenzi wa malambo 20 na majosho 10 katika Tarafa tano zenye idadi kubwa ya mifugo kwa kuzingatia mpango huu Halmashauri katika Bajeti ya mwaka 2014/2015 imetenga shilingi milioni 75 ili kuanza ujenzi wa malambo katika kijiji cha Mchangani.

Kati ya Fedha hizo, Halmashauri itatoa shilingi milioni 45.0 na wananchi watachangia shilingi 30.0 kwa sababu miradi ya aina hii inatekelezwa kwa ubia kati ya Halmashauri na wananchi, kwa utaratibu wa fursa na vikwazo kwa maendeleo *(0&0D)*. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninashukuru pia kwa majibu ya Serikali. Ninaomba kuchukua nafasi hii kumpongeza *RC* wa Mkoa wa Morogoro Mheshimiwa Joel Bendera kwa kazi nzuri aliyofanya kukamilisha zoezi hili. Vilevile niwape pole ndugu zangu wafugaji kwa usumbufu mkubwa waliopata wakati wa kutekeleza zoezi hili. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Katika Bunge hili Wizara ya Ardhi kwa maana ya Serikali walielekeza kusaidia kutatua migogoro hii ya wakulima na wafugaji katika kukamilisha zoezi la matumizi bora ya ardhi katika vijiji. Wilaya ya Ulanga wameanza, lakini wamekwama kutokana na uwezo wa kifedha na kiutaalamu.

Je, kupitia TAMISEMI na Ardhi wako tayari kui *support* Wilaya hii ya Ulanga ili iwe *model*. Yaani iwe ya mfano wa Wilaya ambayo inaweza kukaa pamoja, wakulima na wafugaji katika hali nzuri bila ya mikwaruzo?

Nimewahi kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga katika vikao vyetu halali vya Kisheria kwamba ni bora wakati wa kuboresha miundombinu kwa wafugaji pamoja na malambo na majosho ni vyema sasa waanzishe mfuko wa Maendeleo ya Mifugo yaani *Livestock Development Fund.* Halmashauri wamekubali lakini wamekuwa waki suasua.

Ninaiomba TAMISEMI watoe maelekezo kwa Halmashauri waanze kutekeleza ombi hilo ambalo linaweza kuwa ni muafaka kuwasaidia wafugaji katika maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyofuatilia jambo hili.

Pia ninashukuru kwa *appreciation* yake kwa *Regional Commissioner* ambaye ndiye msimamizi Mkuu wa shughuli zote za Kiserikali katika Mkoa wa Morogoro. Tunashukuru kuwa yeye Mbunge pia ana *appreciate* kazi iliyofanywa na Serikali katika hili zoezi tulilolisema hapa.

Kama anavyoeleza yeye mwenyewe Mheshimiwa Haji Mponda, kuhusu hili suala la Wizara ya Ardhi, tunashirikiana nao sana, tunapozungumza hapa anazungumza habari ya matumizi bora ya ardhi na mimi ninajua kwa upande wetu sisi unapokwenda Wizara ya Ardhi moja watakuambia kwamba wale ambao walikopa na kuomba msaada kwa ajili ya kupima vijiji na ardhi wengine mpaka sasa hivi hawajarudisha mkopo.

Kwa hiyo, ninataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kuwa pamoja na kwamba tungependa Wizara ya ardhi yenyewe ndiyo ijibu swali hili, lakini tutashirikiana nao kufanya nao kazi kwa pamoja. Tutaendelea kuwahimiza watu wetu na sisi wenyewe, tutazungumza na watu wetu ili tufikie hatua hiyo ya kusema kuwa sasa vijiji vyetu vyote katika nchi yetu ya Tanzania vimepimwa. *(Makofi)*

Ili uweze kuwa na matumizi bora ya ardhi na ili tuweze kuondokana na migogoro hii ambayo unaiona kila wakati, huko kati ya wakulima na wafugaji ukitaka kuondoa tatizo hili ninajua watu wamesimama na ninajua wataendelea kusimama.

Nenda sema hapa ni kwa ajili ya kufuga ng'ombe, hapa ni kwa ajili ya kilimo, hapa ni kwa ajili ya watoto kubembea, hapa ni kwa ajili ya barabara na kadhalika. Ukiheshimu hilo hutapata ugomvi. *(Makofi)*

Kuhusu suala la kuanzisha Mfuko wa *Livestock Development* hili suala wala halina matatizo yoyote kuna kitu kinaitwa *(O&OD) Opportunities and Obstacles to Developments* Hii

inaitwa Fursa na Vikwazo kama Halmashauri imefika mahali sasa hivi imewekwa kwenye mpaka mwaka 2018 kwamba itakuwa na mpango wa kuendeleza Mifugo hakuna mtu yoyote ambaye anaweza akabisha kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Ninataka kusema kuwa sisi hili tunawahimiza na tutazungumza na watu wa Ulanga ambao ni pamoja na Mheshimiwa Mama Celina Kombani. Ndiyo tutazungumza nao ili tuwahimize wenzetu wa Ulanga kule na Halmashauri zingine zifikirie habari ya kuanzisha mfuko huu. Mimi ninampongeza Mheshimiwa Haji Mponda, kwa kuangalia jambo hili kwa upana mkubwa kiasi hiki. *(Makofi)*

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa vile Mheshimiwa Mbunge wa Ulanga Magharibi amezungumzia kuhusu tija ya kilimo na ufugaji. Tatizo hili ni kweli Serikali imejitahidi sana kuona kwamba wakulima wanapata tija na wafugaji hali kadhalika na waweze kuishi kwa kupendana bila kudhuriana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada hizi za Serikali imekuwa ni tofauti sana kwa Jimbo langu Mbarali. Nitakachokuambia inawezekana usiamini, lakini ndicho kinachofanyika Wilayani Mbarali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kuhuzunisha sana, Wakulima wamehangaika muda wote mashambani. Akina mama, vijana, wazee, tunasema wajiajiri, leo wanarudisha mazao yao kutoka shambani wanaambiwa walipe ushuru na anayesimamia ni kiongozi ambaye tulitegemea atatusaidia, Mkuu wa Wilaya, anafanya Mikutano kuhamasisha kwamba mkulima anatakiwa asamehe gunia kumi tu, zinazoendelea alipe ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tamko la Serikali, ni halali kuwafanyia wananchi hivi kweli?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba hili jambo tuliweke vizuri hapa tuelewane vizuri. Siyo mara ya kwanza Mheshimiwa Kilufi ameeleza habari hii, amekuja ofisini amezungumza habari hii. Sisi tunaizungumzia Sheria hapa. Kuna kitu kinachoitwa ushuru (*produ-cess)* inaweza ikawa kati ya *3% to 5%.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujibu Swali hili. Mkulima akiwa anabeba Mazao yake kutoka kwenye shamba lake anapeleka nyumbani kwake, hajauza hakuna ushuru. Mkulima anapohamisha Mazao yake kutoka kwenye mikono yake na kwenda kwa Mchuuzi au Mfanyabiashara hapo hapo ushuru unadaiwa pale pale.

Kama Mkulima anapeleka nyumbani kwake amechukua na kwenda nyumbani hivi, hakuna Wakulima na hivi hivi watu wa Mifugo mpaka afike pale kwenye Mnada, ng'ombe wanahama kutoka kwa Mfungaji wanakwenda kwa Mfanyabiashara pale ndio ushuru unapolipwa pale iko katika Sheria pale ndivyo tunavyosema.

Kama atachukuwa huyu mtu katoka shambani anaondoka na mizigo anakwenda nyumbani kwake, hakuna! Sasa kunaweza kukawa na tatizo la kupambanua, kwamba haya yanakwenda nyumbani, haya yanakwenda wapi? Hii ni changamoto ya Halmashauri lakini nataka niseme hapa na nimezungumza na Mheshimiwa Gula Hussein Kiffu na nimemueleza jambo hili.

Nikamwambia Wakulima kwa maana ya Wakulima ni mpaka yanapohama Mazao kutoka mikono mwao yanakwenda kwa Wafanyabiashara ndipo wanapotakiwa kulipia ushuru, lakini kama anapeleka kwenye *go-down* anangoja mpaka biashara itakapokuwa imechanganya kwa maana ya kwamba Mazao yameadimika halipi ushuru, ushuru unalipwa wakati unapokwenda upande wa pili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Laizer, jiandae na Mheshimiwa Kawawa, Mheshimiwa Selasini!

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize Swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alisema kwamba lazima yatengwe maeneo ya Wakulima na Wafugaji na kuna maeneo ambayo yametengwa na yana Hati kisheria ambayo ni eneo la Mifugo na Wakulima wamevamia,

Je, kwanini Serikali inasita kutoa tamko kwa Wakulima hao waondoke katika eneo ambalo limepimwa na Serikali inatambua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi. Wachangiaji wapo wengi, mambo ya Ng'ombe haya ni muhimu sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa lekule Laizer hapa hajasema *in particular* ni eneo lipi analosema, lakini hii migogoro anayosema hii ipo na nataka niseme hapa kwamba mimi naelewa jambo tunaloulizwa hapa ni *very sensitive,* yapo maeneo unakuta Wafugaji wameingia katika maeneo ya Wakulima na yapo maeneo ambayo Wakulima wameingia katika maeneo ya Wafugaji.

Ndio maana tumesema hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa maelekezo akatuagiza tukae sisi wote, tukae na kina Dkt. Titus Kamani, tukae pamoja na Wizara ya Ardhi, TAMISEMI na wadau wote tuzungumze habari hii inayozungumzwa hapa.

Kumekuwa na mtafaruku mwingi, wengine wameingia katika maeneo mbalimbali na kadhalika. Yako maeneo ambayo yanatumika na mengine yanaonekana hayatumiki mpaka sasa hivi.

Yote haya na mengine mengi yatazingatiwa. Ndiyo maana kimeitishwa Kikao cha wadau wote wanaohusika na eneo hili linalohusika hapa, ili wote kwa pamoja tuweze kutafakari tatizo hili ambalo linaonekana kwamba linawatia hofu wananchi wetu kwa jambo ambalo kwa kweli hatuoni maana yake.

Lakini *the bottom line is,* usipokuwa na kitu kinachoita *Land Use Plan,* usipokuwa na matumizi Bora ya Ardhi, migogoro hii mpaka Bwana Yesu atakaporudi hapa duniani, haitakwisha. Lazima tufike mahali tuheshimu mipango iliyopangwa. Wakulima wakipangiwa

mahali pao ni hapa, wanakaa pale pale hawawezi kuingilia maeneo ya Mifugo na wale wa Mifugo wakipangiwa maeneo yao ni hapa hawawezi kuingilia sehemu nyingine ni pale. Suala hili ni pamoja na kuangalia *population* yetu na mambo mengine mengi ambayo siwezi kujibu katika muda huu mfupi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kawawa jiandae Mheshimiwa Selasini.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwakuwa zoezi lile la Wilaya ya Ulanga lilikuwa sio kupunguza Ng'ombe, ila ilikuwa ni kuwafukuzia katika Wilaya ya Namtumbo. Wilaya ya Namtumbo ni Wakulima na Ng'ombe laki tatu wamefukuzwa kutokwa Wilaya ya Ulanga na wapo katika mabonde ya vyanzo vya maji vya Mto Luwego, Mbarangando na Mito mingine inayotia maji katika Mto Ruvuma.

Sisi kule Namtumbo na Mkoa wa Ruvuma ni Wakulima, hatujawahi kuona Ng'ombe, wananchi wanaogopa sasa Ng'ombe mamia kwa mamia.

Je, Serikali inatusaidia nini kuhusu suala hili?
**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wananchi wanaogopa ng'ombe!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kujibu haya ya Mheshimiwa Vita Kawawa, ili nisije nikapata mgogoro hapa.

Kwanza kabisa kuhusu lile zoezi toka juzi, jana hadi leo tulikuwa tunaulizana hivi, hivi wakati zoezi hili linafanyika hawa Ng'ombe walikuwa wanakwenda wapi labda nilieleze vizuri kwa sababu Mheshimiwa Vita sasa ana-*allege* kwamba walipelekwa kule kwao.

Mtu yoyote ambaye alikwenda Ulanga katika zoezi hili na akawa hana kibali, ambaye ameingia pale kama mvamizi hivi, aliambiwa aondoe mifugo yake. Mifugo mingine waliweka masharti wakasema kwenye kijiji kutengemeana na hiyo *holding capacity* yake, mingine ilipelekwa Pugu kwa ajili ya kuuza.

Sasa kwamba tuli-*trace* tukaangalia hawa waliondoka hapa wakaenda kule, hawa walikwenda Namtumbo ama walikwenda wapi ni jambo ambalo itabidi nilifanyie kazi zaidi kujua walikwenda wapi. Lakini nilitaka niseme tu kwamba zoezi lile kama alivyosema Mheshimiwa Haji Mponda, lilifanikiwa kwa sababu Ng'ombe hawa walikuwa karibu laki tatu na themanini, wakarudi mpaka kufikia ng'ombe elfu sitini na tano. Kwa hiyo, sisi tutaendelea kufuatilia huko. *(Makofi)*

Sasa kuhusu hili suala la kuogopa Ng'ombe la kuogopa Maziwa, nyama maana yake ndio chakula tunachokula. Mheshimiwa Vita Kawawa, huyu ni rafiki yangu, mdogo wangu, tunakula naye nyama kila siku hapa pamoja na maziwa tunakunywa wote. Maziwa na nyama ni chakula kizuri, kina vinavirutubisho vya kwenye mwili wa binadamu. Ni chakuala muhimu katika maisha ya binadamu na ndio maana hata ilipotokea kwamba Mungu anamwumba binadamu, katika matiti ya mama hakuweka soda aliweka Maziwa. *(Kicheko/Makofi)*

Alijua watu hawa wazembe wazembe hawa wataleta matatizo akionyesha umuhimu na akafanya hivyo hata kwa wanyama na wale wengine wote. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Vita Kawawa, tutakaa pamoja kwanza tuanze mfano na yeye mwenyewe pale, aanze kufuga Ng'ombe pale kwake ni kitu kizuri.

Botswana ule uchumi wao umepamba moto kwa sababu ya mauzo ya Maziwa na nyama. Ng'ombe mmoja unapata kilo elfu moja na Mheshimiwa Rais huwa anatueleza kila siku.

Kwa hiyo, mimi naomba nimu-*encourage* Ndugu yangu Vita Kawawa, najua ni *dynamic,* ni mtu anayepanda maendeleo, asimame imara awaelimishe wananchi wake kuhusu umuhimu wa kufuga Ng'ombe ili tupate maziwa na nyama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Joseph Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hamisha hamisha na fukuza ya Ng'ombe hawa katika maeneo mbalimbali nchini baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa kutumia Kamati zao za Ulinzi na Usalama wamekuwa wakitumia nguvu ambayo ni kubwa sana dhidi ya Wafugaji na matokeo yake Ng'ombe wengi sana wamekufa katika zoezi hili la hamisha hamisha na fukuza fukuza.

Je, Serikali ipo tayari kuwafidia Wafugaji ambao Ng'ombe zao zilikufa katika zoezi hili la kuhamisha kutoka eneo moja kwenda lingine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, *exercise* hii ilikuwa ni *exercise* kubwa. *Exercise* ambayo ili *involve* mambo mengi. Wakati unapokuwa na *operations* hizi kinachosababisha pale unakuta nguvu zimetumika saa zingine inasababishwa na kurupushani yenyewe inayotokea pale.

Kwa hiyo, kiwango cha nguvu wakati mwingine kinaweza kikawa kimesababisha na hilo. Mimi siwezi kusimama hapa nikambishia *a member of parliament,* Mheshimiwa Selasini nikasema kwamba hapakuwepo na madhara. Kwa mfano pale Ulanga pale, mtu alipigwa risasi akafa halafu mimi nisimame hapa niseme hapakuwa na matatizo pale!

Hatua zilizochukuliwa akaenda Mahakamani askari Yule na askari akaenda akafungwa na akavuliwa madaraka. Kwa hiyo, yapo mambo yamejitokeza hapa hatuwezi kukataa kama Serikali, pale ambapo mtu anaonekana alivunja Sheria hatua hizo zimechukuliwa.

Sasa suala la fidia hapo. Sasa mimi hapa najibu Swali hili hapa nimwambie kutoka leo nawatangazia kwamba wale wote ambao walipata matatizo. Hili jambo ni jambo ambalo litakuja katika utaratibu wa kawaida na tutapima tukiona kwamba kuna hasara zilizotokea, Serikali itatafakari jambo hilo. Lakini kwa hapa mimi siwezi kusema chochote kwa sababu sijui *magnitude* hiyo. Mimi nilikuwa na *deal* na Ulanga lakini kwamba naweza nikai-*commit* Serikali kwamba itatoa fidia, *no!*

**MWENYEKITI:**Tunaendelea! Wizara ya Afya na Ustawi na Jamii. Mheshimiwa Moza Abeid Said Kwa niaba Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga.

Na. 107

**Ugonjwa Sugu wa Malaria**

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA (K.n.y. MOZA ABEID SAIDY)** aliuliza:-

Je, ni nini kinasababisha Serikali kushindwa kutokomeza ugonjwa sugu wa malaria?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Moza Abeidy Saidy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imefanya jitihada mbalimbali katika kupambana na ugonjwa wa malaria hapa nchini. Jitihada hizo ni pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa dawa za kutibu malaria ya kawaida na malaria kali katika vituo vya huduma ya afya, kugawa vyandarua vyenye viutilafu, kutoa dawa za kukinga malaria kwa akina mama wajawazito, kuelimisha jamii jinsi kujikinga na malaria na kusisitiza usafi wa mazingira ili kuzuia mazalio ya mbu.

Aidha, kuanzia mwaka 2006 mpaka 2013 majaribio ya chanjo ya malaria yamefanyika. Chanjo hii imeonekanma salama. Aidha upuliziaji wa dawa za kuuwa mbu majumbani unaendelea. Juhudi nyingi zimefanywa kwa ushirikiano na Serikali ya Cuba ni kujengwa kwa mradi wa kiwanda cha dawa za kuuwa viluwiluwi kilichoko Kibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikilinganishwa na miaka ya nyuma, takwimu za mwaka 2013 zimeonesha kuwa maambukizi ya malaria yamepungua kwa zaidi ya asilimia 47 kati ya mwaka 2008 hadi 2013. Mapambano dhidi ya malaria yamechangia kupungua kwa vifo vya watoto chini ya umri wa miaka 5 kutoka vifo 148 kwa kila vizazi hai 1000 ya watoto waliozaliwa mwaka 1995-1999 kufika vifo 54 kwa kila kizazi hai 1000 mwaka 2013. (Kwa mujibu wa ripoti ya Umoja wa Mataifa ya 2013). Viashiria vya tafiti mbalimbali vinaonyesha kuendelea kupungua zaidi kwa maambukizi ya malaria katika jamii kwenye maeneo mengi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii ni sehemu muhimu katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria nchini hasa ikilenga matumizi sahihi ya dawa za kutibu malaria ili kuzuia kujitokeza kwa malaria sugu, kutumia nyenzo za kinga kama usafi wa mazingira, kudhibiti wa mazalio ya mbu, matumizi ya vyandarua vyenye viutilifu na upulizaji dawa nyumbani. Mpango wa utekelezaji wa mapambano haya unaendelea kufanyika kikamilifu kwa kushirikisha jamii hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kushirikisha jamii, sekta nyingine na wadau hapa nchini katika vita ya kutokomeza ugonjwa wa malaria, ikiwemo kufanya tafiti zinazolenga kuua mazalia ya mbu. Mafanikio yaliyopatikana hadi sasa yanaonyesha kuwa ugonjwa utatokomezwa kabisa hapa nchini siku za hivi karibuni. Tanzania bila malaria inawezekana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga!

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumwuliza Maswali mawili madogo Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwakuwa katika majibu yake amesema Serikali inaendelea na mpango wa kupuliza dawa majumbani na kwa kuwa mpango huu sasa unatakribani zaidi ya miaka minne lakini haujatekelezeka kwa eneo kubwa la Tanzania Bara.

Je, ni lini mpango huu utakamilika kwa Mikoa yote ya Tanzania Bara na ili kuepusha wadudu wanaoambukiza maradhi ya Malaria.

Kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa homa ya Dengue. Wananchi wengi wameshindwa kutofautisha dalili za awali za homa ya Dengue na homa ya Malaria na kupelekea watu kutojua na kuwa na tafrani kwa awali.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendelea kuwaelimisha Wananchi hasa wanaotoka Dar es salaam na kuelekea Mikoa mingine, hasa Vijijini dalili hizi za awali za kuweza kutofautisha homa ya Malaria na homa ya Dengue?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya A suala la kupulizia dawa majumbani ni Mradi ambao unapaswa kuwa endelevu si katika Mikoa michache tu ambayo nguvu kubwa ilikuwa imeekeza kwa sababu ya uhalisia wa ukubwa wa tatizo la Malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni suala la nchi nzima na ndio sababu Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ilipitisha Sheria Namba 1 ya Mwaka 2009 juu ya suala la Afya ya Jamii ikiwemo suala zima la mazingira kwa ajili ya kudhibiti mbu.

Sehemu ya B kwamba wananchi wanaweza kutotafutisha vipi dhidi ya dalili ya awali za ugonjwa wa Dengue na Malaria. Kama ambavyo kauli ya Serikali imetolewa hapa Bungeni kupitia vyombo mbalimbali hapa nchini, pamoja na mikutano ya hadhara na maelekezo ambayo Serikali tumeshayatoa kwa Mikoa yote, kupitia Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Waganga Wakuu wa Mikoa na Waganga Wakuu wa Wilaya kushirikiana na Shirika la Afya ulimwenguni kupitia *fact sheet* yaani dalili zile zikoje, *standard case definition* yaani mgonjwa anaoonekana vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu kubwa inayofanana na ugonjwa wa Malaria wa *Dengue February Fever* yaani homa kali ya *Dengue* ambayo kunakuwa na kichwa kuuma sana, homa kali pamoja na viungo kuuma na ndio sababu katika vipimo vya haraka yaani *Malaria Rapid Dignosis Test*, upimaji ule unasaidia kuainisha kama kuna Dengue au hakuna *Dengue*. Kwa sababu Vituo vyote vya kutoa huduma ya Afya katika nchi tunazo dawa hizi za vitenganishi za kupima ugonjwa wa Malaria na pia Mikoa yote tumeshasambaza dawa hizi za vitenganishi za kubaini kwamba kuna *Dengue* au hakuna *Dengue*.

Kwa hiyo, tunawashauri Watanzania wote, unavyojisikia kuwa na homa kali, kichwa kuuma pamoja na viungo wahi haraka sana katik vituo vya kutoa huduma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**MHE. SULEIMAN NCHAMBI SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru lakini awali ya yote nimwombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu Kishapu inalima Dengu sana, na

kwa jinsi anavyotamka kwamba homa hii ni ya Dengu, wanaweza wakaacha kulima Dengu ni bora atamke Dengue wasije wakaogopa hizo Dengu wakarudi kwenye umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Kishapu na Jimbo la Kishapu linatekeleza mpango kabambe wa ujenzi ya Hospitali ya Wilaya ya kisasa kabisa ambayo hata ndugu zetu wanaokalia Dole, Mkanyageni, Mchambawima hawana Hospitali kama hiyo, hata kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Tundu Lissu. Kwa hiyo, nilikuwa nina Swali moja kwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Je, Waziri aliniahidi kuja Kishapu kwa ajili ya kuhakikisha Hospitali hii inakamilika mapema mwaka huu. Je, waziri yupo tayari yeye na Wataalam wa Wizara kuja kuharakisha Hospitali kabambe kwa sababu homa ya Dengue imewatisha Wanakishapu, hawawezi kutoka Magalata kwenda Shinyanga Mjini? Namwomba sana anipe jibu kwamba yupo tayari yeye na Wataalam kuja kuhakikisha wanasukuma Hospitali hiyo inakwisha mapema mwaka huu 2014?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Jibu fupi tu, uko tayari nenda kaonane naye.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA UTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, namshukuru pia Mheshimiwa Mbunge Nchambi kwa swali lako la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sehemu ya utaratibu wa kawaida kusimamia huduma ya afya katika nchi katika ratiba ya kawaida tutafika Kishapu lakini tunachoomba kwa utaratibu watuletee barua ngazi ya Wizara ya Afya ili tuweze kutuma timu yetu ya watalaam kwenda kukagua hali ya hospitali ile ikoje, ili iweze kuongezea nguvu zaidi.

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana. Ni kweli kwamba malaria inaua watu wengi hasa watoto, lakini pia ninaamini kwamba katika kutokomeza malaria ni lazima tutokomeze mbu. Kuna wakati Serikali ilienda ikatafuta misaada ya *net* wakagawa karibu vijiji vyote wanagawia watu *net*. Je, wanafikiri miradi ya misaada ile waliyotafuta ya kugawia wananchi ilikuwa ni njia sahihi ya kutokomeza malaria badala ya kufanya jitihada kubwa ya kutafuta dawa ya kunyunyizia maeneo mbalimbali ili waue mbu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Waheshimiwa tunatoa nafasi hizi kidogo nyingi kwa sababu tulichelewa kuanza lakini masuala haya ya malaria na *Dengue* ni *serious*. Hivyo tutaongeza kidogo Waheshimiwa Wabunge. Mhesahimiwa Waziri wewe ni mtalaam naomba ulisaidie Bunge namna ya kudhibiti haya mambo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA UTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma kabisa ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba Malaria inatokomezwa kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la upuliazi katika kudhibiti Mbu kuna njia kuu tatu, kuna kunyunyizia katika ngazi ile ya *lava*, kuna kunyunyizia dawa katika ngazi ya viluilui, pia kuna kunyunyizia dawa kwa ajili ya kuua mbu wapevu.

Suala hili ni endelevu nandiyo sababu chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kukubaliana na Serikali ya Cuba kwa nguvu zake na nguvu binafsi tumeweza kupata kiwanda ambacho tunatengeneza dawa za kupulizia ambacho mwezi wa tisa kitafunguliwa baada ya kufanyiwa majaribio mwezi wa sita mwaka huu. Hii ni kazi kubwa ambayo imefanyika chini ya Chama cha Mapinduzi, ni kiwanda cha pekee katika Afrika, ni Tanzania peke yake ndiyo tuna kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za *net*, ni zaidi ya *net* zipatazo milioni 38 zilishagawiwa mpaka mwaka jana na mwaka ujao wa fedha 2014/2015 kazi kubwa sana itafanyika, vyandarua vipatavyo milioni 6.2 zitagawiwa kwa Watanzania bure. Si hilo tu *net* zipatazo 500 zitagawiwa kwa watoto wa shule katia Mikoa ya Lindi, Mtwara pamoja na Ruvuma.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri wa Afya nina swali moja la kumwuliza.

Ni muda mrefu sana sasa ndani ya nchi yetu Serikali imekuwa na kigugumizi kuwaeleza wananchi ni dawa gani ambayo inatibu malaria ndani ya nchi yetu. Mara watu wanaambiwa dawa ya mseto, mara wanaambiwa watumie fansider, sijui dawa gani. Wewe kama Mtalaam wa mambo ya afya waeleze wananchi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa subiri. Waheshimiwa Wabunge tumesema hii ni hoja ya msingi na tumetoa nafasi nyingi ili tuelewe na tukirudi Majimboni tukasaidie wananchi wetu, badala ya hiyo mnaanza zogo humu ndani! Endelea. (*Kicheko*)

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba uliambie Taifa watu wanapopata Malaria ni dawa gani hasa itumike katika kutibu malaria katika nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA UTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa hizi zipo katika makundi matatu. Unapokuwa na malaria kama ni ile ya kawaida unatumia dawa inaitwa *ALU* dawa ya mseto. Pale ambapo malaria inakuwa ni kali unatumia dawa ya *chloroquine* kulingana na uzito wa mgonjwa pamoja na hali ya mgonjwa ilivyo ikiandamana na dawa za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa cha msingi katika tiba ya malaria historia ya nchi yetu tumekwenda na tunavyo vituo vipatavyo nane ambavyo tunafuatilia uwezo na ubora wa dawa. Vituo hivyo vipo katika hospitali zote za Rufaa za Kanda na pia katika Hospitali ambazo zipo mpakani mwa nchi yetu ikiwemo Kigoma, Kagera pamoja na Musoma kwa ajili ya ku-*control* mipaka yetu kwa ajili ya usalama wanchi yetu.

Lakini pia kikubwa cha msingi katika tiba tunapima kuangalia hali ya ubora wa dawa kwa kutumia wakati mwingine maabara zinazohamishika *mini lab* ambayo tunaangalia hali ya ubora wa dawa ile na kulingana na viwango vya kimataifa, shirika la ulimwengu linaelekeza kwamba dawa ile kama ina uwezo wa kufikia asilimia 25 inapaswa itoke katika soko kwa sababu ya hali ya usugu. Tunaomba watanzania wote ile tiba ambayo ni sahihi ndiyo ambayo tunasisitiza. Pale ambapo Mtanzania atajisia kuumwa ni vizuri aende katika tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2001 utakumbuka nchi yetu tuliondosha *chloroquine* baada ya usugu ule kufikia asilimia 52 na ndiyo sababu tukaenda katika dawa ya *SP,* ikatoka katika soko na kuingiza dawa ya *ALU* mwaka 2006 mwezi Januari kwa sababu nchi tuna utaratibu mzuri kuhakikisha hali ya ubora ikoje kwa wakati wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Azzan, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.
Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili wanasema kinga ni bora kuliko tiba. Sisi Dar es Salaam tumepata maafa mawili kwa wakati mmoja.

Kwanza ni mafuriko makubwa ambayo yameleta athari kubwa. Lakini pili ni ugonjwa wa *dengue*. Nataka *commitment* ya Serikali sasa kwa sababu Waziri amesema hapa kwamba moja ya kazi zinazofanyika ni kupulizia dawa ili kuua mazalia ya mbu na mbu wanaosambaza *Dengue*. Ikiwa basi moja la abiria linapuliziwa dawa kwa shilingi 65,000 ni mwananchi gani ataweza kupuliza dawa nyumbani kwake, huu siyo wizi?

Nataka Serikali iniambie sasa, kwa dharura hii ambayo imetokea Dar es Salaam, ili kukinga ugonjwa huu wa *Dengue* ni nini mkakati wa Serikali wa dharura kumwagilia dawa ya kuua mbu hawa kuzuia mazalia yao ili wasienee katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam, hususani maeneo ya Mwananyamala kwa Msisiri, Kinondoni B' Kanazi, Jangwani, Temeke na kadhalika?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri. Gharama ya vipimo, elfu thelathini ni nyingi sana kwa wananchi. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA UTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba *Hansard* iweke *record* vizuri. Katika malaria kali tiba tunatumia *quinine* kulingana na uzito siyo *chloroquine* ambayo tumeshaitoa kwenye soko tangu mwaka 2001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala hili la upuliziaji wa dawa katika magari ya abiria hususani kwa Dar es Salaam, wenzetu wa *SUMATRA* na *TABOA* walikaa wakakubaliana viwango hivi.

Ni imani kwamba kwa ushirikiano mzuri ambao Mkuu wa Mkoa amekaa na kujadiliana pale Dar es Salaam na wamiliki wa vyombo hivi vya usafiri, ilikubalika katika vikao vya pamoja. Hivyo suala la mtu mwenye gari la abiria mfanyabiashara mzuri na mzalendo ambaye anatoa ushirikiano shilingi 65,000 hawezi akaikosa kwa ajili ya kupulizia kwa usalama wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nawahimiza Watanzania wote maeneo yote nchi nzima utaratibu huu uweze kufuatwa. Wenzetu wa *SUMATRA* pamoja na *TABOA* watoe ushirikiano ili vyombo hivi vya usafiri kama tunavyofahamu hata London imewahi kupatikana kesi ya malaria kandokando ya uwanja wa ndege wa *Heathrow* wakaita ni *airport* Malaria. Kwa sababu vyombo hivi vya usafiri vinaweza kusafirisha mbu kwenda sehemu ya mbali sana, ingawaje uwezo wa mbu kuruka ni kilomita mbili hadi tatu ile *flat range*, upepo unaweza kumsafirisha mbu lakini pia vyombo hivi vya usafiri vinaweza kusafirisha mbu kwenda sehemu yeyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili kwa mujibu wa kanuni kwa ruhusa yako ni mipango gani ambayo imeandaliwa ya dharura. Tangu ugonjwa huu ulipojitokeza katika nchi yetu mwaka 2010 ambapo Watanzania takribani 40 waliweza kuathirika, nchi ilitoa maelekezo kwa kushirikiana na Shirika la Afya Ulimwenguni kwamba Mikoa yote kwa kupitia kwa Waganga Wakuu wa Mikoa na pamoja na Wakuu wa Mikoa na Waganga Wakuu wa Wilaya kusimamia suala zima la mazingira.

Mazingira ndiyo yatasaidia katika kuondoa mbu ambayo ndiyo njia sahihi kuweza kutokomeza ugonjwa huu ikiwemo malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeweza kusambaza vitenganishi *Rapid Agnostic Test* za ugonjwa huu wa dengue katika mikoa yote.

Hivi tunavyozungumza saa yeyote vitenganishi vingine vitaingia, viingie katika mfumo wa kawaida wa *MSD* katika bohari ya dawa ili kusudi ziweze kupatikana pale zinapohitajika katika kanda ya karibu pale Wilaya zilipo. *(Makofi)*

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Afya na Ustawiwa Jamii, napenda kuuliza swali moja kama ifuatavyo.

Kumekuwa na kada ya wafanyakazi wanaoitwa Bwana Afya na siku hizi wanaitwa Maafisa Mazingira, hawa wanaelekea kwamba kazi yao ambayo ilikuwa ni ya msingi ya kuhakikisha kwamba mazingira yanakuwa ni masafi. Kuhimiza ujenzi wa vyoo ambavyo ni salama, vyoo na mifuniko na usafi wa mazingira katika makazi ya watu.

Lakini siku hizi hawa Bwana Afya wajibu wao wa kuhakikisha mazingira, ujenzi wa Vyoo salama ili kusudi kuzuia mbu hawafanyi hiyo kazi wanakagua tu maduka ya nyama, wanakagua na migahawa kwa sababu zao wanazozijua.

Je, Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hawa Mabwana Afya wanarudi kufanyakazi yao ya msingi ambayo ni kuhimiza usafi wa mazingira na ujenzi wa vyoo salama ili kuondoa mazalia ya umbu na inzi wanaoeneza magonjwa katika nchi yetu?

**MWENYEKITI:** Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA UTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na tunaomba Watanzania wote Maafisa Afya na tunashukuru TAMISEMI wameajiri kada hii ya Maafisa Mazingira, naomba wafanye kazi kwa pamoja kwa maelekezo ya Serikali ili kusudi kazi ile ya kusimamia usafi wa mazingira na afya kwa ujumla iweze kwenda vizuri.

Tunashukuru TAMISEMI wameweka kada hizi katika ajira, wasaidiane na Maafisa Afya. Maafisa Afya pale wanapokwenda katika maeneo ya kazi tunatoa maelekezo na rai atakayebainika anakwenda katika migahawa, anakwenda katika baa badala ya kusimamia suala zima la usafi a mazingira hatua zichukuliwe.

Kwa wale Waganga wa Wilaya na ninatoa wito na tutatembea nchi nzima kuhakikisha suala hili linasimamiwa vizuri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Zedi.

Na. 108

**Hitaji la Mawasiliano ya Simu Wilayani Nzega**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Kata za Kahama ya Nhalanga, Karitu, Isagenhe na Samembela, zinachangia sana katika mapato ya ndani katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, lakini Kata hizo hazina huduma muhimu ya mawasiliano ya simu za mkononi:-

Je, ni lini Kata hizo zitajengewa minara ya mawasiliano ya simu za mkononi ili wananchi wake wapate huduma ya simu na kuongeza tija katika shughuli za kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sulemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ikishirikiana na wadau mbalimbali hususani watoa huduma za mawasiliano, inaendelea na juhudi za kupeleka huduma ya mawasiliano hapa nchini hasa katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara. Aidha Wizara imeanzisha mfuko wa mawasiliano kwa wote ambao pamoja na mambo mengine utaharakisha kazi hiyo ya kupeleka huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, imeainisha maeneo ya Kata za Kahama, Nyalanga, Karitu, Isagaribe na Samembela yaliyopo Jimbo la Bukene kuwa miongoni mwa maeneo yenye uhitaji wa mawasiliano hapa nchini.

Katika zabuni ya awamu ya kwanza B iliyotolewa mwezi uliopita Kata ya Kahama ya Nhalanga imepata mzabuni ambayo ni kampuni ya *Airtel* ambapo kazi ya upelekaji mawasiliano inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Februari mwaka 2015.

Aidha, maeneo ya Karitu, Isagaribe na Semembela yanatarajiwa kuingizwa katika mpango wa zabuni ya awamu ya pili inayotarajiwa kutangazwa mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara yetu inaendelea kuwahimiza watoa huduma kupeleka huduma za mawasiliano ya simu za viganjani kwenye maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara.

**MHE. JUMANNE S. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongze Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini pia niipongeze kampuni ya *Airtel* kwa kushirikiana na mfuko wa mawasiliano kwa wote kukubali kujenga mnara katika kata ya Kahama ya Nhalanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza nilitaka nijue katika huo mpango wa pili wa zabuni wa awamu ya pili ambapo Kata za Karitu, Isagenhe na Semembela zitatangazwa kwa ajili ya kupata mzabuni wa kujenga minara. Ninataka kujua mpango wa Serikali endapo watoa huduma bado hawatakuwa na nia ya kujenga minara kwenye Kata hizi.

Je, Serikali ina mpango wowote wa kutumia mfuko wa mawasiliano kwa wote kuongeza ruzuku au hata kujenga kwa asilimia mia moja ili maeneo haya ya vijijini ambako watu wanazalisha sana nao wapate huduma muhumi ya mawasiliano ya simu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Zedi, kwa swali zuri la nyongeza. Ni kweli moja ya changamoto tulizozipata ni kwamba kuna nyakati tunatangaza zabuni hizi za ruzuku na bado makampuni hayapeleki mawasiliano kule ambapo tumeweka ruzuku. Kwa hiyo, tulichoamua kama Serikali ni kutafuta fedha zetu wenyewe kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana hapa Wabunge wengi walikuwa wanaomba kupelekewa barabara na itakapokuja Wizara ya Nishati na Madini wataomba kupelekewa umeme, itakuja Wizara ya Maji wataomba kupelekewa maji, lakini Wabunge wanaomba hivyo kwa kuwa wamepangia hizo Wizara fedha.

Sisi Wizara Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Wabunge wanatuomba minara wakati hawajatupangia fedha hata shilingi. Wizara sasa imeamua itafute fedha ili tujenge wenyewe hii minara, ili mnapotuomba minara tuwe na sisi tuna fedha za kujenga minara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilienda India Serikali imeomba mkopo kutoka Serikali ya India wa shilingi dola milioni 154 na tumeorodhesha maeneo yote yasiyo na minara nchini na tumepiga gharama za kujenga wenyewe minara ni karibu shilingi bilioni 320.

Wakati wa Bajeti yetu tutatoa orodha ambayo ninayo hapa ya kila eneo lisilo na mawasiliano na gharama za kupeleka mawasiliano kwenye hilo eneo na ratiba ya kupeleka mawasiliano kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ni kwamba tusifike kwenye jambo alilokuwa anasema Mheshimiwa Selemani Zedi kwamba unatangaza zabuni na bado makampuni hayapeleki minara.

Hivyo, kutokana na umuhimu wa mawasiliano na Wabunge wengi wanafahamu. Yupo Mbunge mmoja hapa ameniambia amepeleka maji, amepeleka umeme kwenye moja ya Kata zake lakini bado wananchi wanasema tutapata shida kukupigia kura kama hatuna mawasiliano. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafahamu *pressure* ya Wabunge kwenye Majimbo yao kuhusu mawasiliano. Sisi tutajitahidi kuwasaidia mawasiliano na kwamba kama hamtarudi Bungeni basi iwe ni kwa sababu nyingine siyo kwa sababu ya mawasiliano. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano aliompa Mbunge wa Jimbo la Namtumbo Mheshimiwa Vita Kawawa kwa kupeleka mawasiliano katika Kata ya Magazine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Mgombasi na Mputa bado wana mahangaiko makubwa na kwa udharura ule ule ulioufanya unaweza ukawasaidia kwa haraka wananchi hawa wa Mgombasi na Mputa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana. Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa maswali umekwisha naongeza dakika kumi kwa sababu tulichelewa kuanza.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kwamba maeneo aliyoyataja ya Jimbo la Namtumbo tutafanya jitihada za maksudi kama nilivyoeleza hapo awali kuhakikisha kwamba zinapata mawasiliano kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Serikali ilitupatia orodha ya miradi na maeneo ambako minara itakwenda kujengwa ikiwemo Jimboni kwangu Momba, lakini bahati mbaya sana kuna maeneo ambayo tangu ile miradi imetangazwa mpaka leo na sisi Wabunge tulikwenda tukawaambia wananchi miradi itakamilika haijatekelezeka. Sasa tukawaambie nini wananchi ambapo miradi haijatekelezeka na sisi tumetangaza tunapeleka hiyo lawama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya kulitokea ucheleweshaji mdogo kwenye utekelezaji wa baadhi ya miradi kwa sababu fedha tulizotumia katika ile miradi tuliyoitangaza awali ni fedha za Benki ya Dunia na taratibu za manunuzi ya Benki ya Dunia Wabunge wote mnazifahamu kutokana na uzoefu wenu kwenye miradi ya maji. Lakini tatizo tumelimaliza mapema, kwa hiyo, miradi Ile itatekelezwa haraka kama tulivyokuwa tunarajia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari, kwa kifupi sana. Jiandae Mheshimiwa Mlata.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mabadiilko yaliyofanyika juzi na Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, mimi nilikuwa Naibu Waziri Kivuli wa Wizara hii, na mwaka 2012 Mheshimiwa Januari Makamba atakumbuka kwamba alinipa hata *list* ya vile vijiji ambavyo vingepata mawasiliano kupitia Mpango wa Mawasiliano kwa Wote yaani UCAF na ile *list* baada ya hapo akatuambia tuongeze vijiji vingine huku ndani ya Bunge na Wabunge waliongeza na akatuahidi kwamba kwa mwaka ule wa fedha ile miradi ingeanza. Mpaka leo hii hakuna mradi uliotekelezwa, kwa mfano mzuri kwenye jimbo langu na kama tunavyofahamu umuhimu wa mawasiliano ya simu hususani kwa wakulima simu ndizo zinazotumika kufanya mawasiliano na madaktari wa mifugo na masoko kwa ajili ya mazao yao na vitu vingine kama hivyo.

Sasa nimulize tena Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba hata mimi niliyekuwa Waziri Kivuli nadanganywa, je, ni lini miradi hii itakwenda kutekelezwa na ni lini kule kwangu Ngarenanyuki na maeneo mengine ambayo mpaka leo hii hayana mawasiliano yanakwenda kupata? Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nakuomba kwa kifupi sana ni lini. Mpe tarehe tu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali huwa haidanganyi hapa Bungeni, wala mimi binafsi huwa sidanganyi, na hata katika ile orodha hata mimi nilikuwa na maeneo yangu kama Mbunge wa Jimbo la Bumbuli ambayo na yenyewe yalichelewa na sababu za ucheleweshaji nimezitoa hapo awali kwamba ni taratibu za ununuzi wa Benki Dunia. Dhamira yetu ya kupeleka mawasiliano kote nchini ipo pale pale na wakati wa bajeti yetu tutaeleza kwa kina hatua tunazochukua na maeneo yote na ratiba ya kupeleka mawasiliano katika maeneo yote.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ili kuweza kutimiza azma ya Serikali kupunguza vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua, inaenda sambamba na barabara ambazo zimetengenezwa vijijini; na barabara hizo zinatumika pale mama mjamzito anapopata tatizo ili kukimbizwa kupelekwa kwenye hospitali, wanapiga simu kwenye *taxi* ambazo ziko kwenye miji na *taxi* inakimbia haraka kuja kumchukua mama mjamzito kuokoa maisha yake. Je, kwa nini Wizara yako isiende sambamba na utengenezwaji wa barabara zile ili kuwafikia wananchi wale kuweza kutumia mitandao kwa ajili ya kuokoa vifo vya akina mama? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana muda wetu umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba huduma ya mawasiliano inatoa msaada mkubwa sana kwenye nyanja nyingi ikiwemo nyanja za huduma na tunafahamu kwamba huduma ya mawasiliano imeokoa maisha

na imerahisisha mambo mengi kufanyika ikiwemo kutoa taarifa za wagonjwa kwa haraka wakaja wakakimbizwa hospitali au kumwita daktari au mganga nyumbani ili kusaidia.

Serikali inayo mipango mbalimbali ya kutumia huduma za simu katika kuhakikisha kwamba huduma za kijamii zinaboreshwa ikiwemo elimu, afya na ufuatiliaji wa upatikanaji wa maji katika maeneo ya vijiji. Kwa hiyo, kasi ya utengenezaji barabara nchini tuna hakika kwamba itaenda pamoja na kasi ya ujenzi wa minara katika maeneo yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa, swali la Wizara hiyo hiyo, *issue* hiyo hiyo, Mheshimiwa Komba!

Na. 109

**Tatizo la Mawasiliano ya simu Mwambao wa Ziwa Nyasa**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Kutokana na hali ya mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi, na maeneo ya mwambao karibu yote hasa Kata ya Mbaha, Ngumbo, Luwundi na Luparamba hakuna mawasiliano kabisa:-

Je, Serikali haioni haja ya kuimarisha mitandao ya simu ili kuharakisha mawasiliano kule Mwambao wa Ziwa Nyasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Damiano Komba, Mbunge wa Mbunge wa Mbinga Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina nia ya kufikisha mawasiliano katika maeneo yote yasiyokuwa na mawasiliano hapa nchini pamoja na maeneo ya mipakani. Aidha tumeandaa mpango maalum kabisa wa kupeleka mawasiliano maeneo yote ya mipakani mwa nchi yetu ambayo hayana mawasiliano kama moja ya hatua za kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, tumeainisha maeneo ya Kata, Mbaha, Ngumbo, Liundi, Liparama na Mpepei ambayo iko kwenye Jimbo la Mbinga Mashariki katika Wilaya ya Mbinga kuwa miongozi mwa maeneo yenye uhitaji wa mawasiliano.

Kata ya Mpepei ilipata mzabuni wa TTCL katika zabuni ya kwanza iliyotolewa mwaka uliopita mwezi Machi na kazi ya kupeleka mawasiliano na ujenzi wa minada inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Julai, mwaka huu.

Kata ya Liparama ilipata mzabuni ambaye ni TTCL katika zabuni ya awamu ya kwanza A iliyotolewa mwezi Februari mwaka ambapo kazi ya kupeleka mawasiliano inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Desemba mwaka huu. Aidha, Kata za Mbaya, Ngumbo na Liundi zitaingizwa katika zabuni ya awamu ya pili inayotarajiwa kutangazwa mwaka ujao wa fedha.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri, lakini nina maswali mawili. Kwa kuwa eneo hili la mwambao ndilo lenye wapiga kura wengi sana na hao ndiyo wanakosa mawasiliano na wamesema watanyima kura kama sitaleta minara kule. Swali, je Wizara iko tayari kunitafutia kazi pale Wizarani pao? *(Kicheko/Makofi)*

Swali la pili; kwa kuwa mmoja wa wagombea urais wa Malawi anadai kuwa ile ni sehemu yake na anasema akishinda ataleta mitandao. Je, mko tayari kumpa ruhusa mama yule au nani mwingine yeyote alete pale minara? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utafiti wangu nimegundua kwamba Mheshimiwa Komba amewasaidia sana wananchi wa Mbinga kule kupata Wilaya, Wilaya ya Nyasa. Kwa hiyo, nina hakika kabisa hawawezi kumnyima kura kutokana na kazi kubwa anayofanya. Lakini ikatokea bahati mbaya, basi labda atazame kama yupo kwenye kambi sahihi kwenye yale masuala makubwa, na kama yuko kwenye kambi sahihi basi atapata kazi bila shaka yoyote. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hilda Ngoye!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, samahani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa bado upo? Haya endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza; Sisi dhamira yetu ya kupeleka mawasiliano kwenye ukanda ule wa Ziwa Nyasa ambao ni Kata za Mbaha, Ngumbo na Liundi ambazo zinapakana na nchi ya Malawi, dhamira yetu ipo pale pale na mtu yeyote wa Malawi kwanza hana mamlaka wala uwezo wa kuleta mawasiliano kwenye maeneo hayo na kazi hiyo tutaifanya sisi kabla ya mwaka 2015.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Hilda Ngoye! Waheshimiwa Wabunge mnasimama wengi, muda wetu umekwisha. Mheshimiwa Hilda Ngoye.

**MHE. CYNHYA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Kata alizozitaja muuliza swali la msingi ni mwendelezo wa Kata nyingine vile vile za mwambao wa Ziwa Nyasa katika Wilaya za Ludewa na Kyela. Kata za Makonde, Lupingu, Lumbila, Matema hazina mvuto wa kibiashara kabisa. Je, Serikali inaweza kutoa mpango gani wa haraka wa kuhakikisha kwamba Kata hizo nazo zinapata mawasiliano ya simu haraka iwezekanavyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba Serikali imeandaa mpango mahususi na tutaueleza wakati wa Bajeti yetu wa kupeleka mawasiliano kwenye maeneo ya mipaka ya nchi yetu kama moja ya hatua za kulinda usalama wa nchi yetu na maeneo niliyoyataja ya ukanda wa Ziwa Nyasa na baadhi ya maeneo ya Jimbo la Ludewa la Mheshimiwa Filikunjombe, kwa Mheshimiwa Ntukamazina, kwa Mheshimiwa Mipata kule Ziwa Tanganyika na kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama kule kwenye mpaka wetu na *Mozambique* na kwa Mheshimiwa Lukuvi.

Wabunge wote wa mipakani nimezungumza nao na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Ngoye naye nimepata kuzungumza naye. Kwa hiyo mpango huo tutaueleza kwa kina wakati wa bajeti yetu na hata kama maeneo haya hayana mvuto wa kibiashara, lakini kutokana na umuhimu wa kupeleka mawasiliano kwenye maeneo ya mipaka, Serikali itajenga minara hii kwa fedha zake ili tuweze kujihakikishia usalama wa nchi yetu.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu suala la mwambao linafanana na Jimbo langu la Njombe Kaskazini, mwaka juzi, nilizungumzia Kata ya Ikuna, Ikondo, Kitandililo, Mahongole kwamba wananchi hawa wanapata tabu sana hasa Kata ya Ikondo. Nilizungumzia kwamba wananchi hawa kufanya mawasiliano mpaka waende kilomita kama 20 wakapande juu ya miti; na nikasema baadhi ya watu wameshavunjika miguu na mikono kwa sababu ya suala la mawasiliano. Serikali mwaka juzi ikaniahidi kwamba itapeleka mnara mmoja katika Jimbo la Njombe Kaskazini katika Kata ya Kidegembye; na Waziri wa Mawasiliano alipokuja mwaka jana mwezi wa Novemba tukiwa kwenye ziara na Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aliwahakikishia wananchi wa Kata Kidegembye pale kwamba watapata mnara na orodha ninayo. Je, mpaka sasa Serikali inasema nini juu ya mnara ambao ilishaahidi kuujenga katika Kata ya Kidegembye? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana muda wetu umekwisha. Waheshimiwa Wabunge wengine tutasubiri kwenye Wizara inapokuja.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika orodha niliyonayo hapa ya maeneo ya kupeleka minara katika nchi yetu, Kata ya Kidegembye imo, ina Vijiji vitatu na tutatumia shilingi milioni 166 kujenga mnara katika eneo lile. Kwa hiyo, ahadi yetu tutaitimiza. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Sanga kwamba ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri itatimizwa kwa uhakika kabisa. *(Makofi*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuliongeza muda kidogo kwa sababu tulichelewa kuanza. Najua Wizara hii ina wachangiaji wengi na mambo mengi. Lakini na mimi vile vile inabidi ni-*manage time* ninapokuwa hapa.

Sasa tutangaza wageni ambao wapo leo kwenye Bunge. Tunaanza na wageni Wabunge wetu ambao ni wawakilishi wetu kwenye Afrika Mashariki. Tukianza na Mheshimiwa Alhaj Adam Kimbisa, Mwenyekiti wa Bunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Ahsante karibu. Yeye ameambatana na Mheshimiwa Bernad Mrunya, Mbunge wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Twaha Isa Tasilima, Mbunge wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Angela Charles Kiziga, Mbunge wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Ndelakindo Kessy, Mbunge wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Makongoro Nyerere, Mbunge wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Shyrose Banji, Mbunge wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Abdula Mwinyi, Mbunge wa Afrika Mashariki. Naona Bernard Mrunya imerudiwa mara mbili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunawapongeza Wabunge wetu hawa kwa kazi nzuri wanayoifanya. Uwakilishi wao ni nzuri na taarifa za Kamati ambazo tunazipata wanajitahidi kulinda maslahi ya Tanzania. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Haji Makame, Waziri wa Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora wa Zanzibar ambaye anaambatana na Ndugu Khamis Ally Khamis, Mkurugenzi wa DIASPORA, Ofisi ya Rais Ikulu Zanzibar. Karibuni Dodoma.

Mheshimiwa Mwangaseme Makete, Mkuu wa Wilaya ya Kaliua ambaye pia ni Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Urambo. Karibu sana.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; Wageni wa Mheshimiwa Samuel Sitta, Mbunge, Waziri wa Ushirikiano Afrika Mashariki ambao ni Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Maafisa kutoka Wizarani wakiongozwa na Bi. Joyce Mapunjo, Katibu Mkuu wa Wizara na Ndugu Mathius Msole, Naibu Katibu Mkuu.

Karibuni sana. Na hongereni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Samuel Sitta ni Waheshimiwa Madiwani 21 kutoka Urambo ambao ni kutoka vyama vya CCM, CHADEMA na CUF, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo. Mheshimiwa Adam Mulukwi. Aidha wameambatana pia na maafisa kutoka Urambo ambao wanaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Ndugu Ruchasi Biakwata. *(Makofi)*

Ngudu Estella Mgala kutoka Mamlaka ya Uendendaji ya Bonde La Ziwa Victoria, Ndugu Simon Msemwa kutoka Mamlaka ya Uendeshaji Bonde la Ziwa Victoria, Dkt. Josephat Kweka, Mkurugenzi Taasisi ya *Trade Mark East Africa. (Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Abdallah Juma Sadala, Mbunge, Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni ndugu Sadala Sadala, mtoto wake. Hassan Wahid, mtoto wake.

Wageni wanane wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mbunge kutoka Chama cha Makatibu Muhtasi Tanzania (TAPS) wakiongozwa na Mrs. Pili Mpenda, Mwenyekiti wa Chama hicho. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Gosbert Blandes ambao ni Mheshimiwa Sabil Wazo, Diwani wa Kata ya Kanoni na ndugu Sevin Sunday, mfugaji toka Kata ya Kyanga.

Wageni wa Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge ambao ni Kiongozi wa Baraza la Wanawake la CHADEMA Mkoa wa Pwani ambaye ni ndugu Luiza Mdachi na Ndugu Zawadi Salimu. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa John Komba, Mbunge ambao ni wanafunzi 47 kutoka *Edgar Maranta School of Nursing ya St. Francis* kutoka Ifakara. Karibuni na mpendekeza sana. Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 80 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma na wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma. Karibuni sana, msome na mmeona juzi mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu imeongezwa, kwa hiyo muipende Serikali yenu. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Abbas Mtemvu, anawatangazia Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam kuwa leo saa saba kutakuwa na kikao cha Wabunge hao Ukumbi wa Msekwa B.

Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 22 saa saba kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa C. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 22 saa saba mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati Ukumbi Namba 227 ghorofa ya pili Jengo la Utawala.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia?

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia Kanuni za Bunge lako Tukufu 68 (7) ya kuomba Mwongozo, sitaisoma kuokoa muda, 46(1) Fasili ya kwanza inayosema,

*"Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa."* Na 64(1)(a) inayoelezea majadiliano ndani ya Bunge, *"Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania majadiliano yanayoendelea katika Bunge ni kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge; Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli"* na (g) inasema, *"Hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba Mwongozo wako, nilipouliza swali hapa la nyongeza kuhusu kuwawezesha wakulima wadogo wa chumvi kule Singida pamoja na Uvinza, ni wakulima wadogo sikutaja mtu. Na ipo sheria ya ku-*empower indiginious,* ku-*empower* wazawa wa nchi hii. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi pia inazungumzia kuwawezesha wazawa wa Taifa hili. Rais, anakuwa anasema kila mara kuwawezesha Watanzania wazawa wa kawaida waweze kunyanyuka vizuri. Lakini Mheshimiwa Waziri, Prof. Sospeter Muhongo, alivyokuwa anajibu ametumia lugha ya kuudhi na mimi nilikuwa najadili hoja, nilikuwa sijadili mtu. Sasa kama yeye Mheshimiwa Profesa ana ugomvi binafsi na Reginald Mengi, na mtu binafsi sioni dhambi… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, mnapiga makofi wala hajamaliza, mimi simsikii sasa, labda mnasikia nyie? Na Mwongozo najibu mimi, sio nyie. Hebu rudia tena?

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo sheria ya kuwawezesha wazawa wa nchi hii na ndiyo sababu kulikuwa na mabilioni ya *JK,* kulikuwa na kuwezesha vikundi mbalimbali vidogo na fedha huwa zinatengwa kwenye Bunge lako Tukufu. Hata Ilani ya Chama Cha Mapinduzi neno uzawa lipo ndani yake kuwawezesha wazawa wan chi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati Mheshimiwa Waziri anajibu swali, amezungumza kana kwamba kuzungumza wazawa ni uhaini katika Taifa hili. Je, anaenda kinyume na Ilani yake ya Chama Cha Mapinduzi na sheria inayo-*empower* wazawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; kama ana ugomvi binafsi na Reginald Mengi, ugomvi wao ambao sioni hata kama Reginald Mengi angekuwa na uwezo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia, hoja yako imefahamika, umeomba Mwongozo, nakushukuru.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia; naomba sasa niombe mwongozo. Nasema kama ana ugomvi binafsi na Reginald Mengi, asisababishe amani na utulivu ndani ya Bunge lako ukaondoka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia, kaa chini nakuomba.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na *arrogance* ya namna hii haifai. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia kaa chini.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mengi ana haki kama Watanzania wengine wote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia, nikisimama mimi wewe unakaa chini. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

**MWENYEKITI:** Ndivyo Kanuni zinavyosema, nikisimama mimi wewe unakaa chini. Mimi nina *red card* na *yellow card* hapa, nikikasirika ninatoa *red. (Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 45(3) ukurasa wa 28, inanipa mamlaka kama nimeridhika na mwongozo au nimeridhika na hoja ya Mbunge niweze kufanya maamuzi.

Kwa vile hoja hii bado ni ndefu na inaonekana vilevile kuna mengine ndani yamejificha, mwongozo huu nitautolea maamuzi baadaye. Katibu?

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 - Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki? *(Makofi)*

**Hotuba ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki Kama Ilivyosomwa Bungeni**

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka katika hali ya afya, ili kuweza kuendelea na kazi zetu leo hii. Na kabla sijaisoma Hotuba yangu naomba Waheshimiwa Wabunge watambue kwamba, hotuba yangu ina viambatanisho vifuatavyo: Kwanza ipo hotuba kwa Kiswahili, iko nakala kwa Kingereza, kiko Kijitabu cha maelezo kuhusu Mtangamano na ndani ya hotuba yangu kuna Kipeperushi kinachoelezea Miradi ya Zanzibar na pia kuna Kichapisho kuhusu Wimbo wa Afrika Mashariki. Kuna Kijitabu cha Taarifa Muhimu kwa Wananchi kuhusu Mtangamano, Mradi wa Hifadhi ya Mazingira Ziwa Victoria, Vituo vya Pamoja na Kamisheni ya Kiswahili iliyokwishaundwa ambayo inaanza kazi yake Zanzibar Mwaka huu wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 2 hadi 9 katika hotuba yangu zinahusu mambo ya shukrani, pole na pongezi ambayo sina ulazima wa kuyakariri katika totuba yangu hii fupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandaaji wa hotuba hii umezingatia hotuba iliyotangulia ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, ambayo imetoa mwelekeo na vipaumbele vya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka huu wa fedha ina sehemu kuu 7, kama ifuatavyo:- Kwanza, Utangulizi ukurasa wa 1. Malengo ya Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2014 ukurasa wa 4, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa 2013/2014 ukurasa wa 8, Changamoto za Utekelezaji wa Mpango ukurasa wa 51, Mpango wa Bajeti 2014/2015 ukurasa wa 52. Shukrani kwa Washirika wetu wa Maendeleo ukurasa wa 56 na inahitimishwa na Maombi ya Fedha kwa Mwaka huu unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Mwaka 2013/2014 Wizara tulijipangia malengo 13 yaliyohusu kusimamia ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya Jumuiya, kuratibu utekelezaji wa makubaliano mbalimbali ya Jumuiya yanayotekelezwa na sekta ya umma na binafsi, kutoa elimu kwa umma kuhusu hatua za mtangamano, kusimamia utaratibu wa kuhusisha Halmashauri za Wilaya katika masuala ya Jumuiya na kuimarisha uwezo wa Wizara kiutendaji, ili ihimili shughuli za mtangamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kawaida sehemu kubwa ya hotuba hii ya bajeti inahusu mapitio ya utekelezaji wa malengo na mpango wa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2014. Katika kipindi hiki cha 2013/2014 Sera zifuatazo zilikamilishwa:- Sera ya Vijana Afrika Mashariki na Sera ya Wananchi Wenye Mahitaji Maalum. Lengo la Sera hizi ni kutuwezesha kubuni miradi itakayoibuliwa na jamii husika, ili kunufaika na fursa za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Mifugo na Sera ya Usalama wa Chakula na Lishe zitakamilishwa katika nusu ya kwanza ya mwaka mpya huu wa fedha 2014/2015. Sera ya Mifugo inakusudia kuweka mwongozo wa kurutubisha mifugo kwa kuzingatia matumizi bora ya ardhi na uhifadhi wa mazingira. Aidha Sera ya Usalama wa Chakula inalenga kuwepo miongozo itakayowezesha uhakika na ubora wa chakula cha kutosheleza katika Kanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya utekelezaji katika hatua zetu nne za mtangamano ni kama ifwatavyo:- Umoja wa Forodha: Mwaka 2013/2014 nchi wanachama zimekamilisha majadiliano ya uanzishwaji wa mfumo wa himaya moja ya forodha na kuanza utekelezaji wake. Mambo makuu yaliyoainishwa katika mfumo wa himaya moja ya forodha ni uthamini wa bidhaa na ukusanyaji wa kodi kufanyika katika nchi bidhaa hizo zinakokwenda. Aidha, baada ya kuthibitisha kuwa kodi imelipwa bidhaa zitaondololewa katika nchi zilipoingilia kwa mara ya kwanza ndani ya Jumuiya na kusafirishwa kwenda nchi husika chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Forodha kwa kutumia mfumo wa ki-*electronic* wa kufuatilia usafirishaji wa bidhaa unaoitwa kwa Kingereza *Electronic Cargo Tracking System.* Bidhaa zitakazokuwa zimelipiwa kodi kwenye nchi husika zitasafirishwa kutoka nchi zilipoingilia na kwenda katika nchi husika bila kuwekewa dhamana *(bond)* kama ilivyo sasa na hivyo kupunguza gharama kwa wafanyabisahara wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya kuwa na himaya moja ya forodha ya Afrika mashariki ni kuongeza kasi ya mzunguko wa bidhaa pamoja na kupunguza gharama za kufanya biashara ndani ya Jumuiya. Aidha, himaya moja ya forodha ya Afrika Mashariki inategemewa kukuza biashara kwa kurahisisha mtiririko wa bidhaa kutoka nje ya Jumuiya kuingia katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kukuza na kuvutia uwekezaji miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na tatu, kupunguza muda wa kusafirisha bidhaa kutoka nchi moja kwenda nyingine mwanachama kwa kupunguza vituo vya forodha vya ukaguzi vilivyopo ndani ya nchi.

Mhesimiwa Mwenyekiti, vilevile utaratibu huu utaongeza ufanisi wa bandari zetu na kuvutia wafanyabiashara kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi nyingine zinazopakana na Tanzania kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi na Zambia kuendelea kuzitumia bandari zetu na hivyo kuongeza pato la Taifa linalotokana na mapato ya bandari na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Forodha wa Afrika Mshariki umeendelea kuimarisha biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na nchi nyingine wanachama. Thamani ya bidhaa za Tanzania zilizouzwa katika nchi wanachama iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 409 mwaka 2011 kufikia Dola milioni 613 mwaka 2012. Aidha kwa mujibu wa takwimu za awali za mwaka 2013, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania katika nchi wanachama imefikia dola za Marekani milioni 1,120 ikiwa ni ongezeko la 82% dhidi ya 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zilizouzwa zaidi ni mashine, mbolea, vifaa vya umeme, vifaa vya boti na meli, nafaka, bidhaa za mafuta na vimiminika, karatasi na bidhaa za nguo. Kiambatisho namba 1 kinabainisha mwendendo wa biashara kati ya Tanzania na nchi wanachama kwa mwaka 2008 hadi 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwendendo huu unaashiria kuendelea kuimarika kwa sekta ya viwanda nchini na wafanyabiashara wa Tanzania kuendelea kuchangamkia fursa zitokanazo na Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Katika kipindi hiki jumla ya miradi saba yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 9.11 iliwekezwa hapa nchini kutoka nchi wanachama na nafasi za ajira zilizopatikana kutokana na uwekezaji huo ni watu 605. Kiambatisho Namba 2 kinabainisha mwenendo wa uwekezaji hapa nchini kutoka nchi wanachama kuanzia 2008 hadi 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha: Kwa mujibu wa Itifaki ya Umoja wa Forodha, nchi wanachama zimekubaliana kuondoleana vikwazo visivyo vya kiforodha ikiwa ni hatua ya kukuza biashara miongoni mwao. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2014 jumla ya vikwazo visivyo vya kiforodha 16 kati ya 33 vilivyokuwa vimesalia viliondolewa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kati ya vikwazo hivyo 11 vilikuwa vinaihusu Tanzania ambavyo ni pamoja na msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam, kulipia mara mbili gharama za kutoa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, usumbufu kwa wafanyabiashara wa Tanzania na Maofisa Uhamiaji wa Kenya katika mpaka wa Namanga, zuio la Uganda kwa net(vyandarua) vya kuzuia mbu vinavyozalishwa na kiwanda cha *A to Z* Arusha na zuio la bidhaa za bia kutoka Burundi kuingia Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza kasi ya uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha na kupunguza gharama za kufanya biashara hapa nchini, Tanzania imeweka mikakati kabambe ya kupunguza vituo vya ukaguzi na vizuizi vya Polisi. Katika mkakati huo vituo vya ukaguzi vitapunguzwa kutoka 15 vya sasa hadi kufikia vituo 3 kati ya Dar es Salaam na Rusumo katika Ukanda wa Kati. Vituo hivyo ni Vigwaza – Pwani, Manyoni – Singida na Nyakanazi –

Kagera. Katika vituo hivi shughuli zote za ukaguzi zikiwemo za upimaji wa mizigo, forodha, Polisi na wadau wengine wa forodha zitafanyika katika eneo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Pamoja la Afrika Mashariki: Katika kipindi cha mwaka huu tunaoumaliza 2013/2014, Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki wa ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki na tulizindua Taarifa ya Hali ya Utekelezaji wa Soko la Pamoja miongoni mwa nchi wanachama (*East African Common Market Scorecard)* kwa mara ya kwanza tangu kuanza kwake mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo imebainisha hatua iliyofikiwa na nchi wanachama katika kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa katika Itifaki ya Soko la Pamoja katika maeneo ya Soko Huru la Mitaji, Soko Huru la Biashara ya Huduma na Soko Huru la Bidhaa. Kwa mujibu wa Taarifa hiyo, nchi zote za Jumuiya hazijatekeleza makubaliano kwa kiwango kilichotarajiwa. Sababu kubwa ya kushindwa kutekeleza matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja ni kasi ndogo ya marekebisho ya sheria za ndani katika kila nchi ili kuruhusu utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wetu sheria husika zimebainishwa nazo ni 14. Wizara za kisekta zimetakiwa kuhakikisha mabadiliko ya sheria hizo yanafanyika ndani ya miaka 2 ijayo.

Umoja wa Fedha: Katika kipindi cha mwaka 2013/2014 nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikamilisha majadiliano ya uanzishwaji wa Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki ambapo, Itifaki ya kuanzisha Umoja huo iliidhinishwa na kutiwa saini na wakuu wa nchi mjini Kampala tarehe 30 Novemba, mwaka jana. Nchi wanachama zinaendelea na taratibu za ndani za kuridhia Itifaki hiyo.

Nchi wanachama pia, zimekubaliana kuwa na utekelezaji wa mpito wa miaka 10, ili kukamilisha masuala ya msingi kabla ya kuwa na Sarafu moja ya Afrika Mashariki mnamo 2023. Masuala ya msingi ya kutekelezwa ili kufanikisha lengo hili ni pamoja na kutekeleza kikamilifu hatua za awali za mtangamano wa Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja. Kufikia vigezo vya muunganiko wa uchumi mpana *(Macro Economic Convegence Criteria)* na kuanzisha Taasisi muhimu za kusimamia utekelezaji wa Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki, ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Fedha ya Afrika Mashariki, Taasisi ya Takwimu ya Afrika Mashariki na Kamisheni ya Huduma za Fedha ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vilivyokubaliwa vya muunganiko wa uchumi mpana kupima utayari wa nchi wanachama kujiunga na umoja wa fedha ni kama ifuatavyo:- Kiwango cha juu cha mfumuko wa bei kisichozidi 8%, kiwango cha juu cha nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada kisichozidi 3% ya pato la Taifa, kiwango cha juu cha deni la Taifa kisichozidi 50% ya pato la Taifa na akiba ya fedha za kigeni ya kutosheleza mahitaji ya nchi kwa muda usiopungua miezi minne na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirikisho la Kisiasa: Katika kipindi hiki nchi wananchama ziliendelea na majadiliano kuhusu uanzishwaji wa Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Nchi wanachama zimekubaliana kuanza maandalizi ya Rasimu ya Katiba ya Shirikisho ikiwa ni pamoja na kuainisha masuala ya msingi ya kutekelezwa kabla ya kukamilisha Rasimu ya Katiba hiyo. Hatua hii ni kufuatia nchi wanachama kukamilisha mashauriano ya ndani kuhusiana na Rasimu ya Modeli ya Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano na Kanda nyingine za Kiuchumi: Kwanza *COMESA – EAC – SADC*. Wizara imeendelea kuratibu, kushiriki na kuongoza majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu wa *COMESA – EAC – SADC*. Katika kipindi hiki Nchi za Jumuiya ya Afrika

Mashariki zimekamilisha maandalizi ya orodha ya viwango vitakavyotumika kupunguza ushuru kwa nchi za *SADC* na *COMESA (EAC Tariff Offers)*. Aidha, imekubalika Tanzania ifungue masoko kwa bidhaa kutoka nchi za *COMESA*, nchi za Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda pia zifungue masoko kwa bidhaa kutoka nchi za *SADC* na Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujumla zifungue masoko yake kwa nchi ambazo hazitekelezi makubaliano yoyote ya eneo huru la *SADC - COMESA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ubia wa kiuchumi kati ya Jumuiya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya. Kuhusu Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya, mwaka huu tunaoumaliza majadiliano yalikamilika katika maeneo yafuatayo:- Sheria ya Uasilia wa Bidhaa *(Original Goods),* Muundo wa Kitaasisi na Utatuzi wa Migogoro *(Conflict Resolution*) katika maeneo yanayohusiana na upeo wa kazi za Kamati ya Kushughulikia Migogoro.

Maeneo mengine ni utatuzi wa migogoro ya kifedha kwa ajili ya Maendeleo, hatua za mpito wakati shauri la msingi likiendelea na ulipaji wa fedha kwa madhara au hasara zitakazojitokeza wakati wa kuchukua hatua za ushirikiano kwa upande mmoja wa mkataba kuzuia bidhaa za upande mwingine. Mkataba wa Ubia wa Biashara na Uwekezaji baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya awali ya Mkataba wa Ubia wa Biashara na Uwekezaji baina yetu na Marekani. Majadiliano haya yanajumuisha Mkataba wa Uwekezaji, Uwezeshaji wa Biashara, Kujenga Uwezo wa Kufanya Biashara na Mdahalo wa Biashara *(Commercial Dialogue)* baina ya wafanyabiashara kutoka katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani zimeweka saini Hati ya Utashi *(Letter of Intent*) ya kuwa na mfumo wa Mdahalo wa pamoja na kukubaliana hadidu za rejea zitakazoongoza mdahalo huo wa Biashara. Mdahalo huo utatoa fursa kwa sekta binafsi kutoka katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani kuibua fursa na changamoto zilizopo kwa pande zote mbili katika masuala ya biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano katika sekta ya uzalishaji: Katika mwaka wa fedha huu wa 2013/2014 nchi wanachama zilisaini Itifaki ya Afya ya Wanyama na Mimea ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa Mpangokazi wa Kilimo na Usalama wa Chakula. Itifaki hii inalenga kukuza biashara ya chakula na bidhaa za kilimo ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuongeza ushirikiano, uratibu na uelewa wa pamoja kwenye masuala ya afya ya wanyama na mimea, kuimarisha matumizi ya kisayansi katika masuala ya Afya za wanyama na Mimea. Aidha, nchi Wanachama zimeandaa Rasimu ya Itifaki ya Utalii na Wanyamapori itakayoimarisha ushirikiano baina ya nchi zetu katika kuendeleza sekta ya utalii na uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori katika Jumuiya yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha maendeleo ya viwanda vya kimkakati katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi wanachama zimekamilisha katika mwaka huu wa fedha maandalizi ya mpango kazi wa utekelezaji wa sera na mkakati wa maendeleo ya viwanda. Aidha, Wizara iliratibu maandalizi ya rasimu ya mpango wa ufugaji wa samaki katika Jumuiya ambao utaweka mazingira bora ya ufugaji wa samaki katika nchi wanachama kwa kuboresha na kuendeleza taasisi za mafunzo ya ufugaji wa samaki na kuanzisha taasisi ya fedha ili kuwawezesha wafugaji wa Samaki kifedha na hivyo kuinua wafugaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendelezaji wa Miundombinu ya Kiuchumi: Katika kipindi hiki rasimu ya mwisho ya taarifa ya usanifu wa kina wa mradi wa ujenzi wa Barabara ya Malindi – Lungalunga/Tanga – Bagamoyo iliwasilishwa na mshauri mwelekezi katika Kamati ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Mradi. Kutokana na upungufu uliobainishwa katika taarifa ya mtaalam mshauri, Kamati imeelekeza kufanyike usanifu sahihi wa urefu wa daraja la Mto Wami ikizingatia kuchukua tahadhari za mafuriko kwenye eneo hilo. Aidha, hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa barabara zinazounganisha Tanzania na nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ni kama inavyoonekana katika kiambatisho Namba 3. Kiambatisho Namba 4 kinaonesha Mtandao wa Barabara wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uendelezaji wa barabara ya Arusha – Holili – Taveta – Voi katika mwaka 2013/2014, mkataba wa mkopo wa ujenzi wa barabara hiyo baina ya Jamhuri ya Muungano na Benki ya Maendeleo ya Afrika ulisainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vituo vya kutoa huduma kwa pamoja mpakani: Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 ujenzi wa vituo vya utoaji huduma kwa pamoja vya Holili na Silali katika mpaka wa Tanzania na Kenya na Kituo cha Mtukula kwenye Mpaka wa Tanzania na Uganda ulikamilika. Kwa upande wa kituo cha Hololo katika mpaka wa Tanzania na Kenya ujenzi umefikia asilimia tisini. Aidha, katika kituo cha Kabanga kwenye mpaka wa Tanzania na Burundi ujenzi umeanza na kituo cha Rusumo katika mpaka wa Tanzania na Rwanda ujenzi umefikia asilimia takribani 80. Matarajio ni kufanyika uzinduzi wa vituo vyote vitano ifikapo mwezi Novemba mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa reli: Jumuiya ya Afrika Mashariki inafanya utafiti wa kuimarisha sekta ya reli ambao pamoja na mambo mengine, utatoa mapendekezo ya ukarabati wa reli zilizopo, kuanzisha njia mpya za reli na mapendekezo ya vyanzo vya rasilimali fedha kwa kuzingatia maagizo ya Wakuu wa Nchi Wanachama. Vilevile, utafiti huu utatoa mapendekezo ya mfumo wa ushirikiano katika sekta ya reli kwa Nchi Wanachama ikiwa ni pamoja na kuhusisha sekta binafsi *(PPP)*, washirika wa maendeleo na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka huu wa fedha upembuzi wa kina kuhusu ujenzi wa reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali na Keza – Gitega – Musongati inayounganisha nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi, kwa kiwango cha *standard gauge* ulikamilika. Aidha, tathmini ya kumpata mshauri wa kuunadi mradi imekamilika na kinachosubiriwa sasa ni ridhaa *(No objection)* ya Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kumtangaza mshauri aliyeshinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Jumuiya wa Uendelezaji wa Sekta ya Reli, Serikali za Tanzania na Burundi zimesaini hati ya makubaliano ya ujenzi wa reli yenye urefu wa kilomita 200 inayounganisha Uvinza Tanzania na Musongati Burundi. Hatua inayofuata ni upembuzi na usanifu wa mradi na reli hii itawezesha nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kutumia kwa urahisi zaidi Bandari ya Dares Salaam. Kiambatisho Namba 5 kinabainisha Mtandao wa Reli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya usafiri wa anga: Katika kipindi hiki Nchi Wanachama zilisaini Makubaliano ya Utekelezaji wa Mkataba wa Utafutaji na Uokoaji wa Afrika Mashariki *(Search and Rescue)*. Ili kuhakikisha kunakuwepo kwa usalama wa usafiri wa anga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Nishati: Nchi wanachama zimekubaliana kuanzisha Kituo cha Nishati jadidifu ili kuwezesha upatikanaji wa nishati endelevu kufikia mwaka 2030.

Tanzania imeonyesha kusudio la kutaka kuwa mwenyeji wa Kituo hiki. Aidha Nchi za Tanzania na Uganda zimeendelea na majadiliano ya Mkataba wa Pande Mbili wa Mradi wa Kufua Umeme wa Murongo/Kikagati utakaozalisha megawati 16 pale mpakani. Lengo la majadiliano haya ni kuwezesha mradi kuwa na sura ya ubia kwa kujenga mtambo wa kufua umeme *(power plant)* eneo la Kikagati Uganda na mtambo wa kuongeza nguvu na kusafirisha umeme *(power station)* katika eneo la Murongo upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mawasiliano: Katika kuimarisha ushirikiano katika sekta ya mawasiliano, mwaka 2013/2014 nchi wanachama zilisaini Itifaki ya Ushirikiano katika Mitandao ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ambayo itawezesha upatikanaji wa taarifa sahihi na huduma za teknolojia ya mawasiliano kwa gharama nafuu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa mwenyekiti, Sekta ya Huduma za Jamii, Afya: Katika mwaka huu nchi wanachama zilianza majadiliano ya uwianishaji wa sera, sheria na taratibu za usajili wa madawa ya msingi kwa binadamu kwa kuzingatia viwango vya ubora katika nchi wanachama kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa dawa kwa urahisi na kwa gharama nafuu. Katika kipindi hiki miongozo uwiainishaji iliyoidhinishwa na nchi wanachama ni tathmini na usajili wa dawa, utengenezaji wa dawa kwa kuzingatia taratibu za afya, mfumo wa usimamizi wa ubora na mfumo wa utoaji taarifa za dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wanachama zimeidhinisha asasi za elimu zenye ubora uliobobea *(Centres of Excellence)* katika kutoa mafunzo yatakayowezesha Jumuiya kuwa na wataalam wa afya waliobobea katika nyanja tofauti za sayansi za afya na tiba, dawa, uhandisi wa kibayolojia na utafiti. Kulingana na mgawanyo huo, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi ya Tiba-Muhimbili kimeteuliwa na Jumuiya kuwa ni asasi ya elimu yenye ubora uliobobea ya magonjwa ya Moyo *(East African Community Regional Heart Institute)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu: Ili kuwawezesha Watanzania na Wanaafrika Mashariki kuwa na kiwango cha elimu kinachoshabihiana na hivyo kuwa na sifa na viwango sawa vya elimu kama ilivyoainishwa katika Itifaki ya Soko la Pamoja ya Jumuiya, nchi wanachama zimeendelea katika mwaka huu na majadiliano kuhusu uwianishaji wa mifumo ya elimu na mitaala katika jumuiya. Katika kipindi hiki nchi wanachama ziliidhinisha mikakati ya uwiainishaji wa mitaala katika maeneo ya maeneo ya Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Mafunzo ya Ualimu, Mafunzo ya Makundi Maalumu, Mafunzo ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi pia Mafunzo Nje ya Mfumo Rasmi na Elimu ya Watu Wazima. Zoezi la uwianishaji litafanyika hadi mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya walizitambua rasmi taasisi za elimu zenye ubora uliobobea za sekta ya elimu katika Jumuiya. Kwa upande wa Tanzania, asasi zilizotambuliwa ni zifuatazo:- Chuo cha Ubaharia cha Dar es Salaam, Chuo cha Wanyamapori Mweka, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Moshi. Natoa wito kwa Asasi hizo kuendelea kujiimarisha ili ziweze kuhudumia wananchi wote wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashindano ya Insha ya Jumuiya: Kama ilivyo utaratibu mwaka 2013/2014 kulifanyika shindano la uandishi wa insha la Jumuiya ya Afrika Mashariki linaloshirikisha wanafunzi wa shule za sekondari katika nchi wanachama. Washindi wa Shindano la Uandishi wa Insha mwaka 2013 walipewa tuzo na Wakuu wa Nchi Wanachama kule Kampala katika Mkutano wao wa 15 tarehe 30 Novemba, mwaka jana. Mshindi wa kwanza ni kijana Mtanzania Peter Robert kutoka Shule ya Sekondari Tushikamane iliyopo Mkoa wa Morogoro. Wale wanaosema elimu inashuka inashuka ee haya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, shindano la mwaka 2014 litakuwa na mada isemayo "*Ni jinsi gani mwingiliano wa Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki utakavyoathiri maisha yao ndani ya Jumuiya*". Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na walimu wote wa sekondari kuendelea kuhamasisha wanafunzi wetu kujitokeza kwa wingi kushiriki katika mashindano haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki: Zanzibar ndiyo Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamisheni ya Kiswahili itaanza utekelezaji wa majukumu yake katika mwaka mpya wa fedha mwaka 2014/2015 na mwaka huu tumeendelea kuratibu na kushiriki kukamilisha majadiliano ya Mkataba wa Makao Makuu *(Headquarter's Agreement)* na kamisheni hiyo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sekretarieti ya Jumuiya. Bajeti ya Tume hiyo kwa kuanzia kwa mwaka 2014 ni dola za Kimarekani laki saba, takribani shilingi bilioni moja na ushee hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Jumuiya ya Hifadhi ya Mazingira: Utekelezaji wa miradi ya Jumuiya ya uhifadhi wa ikolojia ya Ziwa Victoria uliendelea mwaka 2013/2014. Miradi hiyo ni mradi wa hifadhi ya mazingira katika ziwa Victoria awamu ya pili, *program* ya hifadhi ya mazingira kwa kuboresha sera, mabadiliko ya tabia nchi, utafiti na maendeleo ya kiuchumi na mradi wa Jamii wa kuboresha huduma ya maji safi na usafi wa mazingira. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hii ni kama inavyoonekana katika aya ya 75 hadi 78 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama: Katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika zoezi la kufanya mapitio ya Mkakati wa Kikanda wa Amani na Usalama kwa lengo la kutathmini utekelezaji wake ili uendane na mahitaji ya sasa. Katika mapitio hayo maeneo mapya sita yamependekezwa kuongezwa ambayo ni haya:- Uharamia, Ugaidi, Utakatishaji wa Fedha Haramu, Uhalifu wa Kimtandao, Uhalifu wa Mazingira na Mauaji ya Kimbari. Zoezi hili linatarajiwa kukamilika katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano Katika Masuala ya Kipolisi: Katika kipindi hiki nchi wanachama zimeendelea na majadiliano ya mfumo wa kisheria wa uendeshaji wa Kituo cha Kanda cha Rufaa cha Mahabara ya utambuzi wa vielelezo *(Regional Forensic Referral Centre)* ambacho mwenyeji wake ni Jamhuri ya Uganda. Kituo hiki kitakuwa chachu ya maendeleo ya vituo vya utambuzi wa vielelezo vilivyopo katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wanachama zinaendelea kushirikiana katika operesheni za pamoja za mara kwa mara kwa lengo la kukabiliana na uhalifu katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na wizi wa magari, mifugo na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano katika Siasa: Katika kipindi hiki nchi wanachama zimeendelea na majadiliano ya uundwaji wa itifaki za kinga na hadhi ya kidiplomasia, kuzuia na kupambana na rushwa na kuimarisha utawala bora ambapo rasimu za itifaki hizi zimewasilishwa katika Baraza la Mawaziri la kisekta la Sheria na Mahakama kwa ajili ya kupata maoni ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kupandisha Hadhi Pasi ya Kusafiria ya Afrika Mashariki: Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba nchi wanachama zimeendelea na majadiliano kuhusu kuipandisha hadhi hati ya kusafiria ya Afrika Mashariki kuwa ya Kimataifa. Inatarajiwa kuwa majadiliano hayo yatakamilika katika mwaka mpya wa fedha ili pasi hii ianze kutumika rasmi kwa wananchi wote wa Afrika Mashariki ifikapo Novemba, 2015 kama tulivyoagizwa na Wakuu wa nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi ya Jamhuri ya Sudan Kusini Kujiunga na Jumuiya: Katika kipindi hiki nchi wanachama ziliandaa mwongozo *(negotiation framework)* utakaotumika katika majadiliano kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jamhuri ya Sudan Kusini. Majadiliano kwa maombi ya Sudan wenyewe yataanza mwezi Septemba, 2014 kufuatia wao kuomba muda zaidi wa kufanya maandalizi ya ndani ikiwa pamoja na nchi hiyo kuelimisha wananchi wake juu ya umuhimu wa nchi hiyo kujiunga na Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie Bunge la Afrika Mashariki. Katika kipindi hiki Bunge la Afrika Mashariki lilijadili Miswada mbalimbali, kupitisha sheria za Jumuiya pamoja na maazimio. Sheria zilizopitishwa na Miswada inayoendelea kujadiliwa katika Bunge hilo pamoja na maazimio yaliyopitishwa ni kama inavyoonekana katika kiambatanisho Namba 6. Aidha, imebainika kuwepo kwa mgogoro kati ya Spika na Wabunge wa Wabunge la Afrika Mashariki uliosababisha hatua za kutaka kupitisha azimio la kumuondoa katika wadhifa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Afrika Mashariki: Katika mwaka huu tunaomaliza, Mahakama ya Afrika Mashariki ilizindua mfumo wa ki-*electronic* wa kusajili na kufuatilia mienendo ya mashauri *(electronic case management system)*. Aidha, Majaji wawili wa Mahakama hiyo kutoka Tanzania, Mheshimiwa Jaji Harold Nsekela, Rais wa Mahakama na Jaji wa Kitengo cha Rufaa na Mheshimiwa Jaji John Joseph Mkwawa, Jaji wa Kitengo cha Awali, watamaliza muda wao mwezi Juni, 2014. Wakuu wa nchi wanachama wamewateua Mheshimiwa Jaji Edward M. K. Rutakangwa, kuwa Jaji wa Kitengo cha Rufaa na Mheshimiwa Jaji Fakihi A. Jundu kuwa Jaji wa Kitengo cha Awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu kwa Umma: Katika mwaka 2013/2014 Wizara iliendelea kutekeleza mkakati wake wa mawasiliano wa miaka mitano, 2012 hadi 2016. Katika kipindi hiki elimu kwa umma ilitolewa kupitia vipindi vya TV na redio, mikutano na vyombo vya habari, maonesho na machapisho mbalimbali na ziara za mipakani mwa nchi wanachama. Maelezo ya kina kuhusu utoaji wa elimu kwa umma katika kipindi hiki ni kama inavyoonekana katika aya za 97 hadi 105 za hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto na Hatua zilizochukuliwa: Pamoja na mafaniko yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi hiki kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo Wizara inaendelea kukabiliana nazo. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa zimeainishwa katika sehemu 4 ya hotuba hii. Aidha, pamoja na kujitokeza kwa changamoto hizi Tanzania imepata mafaniko mbalimbali kupitia wanachama wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kipindi hiki. Jumuiya ya Afrika Mashariki inapanua soko la bidhaa za Tanzania kutoka Watanzania milioni 46 hadi wananchi milioni 142 wa Afrika Mashariki.

Aidha, kama nilivyobainisha awali, nchi yetu inapakana na nchi zote nne, wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tatu kati ya hizo zikiwa hazina bandari, hivyo ni dhahiri kuwa Tanzania ina fursa nyingi katika Jumuiya hii ambazo kama tukijipanga vizuri na kuendelea kutekeleza mikakati madhubuti ya pamoja zitachangia katika kasi ya ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015. Katika mwaka huu ujao Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:- Kuratibu maandilizi na kuongoza majadiliano katika mikutano ya kisheria ya Wakuu wa nchi wanachama, Baraza la Mawaziri la Jumuiya, Mabaraza ya Mawaziri ya kisekta ya Jumuiya, vikosi kazi na mikutano ya wataalam. Pia kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya na kwa kufupisha tu pamoja maeneo mengine yaliyomo katika hotuba ambayo ni maeneo 22, ambayo mtayaona katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha makubaliano ya itifaki, sera na mikakati inayoingiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki inazingatia maslahi ya Taifa na kunufaisha Watanzania kama inavyotarajiwa, Wizara kwa kushirikiana na sekta za umma, sekta binafsi na wadau wengine itaendelea kufanya tafiti na chambuzi za kina zitakazowezesha kuandaa misimamo ya Taifa ya kuongoza majadiliano katika jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia mkakati wa mawasiliano wa Wizara wa utoaji elimu kwa umma, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa zinazotokana na utekelezaji wa hatua mbalimbali za mtangamano katika nyanja za biashara, jamii, kiuchumi, kisiasa na taratibu za kuzitumia ili Watanzania wazichangamkie zaidi na kunufaika nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani: Kabla ya kuyatamka maombi ya fedha ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Sina budi kuwashukuru washirika mbalimbali wa maendeleo waliofadhili utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya maendeleo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Shukrani maalum ziwaendee Serikali za Uingereza, Finland, Norway, Marekani, Ujerumani, Ufaransa, Canada, Sweden, Ubelgiji, Denmark na Japan.

Aidha, natoa shukrani kwa mashirika na taasisi za kimataifa kama vile Shirika la Maendeleo la Ujerumani, Shirika la Misaada ya Maendeleo la Marekani, Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya, Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan, Benki ya Japan ya Maendeleo ya Kimataifa, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *Rockefeller Foundation*, Shirika la Kimataifa la Uhamiaji, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, *Investment Climate Facility for Africa*, Shirika la Maendeleo la Uingereza *(DFID), African Capacity Building Facility, The Association of European Parliamentarian with Africa (AWEPA) na Trade Mark East Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu y ake kwa mwaka 2014/2015, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya bilioni 23,785,246,000/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2014/2015. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 22,251,992,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 1,533,254,000/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi. Aidha, pamoja na hotuba hii nimejumuisha kama nilivyosema awali viambatisho mbalimbali, naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kuwa ni vielelezo vya hotuba hii.

Aidha, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.meac.go.tz.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe nukuu ya Kauli Mbiu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni "*One People, One Destiny*", maana yake sisi wana Afrika Mashariki ni wamoja na hatma yetu ni moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**
**KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

1. Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa

Kimataifa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

2. Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli. Kamati hii ilijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 tarehe 02 Mei, 2014, kutoa ushauri na kuyapitisha kwa kauli moja. Wizara yangu imezingatia ushauri wa Kamati katika maandalizi ya Hotuba hii ya Bajeti.

3. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Bunge lako Tukufu lilipata simanzi kubwa kufuatia vifo vya Wabunge wawili ambao ni Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa aliyekuwa Mbunge wa Kalenga na Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Saidi Ramadhani Bwanamdogo aliyekuwa Mbunge wa Chalinze. Nachukua fursa hii kuwapa pole familia za marehemu na wananchi wa majimbo hayo kwa kuwapoteza waliokuwa wawakilishi wao katika Bunge hili.

Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze.

4. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 kulitokea mashambulio ya kigaidi Nchini Kenya katika miji ya Nairobi na Mombasa yaliyosababisha vifo na majeruhi kwa majirani zetu. Nachukua fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya na Wananchi wote kwa matukio hayo ya kinyama.

5. Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 26 Aprili, 2014, Nchi yetu ilitimiza miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Mohamed Shein Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Watanzania wote kwa kuudumisha na kuulinda Muungano huu ambao ni wa kihistoria katika bara letu la Afrika.

6. Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa watumishi waandamizi walioteuliwa na kuhamishwa kutoka Wizara yangu ambao ni; Dkt. Stergomena L. Tax aliyeteuliwa kuwa Katibu Mkuu Mtendaji wa SADC, Bw. Uledi A. Mussa aliyeteuliwa kuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara, Bibi Rose M. Shelukindo aliyeteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Bw. Kagyabukama E. Kiliba aliyeteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI. Aidha, nampongeza Bw. Amantius C. Msole aliyeteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

7. Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kumpongeza na kumkaribisha Bibi Joyce K.G. Mapunjo aliyehamishiwa katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama Katibu Mkuu.

8. Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Abdulla J. Saadalla (Mb), Naibu Waziri; Bibi Joyce K.G. Mapunjo, Katibu Mkuu; Bw. Amantius C. Msole, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara na Vitengo; na watumishi wote katika Wizara yangu kwa

ushirikiano wanaonipa na moyo wao wa kujituma katika kutekeleza majukumu ya Wizara kikamilifu na hivyo kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu.

9. Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha Hotuba hii kwa umakini na kwa wakati.

10. Mheshimiwa Mwenyekiti, uandaaji wa Hotuba hii umezingatia maudhui ya Hotuba ya Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Bunge lako Tukufu. Hotuba hiyo imetoa mwelekeo na vipaumbele katika utekezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2014/2015.

## 2.0 MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

11. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Wizara ilipanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kuratibu, kushiriki na kuongoza Mikutano ya kisheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikiwemo Mikutano ya Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama, Mikutano ya Baraza la Mawaziri, Mabaraza ya Mawaziri ya Kisekta na kusimamia uendelezaji wa mtangamano unaozingatia maslahi ya Taifa na Jumuiya;

ii. Kuratibu, kushiriki, na kuongoza majadiliano ya uanzishwaji wa Himaya Moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

iii. Kuratibu, kushiriki na kuongoza majadiliano ya Itifaki ya uanzishwaji wa Umoja wa Fedha wa Jumuiya;

iv. Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano ya uanzishwaji wa Utatu wa SADC-EAC-COMESA, pamoja na majadiliano ya Ubia wa Kiuchumi baina ya Jumuiya na Umoja wa Ulaya (Economic Partnership Agreement - EPA);

v. Kukamilisha ukusanyaji wa maoni ya wadau na kukamilisha taarifa ya Mpangokazi wa kutekeleza Mapendekezo ya Kukabiliana na Hofu, Kero na Changamoto za Uanzishwaji wa Shirikisho la Kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki; na kuhusu Modeli ya Mfumo wa Shirikisho la Kisiasa;

vi. Kuratibu utekelezaji wa Mipango ya Jumuiya ya Uendelezaji Viwanda, Mifugo na Uvuvi na Mpango Kazi wa Uzalishaji wa Chakula katika Jumuiya;

vii. Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Programu na Miradi ya Jumuiya ikiwa ni pamoja na miradi ya uendelezaji wa miundombinu ya barabara, reli, bandari na nishati iliyoidhinishwa na Wakuu wa Nchi kama miradi ya kipaumbele katika Jumuiya;

viii. Kuratibu na kushiriki katika vikao vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge la Afrika Mashariki;

ix. Kutekeleza Mpango wa Mawasiliano wa Wizara wa utoaji Elimu kwa Umma kuhusu mtangamano wa Jumuiya na fursa zake;

x. Kuimarisha na kuendeleza Kituo cha Habari cha Wizara;

xi. Kufanya chambuzi, tafiti na tathmini mbalimbali kuhusu uendelezaji wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutekeleza mikakati ya uendelezaji mtangamano inayozingatia maslahi ya Taifa katika Jumuiya;

xii. Kukamilisha Mpango wa Ushirikiano baina ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wa kujumuisha masuala ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mipango ya TAMISEMI;

xiii. Kuimarisha uwezo wa Wizara kiutendaji.

12. Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 uliongozwa na vipaumbele vya Wizara vilivyobainishwa katika Mpango na Bajeti ya Wizara ambao uliandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/16); Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania Awamu ya Pili (MKUKUTA II), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar Awamu ya Pili (MKUZA II) na Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2013/14 – 2017/18. Aidha, Mpango huo ulizingatia pia Mkakati wa Nne wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 2011/2012 -2015/2016; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Maagizo ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya.

13. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliidhinishiwa Shilingi 20,470,107,000 ambapo kati ya fedha hizo Shilingi 19,000,000,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na Shilingi 1,470,107,000 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Kati ya fedha zilizoidhinishwa kwa Matumizi Mengineyo, Shilingi 12,452,253,440 zilikuwa ni Mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Shilingi 6,547,746,560 kwa ajili ya kutekeleza majukumu mengine ya Wizara.

Hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 Wizara ilikuwa imepokea Shilingi 17,554,343,368 kutoka Wizara ya Fedha; Shilingi 1,311,335,740 zikiwa ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 16,243,007,628 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kati ya kiasi cha fedha kilichopokelewa Shilingi 12,452,253,440 zilikuwa ni kwa ajili ya mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Shilingi 3,790,754,188 kwa ajili ya kutekeleza makujumu mengine ya Wizara.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO NA MPANGO YA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

### 3.1 SERA NA MIKAKATI

**Sera ya Takwimu za Hali ya Hewa (Meteorological Data Policy)**

14. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Nchi Wanachama zilisaini Sera ya Takwimu za Sekta ya Hali ya Hewa (Meteorological Data Policy). Sera hii itawezesha Nchi Wanachama kuwa na utaratibu unaofanana wa uhifadhi wa kumbukumbu na ubadilishanaji wa taarifa za Hali ya Hewa.

15. Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kutekeleza Sera hii, mwaka 2014/2015 Wizara itaratibu uandaaji wa vipaumbele katika Sera hii kulingana na vipaumbele vya Nchi Wanachama katika takwimu za Sekta ya Hali ya Hewa.

Sera ya Jumuiya ya Vijana na Sera ya Watu Wenye Mahitaji Maalum

16. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliratibu ukamilishaji wa Sera ya Vijana na Sera ya Watu wenye Mahitaji Maalum za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zilipitishwa na mkutano wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Masuala ya Jinsia, Vijana, Watoto, Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Lengo la Sera hizo ni kutoa mwongozo wa ushirikishwaji wa watu wenye mahitaji maalum na vijana katika masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

17. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Sera hizo, mwaka 2014/2015 Wizara itaratibu mchakato wa kubuni miradi itakayoibuliwa na Wananchi wenyewe katika kuziwezesha jamii zinazoishi mipakani hususan kina mama, vijana na wazee kunufaika na fursa za Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Sera ya Mifugo ya Afrika Mashariki**

18. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Wizara iliratibu maandalizi ya Sera ya Mifugo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi Wanachama kwa sasa zinaendelea na majadiliano ya Rasimu ya Sera hiyo. Baada ya majadiliano kukamilika Nchi Wanachama zitaandaa mikakati ya utekelezaji wa sera kulingana na mahitaji ya wafugaji wakubwa na wadogo. Sera hii itakapokamilika itatoa mwongozo wa uendelezaji wa sekta ya mifugo katika Nchi wanachama kwa kuzingatia matumizi bora ya ardhi na uhifadhi wa mazingira. Sera ya Usalama wa Chakula na Lishe ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

19. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Wizara iliratibu uandaaji wa Sera ya Usalama wa Chakula na Lishe ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sera hii itatoa mwongozo utakaowezesha kuongeza ubora na uhakika wa chakula katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuhamasisha uongezaji thamani kwa bidhaa za kilimo. Majadiliano kuhusu Rasimu ya Sera hii yanatarajiwa kukamilika katika mwaka 2014/2015.

**3.2 UTEKELEZAJI WA HATUA ZA MTANGAMANO**

20. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa hatua za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ifuatavyo:

**a. Umoja wa Forodha**

21. Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kipindi hiki, Nchi Wanachama zimekamilisha majadiliano ya Mfumo wa Himaya Moja ya Forodha na kuanza utekelezaji wake. Madhumuni ya kuwa na Himaya Moja ya Forodha ya Afrika Mashariki ni kuongeza kasi ya mzunguko wa bidhaa pamoja na kupunguza gharama za kufanya biashara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

22. Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo makuu yaliyoainishwa katika mfumo wa Himaya Moja ya Forodha ni:

i) Uthamini wa bidhaa na ukusanyaji wa kodi utafanyika katika nchi bidhaa hizo zinapokwenda;

ii) Baada ya kuthibitisha kuwa kodi imelipwa bidhaa zitaondolewa katika Nchi zilipoingilia kwa mara ya kwanza ndani ya Jumuiya na kusafirishwa kwenda nchi husika chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Forodha kwa kutumia Mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia usafirishaji wa bidhaa (Electronic Cargo Tracking System); na

iii) Bidhaa zitakazokuwa zimelipiwa kodi kwenye nchi husika zitasafirishwa kutoka nchi zilipoingilia kwenda katika nchi husika bila kuwekewa dhamana (bond) na hivyo kupunguza gharama kwa mfanyabiashara.

23. Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa ya mfumo wa Himaya Moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni pamoja na:

i) Kukuza biashara kwa kurahisisha mtiririko wa bidhaa kutoka nje ya Jumuiya kuingia katika Nchi za Jumuiya na bidhaa zinazosafirishwa miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki;

ii) Kukuza na kuvutia biashara na uwekezaji miongoni mwa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

iii) Kupunguza muda wa kusafirisha bidhaa kutoka nchi moja kwenda nyingine ndani ya Jumuiya kwa kupunguza vituo vya forodha vya ukaguzi vilivyopo ndani ya nchi.

24. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo huu wa Himaya Moja ya Forodha utaongeza ufanisi wa bandari zetu na kuvutia wafanyabiashara kutoka Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi nyingine kama Jamhuri y Kidemokrasia ya Kongo, Malawi na Zambia kuendelea kuzitumia bandari zetu, na hivyo kuongeza pato la taifa linalotokana na mapato ya bandari na usafirishaji.

25. Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2014 jumla ya vikwazo Visivyo vya Kiforodha 16 kati ya 33 vilivyokuwa vimesalia viliondolewa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kati ya vikwazo hivyo 11 vilikuwa vinaihusu Tanzania ambavyo ni pamoja na msongamano katika bandari ya Dare-es-Salaam, kulipia mara mbili gharama za kutoa mzigo katika bandari ya Dar-es-Salaam, usumbufu kwa wafanyabiashara wa Tanzania na Maofisa uhamiaji wa Kenya katika mpaka wa Namanga, zuio la Uganda kwa neti za kuzuia mbu zinazozalishwa na kiwanda cha A TO Z Arusha na zuio la bidhaa za bia kutoka Burundi kuja Tanzania.

26. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ripoti ya utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya, ambao pamoja na mambo mengine uliangalia hali ya uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha, ilibainika kuwa Tanzania inaongoza katika kuondoa Vikwazo Visivyo Vya Kiforodha miongoni mwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

27. Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuongeza kasi ya uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha na kupunguza gharama za kufanya biashara, Tanzania imeweka mkakati kabambe wa kupunguza vituo vya ukaguzi na vizuizi vya polisi.

Katika Mkakati huo vituo vya ukaguzi vitapungua kutoka 15 vya sasa hadi kufikia vituo vitatu kati ya Dar es Salaam na Rusumo katika ukanda wa kati. Vituo hivyo ni Vigwaza, Manyoni na Nyakanazi. Katika vituo hivi shughuli zote za ukaguzi zikiwemo za upimaji wa mizigo (mizani), forodha, polisi na wadau wengine wa forodha zitafanyika katika eneo moja.

28. Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama zimeandaa rasimu ya Sheria ya Jumuiya ya uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha. Rasimu hiyo imewasilishwa katika Baraza la Kisekta la Mawaziri wa masuala ya Sheria na Mahakama kwa ajili ya kupata ushauri wa kisheria. Sheria hii itaweka mwongozo wa uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha katika Jumuiya.

29. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na biashara ya bidhaa bandia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi Wanachama zimeandaa Rasimu ya Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kuzuia Biashara ya Bidhaa Bandia katika Nchi Wanachama. Rasimu hiyo imewasilishwa katika Baraza la Kisekta la Mawaziri wa masuala ya Sheria na Mahakama kwa ushauri wa kisheria. Sheria hii itasaidia kuzuia wimbi la bidhaa bandia kutoka nje kuingia ndani ya Jumuiya.

Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa kati ya Tanzania na Nchi Wanachama wa Jumuiya

30. Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013/2014, biashara kati ya Tanzania na Nchi Wanachama iliendelea kuimarika. Thamani ya bidhaa za Tanzania zilizouzwa katika Nchi Wanachama iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 409 mwaka 2011 na kufikia kufikia Dola za Marekani milioni 613.30 mwaka 2012. Aidha, kwa mujibu wa takwimu za awali za mwaka 2013 thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania katika Nchi Wanachama ilikuwa ni Dola za Marekani million 1,120.1 ikiwa ni ongezeko la asilimia 82. Bidhaa zilizouzwa zaidi ni mashine, mbolea, vifaa vya umeme, vifaa vya boti na meli, nafaka, bidhaa za mafuta na vimiminika, karatasi na bidhaa za nguo. Hii inaashiria kuendelea kuimarika kwa sekta ya viwanda nchini na wafanyabiashara wa Tanzania kuendelea kuchangamkia fursa zitokanazo na Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki.

31. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa manunuzi ya bidhaa toka Nchi Wanachama, Tanzania ilinunua bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 678.6 mwaka 2012 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 378.1 za mwaka 2011. Aidha, kwa mujibu wa takwimu za awali za mwaka 2013 thamani ya manunuzi ya bidhaa toka Nchi Wanachama ilikuwa ni Dola za Marekani milioni 410.2 ikiwa ni punguzo la asilimia 39.5. Bidhaa zilizonunuliwa kwa wingi zilikuwa ni vipuri vya magari, vifaa vya umeme na spea zake, nafaka, mafuta ya kupikia, sabuni na vifungashio.

32. Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa thamani ya mauzo na manunuzi ya Tanzania katika Nchi Wanachama pamoja na urari wa biashara kwa kipindi cha mwaka 2008 – 2013 ni kama inavyoonekana katika Grafu Na.1 na Kiambatisho Na. 1.

Grafu Na. 1: Mwenendo wa Biashara Kati ya Tanzania na Nchi Wanachama 2008 – 2013

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Uwekezaji**

33. Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki umeendelea kuchangia katika jitihada za Serikali za kuvutia na kukuza uwekezaji hapa Nchini. Katika kipindi hiki jumla ya miradi saba (7) yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 9.11 iliwekezwa hapa Nchini kutoka Nchi Wanachama. Nafasi za ajira zilizozalishwa kutokana na uwekezaji huo ni 605. Kiambatisho Na. 2 kinabainisha mwenendo wa uwekezaji hapa Nchini kutoka Nchi Wanachama kwa kipindi cha mwaka 2008 – 2013.

**b. Soko la Pamoja la Afrika Mashariki**

34. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hiki Jumuiya ya Afrika Mashariki ilizindua Ripoti ya Hali ya Utekelezaji wa Soko la Pamoja miongoni mwa Nchi Wanachama (EAC Common Market Scorecard) tangu kuanza kwake mwaka 2010.

35. Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo inabainisha hatua iliyofikiwa na Nchi Wanachama katika kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa katika Itifaki ya Soko la Pamoja katika maeneo ya Soko Huru la Mitaji, Soko Huru la Biashara ya Huduma na Soko Huru la Bidhaa. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Nchi zote za Jumuiya hazijatekeleza makubaliano kwa kiwango kilichotarajiwa. Sababu kubwa ya kushindwa kutekeleza matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja ni kasi ndogo ya marekebisho ya sheria za ndani ili kuruhusu

utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa. Taarifa hii itasaidia kujipanga kuboresha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja na kuzifanyia kazi changamoto zilizoainishwa.

**c. Umoja wa Fedha**

36. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikamilisha majadiliano ya Uanzishwaji wa Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki ambapo Itifaki ya kuanzisha Umoja huo iliidhinishwa na kutiwa saini na Wakuu wa Nchi mwezi Novemba, 2013. Nchi Wanachama zinaendelea na taratibu za ndani za kuridhia Itifaki hiyo.

37. Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama zimekubaliana kuwa na utekelezaji wa mpito wa miaka kumi ili kukamilisha masuala ya msingi kabla ya kuwa na Sarafu Moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Masuala ya msingi ya kutekelezwa katika kipindi hicho ni pamoja na kutekeleza kikamilifu hatua za awali za mtangamano za Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja; kufikia vigezo vya muunganiko wa uchumi mpana (Macro - Economic Convergence Criteria) na kuanzisha Taasisi muhimu za kusimamia utekelezaji wa Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Fedha ya Afrika Mashariki, Taasisi ya Takwimu ya Afrika Mashariki na Kamisheni ya Huduma za Fedha ya Afrika Mashariki.

38. Mheshimiwa Mwenyekiti, makubalino yaliyofikiwa katika kutimiza vigezo vya muunganiko wa uchumi mpana vitakavyotumika kupima utayari wa Nchi Wanachama kujiunga na Umoja wa Fedha na kufuatilia mwenendo wa utekelezaji wake ni: kiwango cha juu cha mfumuko wa bei kisichozidi asilimia 8; kiwango cha juu cha nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada kisichozidi asilimia 3 ya pato la Taifa; kiwango cha juu cha deni la Taifa kisichozidi asilimia 50 ya pato la Taifa; na akiba ya fedha za kigeni ya kutosheleza mahitaji ya miezi minne na nusu.

39. Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama zitaanza utekelezaji wa mpangokazi ulioidhinishwa ili kufikia hatua ya kuwa na Sarafu Moja ya Jumuiya katika kipindi cha miaka kumi mara baada ya Itifaki kuridhiwa na Nchi zote na hivyo kupata nguvu ya kisheria.

**d. Shirikisho la Kisiasa**

40. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba yangu ya mwaka 2013/2014 nilitoa taarifa kuwa Nchi Wanachama zilitakiwa kutoa maoni kuhusu Rasimu ya Mpango Kazi na Modeli ya Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara iliwasilisha maoni ya Tanzania kuhusu suala hili katika Mkutano wa 28 wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika mwezi Novemba, 2013, Kampala, Uganda.

41. Mheshimiwa Mwenyekiti, Kufuatia Nchi Wanachama kukamilisha mashauriano ya ndani kuhusiana na Rasimu ya Modeli ya Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki iliyopendekezwa, Wakuu wa Nchi Wanachama wameliagiza Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanza mchakato wa maandalizi ya uandaaji wa Rasimu ya Katiba ya Shirikisho, ikiwa ni pamoja na kuainisha masuala ya msingi ya kutekelezwa kabla ya kukamilisha Rasimu ya Katiba hiyo.

42. Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala hayo ya msingi ni pamoja na kutoa mapendekezo ya Modeli ya Shirikisho, kufanya tathmini ya kina ya kiwango cha utekelezaji wa Itifaki za

Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja na Umoja wa Fedha na Sheria mbalimbali za Jumuiya. Taarifa ya utekelezaji wa maagizo haya inatarajiwa kuwasilishwa katika mkutano wa Kumi na Sita (16) wa Wakuu wa Nchi Wanachama unaotarajiwa kufanyika mwezi Novemba 2014.

"Watanzania wengi sana wanaunga mkono kuwepo kwa Shirikisho la Afrika Mashariki lakini wanataka jambo hilo lisifanywe haraka haraka. Wanataka lifanywe kwa umakini mkubwa na tuende hatua kwa hatua kama ilivyoainishwa katika Mkataba uliounda Jumuiya ya Afrika Mashariki". Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 7 Novemba, 2013.

## 3.3 **USHIRIKIANO NA KANDA NYINGINE ZA KIUCHUMI**

### a. Utatu wa COMESA- EAC-SADC

43. Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu, kushiriki na kuongoza majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA – EAC- SADC. Katika kipindi hiki Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekamilisha maandalizi ya orodha ya viwango vitakavyotumika kupunguza ushuru kwa nchi za SADC na COMESA (EAC Tariff Offers).

44. Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hatua ambazo nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimefikia katika ufunguzi wa masoko yake kwa nchi za SADC na COMESA, imekubalika kuwa Tanzania kufungua masoko kwa bidhaa kutoka Nchi za COMESA; Nchi za Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda kufungua masoko kwa bidhaa kutoka nchi za SADC; na Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kufungua masoko yake kwa nchi ambazo hazitekelezi makubaliano yoyote ya eneo huru la SADC na COMESA.

45. Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa majadiliano ya Utatu wa COMESA- EAC-SADC kutawawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kufanya biashara katika Nchi zote za COMESA, EAC na SADC zipatazo 26 bila vikwazo na hivyo kuongeza ukubwa wa soko la bidhaa zetu.

### b. Ubia wa Kiuchumi Kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya (EAC-EU- EPA)

46. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2013/14, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya. Katika kipindi hiki majadiliano yalikamilika katika maeneo yafuatayo: Sheria ya Uasilia wa Bidhaa; Muundo wa Kitaasisi; na Utatuzi wa Migogoro katika maeneo yanayohusiana na upeo wa kazi za Kamati ya kushughulikia migogoro.

Maeneo mengine ni Utatuzi wa Migogoro ya kifedha kwa ajili ya maendeleo; Hatua za Mpito wakati shauri la msingi likiendelea; na Ulipaji wa Fidia kwa madhara/hasara zitakazojitokeza kwa hatua zilizochukuliwa na upande mmoja wa mkataba kuzuia bidhaa za upande mwingine.

47. Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano yanaendelea katika maeneo ya Kodi na Ushuru kwa Mauzo ya Nje (Export Taxes); Ruzuku kwa wakulima; Ruzuku kwa mauzo ya nje kwa bidhaa za kilimo; na Mahusiano ya EPA na Mkataba wa Cotonuo katika vipengele vilivyo nje ya makubaliano ya Ubia wa Kiuchumi. Maeneo mengine ni utawala bora kwenye eneo la kodi; na madhara yatokanayo na Umoja wa Ulaya kuingia kwenye

Umoja wa Forodha na kanda nyingine. Masuala yote yenye manufaa kwa Tanzania na Nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujumla yatazingatiwa kwa lengo la kusaini Mkataba utakaokuwa na manufaa kwa pande zote.

**c. Mkataba wa Ubia wa Biashara na Uwekezaji Baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani**

48. Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya awali ya Mkataba wa Ubia wa Biashara na Uwekezaji baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani. Majadiliano haya yanajumuisha Mkataba wa Uwekezaji, Uwezeshaji wa Biashara, Kujenga Uwezo wa Kufanya Biashara na Mdahalo wa Biashara (Commercial Dialogue) baina ya wafanyabiashara kutoka katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani.

49. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani zimeweka saini Hati ya Utashi (Letter of Intent) ya kuwa na mfumo wa Mdahalo wa pamoja na kukubaliana Hadidu za Rejea zitakazoongoza mdahalo wa Biashara. Mdahalo huu utatoa fursa kwa sekta binafsi kutoka katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani kuibua fursa na changamoto zilizopo kwa pande zote mbili katika masuala ya Biashara na Uwekezaji.

50. Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakavyoona Majadiliano bado yapo katika hatua za awali. Wizara itaendelea kutoa taarifa ya maendeleo ya majadiliano kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na hatimaye katika Bunge lako tukufu.

**3.4 USHIRIKIANO KATIKA SEKTA ZA UZALISHAJI**

51. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 kazi zilizofanyika katika Sekta za Uzalishaji ni kama ifuatavyo:

(a) Nchi Wanachama zilisaini Itifaki ya Afya ya Wanyama na Mimea ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Sanitary and Phytosanitary Protocol) ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa Mpangokazi wa Kilimo na Usalama wa Chakula.

Itifaki hii inalenga kukuza biashara ya chakula na bidhaa za kilimo ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; kuongeza ushirikiano, uratibu na uelewa wa pamoja kwenye masuala ya afya ya wanyama na mimea; kuimarisha matumizi ya kisayansi katika masuala ya Afya za wanyama na Mimea. Taratibu za kuridhia Itifaki hii miongoni mwa Nchi Wanachama zinaendelea.

(b) Nchi Wanachama zimeandaa Rasimu ya Itifaki ya Utalii na Wanyamapori ya Jumuiya ya Afrika Mashariki itakayoimarisha ushirikiano baina ya Nchi hizi katika kuendeleza Sekta ya Utalii na kuhakikisha kunakuwepo na uhifadhi na matumizi endelevu ya raslimali za wanyamapori katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Rasimu hii inatarajiwa kukamilika katika mwaka 2014/2015.

(c) Mpangokazi wa utekelezaji wa Sera na Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikamilishwa. Mpangokazi huu unabainisha hatua za kuchukuliwa ili kuwezesha maendeleo ya Viwanda vya Kimkakati katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(d) Utafiti ulifanyika kuhusu kuongeza thamani katika bidhaa za kilimo, nishati na chuma; kubainisha fursa za uwekezaji katika Sekta hizo ili ziweze kutangazwa kwa ajili ya

uwekezaji; na kubainisha vikwazo vya Kisera na Kisheria vinavyotakiwa kuondolewa ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Sekta ya Viwanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(e) Wizara iliratibu maandalizi ya rasimu ya Mpango wa Ufugaji wa Samaki wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mpango huu unalenga kuweka mazingira bora ya ufugaji wa samaki katika Nchi Wanachama kwa kuboresha na kuendeleza taasisi za mafunzo ya ufugaji wa samaki na kuanzisha Taasisi ya fedha itakayokuwa inasaidia wafugaji wa Samaki kifedha na hivyo kuinua wafugaji wadogo

### 3.5 UENDELEZAJI WA MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI

52. Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Programu na Miradi ya Kitaifa iliyoainishwa katika Mipango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya uendelezaji wa Miundombinu ya Kiuchumi. Hatua zilizofikiwa katika uendelezaji wa programu na miradi hii ni kama ifuatavyo:

**(a). Mradi wa Barabara ya Malindi-Lungalunga/Tanga-Bagamoyo**

53. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Rasimu ya Mwisho ya taarifa ya Usanifu wa Kina wa mradi wa ujenzi wa Barabara ya Malindi-Lungalunga/Tanga-Bagamoyo iliwasilishwa na Mshauri Mwelekezi katika Kamati ya Usimamizi wa Utekelezaji wa mradi. Kutokana na upungufu uliobainishwa katika taarifa ya Mtaalam Mshauri, Kamati imeelekeza kufanyika kwa usanifu sahihi wa urefu wa daraja la mto Wami ikizingatia kuchukua tahadhari za mafuriko kwenye eneo hilo.

Aidha, hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa barabara zinazounganisha Tanzania na Nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 3. Aidha, Kiambatisho Na. 4 kinaonesha Mtandao wa Barabara wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**(b). Barabara ya Arusha – Holili – Taveta - Voi**

54. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 Mkataba wa mkopo wa ujenzi wa barabara ya Arusha-Holili-Taveta-Voi baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika ulisainiwa. Madhumuni ya mradi huu ni kuendeleza mtandao wa barabara kati ya Tanzania na Kenya ambazo ziko kwenye Mtandao wa barabara za Kikanda ili kunufaika na mtangamano kupitia uendelezaji wa utalii na mawasiliano ya wanajumuiya.

Aidha, barabara hii inaunganisha Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Kati kupitia Tanzania hadi Kenya kupitia mpaka wa Holili/Taveta. Barabara hii pia inaiunganisha Arusha na Kanda ya Kati kupitia Minjingu na Babati hadi Dodoma.

55. Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa upande wa Kaskazini, barabara hii inaunganishwa na barabara ya Arusha-Namanga-Athi River. Chini ya mradi huu kwa upande wa Tanzania utahusisha kazi zifuatazo:

(i) Ujenzi wa barabara ya kuzunguka jiji la Arusha (Arusha Bypass) – km 42.4;

(ii) Upanuzi (dualling ) wa sehemu ya Sakina-Usa River – km 22.3;
(iii) Ukarabati wa barabara ya Usa River-Holili – km 93.9; na

(iv) Ujenzi wa barabara ya Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro – km 5.8.

**(c). Uwianishaji wa Uzito wa Mizigo Kwenye Magari Katika Barabara za Jumuiya**

56. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/14 Nchi Wanachama za Jumuiya zimeandaa Rasimu ya Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Kudhibiti Uzito wa mizigo kwenye Magari *(Vehicle Load Control Act, 2013)* iliyopitishwa na Bunge la Afrika Mashariki mwezi Aprili, 2013.

Sheria ya Kudhibiti Uzito wa Magari pamoja na mambo mengine, inatoa mwongozo wa ukomo wa uzito wa mizigo kwenye magari baina ya Nchi Wanachama ambao ni Tani 56. Lengo la hatua hii ni kulinda barabara zetu dhidi ya uharibifu unaosababishwa na magari kubeba mizigo mizito kupita uwezo wa barabara.

**(d). Ujenzi wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani (OSBPs)**

57. Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2014 ujenzi wa vituo vya utoaji huduma kwa pamoja vya Holili na Sirari katika mpaka wa Tanzania na Kenya na kituo cha Mutukula kwenye mpaka wa Tanzania na Uganda ulikamilika. Kwa upande wa Kituo cha Horohoro katika mpaka wa Tanzania na Kenya, ujenzi wake umefikia asilimia 90%. Aidha, katika kituo cha Kabanga kwenye mpaka wa Tanzania na Burundi ujenzi umeanza na kituo cha Rusumo katika mpaka wa Tanzania na Rwanda ujenzi umefikia asilimia 79 hadi kufikia mwezi Machi, 2014. Matarajio ni kufanyika uzinduzi wa vituo vyote ifikapo mwezi Novemba, 2014.

**(e). Mtandao wa Reli**

58. Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki inafanya utafiti wa kuimarisha Sekta ya Reli ambao pamoja na mambo mengine, utatoa mapendekezo ya ukarabati wa Reli zilizopo, kuanzisha njia mpya za reli na mapendekezo ya vyanzo vya raslimali fedha kwa kuzingatia maagizo ya Wakuu wa Nchi Wanachama. Vilevile, utafiti huu utatoa mapendekezo ya mfumo wa ushirikiano katika Sekta ya Reli kwa Nchi Wanachama ikiwa ni pamoja na kuhusisha sekta binafsi (PPP), washirika wa maendeleo na wawekezaji.

59. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2013 – 2014, upembuzi wa kina kuhusu ujenzi wa reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali / Keza – Gitega – Musongati inayounganisha Nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi, kwa kiwango cha standard gauge ulikamilika. Aidha, tathmini ya kumpata Mshauri wa kuuza Mradi imekamilika na kinachosubiriwa sasa ni ridhaa (No objection) ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kumtangaza Mshauri aliyeshinda.

60. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Jumuiya wa Uendelezaji wa Sekta ya Reli, Serikali za Tanzania na Burundi zimesaini hati ya Makubaliano ya ujenzi wa reli yenye urefu wa kilomita 200 inayounganisha Uvinza na Musongati. Hatua inayofuata ni upembuzi na usanifu wa mradi. Reli hii itawezesha nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kutumia kwa urahisi bandari ya Dares Salaam. Kiambatisho Na. 5 kinabainisha Mtandao wa Reli wa Jumuiya ya Afrika Masharki.

**Sekta ya Usafiri wa Anga**

61. Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika maandalizi ya taratibu za matumizi ya Mfumo Rahisi wa Mawasiliano ya Anga unaotumia mfumo wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Satelaiti. Mfumo huu unatarajiwa kutumika katika viwanja vya ndege vya kimataifa na vya kitaifa katika Nchi Wanachama ili kurahisisha mawasiliano ya anga.

Vilevile, Nchi Wanachama zilisaini Makubaliano ya Utekelezaji wa Mkataba wa Utafutaji na Uokoaji wa Afrika Mashariki ili kuhakikisha kuwepo kwa usalama wa usafiri wa anga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Sekta ya Nishati**

62. Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kuratibu ushirikiano na Nchi Wanachama katika Sekta ya Nishati katika maeneo ya Nishati Jadidifu, Nishati ya Umeme na Nishati ya Mafuta na kukamilisha mambo yafuatayo:

**a. Uanzishwaji wa Mradi wa Kituo cha Nishati Jadidifu cha Afrika Mashariki**

63. Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama zimekubaliana kuanzisha Kituo cha Nishati jadidifu ili kuwezesha upatikanaji wa nishati endelevu kufikia mwaka 2030. Tanzania imeonyesha kusudio la kutaka kuwa mwenyeji wa Kituo hiki.

**b. Mradi wa Kufua Umeme wa Murongo/Kikagati**

64. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Nchi za Tanzania na Uganda zimeendelea na majadiliano ya Mkataba wa Pande Mbili wa Mradi wa Kufua Umeme wa Murongo/Kikagati utakaozalisha megawati 16. Makubaliano yamefikiwa katika maeneo yote isipokuwa katika Ibara ya 2 inayohusu maelezo ya Mradi. Katika Ibara hiyo Tanzania inapendekeza mtambo wa kufua umeme (power plant) ujengwe Kikagati upande wa Uganda na Mtambo wa kuongeza nguvu na kusafirisha umeme (power station) ujengwe Murongo upande wa Tanzania ili kuhakikisha mradi unakuwa na sura halisi ya ubia. Inatarajiwa kuwa majadiliano haya yatakamilika katika mwaka 2014/2015.

**Sekta ya Mawasiliano**

65. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Nchi Wanachama zilisaini Itifaki ya Ushirikiano katika Mitandao ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Lengo la Itifaki hii ni kuimarisha upatikanaji wa taarifa sahihi na huduma za teknologia ya mawasiliano kwa gharama nafuu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi Wanachama zinaendelea na hatua ya kuridhia Itifaki hii ili kuiwezesha ianze kutekelezwa.

**3.6 SEKTA ZA HUDUMA ZA JAMII**

**Sekta ya Afya**

66. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliratibu maandalizi ya miongozo ya uwianishaji wa sera, sheria na taratibu za usajili wa madawa ya msingi kwa binadamu kwa kuzingatia viwango vya ubora katika Nchi Wanachama. Lengo la uhuishaji huo ni kuboresha upatikanaji wa dawa kwa urahisi na gharama nafuu.

Katika kipindi hiki miongozo iliyoidhinishwa na Nchi Wanachama ni Tathmini na Usajili wa Madawa; Utengenezaji wa Madawa kwa Kuzingatia Taratibu za Afya; Mfumo wa Usimamizi wa Ubora; na Mfumo wa Utoaji Taarifa za Madawa.

67. Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeimarisha Mtandao wa Maabara za Afya katika Nchi Wanachama kwa ajili ya ugonjwa wa Kifua Kikuu na magonjwa mengine ya kuambukiza. Tanzania imepiga hatua kwa kuanza ujenzi wa maabara itakayoshugulika na magonjwa ya Kifua Kikuu na magonjwa mengine ya kuambukiza.

68. Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama zimeidhinisha asasi za elimu zenye ubora uliobobea (Centres of Excellence) katika kutoa mafunzo yatakayowezesha Jumuiya kuwa na wataalam wa afya waliobobea katika nyanja tofauti za Sayansi za Afya na Tiba, Madawa, Uhandisi wa Kibayolojia na Utafiti. Kulingana na mgawanyo huo Chuo Kikuu cha Tiba-Muhimbili kimeteuliwa kuwa asasi ya elimu yenye ubora uliobobea ya magonjwa ya Moyo ya Afrika Mashariki "East African Community Regional Heart Institute (EACHI).

**Sekta ya Elimu**

**(a). Kuwianisha Mifumo ya Elimu**

69. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliratibu na kushiriki katika kuwianisha Mifumo ya Elimu na Mitaala katika Jumuiya. Uwianishaji huo unalenga kuwawezesha Watanzania na Wanaafrika Mashariki kuwa na kiwango cha elimu kinachoshabihiana na hivyo kuwawezesha kuwa na sifa na viwango sawa vya elimu kama ilivyoainishwa katika Itifaki ya Soko la Pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

70. Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama ziliidhinisha Mikakati ya uwianishaji wa mitaala katika maeneo ya Elimu ya Awali; Elimu ya Msingi; Elimu ya Sekondari; Mafunzo ya Ualimu; Mafunzo ya Makundi Maalumu; Mafunzo ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi; na Mafunzo Nje ya Mfumo Rasmi na Elimu ya Watu Wazima. Zoezi la uwianishaji litafanyika mwaka 2014/15.

**(b). Asasi za Elimu Zenye Ubora uliobobea**

71. Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya katika Mkutano wao wa 15 uliofanyika mwezi Novemba, 2013, Kampala, Uganda walizitambua rasmi Taasisi za elimu zenye ubora uliobobea za Sekta ya Elimu katika Jumuiya. Kwa upande wa Tanzania, Asasi zilizotambuliwa ni Chuo cha Ubaharia cha Dar es Salaam; Chuo cha Wanyamapori Mweka; Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo; na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Moshi. Natoa wito kwa Asasi hizo kuendelea kujiimarisha ili ziweze kutumika na Nchi Wanachama.

**(c). Mashindano ya Insha ya Jumuiya**

72. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliratibu shindano la uandishi wa Insha la Jumuiya ya Afrika Mashariki linaloshirikisha wanafunzi wa shule za sekondari katika Nchi Wanachama. Lengo la mashindano haya ni kuwapa wanafunzi uelewa wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Washindi wa Shindano la Uandishi wa Insha mwaka 2013 walipewa tuzo na Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya katika Mkutano wao wa 15. Mshindi wa kwanza ni kijana Peter Robert kutoka Shule ya Sekondari Tushikamane, iliyopo mkoani Morogoro. Tunampongeza yeye binafsi na shule husika kwa ushindi huo.

73. Mheshimiwa Mwenyekiti, Shindano la mwaka 2014 litakuwa na mada isemayo "Ni jinsi gani mwingiliano wa Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki utakavyoathiri maisha yao ndani ya Jumuiya".

Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Walimu kuendelea kuhamasisha wanafunzi kujitokeza kwa wingi kushiriki katika mashindano haya.

**Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki**

74. Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar ni mwenyeji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamisheni ya Kiswahili itaanza utekelezaji wa majukumu yake mwaka 2014/2015.

Katika mwaka 2013/2014 Wizara iliratibu na kushiriki kukamilisha majadiliano ya Mkataba wa Makao Makuu (Headquarter's Agreement) ya Kamisheni hiyo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Miradi ya Jumuiya ya Hifadhi ya Mazingira**

**(a). Mradi wa Hifadhi ya Mazingira Katika Ziwa Victoria (LVEMP II)**

75. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/14, Wizara iliratibu utekelezaji wa Mradi wa Utunzaji wa Mazingira ya Bonde la Ziwa Victoria katika ngazi ya Kitaifa na Kikanda yenye lengo la kupunguza umaskini na uharibifu wa mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria. Katika kipindi hicho, mradi uliwezesha utekelezaji wa miradi midogo midogo 176 yenye thamani ya Dola za Marekani 4,504,813 katika mkoa wa Geita na Simiyu na katika Wilaya za Sengerema, Magu na Bariadi.

76. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu pia uliongeza upatikanaji wa wadudu wajulikanao kama Mbawa Kavu katika ukanda wa Ziwa Victoria eneo la Mwanza ili kukabiliana na tatizo la magugu maji. Hatua hii imewezesha kupungua kwa magugu maji kwa kiasi cha hekta 7.45 kutoka hekta 263.3 mwaka 2012 hadi kufikia hekta 255.85 mwaka 2013.

**(b). Programu ya Hifadhi ya Mazingira kwa Kuboresha Sera, Mabadiliko ya Tabia Nchi, Utafiti na Maendeleo ya Kiuchumi (PREPARED)**

77. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/14 Wilaya za Chato, Bunda na Itilima ziliteuliwa kuwa maeneo ya utekelezaji wa mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira ambao ni sehemu ya Programu hii. Mradi huu ambao ni wa miaka mitano (2012 – 2016) unalenga kuboresha mazingira, huduma ya maji, usafi wa mazingira na maendeleo ya

jamii. Katika mwaka 2014/2015 utekelezaji wa mradi utaanza katika maeneo yaliyoteuliwa.

**(c). Mradi wa Jamii wa Kuboresha Huduma ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (LVWATSAN)**

78. Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliratibu utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Awamu ya Pili (2010 -2015) ambao unatekelezwa katika miji ya Geita, Nansio na Sengerema.

Katika mwaka 2013/14, Serikali ya Tanzania ilisaini Hati ya Makubaliano na Serikali ya Kenya kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Maji katika mji wa Sirari, mkoani Mara kutokea Isebania, Kenya kutokana na upande wa Sirari kutokuwa na chanzo cha maji. Aidha, katika kipindi hiki, magari 5 ya kubebea taka ngumu, matrekta 8, pikipiki 8 na makasha ya kuhifadhia taka 104 yamenunuliwa kwa ajili ya miji midogo ya Geita, Nansio na Sengerema. Mwaka 2014/15 Wizara itaratibu na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mradi wa maji wa Sirari/Isebania.

**3.7 USHIRIKIANO KATIKA SIASA, ULINZI NA USALAMA**

**(a). Mkakati wa Kikanda wa Kusimamia Amani na U  Usalama**

79. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika zoezi la kufanya mapitio ya Mkakati wa Kikanda wa Amani na Usalama kwa lengo la kutathmini utekelezaji wake ili uendane na mahitaji ya sasa. Katika mapitio hayo maeneo mapya sita yamependekezwa kuongezwa ambayo ni pamoja na kukabiliana na: Uharamia; Ugaidi; Utakatishaji wa Fedha Haramu; Uhalifu wa Kimtandao; Uhalifu wa Mazingira; na Mauaji ya Kimbari. Zoezi hili linatarajiwa kukamilika katika mwaka 2014/2015.

**(b). Ushirikiano Katika Masuala ya Kipolisi**

80. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya mwaka 2013/2014 nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Nchi Wanachama zimeiteua Jamhuri ya Uganda kuwa mwenyeji wa Kituo cha Kikanda cha Rufaa cha Maabara ya Utambuzi wa Vielelezo (Regional Forensic Referral Centre). Katika kipindi hiki Nchi Wanachama zimeendelea na majadiliano ya mfumo wa kisheria wa uendeshaji wa Kituo hiki pamoja na mpango mkakati ambao pamoja na mengine utawezesha Kituo hiki kuwa chachu ya maendeleo ya vituo vya utambuzi wa vielelezo vilivyopo katika Nchi Wanachama.

81. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kuongeza weledi katika majeshi ya polisi ya nchi wanachama na pia kupunguza gharama za kuanzisha taasisi za mafunzo zenye majukumu na malengo yanayofanana, Nchi Mwanachama zimegawana maeneo ambayo taasisi zake zitahusika katika kutoa mafunzo kwa askari wa polisi kutoka katika majeshi ya polisi katika Jumuiya. Kwa upande wa nchi yetu maeneo yaliyotengwa ni mafunzo ya kudhibiti maandamano, fujo na vurugu; kozi za awali za kijeshi kwa upande wa polisi; na Polisi Majini. Naomba nitoe rai kwa taasisi zetu zilizoteuliwa kujiimarisha katika kutoa mafunzo haya ili tuvutie wanafunzi wengi toka nchi wanachama.

82. Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama wa Jumuiya zinaendelea kushirikiana katika operesheni za pamoja za mara kwa mara kwa lengo la kukabiliana na uhalifu katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na wizi wa magari, mifugo na biashara haramu ya usafirishaji wa Binadamu.

**(c). Mapambano Dhidi ya Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya**

83. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika vikao vya Jumuiya vya Wakuu wa Taasisi za kupambana na dawa haramu za kulevya. Pamoja na mambo mengine, lengo la vikao hivi ni kubadilishana taarifa, uzoefu na kujenga uelewa wa pamoja katika kudhibiti uhalifu huo kwa Nchi Wanachama.

Aidha, Nchi Wanachama zinaendelea na zoezi la kupitia sheria za Nchi zao kwa lengo la kuhuisha sheria hizo ili zitoe adhabu zinazoshabihiana katika Nchi Wanachama kwa makosa yanayohusu biashara haramu ya dawa za kulevya.

84. Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama zimekubaliana kila moja kuunda Kamati za kitaifa za kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya na kuandaa mkakati wa kuelimisha wananchi ili kuimarisha usalama na kuongeza uelewa miongoni mwao.

**(d). Mapambano Dhidi ya Uharamia**

85. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Nchi Wanachama zilikamilisha na kuidhinisha Mkakati wa Kikanda wa kupambana na uharamia katika Bahari ya Hindi ambao unahusisha pia Kanda za SADC, COMESA na IGAD. Majukumu ya utekelezaji wa Mkakati huu yamegawanywa kikanda ambapo Jumuiya ya Afrika Mashariki imepangiwa jukumu la kuhifadhi watuhumiwa wa uharamia watakaokamatwa, kuendesha mashtaka dhidi yao na kuwafunga watakaopatikana na hatia na kisha kuwasafirisha kurudi makwao mara baada ya kumaliza vifungo. Kwa msingi huo, Jumuiya ya kimataifa imetakiwa kusaidia Nchi Wanachama kujenga uwezo wa mahakama na vyombo vya sheria katika maeneo yahusuyo uharamia, kutunga au kurekebisha sheria ili ziendane na mazingira ya sasa.

86. Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa mkakati huu utaziwezesha Nchi Wanachama kukabiliana na tishio la uharamia katika Bahari ya Hindi na hivyo kupunguza gharama za kusafirisha mizigo kupitia bahari ya Hindi na vilevile kupunguza gharama za kufanya biashara katika Jumuiya. Ongezeko la gharama linatokana na makampuni ya bima kuongeza gharama za bima baada ya kuongezeka kwa vitendo vya uharamia katika Bahari ya Hindi. Mkakati huu pia umepitishwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Afrika kwa ajili kutumika katika Kanda ya Bahari ya Hindi.

**(e). Mapambano Dhidi ya Ugaidi**

87. Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za hivi karibuni kumejitokeza matukio ya mashambulizi ya kigaidi katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo yamesababisha pamoja na mambo mengine wananchi kupoteza maisha, vilema kwa wananchi wasio na hatia na uharibifu wa mali. Kutokana na hali hiyo Nchi Wanachama zimekubaliana kuimarisha mapambano dhidi ya ugaidi kwa kuandaa Mkakati wa Kupambana na ugaidi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Mkakati huu utaimarisha ushirikiano katika kubadilishana taarifa na mienendo ya magaidi na pia kufanya operesheni za pamoja pale itakapohitajika. Katika mwaka 2014/2015 Nchi Wanachama zinatarajia kukamilisha mpangokazi wa utekelezaji wa mkakati huo.

**(f). Mazoezi ya Pamoja ya Kijeshi**

88. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ushirikiano miongoni mwa majeshi ya Nchi Wanachama katika mwaka 2013/2014, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika zoezi la pamoja la Vituo vya kijeshi vya uongozaji wa operesheni lijulikanalo kama Command Post Excercise lililofanyika mwezi Oktoba, 2013 nchini, Burundi. Aidha, katika kipindi hiki Wizara iliratibu maandalizi ya zoezi la Kijeshi lijulikanalo kama 'Ushirikiano Imara 2014 - Field Training Exercise 2014 (FTX)' linalotarajiwa kufanyika nchini Burundi mwezi Oktoba, 2014. Zoezi hili linalenga kujenga na kuimarisha mfumo na uelewa wa pamoja wa utendaji katika operesheni za kurejesha amani, kukabiliana na maafa, kukabiliana na ugaidi, na kukabiliana na uharamia.

89. Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha hali ya urafiki, ushirikiano na kuaminiana miongoni mwa askari wa ngazi zote katika majeshi ya Nchi Wanachama, Jumuiya ya Afrika Mashariki huandaa wiki ya Michezo na Utamaduni ya majeshi ya Afrika Mashariki. Napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa katika mwaka 2014/2015 Tanzania itakuwa mwenyeji wa michezo hiyo ambayo imepangwa kufanyika Zanzibar. Wizara itaratibu ushiriki wa nchi katika maandalizi na kuleta ushiriki wenye tija.

**(g). Ushirikiano Katika Siasa**

90. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba yangu ya mwaka 2013/2014 nilielezea kuhusu Nchi Wanachama kuendelea na majadiliano katika kuunda Itifaki za Kinga na Hadhi ya Kidiplomasia; Kuzuia na Kupambana na Rushwa; na Utawala Bora. Katika kipindi hiki majadiliano kuhusu Itifaki hizi yaliendelea na rasimu za Itifaki zimewasilishwa katika Baraza la Mawaziri la Kisekta la Sheria na Mahakama kwa ajili ya kupata maoni ya kisheria.

**(h). Haki za Binadamu na Utawala Bora**

91. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliratibu majadiliano ya ukamilishaji wa Mkakati wa Pili wa Kikanda wa kulinda, kukuza na kutetea utekelezaji wa Haki za Binadamu miongoni mwa Nchi Wanachama. Mkakati huu unalenga kuimarisha utekelezaji wa haki za binadamu, kuwianisha sheria, sera na programu zinazohusiana na haki za binadamu na kuongeza ushirikiano kati ya Taasisi zinazosimamia haki za binadamu miongoni mwa Nchi Wanachama wa Jumuiya. Kuwepo kwa Mkakati huu pamoja na mambo mengine, kutawezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, hususan vipengele vya uhuru wa kutembea na uhuru wa kuwekeza vilivyomo katika Itifaki hiyo.

**(i). Uratibu wa Sera za Mambo ya Nje**

92. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliratibu na kushiriki majadiliano kuhusu mapendekezo ya Nchi Wanachama kuwa na msimamo wa pamoja katika baadhi ya masuala ya Sera za Nje. Wizara inaendelea kuratibu uibuaji wa maeneo yatakayowekewa msimamo wa pamoja kwa kushirikisha wadau.

**(j). Kupandisha Hadhi Pasi ya kusafiria ya Afrika Mashariki.**

93. Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kuratibu majadiliano kuhusu kuipandisha hadhi Hati ya Kusafiria ya Afrika Mashariki kuwa ya Kimataifa. Inatarajiwa kuwa majadiliano haya yatakamilika katika mwaka ujao wa fedha ili Pasi hii ianze kutumika rasmi kimataifa ifikapo Novemba, 2015 kama ilivyoagizwa na Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### 3.8 MAOMBI YA JAMHURI ZA SUDAN KUSINI KUJIUNGA NA JUMUIYA

94. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya mwaka 2013/2014, nililitaarifu Bunge lako kuhusu maombi ya Jamhuri ya Sudan Kusini kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hiki Nchi Wanachama ziliandaa Mwongozo (negotiation framework) utakaotumika katika majadiliano kati ya Jumuiya na Jamhuri ya Sudan Kusini. Mwongozo huo uliidhinishwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya mwezi Novemba, 2013. Pande zote mbili zimekwishaunda Vikosi Kazi vitakavyoshiriki katika majadiliano haya yanayotarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2014. Hii ni kufuatia Jamhuri ya Sudan Kusini kuomba muda zaidi wa kufanya maandalizi ya ndani ikiwa ni pamoja na kuelimisha wananchi wake juu ya umuhimu wa Nchi hiyo kujiunga na Jumuiya.

### 3.9 BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI

95. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 Bunge la Afrika Mashariki lilikutana mara tano ambapo lilijadili Miswada mbalimbali na kupitisha Sheria za Jumuiya pamoja na Maazimio. Sheria zilioopitishwa na Miswada inayoendelea kujadiliwa katika Bunge hilo pamoja na Maazimio yaliyopitishwa ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 6. Katika kipindi hiki Bunge la Afrika Mashariki lilipitisha azimio la kufanya mikutano ya Bunge hilo kwa mzunguko katika Nchi Wanachama kwa utaratibu wa Mikutano miwili kufanyika Arusha (Mkutano wa Bajeti na Mkutano wa Kujadili Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Jumuiya); na Mikutano minne kufanyika kwa mzunguko katika Nchi zote Wanachama wa Jumuiya.

Aidha, imebainika kuwepo kwa mgogoro kati ya Spika na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki uliopelekea kutaka kumwondoa katika wadhifa wa uspika. Mgogoro huo kwa sasa unapatiwa ufumbuzi kwa njia za kiutawala.

### 3.10 MAHAKAMA YA AFRIKA MASHARIKI

96. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 Mahakama ya Afrika Mashariki ilizindua mfumo wa Kielektroniki wa kusajili na kufuatilia mienendo ya mashauri (Eletronic case management system).

Aidha Majaji wawili wa Mahakama hiyo kutoka Tanzania, Mheshimiwa Jaji Harold Nsekela aliyekuwa Rais wa Mahakama na Jaji wa Kitengo cha Rufaa na Mheshimiwa Jaji John Joseph Mkwawa aliyekuwa Jaji wa Kitengo cha Awali watamaliza muda wao mwezi Juni, 2014. Wakuu wa Nchi Wanachama wamewateua Mheshimiwa Jaji Edward M. K. Rutakangwa kuwa Jaji wa Kitengo cha Rufaa na Mheshimiwa Jaji Fakihi A. Jundu kuwa Jaji wa Kitengo cha Awali.

### 3.11 ELIMU KWA UMMA

97. Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina Mkakati wa miaka mitano (2012 – 2016) wa Kutoa Elimu kwa Umma. Mkakati huu unatoa mwongozo wa utoaji Elimu kwa Umma kuhusu mtangamano wa Afrika Mashariki kwa makundi mbalimbali na kwa kutumia mbinu

mbalimbali ikiwa ni pamoja na mikutano ya ndani na hadhara, semina na makongamano, maonesho ya kitaifa na kimataifa, vipindi vya luninga na redio, vipeperushi pamoja na machapisho, majarida, na ujumbe mfupi wa simu.

Aidha, Mkakati unabainisha namna ya kupata mrejesho kutoka kwa wadau.

98. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano kama ifuatavyo:-

**(a). Vipindi vya Luninga na Redio**

99. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliandaa vipindi kuhusu Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne (2005-2013) katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kongamano la mtangamano wa Afrika Mashariki katika maadhimisho ya Miaka Hamsini ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Vipindi hivyo vilirushwa hewani kupitia Vituo vya televisheni vya TBC 1, Star TV, Channel Ten na Radio Times FM.

**(b). Mikutano na vyombo vya Habari**

100. Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina utaratibu wa kukutana na vyombo vya habari kila mwezi kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali kuhusu Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hiki, Wizara imekutana na vyombo vya habari mara tano (5) na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

Hatua iliyofikiwa katika Majadiliano ya Umoja wa Fedha, hatua zilizofikiwa katika Shirikisho la Kisiasa, Utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Jumuiya, hususani uanzishwaji wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa pamoja mipakani, Uanzishwaji wa Himaya Moja ya Forodha, na Ufafanuzi kuhusu mikutano inayoendelea ya Utatu wa nchi za Kenya, Uganda na Rwanda.
Aidha, kupitia mikutano hiyo ufafanuzi ulitolewa kuhusu maamuzi yaliyofikiwa katika mikutano ya Wakuu wa Nchi Wanachama.

**(c). Maonesho Mbalimbali**

101. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeshiriki katika maonesho ya Nane Nane na Kongamano la Miaka Hamsini (50) ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Katika maonesho hayo, Wizara ilitoa Elimu kwa Umma kuhusu hatua za Mtangamano wa Afrika Mashariki na fursa zilizopo, miradi na programu zinazotekelezwa na Jumuiya pamoja na kusambaza majarida, vipeperushi na machapisho mbalimbali ya Jumuiya.

102. Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wizara iliratibu na kushiriki katika maonesho ya Juakali/Nguvu Kazi yaliyofanyika mwezi Desemba, 2013 jijini Nairobi, Kenya. Katika maonesho hayo, wajasiriamali 271 kutoka Tanzania walishiriki ikiwa ni ongezeko la wajasiriamali 188 ikilinganishwa na wajasiriamali 83 walioshiriki mwaka 2012/2013.

**(d). Machapisho Mbalimbali**

103. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imetayarisha Jarida la Wizara Toleo la Tano na Kipeperushi cha Maswali yanayoulizwa mara kwa mara na Wananchi kuhusu mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Toleo la Tatu.

Aidha, Wizara ilisambaza machapisho mbalimbali ikiwemo kitabu cha Taarifa za Mwenendo wa Biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Taasisi za Serikali, Vyuo vya Elimu ya Juu, Sekta Binafsi na Makatibu Tawala wa Mikoa.

**(e). Tovuti ya Wizara**

104. Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa zitakazowezesha wadau kujenga uelewa wa masuala mbalimbali ya mtangamano wa Afrika Mashariki na shughuli za Wizara kwa ujumla, Wizara imeendelea kuboresha Tovuti yake inayopatikana kupitia *www.meac.go.tz.*

**(f). Ziara za Mipakani**

105. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara ilifanya ziara katika mipaka ya Manyovu, Rusumo, Sirari, Namanga na Holili. Ziara hizo zililenga kuelimisha wananchi na watendaji mipakani kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuwahimiza kuzitumia fursa zitokanazo na Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja na vilevile kutoa ufafanuzi wa Sera, Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo katika Jumuiya. Ziara hizo pia imewezesha kubaini changamoto zilizopo na kuandaa mikakati ya pamoja ya kukabiliana nazo.

**3.12 MCHANGO KATIKA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

106. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Wizara ilikamilisha malipo ya Mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2013/2014 ambao ni kiasi cha Shilingi 12,452,253,440.

**3.13 UTAWALA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU**

**(a). Kuimarisha Uwezo wa Wizara Kiutendaji**

107. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara ilipata Ofisi mpya katika jengo la Wizara ya Fedha mjini Dodoma ambayo imeanza kutumika kuanzia mwezi Februari, 2014. Kupatikana kwa Ofisi hiyo kumewezesha Wizara kutekeleza majukumu yake katika mazingira tulivu. Nachukua nafasi hii kuishukuru Wizara ya Fedha kwa kutupatia ofisi.

**(b). Ajira za Watumishi**

108. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara ilipata kibali cha ajira mpya kwa watumishi thelathini na sita (36) katika kada mbalimbali.

**(c). Upandishaji Vyeo na Kuthibitishwa Kazini**

109. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Makisio ya Ikama na Bajeti ya Mishahara ya Wizara kwa mwaka 2013/2014, Wizara iliidhinishiwa kuwapandisha vyeo watumishi kumi na tatu (13) ambao wamekidhi vigezo vya Miundo yao ya Utumishi na Utendaji mzuri wa kazi kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma. Aidha, Wizara iliidhinishiwa kumbadilisha kada Mtumishi mmoja (1).

110. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliwathibitisha katika Vyeo jumla ya Watumishi watano (5) na Mtumishi mmoja (1) alithibitishwa katika Madaraka.

Watumishi hao walithibitishwa baada ya kukamilisha kipindi cha matazamio na kuthibitisha kuyamudu majukumu yao mapya ya vyeo walivyopandishwa.

**d. Mafunzo kwa Watumishi**

111. Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013/2014, Wizara iliandaa Mpango wa mafunzo na utekelezaji wake umewezesha watumishi tisa (9) kugharamiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi kumi na watano (15) kugharamiwa mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi.

**(e). Maadili ya Utumishi wa Umma**

112. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 Wizara ilitoa mafunzo ya uzingatiaji wa Kanuni za Maadili katika Utumishi wa Umma kwa watumishi wa Wizara. Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwakumbusha Watumishi kuhusu wajibu wa kuzingatia Maadili ya Utumishi wa Umma katika utekelezaji wa majukumu yao.

**(f). Ushirikishwaji wa Watumishi**

113. Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013/14, Wizara iliendelea kushirikisha Wafanyakazi katika utoaji wa maamuzi kupitia Vikao vya Idara/Vitengo, Baraza la Wafanyakazi na Mikutano ya Watumishi wote. Menejimenti ya Wizara hukutana kila wiki kwa lengo la kupitia na kujadili utekelezaji wa majukumu ya wiki iliyomalizika na kujipanga kwa wiki inayofuata.

Aidha, Idara na Vitengo hufanya Vikao kila wiki ambapo Watumishi wa Idara na Vitengo hupata fursa ya kukutana na viongozi wao na kujadili kwa pamoja masuala yanayohusu Idara/Vitengo ili kuboresha utendaji kazi.

114. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara ilifanya kikao cha Baraza la Wafanyakazi ambacho pamoja na mambo mengine kilijadili na kuidhinisha Rasimu ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015.

**(g). Ushiriki wa Wizara Katika Michezo ya SHIMIWI**

115. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha afya za watumishi, ushirikiano na mshikamano miongoni mwa Watumishi wa Umma, mwaka 2013/2014 Wizara iliwezesha watumishi 30 kushiriki katika michezo ya SHIMIWI iliyofanyika mkoani Dodoma mwezi Novemba, 2013.

**(h). Mapambano Dhidi ya Maambukizi ya VVU na UKIMWI**

116. Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na athari zitokanazo na maambuzi ya VVU na UKIMWI katika sehemu ya kazi, mwaka 2013/2014, Wizara ilitoa mafunzo kwa waelimisha rika kumi na tano (15) kutoka katika Idara na Vitengo vya Wizara. Lengo la mafunzo hayo ni kuwezesha elimu ya VVU na UKIMWI kuwafikia watumishi wengi wa Wizara kwa muda mfupi.

**(i). Usimamizi wa Mapato na Matumizi**

117. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliendelea kusimamia mapato na matumizi ya fedha za Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 na Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 na miongozo mbalimbali ya Serikali.

Katika mwaka 2013/2014 Wizara imeendelea kufanya vikao vya kila robo mwaka vya Kamati ya Udhibiti wa Mapato na Matumizi na kuwasilisha Taarifa za vikao hivi kwa wakati kwa Waziri Mkuu kama ulivyo utaratibu.

118.Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kulitaarifu Bunge lako kuwa katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu imeweza kupata Hati Safi ya Ukaguzi wa Hesabu toka Ofisi ya Mdhitibi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

## 4.0 CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

119. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu ya mwaka 2013/2014, Wizara ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

a. Kutokana na Wizara kutokuwa na jengo lake la Ofisi, tumeendelea kutumia fedha nyingi kulipia kodi ya pango kwa Ofisi zake zilizopo Dar es Salaam na Zanzibar hivyo kuendelea kuathir bajeti ya Wizara.

b. Uhaba wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na chache wa magari ya kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi ya Jumuiya na utoaji wa Elimu kwa Umma umeendelea kuwa changamoto katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Wizara itaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Wadau wa Maendeleo ili kupata fedha za kutatua changamoto hii.

c. Vikwazo Visivyo vya Kiforodha (Non Tariff Barriers – NTB) ikiwa ni pamoja na vizuizi vya barabarani vimeendelea kuwepo na hivyo kutoiwezesha Tanzania na Nchi nyingine Wanachama kunufaika kikamilifu na utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki.

Wizara imeendelea kushirikiana na Wadau katika kubainisha na kuondoa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha ili kuliwezesha Taifa kunufaika na fursa za kibiashara zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki na vilevile kuitumia vyema fursa ya asili ya kijiografia tuliyo nayo.

d. Kasi ndogo ya urekebishwaji wa Sheria za ndani ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja. Wizara inahimiza Sekta husika kuongeza kasi ya mapitio ya Sheria husika ili kuliwezesha Taifa kunufaika na fursa zitokanazo na Soko la Pamoja.

e. Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zilizopo katika Jumuiya hiyo. Hali hii imewafanya Watanzania kutozitumia kikamilifu fursa zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kujiletea maendeleo. Wizara inaendelea kutekeleza Mkakati wake wa Mawasiliano ili kuwawezesha Watanzania kunufaika na mtangamano wa Afrika Mashariki.

## 5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

120. Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014/2015 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuratibu maandalizi na kuongoza majadiliano katika mikutano ya Kisheria ya Wakuu wa Nchi Wanachama, Baraza la Mawaziri la Jumuiya, Mabaraza ya Mawaziri ya Kisekta ya Jumuiya, Vikosi Kazi na mikutano ya Wataalam;

ii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya na Baraza la Mawaziri la Jumuiya;

iii. Kuratibu Utekelezaji wa Mpangokazi wa Miaka Kumi wa Kuelekea katika eneo la Sarafu Moja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;

iv. Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya (EAC – EU Economic Partnership Agreement); na Mkataba wa Biashara na Uwekezaji baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani;

v. Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano ya utatu wa COMESA-EAC-SADC;

vi. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Miradi na Programu za Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na miradi ya uendelezaji wa miundombinu (barabara, reli, bandari, nishati, viwanja vya ndege na hali ya hewa) na miradi katika sekta ya kijamii na mazingira ya Jumuiya;

vii. Kuratibu ukamilishaji na ujenzi wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja katika Mipaka ya Tanzania na Nchi Wanachama wa Jumuiya;

viii. Kuratibu uandaaji wa Kanuni za Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Uendeshaji wa Vituo vya kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani na Sheria ya Jumuiya ya Kudhibiti Uzito wa Magari;

ix. Kuratibu utekelezaji wa mikakati ya uwianishaji wa Mifumo ya Elimu na Mitaala kwenye maeneo ya Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Mafunzo ya Ualimu, Mafunzo ya Makundi Maalumu, Mafunzo ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Mafunzo yasiyo Rasmi na Elimu ya Watu Wazima;

x. Kuratibu uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha katika biashara baina ya Nchi Wanachama;

xi. Kuratibu ushiriki wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA) na vikao vya pamoja kati ya Wizara na Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki;

xii. Kuratibu ushiriki wa Wizara katika vikao vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

xiii. Kukamilisha mapitio ya sheria za Tanzania ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xiv. Kuratibu na kushiriki katika majadiliano kuhusu Jamhuri za Sudan Kusini na Somalia kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xv. Kuratibu na kushiriki katika mchakato wa maandalizi ya Rasimu ya Katiba ya Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki;

xvi. Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya maeneo ya kuwa na msimamo wa pamoja katika masuala ya Sera za Mambo ya Nje;

xvii. Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuipandisha hadhi Hati ya kusafiria ya Afrika Mashariki kuwa ya Kimataifa;

xviii. Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zilizopo kupitia Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara;

xix. Kuratibu mapitio, utafiti, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mtangamano wa Afrika Mashariki. Eneo hili linalenga kupata taarifa za uhakika zitakazowezesha kupata msimamo wa Tanzania katika kuongoza majadiliano mbalimbali katika Jumuiya;

xx. Kuratibu utoaji wa huduma za masuala ya Utumishi na Utawala pamoja na Kutekeleza masuala mtambuka (Ukimwi, Jinsia, na Utawala Bora);

xxi. Kuimarisha mifumo ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Mifumo ya Ununuzi pamoja na kuandaa Mikakati ya Kusimamia Vihatarishi vya utendaji wa Wizara; na

xxii. Kuratibu uandaaji wa Mipango na Bajeti ya Wizara na taarifa mbalimbali za utendaji wa majukumu ya Wizara.

121. Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha makubaliano ya Itifaki, Sera na Mikakati inayoingiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki inazingatia maslahi ya Taifa na kunufaisha watanzania kama inavyotarajiwa, Wizara kwa kushirikiana na Sekta za Umma, Sekta Binafsi na wadau wengine, itaendelea kufanya tafiti na chambuzi za kina zitakazowezesha kuandaa misimamo ya Taifa ya kuongoza majadilino katika Jumuiya.

122. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Mkakati wa Wizara wa Mawasiliano na Mpango Kabambe wa Utoaji Elimu kwa Umma, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa zinazotokana na utekelezaji wa hatua mbalimbali za mtangamano katika nyanja za kibiashara, kijamii, kiuchumi na kisiasa na taratibu za kuzitumia ili Watanzania wazichangamkie na kunufaika nazo.

## 6.0 SHUKRANI

123. Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuyatamka maombi ya fedha ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/15 sina budi kuwashukuru Washirika mbalimbali wa Maendeleo waliofadhili utekelezaji wa Programu na miradi mbalimbali ya maendeleo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2013/2014.

Shukrani za pekee ziwaendee Serikali za Uingereza, Finland, Norway, Marekani, Ujerumani; Ufaransa, Kanada, Sweden, Ubelgiji, Denmark na Japan. Aidha, natoa shukrani kwa Mashirika na Taasisi za Kimataifa za Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Marekani (USAID), Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA), Benki ya Japan ya Maendeleo ya Kimataifa, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Rockefeller Foundation, Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IMO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), Investment Climate Facility for Africa (ICF), Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID), African Capacity Building Facility (ACBF), The Association of European Parliamentarians with Africa (AWEPA) na TradeMark East Africa (TMEA).

## 7.0 MAOMBI YA FEDHA ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

124. Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2014/2015, naliomba Bunge lako liidhinishe jumla ya Shilingi 23,785,246,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2014/2015. Kati

ya fedha hizo, Shilingi 22,251,992,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na Shilingi 1,533,254,000 kwa ajili ya mishahara ya Watumishi (PE).

Aidha, pamoja na hotuba hii nimejumuisha viambatisho mbalimbali. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kuwa ni vielelezo vya hoja hii. Aidha, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya *www.meac.go.tz.*

125. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe nukuu ya Kauli Mbiu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni "One People, One Destiny" (Yaani "sisi wana Afrika Mashariki ni wamoja na hatma yetu ni moja").

126. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo, Mheshimiwa Moses Machali kwa niaba ya Katibu wa Kambi Rasmi ya Upinzani anawatangazia Wabunge wote wa Kambi Rasmi Upinzani Bungeni, kufika kwenye kikao kitakachofanyika ukumbi wa Msekwa saa saba kamili. Wote mnaombwa mhudhurie.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Sitta, Waziri wa Afrika Mashariki, sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

**Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama ilivyowasilishwa Bungeni**

**MHE. SELEMAN S. JAFO – (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Edward Lowassa, sasa naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) na 117(11) ya kanuni za Kudumu za Bunge toleo la mwaka 2013, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri unaotolewa na Kamati hii unatokana na ibara ya 63(3)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni na lengo la maoni na ushauri huu pamoja na mambo mengine ni kuisaidia Serikali katika kukamilisha kwa ufanisi, dira, dhamira na kauli mbiu ya Wizara hii ambayo inalenga katika kuimarisha ushirikiano wa nchi nyingine za Afrika Mashariki katika kuleta maisha bora kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utandawazi uliopo hivi sasa duniani ni dhahiri kabisa huwezi kujifungia ndani ya nchi yako na kisha kutegemea kuimarisha uchumi wa nchi na kuwaletea maisha bora wananchi wake, ni lazima ushirikiane na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dhana hiyo, Kamati ilitumia ujuzi na uzoefu wake wote kuishauri Wizara hii kwa wakati wote ili hadhi na heshima ya Tanzania mbele ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iweze kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Majukumu na malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014, fedha zilizoidhinishwa na zilizotolewa: Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha, 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 20,470,107,000/= ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 19 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 1,470,107,000/= kwa ajili ya mishahara ya watumishi. Wizara hii katika mwaka wa fedha 2013/2014 haikutengenewa fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2014, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 16,852,353,780/= kutoka Wizara ya Fedha, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1,185,603,780/= zikiwa ni malipo ya mishahara, shilingi bilioni 15,666,750,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa shilingi bilioni 12,452,253,440/= ni kwa ajili ya malipo ya mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo ya fedha Wizara hii ilibaki na shilingi bilioni 3,214,496,560/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu mengine ya Wizara ambayo ni sawa na asilimia 40 tu ya fedha zote ambazo zilistahili kupatiwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi inaonesha wazi kuwa Wizara ilipewa fedha kidogo sana za kuendeleza majukumu yake ikizingatia kwamba kwa njia moja au nyingine inahusiana na mambo ya ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imesababisha baadhi ya watendaji wa Wizara kukosa kushiriki baadhi ya mikutano muhimu ya Afrika Mashariki, jambo ambalo linaweza kutoelewa mwelekeo wa Jumuiya kupitia makubaliano ya mikutano hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kazi zilizotekelezwa na Wizara: Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 hadi mwezi Machi, 2014 Wizara ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuratibu na kushiriki katika mikutano ya Wakuu wa wananchi na Baraza la Maziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika utekelezaji wa kipengele hiki Wizara hii iliweza kuratibu na kusimamia kufanyika kwa mambo yafuatayo:-

(i) Mkutano wa 15 wa Wakuu wa Nchi wa Wanachama ulifanyika Mwezi Novemba, 2013 nchini Uganda, ambapo nchi zilitakiwa kukamilisha taratibu za kuridhia itifaki ya umoja wa fedha wa jumuiya ifikapo Julai, 2014.

(ii) Mkutano wa 27 wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya uliofanyika *August*, 2013 ambapo Sekretarieti ya Jumuiya iliwasilisha pendekezo la namna mbadala ya kuchangia katika Jumuiya.

(iii) Mkutano wa 28 wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ulifanyika Novemba, ambapo uliidhinisha mpango wa maendeleo wa sekta ya hali ya hewa pamoja na mkakati wa usalama wa vyombo vya majini katika ukanda wa bahari ya Hindi, wa Kusini na Mashariki ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliendelea kuishauri Wizara kuwashirikisha wadau wote wakati wa kushiriki mikutano hii ili kila sekta ijue wajibu wake katika kutekeleza mtangamano huu wa Afrika Mashariki.

(b) Utekelezaji wa hatua za mtangamano, katika utekelezaji wa kipengele hiki Wizara iliweza kuratibu na kusimamia kufanyika kwa mambo yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Umoja wa Forodha, ambao Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki, ambapo Serikali hatimaye walipata faida ya kukuza biashara ndani na nje ya Jumuiya. Kukuza uwekezaji wa nchi za jumuiya wenyewe, kupunguza muda wa kusafirisha bidhaa kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine ndani ya Jumuiya na kupunguza usafirishaji bidhaa ndani ya Jumuiya.

(ii) Uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha ambavyo nchi wanachama waliandaa rasimu ya sharia ya Jumuiya ya uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha ambapo vikwazo mbalimbali vimeanza kutatuliwa na vinginevyo vinaendelea kushughulikiwa.

(iii) Soko la pamoja la Afrika Mashariki ambapo katika kipindi hiki Jumuiya ilizindua ripoti ya hali ya utekelezaji wa soko la pamoja miongoni mwa nchi wanachama.

(iv) Umoja wa Fedha ambapo nchi wanachama wa Jumuiya zilikamilisha majadiliano ya uanzishwaji wa Umoja wa Fedha wa Afrika, ambapo itifaki ya kuanzisha umoja huo iliidhinishwa na kutiwa saini na wakuu wa nchi, mwezi Novemba, 2013.

(v) Shirikisho la kisiasa, ambapo Wizara iliendelea kuratibu upatikaji wa maoni ya Tanzania kuhusu Jambo hili. Mheshimiwa kama ambavyo kamati yangu ilitoa ushauri katika siku zilizopita, bado tunasisitiza Serikali kuchukua hatua za kipekee za kuwaelimisha wananchi kuhusu maana na lengo la mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati mara kadhaa, ilishauri Serikali kukamilisha sera ya mtangamano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini kwa taarifa zilizopo, hadi sasa sera hiyo bado haijakamilika. Kutokana na kutokamilika kwa sera hiyo na kutotekelezwa kumeleta tabu hata kwa Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kujua mwelekeo kuhusu sera na utekelezaji wa mtangamano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Watanzania walio wengi hii dhana mpya ambayo haieleweki wala hawajui faida zake na hivyo kupoteza haki zao ambazo wanastahili kuzipata bila vikwazo. Kamati inashauri Wizara kuzidisha nguvu katika kuratibu uanzishwaji wa Soko la Pamoja, kwani Watanzania watapata faida kubwa ya kutatua changamoto zinazohusiana na upatikanaji wa huduma mbalimbali za soko hilo zikiwemo za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na jambo hilo ambalo Watanzania linawapa hofu kubwa katika mtangamano wa Afrika Mashariki ni Shirikisho la Kisiasa. Pamoja na Serikali kuthibitisha na kudhihirisha kuwa jambo hili linaratibiwa kwa uangalifu mkubwa. Kamati inashauri kutofanya haraka katika suala hili ili kuyafanyia kazi mambo yote muhimu na kuingia katika hatua ya shirikisho kwa uhakika.

(c) Ushirikiano na Kanda nyingine: Kamati ilielezwa jinsi Wizara ilivyoratibu na kusimamia shughuli mbalimbali za ushirikiano wa Afrika Mashiriki na Jumuiya zingine za kikanda zikiwemo COMESA, SADC, EAC, AWEPA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kutosaini mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaohusu ushirikiano wa Jumuiya ya Ulaya kuhusu mambo ya kiuchumi uitwao

*Economic Partnership Agreement (EPA)* kwa sasa. Hadi hapo Jumuiya ya Ulaya, itakaporidhia ushauri wa kujenga viwanda hapa hapa Afrika Mashariki badala ya kuchukua malighafi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni ya Kamati ukubali kusaini mkataba huu utaleta matatizo makubwa kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, hususan Tanzania ambayo ina malighafi nyingi za baharini nan chi kavu. Aidha, moja ya tatizo la msingi ambalo linaweza kujitokeza ni uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa mwenyekiti, Kamati pia ilielezwa kuhusu majadiliano ya mkataba wa ubia wa biashara na uwekezaji baina ya Jumuiya ya Afrika na Marekani ambapo pande mbili zilibadilishana taarifa muhimu katika maeneo yaliyopendekezwa kuwa sehemu ya ubia ya biashara na uwekezaji iliyowezesha kuandaliwa kwa taratibu za kuanza majadiliano ya kina kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuendelea kutafuta kanda nyingine ambazo zinaweza kushirikiana na kuiletea tija zikiwemo za Asia, America, Mashariki ya Kati, *BRICKS* (Brazil, Russia, India, China and South Africa).

(d) Ushirikiano katika sekta ya uzalishaji: Kamati inaeleza jinsi Wizara ilivyosimamia na kuratibu utekelezaji wa ushirikiano katika sekta mbalimbali za uzalishaji zikiwemo za kilimo na usalama wa chakula, sera ya mifugo, sera ya chakula na lishe, sera ya masuala ya utalii na wanyamapori, maendeleo ya viwanda na ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara kuratibu mpangilio ambao ushirikiano huu utafika mpaka ngazi ya jamii ambapo wananchi wanaweza kutembeleana katika nchi za Jumuiya na kubadilishana uzoefu baina ya sekta zinazofanana.

(e) Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu na miradi ya Miundombinu ya Kiuchumi. Kamati ilielezwa kuwa, Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa programu na miradi ya Kikanda ya uendelezaji wa miundombinu ya kiuchumi, ikiwemo Mradi wa Barabara, Ujenzi wa Vituo vya utoaji wa huduma kwa pamoja mipakani yaani *One Stop Border Posts,* Uwianishaji wa uzito wa magari katika barabara, Reli, Sekta ya Hali ya Hewa, Sekta ya Anga na Sekta ya Nishati.

(f) Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama. Kamati ilielezwa kuhusu mchakato unaoendelea wa kujiunga kwa Jamhuri ya Sudan Kusini katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Mkutano wa 15 wa Wakuu wa Nchi Wanachama uliliagiza Baraza la Mawaziri kuanza majadiliano rasmi na nchi hiyo.

(g) Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Afrika Mashariki. Kamati ilielezwa kuwa, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 hadi kufikia mwezi Machi, 2014, Wizara iliratibu vikao vitano vya Bunge la Afrika Mashariki ambavyo vilijadili Miswada ya Sheria na kupitisha Maazimio mbalimbali. Katika kipindi hicho ilielezwa kuwa, Bunge hilo lilipitisha Sheria mbili na Miswada mitatu ilisomwa kwa mara ya kwanza na kupitisha Maazimio kumi na tatu.

(h) Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu kwa Umma. Kamati ilielezwa kuwa Wizara imeendelea kutoa Elimu kwa Umma kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kuzifahamu na kunufaika na fursa zinazotokana na Tanzania kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hiki, Wizara iliendelea kutoa elimu kwa umma kupitia utekelezaji wa Mkakati wake wa Mawasiliano kwa Umma.

(i)Mheshimiwa Mwenyekiti, Uimarishaji uwezo wa Wizara kiutendaji na masuala mtambuka. Kamati ilielezwa kuhusu namna Wizara ilivyotekeleza masuala mbalimbali ya Utawala na Utumishi yakiwemo ya kupatikana kwa sehemu ya kufanyia kazi zake Mjini Dodoma, ajira, mafunzo na upandishwaji vyeo kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya Mwaka uliopita wa 2013/2014. Wakati Kamati ilipokuwa ikijadili Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2013/2014, ilitoa maoni na ushauri wa mambo mbalimbali ili utekelezaji wa kazi za Wizara uende sawia na maoni na ushauri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilitoa taarifa ya jinsi ilivyotekeleza maoni na ushauri huo wakati wa utekelezaji wa kazi za Wizara hiyo kwa kipindi hicho cha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa maoni na ushauri huo uligubikwa na changamoto ya ufinyu wa Bajeti kutokana na fedha kidogo zilizoidhinishwa na kutolewa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kama taarifa hii ilivyoeleza hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine, Kamati yangu inaishauri Serikali kuipatia Wizara hii mgao wake wa fedha kwa wakati kama zitakavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu, vinginevyo itakwama kutekeleza malengo yake yanayoambatana na maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa wakati wa mjadala wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maoni na ushauri wa Kamati yangu kwa Wizara hii ni jambo endelevu, hivyo bado Kamati inaishauri Wizara kuendelea na utekelezaji wa maagizo yake ambayo hayakukamilika au yalitekelezwa kwa kiwango kidogo kutokana na changamoto mbalimbali kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri ambao ulitolewa mwaka 2013/2014 na bado Kamati inatoa msisitizo kuwa Wizara iendelee na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Hoja namba tano ambayo ni, Serikali itumie uwezo walionao Watanzania kuwawezesha kupata ajira katika nchi nyingine Wanachama. Aidha, kasi ya kuingia mkataba na nchi hizo kwa madhumuni hayo iongezwe.

(ii) Hoja namba saba, pamoja na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa kwa mwaka huu wa 2013/2014, bado Kamati inaishauri Wizara kufuatilia kwa karibu zaidi na kuhakikisha Muundo mpya wa Wizara ikiwemo Idara ya Utafiti unakamilika na kuanza kazi katika mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2014/2015. Kazi walizopanga kwa mwaka huu. Kamati ilielezwa kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(1) Kuratibu maandalizi na kuongoza majadiliano katika mikutano ya kisheria ya Wakuu wa nchi Wanachama, Baraza la Mawaziri la Jumuiya, Mabaraza ya Mawaziri ya Kisekta ya Jumuiya, Vikundi vya Kazi na Wataalam;

(2) Kuratibu utekelezaji wa Mpangokazi wa miaka kumi wa kuelekea katika eneo la sarafu moja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(3) Kuratibu utekelezaji wa Himaya moja ya Forodha ya Afrika Mashariki;

(4) Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya;

(5) Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano ya utatu wa *COMESA, EAC – SADC;* na
(6) Kuratibu utekelezaji wa mradi wa Reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali/Keza – Gitega – Msongati pamoja na utafiti wa kuimarisha sekta ya reli utakaotoa mapendekezo ya kuanzisha njia mpya za reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni kazi ambazo hata Mheshimiwa Waziri alizitaja, naomba zinukuliwe katika *hansard* kama zilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha, ili kuweza kutekeleza kazi zote zilizoelezwa hapo juu wizara hii, imepangiwa kupatiwa fedha shilingi 23,785,246,000/= kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Sh. 1,533,254,000/= kwa ajili ya mishahara.

(ii) Sh. 22,251,992,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo, ambapo sh. 13,704,245,000/= ni kwa ajili ya mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na sh. 8,547,747,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 kama yalivyooneshwa katika kifungu nambari (i) – (xxx) hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2014/2015. Pamoja na maoni na ushauri uliotolewa na Kamati yangu katika vipengele mbalimbali vilivyotangulia awali katika taarifa hii, Kamati pia inatoa maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara katika utekelezaji wa kazi zake kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kama ifuatavyo:-

(i) Badala ya kulalamikia nchi ambazo zinakumbatiana katika utatu wa mambo yao ya kiuchumi, Tanzania itumie fursa za Kijiografia ilizonazo kutafuta mbinu za kuimarisha uchumi wake.
(ii) Katika utekelezaji wa Miradi mbalimbali inayohusiana na mtangamano wa Afrika Mashariki, Tanzania ihakikishe inalinda ardhi yake ili isije ikawa chanzo cha mgogoro wa ndani.

(iii) Bado elimu inahitajika kwa wananchi na wadau wote kuhusu hatua zilizizoafikiwa, zinazoendelea na zinazokusudiwa kuchukuliwa katika ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hivyo, Serikali ichukue hatua muafaka za kuweka mkakati utakaohakikisha kila mtu anafikiwa katika kupatiwa elimu kuhusiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(iv) Serikali kupitia Wizara ya Fedha (Hazina) ilipe moja kwa moja michango yote ya Jumuiya ya Afrika Mashariki bila ya fedha hizi kupitishiwa Fungu 97. Naomba kurudia kifungu hiki, Serikali kupitia Wizara ya Fedha yaani Hazina ilipe moja kwa moja michango yote ya Jumuiya ya Afrika Mashariki bila ya fedha kupitishwa Fungu 97 la Wizara hii.

(v) Serikali iwapatie kwa wakati fedha za matumizi mengineyo yaani *OC* ili kuweza kushiriki vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa wakati kama vinavyopangwa.

(vi) Serikali iendelee kutafuta utaratibu mzuri wa kutoa na kupokea taarifa za kawaida, za haraka na za dharura kutoka kwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na kufanyiwa kazi ipasavyo na kwa wakati. Aidha, Serikali iendelee na uratibu muafaka wa kuhakikisha Wabunge hao wanawakilisha matakwa ya Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Serikali ifikirie Miradi ya Maendeleo ambayo inaweza kutekelezwa na Wizara hii, ili kuimarisha uchumi wa nchi yetu, kwa kutumia fursa zinazopatikana katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(vii) Katika kujadili suala la kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa nchi ya Jamhuri ya Sudan Kusini na Somalia, wawakilishi wetu katika Jumuiya hiyo waliangalie na kulichambua kwa umakini mkubwa jambo hili ili kuhakikisha usalama wa nchi yetu hautaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kwa Kamati ya Bajeti ya Bunge kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2014/2015. Katika kupokea na kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2014/2015, Kamati yangu imejadili kwa kina suala la Serikali kulipia michango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Fungu 97 la Wizara hii na kugundua kuwa, inaonekana Wizara inapewa fedha nyingi wakati ni kinyume na uhalisia uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo, Kamati yangu inaishauri Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhamisha fedha zote za michango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuziweka moja kwa moja chini ya Wizara ya Fedha (Hazina) ambayo italipia gharama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vile vile inaishauri Kamati ya Bajeti ya Bunge kuitengea fedha za Miradi wa Maendeleo Wizara hii itakayolenga kuimarisha uchumi kutokana na fursa zilizopo katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, naomba tena kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niwasilishe taarifa hii pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Samuel John Sitta na Mheshimiwa Juma Abdallah Sadalla kwa ushirikiano mzuri wanaoipatia Kamati katika utekelezaji wa kazi zake. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu wao Ndugu Joyce Mapunjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Ushirikiano wao wakati wa kupitia, kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Kwa kuthamini kwa vile muda bado ninao, naomba kuwataja Wajumbe wa Kamati hiyo.

Kwanza, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, omba pesa maliza na kama umeshaomba basi.

**MHE. SELEMANI SAIDI JAFO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu. Nashukuru Katibu wa Bunge Ndugu …

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kujadili pamoja na kuyakubali makadirio na mapato na matumizi ya Wizara hii, Fungu namba 97 kama ilivyowasilishwa na Mtoa hoja kwa kuzingatia maoni ya Kamati kuhusu Wizara ya Fedha (Hazina) kulipia michango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante umesoma vizuri kwa muda uliopangwa.

**Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Afrika Mashariki kama ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA YA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2013/2014; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HII KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

**1.0 UTANGULIZI:**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na 117 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, nomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014; pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni na Ushauri utakaotolewa na Kamati hii unatokana na Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni na lengo la maoni na ushauri huu pamoja na mambo mengine ni kuisadia Serikali katika kukamilisha kwa ufanisi, dira, dhamira na kaulimbiu ya Wizara hii ambazo zinalenga katika kuimarisha ushirikiano na Nchi nyingine za Afrika Mashariki katika kuleta maisha bora kwa wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na utandawazi uliopo hivi sasa duniani, ni dhahiri kabisa huwezi kujifungia ndani ya nchi yako na kisha utegemee kuimarisha uchumi wa nchi na kuwaletea maisha bora wananchi wake ni lazima ushirikiane na wengine.

**Mheshimiwa Spika,** katika dhana hiyo, Kamati ilitumia ujuzi na uzoefu wake wote kuishauri Wizara hii kwa wakati wote ili hadhi na heshima ya Tanzania mbele ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iweze kuimarika.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2013/2014;

### 2.1 Fedha zilizoidhinishwa na zilizotolewa:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa shilingi 20,470,107,000/= ambapo kati ya fedha hizo shilingi 19,000,000,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na shilingi 1,470,107,000/= kwa ajili ya mishahara ya watumishi. Wizara hii katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 haikutengewa fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, hadi kufikia mwezi Machi 2014 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 16,852,353,780/= kutoka Wizara ya Fedha kati ya fedha hizo, shilingi 1,185,603,780/= zikiwa ni malipo ya mishahara, shilingi 15,666,750,000/= ni kwa ajili ya maatumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa, shilingi 12,452,253,440/= ni kwa ajili ya malipo ya mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo ya fedha, Wizara hii ilibaki na shilingi 3,214,496,560/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu mengine ya Wizara, ambayo ni sawa na asilimia arubaini (40%) ya fedha zote ambazo inastahili kupatiwa kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.
**Mheshimiwa Spika,** katika hali halisi inaonyesha wazi kuwa, Wizara ilipewa fedha kidogo sana za kuendeshea majukumu yake, ukizingatia kwamba, kwa njia moja au nyingine inahusiana na mambo ya Ushirikiano wa Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii imesababisha baadhi ya watendaji wa Wizara kukosa kushiriki baadhi ya Mikutano muhimu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, jambo ambalo linaweza kusababisha kutoelewa mwelekeo wa Jumuiya kupitia makubaliano ya mikutano hiyo.

### 2.2 Kazi zilizotekelezwa na Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, katika kipindi cha 2013/2014 hadi mwezi Machi, 2014, Wizara ilitekeleza mambo yafuatayo:-

**a) Kuratibu na kushiriki katika mikutano ya Wakuu wa Nchi na Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki;**

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa kipengele hiki, Wizara hii iliweza kuratibu na kusimamia kufanyika kwa mambo yafuatayo:-

i) Mkutano wa 15 wa Wakuu wa Nchi Wanachama uliofanyika mwezi Novemba, 2013 nchini, Uganda, ambapo nchi zilitakiwa kukamilisha taratibu za kuridhia itifaki ya Umoja wa Fedha wa Jumuiya ifikapo Julai, 2014.

ii) Mkutano wa 27 wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya uliofanyika Agosti, 2013 ambapo Sekretarieti ya Jumuiya iliwasilisha pendekezo la namna mbadala ya kuchangia katika Jumuiya.

iii) Mkutano wa 28 wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya uliofanyika Novemba, ambao uliidhinisha Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Hali ya Hewa pamoja na mkakati wa usalama wa vyombo vya majini katika ukanda wa Bahari ya Hindi wa Kusini na Mashariki mwa Afrika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Wizara kuwashirikisha wadau wote wakati wa kushiriki mikutano hii ili kila sekta ijue wajibu wake katika kutekeleza mtangamano huu wa Afrika Mashariki.

**b) Utekelezaji wa hatua za mtangamano:**

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa kipengele hiki, Wizara iliweza kuratibu na kusimamia kufanyika kwa mambo yafuatayo:-

i) Utekelezaji wa Umoja wa Forodha ambapo Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki ambapo serikali hatimaye watapata faida ya kukuza biashara ndani na nje ya Jumuiya, kukuza uwekezaji wa nchi za Jumuiya wenyewe kwa wenyewe, kupunguza muda wa kusafirisha bidhaa kutoka nchi moja kwenda nyingine ndani ya Jumuiya na kupunguza kusafirisha bidhaa ndani ya Jumuiya.

ii) Uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha ambapo nchi wanachama zimeandaa rasimu ya sheria ya Jumuiya ya Uondoaji wa Vikwazo visivyo vya kiforodha ambapo vikwazo mbalimbali vimeanza kutatuliwa na vingine vinaendelea kushughulikiwa.

iii) Soko la pamoja la Afrika Mashariki, ambapo katika kipindi hiki Jumuiya ilizindua ripoti ya hali ya utekelezaji wa soko la pamoja mongoni mwa nchi wanachama *(EAC Common Market Scorecard)* kwa mwaka 2014.

iv) Umoja wa fedha, ambapo nchi wanachama wa Jumuiya zilikamilisha majadiliano ya uanzishwaji wa umoja wa fedha wa Afrika Mashariki ambapo itifaki ya kuanzisha umoja huo iliidhinishwa na kutiwa sahihi na Wakuu wa Nchi mwezi Novemba, 2013.

v) Shirikishi la kisiasa, ambapo Wizara inaendelea kuratibu upatikanaji wa maoni ya Tanzania kuhusu jambo hili.

**Mheshimiwa Spika,** kama ambavyo Kamati yangu ilitoa ushauri katika siku zilizopita, bado tunasisitiza serikali kuchukua hatua za kipekee za kuwaelimisha wananchi kuhusu maana na lengo la **"Mtangamano wa Afrika Mashariki"**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati mara kadhaa iliishauri Serikali kukamilisha Sera ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini kwa taarifa zilizopo hadi sasa Sera hiyo bado haijakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** kutokamilika kwa Sera hiyo na kutekelezwa kumeleta taabu hata kwa Wabunge wetu wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashriki kujua mwelekeo wa Tanzania kuhusu Sera na utekelezaji wa mtangamano huo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa Watanzania walio wengi hii ni dhana mpya ambayo hawaielewi wala hawajui faida zake na hivyo kupoteza haki zao ambazo wanastahili kuzipata bila vikwazo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara kuzidisha nguvu katika kuratibu uanzishwaji wa soko la pamoja kwani Watanzania watapata faida kubwa ya kutatua changamoto zinazohusiana na upatikanaji wa huduma mbali mbali za soko hilo zikiwemo za ajira.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya jambo ambalo Watanzania linawapa hofu kubwa katika mtangamano wa Afrika ya Mashariki ni Shirikisho la Kisiasa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Serikali kuthibitisha kuwa jambo hili linaratibiwa kwa **"Uangalifu Mkubwa",** Kamati inaishauri kutofanya haraka katika suala hili ili kuyafanyia kazi mambo yote muhimu na kuingia katika hatua ya shirikisho kwa uhakika.

**c) Ushirikiano wa kanda nyingine:**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa jinsi Wizara ilivyoratibu na kusimamia shughuli mbalimbali za ushirikiano wa Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine za kikanda zikiwemo COMESA, SADC na EAC – EU-EPA.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri serikali kutosaini Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaohusu Ushirikiano na Jumuiya ya Ulaya kuhusu mambo ya kiuchumi uitwao " Economic Partnership Agreement – EPA " kwa sasa, hadi hapo Jumuiya ya Ulaya (EU) itakaporidhia ushauri wa kujenga viwanda hapa hapa Afrika Mashariki badala ya kuchukua mali ghafi zetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa maoni ya Kamati kukubali kusaini Mkataba huu kutaleta matatizo makubwa kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki hususan Tanzania ambayo inazo mali ghafi nyingi za baharini na nchi kavu. Aidha moja ya tatizo la msingi ambalo linaweza kujitokeza ni la uchafuzi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilielezwa kuhusu majadiliano ya Mkataba wa ubia wa biashara na uwekezaji baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani, ambapo pande mbili zilibadilishana taarifa muhimu katika maeneo yanayopendekezwa kuwa sehemu ya ubia wa biashara na uwekezaji ili kuwezesha kuandaliwa kwa taratibu za kuanza majadilinao ya kina kwenye maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri serikali Jumuiya kuendelea kutafuta Kanda nyingine ambazo wanaweza kushirikiana na kuiletea tija, zikiwemo za Asia, Amerika, Mashariki ya Kati na BRICS (Brazil,Russia,India, China and South Africa).

**d) Ushirikiano katika sekta za uzalishaji:**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa jinsi Wizara ilivyosimamia na kuratibu utekelezaji wa ushirikiano katika sekta mbali mbali za uzalishaji zikiwemo za kilimo na usalama wa chakula, Sera ya Mifugo, Sera ya chakula na lishe, masuala ya utalii na wanyamapori, Maendeleo ya viwanda na ufugaji wa samaki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara kuratibu mpangilio ambao ushirikiano huu utafika mpaka ngazi ya jamii ambapo wananchi wanaweza kutembeleana katika nchi za Jumuiya na kubadilishana uzoefu baina ya sekta zinazo fanana.

**e) Programu na miradi ya Miundombinu ya Kiuchumi:**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa programu na miradi ya kikanda ya uendelezaji wa Miundombinu ya kiuchumi, ikiwemo Mradi wa Barabara, Ujenzi wa Vituo vya uotaji wa huduma kwa pamoja mipakani *(One Stop Border Posts),* Uwianishaji wa uzito wa magari katika barabara, Reli, Sekta ya hali ya hewa, Sekta ya anga na Sekta ya Nishati.

**f) Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama:**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuhusu mchakato unaoendelea wa kujiunga kwa Jamhuri ya Sudan Kusini katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Mkutano wa 15 wa Wakuu wa Nchi Wanachama uliliagiza Baraza la Mawaziri kuaza majadiliano rasmi na Nchi hiyo.

**g) Bunge la Afrika Mashariki:**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 hadi kufikia mwezi Machi, 2014, Wizara iliratibu vikao vitano vya Bunge la Afrika Mashariki ambavyo vilijadili Miswada ya Sheria na kupitisha maazimio mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho ilielezwa kuwa, Bunge hilo lilipitisha sheria mbili na miswada mitatu ilisomwa kwa mara ya kwanza na kupitisha maazimio kumi na tatu.

**h) Elimu kwa Umma:**

(1) Kuratibu maandalizi na kuongoza majadiliano katika mikutano ya kisheria ya Wakuu wa nchi Wanachama, Baraza la Mawaziri la Jumuiya, Mabaraza ya Mawaziri ya Kisekta ya Jumuiya, Vikundi vya Kazi na Wataalam;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Wizara imeendelea kutoa Elimu kwa Umma kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kuzifahamu na kunufaika na fursa zinazotokana na Tanzania kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hiki, Wizara iliendelea kutoa Elimu kwa Umma kupitia utekelezaji wa Mkakati wake wa mawasiliano kwa umma.

**i) Kumarisha uwezo wa Wizara kiutendaji na masuala mtambuka:**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuhusu namna Wizara ilivyotekeleza masuala mbalimbali ya Utawala na Utumishi yakiwemo ya kupatikana kwa sehemu ya kufanyia kazi zake mjini Dodoma, Ajira, mafunzo na upandishwaji vyeo kwa watumishi.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI YALIYOTOLEWA WAKATI WA KUJADILI BAJETI YA MWAKA ULIOPITA WA 2013/2014:

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati ilipokuwa ikijadili Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka uliopita wa 2013/2014 ilitoa maoni na ushauri wa mambo mbalimbali ili utekelezaji wa kazi za Wizara uende sawia na maoni na ushauri huo.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ilitoa taarifa ya jinsi ilivyotekeleza maoni na ushauri huo wakati wa utekelezaji wa kazi za Wizara hiyo kwa kipindi hicho cha 2013/2014.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa maoni na ushauri huo uligubikwa na changamoto ya ufinyu wa Bajeti kutokana na fedha kidogo zilizoidhinishwa na kutolewa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kama taarifa hii ilivyoeleza hapo awali.

**Mheshimwa Spika,** kwa mara nyingine Kamati yangu inaishauri Serikali kuipatia Wizara hii mgao wake wa fedha kwa wakati kama zitakavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu, vinginevyo itakwama kutekeleza malengo yake yanayoambatana na maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa wakati wa mjadala wa Bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa maoni na ushauri wa Kamati yangu kwa Wizara hii ni jambo endelevu, hivyo bado Kamati inaishauri Wizara kuendelea na utekelezaji wa maagizo yake ambayo hayakukamilika au yalitekelezwa kwa kiwango kidogo kutokana na changamoto mbali mbali kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

**Mheshimiwa Spika,** maoni na ushauri ambao ulitolewa mwaka 2013/2014 na bado Kamati inatoa msisitizo kuwa Wizara iendelee na utekelezaji wake ni:-

i. **Hoja namba tano ambayo ni**: Serikali itumie uwezo walionao Watanzania kuwawezesha kupata ajira katika nchi nyingine Wanachama. Aidha, kasi ya kuingia mkataba na nchi hizo kwa madhumuni hayo iongezwe.

ii. **Hoja namba saba**: pamoja na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa kwa mwaka huu wa 2013/2014, bado Kamati inaishauri Wizara kufuatilia kwa karibu zaidi na kuhakikisha Muundo mpya wa Wizara ikiwemo Idara ya Utafiti unakamilika na kuanza kazi katika mwaka wa fedha wa 2014/2015.

## 4.0 MAPENDEKEZO YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2014/2015;

### (a) Kazi walizopanga:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i) Kuratibu maandalizi na kuongoza majadiliano katika mikutano ya kisheria ya Wakuu wa nchi Wanachama, Baraza la Mawaziri la Jumuiya, Mabaraza ya Mawaziri ya Kisekta ya Jumuiya, Vikundi vya Kazi na Wataalam;

ii) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Wakuu wa nchi Wanachama wa Jumuiya na Baraza la Mawaziri la Jumuiya;

iii) Kuratibu utekelezaji wa Mpangokazi wa miaka kumi wa kuelekea katika eneo la sarafu moja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;

iv) Kuratibu uridhiwaji wa Itifaki mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilizokwisha sainiwa na nchi wanachama.

v) Kuratibu utekelezaji wa Himaya moja ya Forodha ya Afrika Mashariki;

vi) Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya *(EAC – EU Economic Partinership Agreement);*

vii) Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano ya utatu wa *COMESA EAC – SADC;*

viii) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Miradi na Programu za Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na miradi ya uendelezaji wa Miundombinu na miradi katika sekta ya kijamii na mazingira ya Jumuiya;

ix) Kuratibu ujenzi wa vituo vya kutoa huduma kwa pamoja katika mipaka ya Tanzania na nchi wananchama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Rusumo ikiwa ni pamoja na kuratibu uandaaji wa kanuni za sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Uendeshaji wa vituo vya kutoa huduma kwa pamoja mipakani na sheria ya Jumuiya ya kudhibiti uzito wa magari;

x) Kuratibu utekelezaji wa mradi wa Reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali/Keza – Gitega – Musongati pamoja na utafiti wa kuimarisha sekta ya reli utakaotoa mapendekezo ya kuanzisha njia mpya za reli;

xi) Kuratibu mapitio ya mradi wa mkongo wa mawasiliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuendana na mahitaji ya sasa kwa kuzingatia hatua zilizofikiwa na nchi wanachama katika kuendeleza mtandao wa mawasiliano;

xii) Kuratibu utekelezaji wa mpango wa maendeleo na mkakati wa uwekezaji wa miaka 5 (2013-2018) katika sekta ya Hali ya Hewa na ukamilishaji wa Kanuni za udhibiti wa huduma za usafiri wa anga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xiii) Kuratibu uanzishwaji wa mradi wa kituo cha nishati jadidifu na uanzishwaji wa mpango wa pamoja wa kuunganisha njia kuu za umeme *(power pool)* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xiv) Kuandaa vigezo na viashiria vitakavyotumika kupima utekelezaji wa mpango wa uwazi katika afya *(Open Health Initiave);*

xv) Kuratibu mpango wa kuziendeleza taasisi tano zilizochaguliwa kuwa, taasisi zilizobobea za Jumuiya;

xvi) Kuratibu tathmini ya utekelezaji wa mradi wa utunzaji wa mazingira katika bonde la ziwa Victoria;

xvii) Kuratibu utekelezaji wa mikakati ya uwianishaji wa mifumo ya elimu na mitaala kwenye maeneo ya elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, mafunzo ya ualimu, mafunzo ya makundi maalum, mafunzo ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na mafunzo yasiyo rasmi na elimu ya watu wazima;

xviii) Kuratibu uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha katika biashara baina ya nchi wanachama;

xix) Kuratibu ushiriki katika mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki (EALA) na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na mikutano kati ya wizara na wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki;

xx) Kukamilisha mapitio ya sheria za Tanzania ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xxi) Kuratibu na kushiriki katika majadilino kuhusu Jamhuri za Sudani Kusini na Somalia ya kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xxii) Kuratibu na kushiriki katika majadiliano kuhusu Mpango kazi na Muundo wa Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki;

xxiii) Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya maeneo ya kuwa na msimamo wa pamoja katika masuala ya sera za Mambo ya Nje;

xxiv) Kuratibu na kushiriki katika majadiliano kuhusu kuwa na "*mutual Defence Pact*" miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

xxv) Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuifanya pasi ya kusafiria ya Afrika Mashariki kuwa ya Kimataifa;

xxvi) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zilizopo kupitia mkakati wa mawasiliano wa Wizara.

xxvii) Kuratibu mapitio, utafiti, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mtangamano wa Afrika Mashariki.

xxviii) Kuratibu utoaji wa huduma za masuala ya Utumishi na Utawala pamoja na kutekeleza masuala mtambuka.

xxix) Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za Umma, Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Mifumo ya ununuzi pamoja na kuweka Mikakati ya kusimamia vihatarishi *(Risk Management Strategies)* vya utendaji wa Wizara; na

xxx) Kuratibu uandaaji wa mipango na bajeti ya Wizara na taarifa mbalimbali za utendaji wa majukumu ya Wizara.

**(b) Maombi ya Fedha:**

**Mheshiwa Spika,** ili kuweza kutekelza kazi zote zilizoelezwa hapo juu wizara hii, imepangiwa kupatiwa fedha shilingi 23,785,246,000/= kwa mchanganuo ufuatao:-

i) Shilingi 1,533,254,000/= kwa ajili ya mishahara.

ii) Shilingi 22,251,992,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo, ambapo shilingi 13,704,245,000/= ni kwa ajili ya mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na shilingi 8,547,747,000/= ni kuwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 kama yalivyoonyeshwa katika kifungu nambari (i) – (xxx) hapo juu.

**(c) Maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2014/2015:**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maoni na ushauri uliotolewa na Kamati yangu katika vipengele mbali mbali vilivyotangulia awali katika taarifa hii, Kamati pia inatoa maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara katika utekelezaji wa kazi zake kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kama ifuatavyo:-

i) Badala ya kulalamikia nchi ambazo zinakumbatiana katika utatu wa mambo yao ya kiuchumi, Tanzania itumie fursa za Kijografia ilizonazo kutafuta mbinu za kuimarisha uchumi wake.

ii) Katika utekelezaji wa Miradi mbali mbali inayohusiana na mtangamano wa Afrika Mashariki, Tanzania ihakikishe inalinda Ardhi yake ili isije ikawa chanzo cha mgogoro wa ndani.

iii) Bado elimu inahitajika kwa wananchi na wadau wote kuhusu hatua zilizizoafikiwa, zinazoendelea na zinazokusudiwa kuchukuliwa katika ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hivyo Serikali ichukuwe hatua mwafaka za kuweka mkakati utakaohakikisha kila mtu anafikiwa katika kupatiwa elimu kuhusiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

iv) Serikali kupitia Wizara ya Fedha (Hazina) ilipe moja kwa moja michango yote ya Jumiya ya Afrika Mashariki bila ya fedha hizi kupitishiwa Fungu 97 la Wizara hii.

v) Serikali iwapatie kwa wakati fedha za matumizi mengineyo (OC) ili kuweza kushiriki vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa wakati kama vinavyopangwa.

vi) Serikali iendelee kutafuta utaratibu mzuri wa kutoa na kupokea taarifa za kawaida, za haraka na za dharura kutoka kwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na kufanyiwa kazi ipasavyo na kwa wakati. Aidha Serikali iendelee na uratibu mwafaka wa kuhakikisha Wabunge hao wanawakilisha matakwa ya Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

vii) Serikali ifikirie Miradi ya Maendeleo ambayo inaweza kutekelezwa na Wizara hii, ili kuimarisha uchumi wa nchi yetu, kwa kutumia fursa zinazopatikana katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

viii) Katika kujadili suala la kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa nchi ya Jamhuri ya Sudan Kusini na Somalia, wawakilishi wetu katika Jumuiya hiyo waliangalie na kulichambua kwa umakini mkubwa jambo hili ili kuhakikisha usalama wa nchi yetu hautaathirika.

**(d) Maoni na ushauri wa Kamati kwa Kamati ya Bajeti ya Bunge kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2014/2015:**

**Mheshimiwa Spika,** katika kupokea na kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2014/2015, Kamati yangu imejadili kwa kina suala la serikali kulipia michango ya Jumuiya ya Afrika

Mashariki kupitia Fungu 97 la Wizara hii na kugundua kuwa, inaonekana Wizara inapewa fedha nyingi wakati ni kinyume na uhalisia uliopo.

**Mheshimiwa Spika,** katika hali hiyo Kamati yangu inaishauri Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhamisha fedha zote za michango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuziweka moja kwa moja chini ya Wizara ya Fedha (Hazina) ambayo italipia gharama hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati vilevile inaishauri Kamati ya Bajeti ya Bunge kuitengea fedha za Miradi wa Maendeleo Wizara hii itakayolenga kuimarisha uchumi kutokana na fursa zilizopo katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**HITIMISHO:**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuhitimisha , naomba tena kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niwasilishe taarifa hii pamoja na maoni na ushauri wa kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Samuel John Sitta (Mb) na Mheshimiwa Juma Abdallah Sadalla(Mb) kwa ushirikiano mzuri wanaoipatia Kamati katika utekelezaji wa kazi zake. Aidha nawashukuru watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu wao Ndugu Joyce Mapunjo.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Ushirikiano wao wakati wa kupitia, kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Kwa kuthamini michango yao naomba kuawatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Edward N. Lowassa(Mb) - Mwenyekiti
2. Mhe. Mussa Zungu Azzan (Mb) - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Suleiman Said Jaffo (Mb) - Mjumbe
4. Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa (Mb) - Mjumbe
5. Mhe. Susan A. Jarome Lyimo (Mb) - Mjumbe
6. Mhe. Betty Eliezer Machangu (Mb) - Mjumbe
7. Mhe. Eng. Yussuf H. Masauni (Mb) - Mjumbe
8. Mhe. Faith Mohammed Mitambo (Mb)- Mjumbe
9. Mhe. Thuwaiba Idrissa Muhamed (Mb)- Mjumbe
10. Mhe. Leticia Mageni Nyerere (Mb) - Mjumbe
11. Mhe. Muhammad Ibrahim Sanya (Mb)- Mjumbe
12. Mhe. John Magale Shibuda (Mb) - Mjumbe
13. Mhe. Anastanzia James Wambura (Mb)- Mjumbe
14. Mhe. Khamis Sued Kagasheki (Mb) - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu namshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah, kwa kuhakikisha kuwa Kamati inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha namshukuru Katibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhan Issa kwa kufanikisha kazi za Kamati na kuandaa Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo sasa naomba Bunge lako tukufu lipokee Taarifa hii na kujadili pamoja na kuyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Fungu 97 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja kwa kuzingatia maoni ya Kamati

kuhusu Wizara ya Fedha (Hazina) kulipia michango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Edward N. Lowassa, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Godfrey Zambi, anawatangazia Wabunge wote wanaotoka kwenye Mikoa inayozalisha pamba kwamba leo kutakuwa na kikao saa saba na nusu katika Ofisi za Wizara karibu na *VETA*.

Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. (*Makofi*)

**Taarifa ya Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Afrika Mashariki kama ilivyosomwa Bungeni**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI- MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Kwa dhati Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, kwa kuniteua kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wizara ya hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Nampongeza Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed kwa kuteuliwa kuwa Naibu wangu. Tunaahidi kuchapa kazi kwa kadiri ya uwezo wetu ili kulinda maslahi ya Taifa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa ikilaumiwa sana na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba inakwamisha utekelezaji wa haraka wa kuingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki kwa kuchukua muda mrefu mno wa kufanya uamuzi kuhusu masuala ya Shirikisho. Lawama hizo zilifikia hatua hata baadhi ya nchi za Jumuiya kuanza kushirikiana katika baadhi ya mambo na kuitenga Tanzania katika kile kinachoitwa *coalition of the willing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa utafiti ilioufanya na kwa kuzingatia historia ya mahusiano ya nchi za ukanda wa Afrika Mashariki, imebaini kwamba, Tanzania ndio nchi pekee katika Jumuiya hiyo yenye nia ya dhati ya kuwa katika shirikisho la kweli kuliko nchi nyingine ambazo msukumo wao wa kuingia katika Shirikisho kwa kasi, unatokana na maslahi fulani na pengine nje ya maslahi hayo nia ya kuwa katika shirikisho haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui ya Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tarehe 7 Novemba, 2013 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alilihutubia Bunge kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo juu ya Jumuiya

ya Afrika Mashariki na sintofahamu iliyokuwa inaendelea. Mara baada ya hotuba hiyo kulipitishwa azimio la kumpongeza Rais na ilitolewa ahadi kwamba hotuba hiyo ingepangiwa ratiba ya kujadiliwa, ahadi ambayo mpaka sasa Mwezi Mei 2014, miezi sita baadaye, haijatekelezwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka majibu yatolewe Bungeni na Waziri wa Afrika Mashariki au na Spika wa Bunge juu ya sababu za hotuba hiyo kutokujadiliwa na lini hasa hotuba hiyo itajadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana na Hotuba ya Rais kwamba Tanzania imo, itaendelea kuwemo na haina mpango wa kujiondoa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, licha ya tofauti zilizojitokeza baina ya viongozi wetu na viongozi wa nchi za Kenya, Uganda na Rwanda. Hata hivyo, maswali ambayo Rais aliyauliza katika Hotuba yake na kueleza kukosa majibu ya kwamba, namnukuu "wanachukia nchi yetu, wanataka kuunda jumuiya yao au wananichukia mimi mwenyewe?" Haya yanapaswa kutolewa majibu na Waziri wa Afrika Mashariki katika majumuisho ya Hotuba yake kwa kurejea yaliyojiri katika Vikao vya Jumuiya vilivyofuatia baada ya Hotuba ya Rais na mawasiliano mbalimbali ya Kiserikali kuhusu tofauti zilizojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Rais juu ya kwamba viongozi wa nchi tatu walioitwa *Coalition of the Willing* wana madai ya kuwa ushirikiano wa utatu huo ni wa nchi ambazo ziko tayari kuharakisha maendeleo ya Jumuiya hiyo, pamoja na kuitwa na Rais kuwa ni ya uongo yanahitaji kutafakariwa kuiwezesha nchi kufanya maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba Rais alilieleza Bunge kwamba haiwezekani tutumie dola za Marekani milioni 12 kila mwaka kuchangia Jumuiya hii halafu tuidhoofishe na kutaja kwamba kinachoonekana kuwakera viongozi wa nchi zingine ndani ya Jumuiya hiyo, ni msimamo wa Tanzania katika kupinga kuharakisha kuundwa kwa shirikisho, hasa katika eneo la umiliki wa ardhi, uhamiaji na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana na msimamo wa Mheshimiwa Rais wa kujenga Jumuiya hatua kwa hatua kama ilivyoainishwa kwenye mkataba na sio kuruka baadhi ya hatua. Hatua hizo ni Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Umoja wa Fedha na baadaye ndipo kuundwa kwa Shirikisho la Kisiasa kutakakotanguliwa na kura ya maoni ya kupitisha muundo huo wa Shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu utatu ulioanza, nchi za Kenya, Uganda na Rwanda walifanya vikao vitatu huko Mombasa, Kampala na Kigali ambapo pamoja na mambo mengine waliamua mambo nane ya msingi kwa kile walichokiita ni kuendeleza utangamano wa Nchi hizo Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mambo hayo ni:-

(1) Kujenga reli ya kisasa kutoka Mombasa hadi Kampala, Kigali na Bujumbura;

(2) Ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Kenya hadi Uganda na Sudan ya Kusini;

(3) Kujenga Kiwanda cha Kusafisha Mafuta nchini Uganda; na

(4) Kuanzisha himaya moja ya ushuru wa forodha ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine ni:-

(5) Kuharakisha Shirikisho la Afrika Mashariki ambapo waliunda Kamati ya Kuandaa Rasimu ya Katiba ya Shirikisho;

(6) Kuharakisha uanzishwaji wa hati ya pamoja ya kuishi ndani ya nchi hizo tatu, *Visa* ya pamoja ya utalii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(7) Kuandaa utaratibu wa kutumia vitambulisho vya Taifa kuwa hati ya kusafiria katika nchi zao; na

(8) Kuongeza uzalishaji na usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi orodha hiyo imechanganya mambo ya Jumuiya na yale yasiyo ya Jumuiya; ambapo mambo manne kati ya hayo manane, hayamo kwenye masharti ya kutofanyika bila ya kuihusisha au kupata ridhaa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuelekea Shirikisho la Afrika Mashariki. Katika mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 30 Aprili, 2014 pamoja na mambo mengine, kikao hicho kiliagiza Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki kuandaa Rasimu ya Katiba ya Shirikisho la Afrika Mashariki. Aidha, Baraza la Mawaziri limeelekezwa pia kutoa mwelekeo kuhusu utungwaji wa Katiba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa suala la uharakishwaji wa kuundwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki lilipata upinzani mkubwa kutoka kwa wananchi wa Tanzania wakati walipoulizwa na Kamati au Tume ya Profesa Samuel Wangwe. Kwa kuwa nchi yetu kwa sasa ipo katika mchakato wa kutunga Katiba Mpya, ni muhimu kutafakari mchakato wa Shirikisho la Afrika Mashariki katika muktadha wa mchakato wa Mabadiliko ya Katiba, Muundo wa Muungano wetu ili kutoongeza kero nyingine ya Muungano juu ya hadhi, haki na nafasi ya nchi za Tanganyika na Zanzibar katika Shirikisho la Afrika Mashariki pindi Shirikisho hilo litakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi, kwa misingi ya maamuzi ya viongozi wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, pamoja na kuwa uharakishaji wa Shirikisho la Kisiasa ulikataliwa na Nchi Wanachama; viongozi walishafanya maamuzi kwamba Shirikisho la Afrika Mashariki litaundwa; tofauti ni kuwa utangamano utafanyika hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba mwelekeo ni kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Afrika Mashariki wakati wa majumuisho kulishauri Bunge la Tanzania kukubali muundo wa Muungano wa Shirikisho la Tanzania lenye nchi za Tanganyika na Zanzibar ili iwe rahisi kwa nchi hizo mbili kujiunga na Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba, ushauri huo uzingatie maoni ya wananchi waliyoyatoa kwa Tume ya Wangwe juu ya uharakishwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki na maoni ya wananchi yaliyokusanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba; Shirikisho la Tanzania, litawezesha Watanzania na wananchi wote wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupata uzoefu wa Shirikisho ikiwa ni hatua ya kuelekea Shirikisho la Afrika Mashariki kwa mujibu wa Mkataba wa Jumuiya, itifaki na hatua mbalimbali za utangamano ambazo nchi yetu imeridhia na majadiliano yanayoendelea katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Hivyo, Kama ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikitoa kauli mbiu isemayo "*Tumethubutu na Tumeweza*" basi kwa ari hiyo hiyo, ithubutu kukubaliana na maoni ya

wananchi juu ya Muundo wa Shirikisho la Serikali tatu hapa kwetu ili iweze kuwa mfano wa kuigwa tunapoelekea katika Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha kuwa, kabla uamuzi wa mwisho wa kuunda Shirikisho la Afrika Mashariki wananchi wa Tanzania wanashirikishwa kikamilifu kupitia kura ya maoni kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafasi ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka wazi kwamba; moja ya kero za Muungano wetu, wa Tanganyika na Zanzibar, ni pamoja na ushiriki wa Zanzibar na manufaa ya ushiriki huo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imeahidi miradi mbalimbali inayotakiwa kutekelezwa huko Zanzibar lakini mpaka leo hii, miradi hiyo inasuasua. Miradi hiyo ni kama ilivyoelekezwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii mpaka sasa haina taarifa za rasmi kuhusu utekelezaji wake. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na kuitaka Serikali kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo, vinginevyo miradi hii ya muda mrefu ambayo haitekelezwi inaweza kutafsiriwa kuwa ni kero nyingine ya Muungano. Hii ni kwa sababu baadhi ya miradi inayotakiwa kushughulikiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki inahusu mambo ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto kubwa hasa kipindi hiki ambacho Jumuiya ya Afrika Mashariki inaelekea kuwa Shirikisho la Kisiasa. Suala muhimu la kujiuliza hapa ni kwamba; nafasi na hadhi ya Zanzibar itakuwaje katika Shirikisho hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kuhusu Mahakama ya Afrika Mashariki. Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 23 ya Mkataba wa Kuanzishwa kwa Afrika Mashariki wa mwaka 1999. Mahakama hiyo ilianzishwa na kuanza kufanya kazi mwaka 2001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa Majaji wanaohudumu katika Mahakama hii hufanywa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi wanaounda Jumuiya hiyo kwa mujibu wa ibara ya 24 (2). Muda wa kukaa katika mamlaka za Kijaji kwa Majaji wa Afrika Mashariki ni miaka saba kutokana na muda walioteuliwa toka kuanzishwa kwa Mahakama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa Mahakama hii, bado kuna changamoto mbalimbali zinazoikabili kama ifuatavyo:-

Mosi, Majaji wengi wapya wanaoteuliwa wanatakiwa kupatiwa mafunzo kutokana na utofauti uliopo katika mifumo ya Sheria baina ya Nchi Washirika wa Afrika Mashariki. Hii ni kwa sababu nchi za Tanzania, Kenya na Uganda zina mfumo sawa wa kisheria tofauti na nchi nyingine washirika kama vile Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majaji hawa ambao wanateuliwa wanachukua muda mrefu kupata mafunzo na hivyo wakishamaliza mafunzo hutumikia kwa muda mfupi tu katika Mahakama hizi tofauti na jinsi ilivyokuwa imekusudiwa. Hii ni kwa sababu baadhi ya Majaji inabidi wapelekwe katika mafunzo nje ya nchi ambayo wakati mwingine huchukua muda mrefu.

Pili, Majaji katika Mahakama hii hufanya kazi kwa muda mfupi na siyo moja kwa moja ofisini kama Majaji wa Mahakama za Nchi Washirika. Hii ni changamoto kubwa sana kwa uendeshaji wa Mahakama hii, kwa sababu mashauri yanaposajiliwa huwa inakuwa vigumu katika kuwapangia Majaji hao namna ya kusikiliza mashauri hayo bila kwanza kujua ratiba ya Jaji husika.

Tatu, itifaki zote mbili zinazoanzisha Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki pamoja na Soko la Pamoja zinaanzisha Mabaraza au Kamati za Usuluhishi ambazo zina hadhi sawa na Mahakama ya Afrika ya Mashariki kimamlaka. Hali hii inafanya Mahakama hii kukosa nguvu ya kiutendaji kutoa maamuzi ambayo yataendeleza ushirikiano kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu na changamoto hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhakikisha kuwa Tanzania kama Nchi Mshirika, inapeleka mapendekezo katika Kikao cha Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki *(Council of Ministers)* ili kupendekeza kwa Wakuu wa Nchi Washirika kufanyia marekebisho Mkataba wa Afrika Mashariki kwa ajili ya kuzifanyia kazi changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Afrika Mashariki ina Makao yake Makuu Jijini Arusha Tanzania. Kuna taarifa ambazo siyo rasmi kuwa zipo juhudi zinazofanywa na baadhi ya Nchi Washirika kuhamisha Makao Makuu ya Mahakama hii kwenda Jijini Nairobi nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli Bungeni pamoja na msimamo wa Serikali juu ya taarifa hizi za kuhamisha Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EALA)*. Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, pamoja na mambo mengine, lina jukumu la kutunga Sheria za Jumuiya katika mambo muhimu yaliyokubaliwa kwa mujibu wa mkataba wa Afrika Mashariki. Bunge hili kwa sasa lina Wabunge 45 ambao huchaguliwa na kila Bunge la Nchi Washirika. Kwa sasa Bunge hilo ni la tatu na lilianza kufanya kazi zake tarehe 5 Juni, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa kwenye uchaguzi wa Wabunge wa Afrika Mashariki kumekuwa na malalamiko ya namna unavyoendeshwa na kuwapata wawakilishi hao. Tatizo hili ni kubwa kwa sababu Mkataba wenyewe kupitia ibara ya 50 ndio umeyapa Mabunge ya Nchi Washirika kufanya uchaguzi wa Wabunge hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mifumo mibovu ya uchaguzi katika Mabunge ya Nchi Washirika imepelekea mara kadhaa kwa Mahakama ya Afrika Mashariki kutakiwa kutoa mwongozo juu ya namna ya kuondoa upungufu wa kiuchaguzi katika Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwa Wizara kufanya mchakato wa kupeleka mapendekezo ya namna ya kufanya uchaguzi wa Wabunge wa Afrika Mashariki ili kuwe na ushiriki mpana wa wananchi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na mfumo wa uchaguzi wa Wabunge unaowashirikisha wananchi kutalifanya Bunge la Afrika Mashariki sio tu kuwa na uhalali kwa wananchi wote lakini pia kutawafanya wananchi kuhoji na kuelewa masuala muhimu ya Jumuiya hiyo kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia kushauri kwamba, kuwe na mfumo rasmi ambao utawezesha Wabunge wa Afrika Mashariki kutoa mrejesho wa

mambo yanayoendelea katika Bunge la Afrika Mashariki na mfumo huo uwe na wigo mpana ili kuwezesha wananchi kupata taarifa hizo kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wizara, kuwataka Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kuleta taarifa ya mara kwa mara ya namna wanavyofanya kazi na pia inaitaka Wizara ieleze ni kwa namna gani wameshiriki katika kuwajengea uwezo Wabunge hao katika chombo hiki muhimu na namna wanavyohakikisha kuwa maslahi ya nchi yanazingatiwa katika mijadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kupitia vyombo vya habari umeripotiwa mgogoro katika Bunge la Afrika Mashariki ambapo baadhi ya Wabunge wa Bunge hilo wamenuia kupiga kura ya kutokuwa na imani na Spika wa Bunge lao. Hata hivyo, tarehe 9 Mei, 2014 Mahakama ya Afrika Mashariki imeamuru mchakato wa kumwondoa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki usimamishwe hadi shauri la msingi lililowasilishwa litakapoamuliwa hapo 29 Mei, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na kwa vyovyote vile na Bunge lako Tukufu halijapata kwa undani taarifa juu ya mgogoro huo ambao unaendelea katika Bunge hilo dhidi ya Spika wa Bunge hilo Bi Margareth Nantongo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia Bunge hili kutoa taarifa Bungeni kuhusu sakata hili bila kuathiri mwenendo wa kesi iliyopo katika Mahakama ya Afrika ya Mashariki ili Bunge lako Tukufu likiwa kama mojawapo ya Jimbo la Uchaguzi liweze kupewa taarifa ya kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kuhusu Ulinzi na Usalama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jumuiya Afrika Mashariki inakabiliwa na tishio kubwa sana la ugaidi. Mpaka sasa nchi za Kenya na Uganda zimeathirika kutokana na tatizo hilo. Hivi karibuni tumeshuhudia milipuko mbalimbali nchini Kenya ambapo mara zote imegharimu maisha ya watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha ulinzi na usalama ndani ya Jumuiya ni jambo muhimu sana kwa sababu hata Tanzania haipo salama kutokana na kuzungukwa na majirani ambao wanapata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ulinzi na usalama ndani ya Jumuiya linagusa pia tatizo la madawa ya kulevya ambapo nchi yetu limekuwa ni tatizo kubwa sana. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua juhudi zinazofanywa hasa baada ya kusaini Itifaki ya Ulinzi na Usalama lakini Serikali kupitia Wizara ieleze Bunge lako Tukufu ni kwa namna gani watashirikiana na Nchi Washirika chini ya mwavuli wa Itifaki hiyo kuondoa tatizo la ugaidi na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wahamiaji haramu kutoka kwa Nchi Washirika. Mwezi Agosti, 2013 Rais alipotembelea Mkoa wa Kagera alitangaza kuwaondoa wahamiaji haramu ambapo zilitolewa wiki mbili kwa ajili ya kuwaondoka kwa hiari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani haina matatizo na kuwaondoa wahamiaji haramu ndani ya nchi yetu. Wahamiaji haramu wamekuwa kichaka cha kuzagaa kwa silaha za moto, kuvamia maeneo ya nchi yetu kwa ajili ya ufugaji, kugeuza mipaka kuwa sehemu ya kuendesha biashara kwa manufaa ya nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tulionesha jinsi alama za mipaka katika mipaka yetu zilivyong'olewa na hivyo kuwa na ishara ya kuwa na migogoro ya mipaka hapo baadaye. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuwa ni lazima Serikali ihakikishe mipaka yetu ipo salama na alama hizo zinarejeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu wa kulinda mipaka yetu zaidi ya kuwa rahisi kwa wahamiaji haramu kuingia nchini pia kama nchi tunakosa mapato na usalama wa wananchi wa pembezoni unakuwa mashakani. Hata hivyo taarifa zinaonesha kuwa zoezi la kuwaondoa wahamiaji haramu lililopewa jina maarufu la Operesheni Kimbunga liligubikwa na udhaifu wa hali ya juu wa ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zoezi hilo baadhi ya watendaji wa Vijiji na Kata ambao sio waaminifu wanatuhumiwa kuchukua rushwa na hivyo kusababisha watu ambao hawana kipato kuondolewa kama wahamiaji haramu, kuteswa, kupigwa na hata wengine kubakwa. Aidha, baadhi ya Watanzania walikataliwa nchini Rwanda na Burundi kuwa sio raia na hivyo kusababisha wakose sehemu ya kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na rai ya kurudisha alama za mipakani na kuboresha ulinzi na usalama mipakani, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuharakisha zoezi la kuandikisha vitambulisho vya Taifa, kufanya tathmini ya kina ya raia walioingia nchini kabla ya uhuru na au walioingia kabla ya mwaka 1990 na ambao wamethibitika kutii sheria za nchi kupewa uraia wa kudumu. Pia wale ambao wameingia nchini baada ya 1990 na wanafanya shughuli za kiuchumi pamoja na kutii sheria za nchi wapewe hati ya ukaazi ili kuendelea kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba ushirikiano wa Afrika Mashariki utaleta manufaa ya kujenga uchumi imara na kuimarisha ulinzi madhubuti katika nchi yetu hasa kwa kipindi hiki ambapo kumekuwa na matukio mengi ya kigaidi na kiharamia katika ukanda wa Afrika Mashariki. Pamoja na umuhimu huo wa kushirikiana, ni vema Nchi Wanachama wa Jumuiya zikaheshimiana katika kutekeleza azma hiyo ya ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa ushirikiano katika Jumuiya kwa sasa hauleti matumaini sana kwa kuwa kuna dalili za baadhi ya nchi wanachama kudharau au kubeza nafasi ya nchi nyingine katika Jumuiya. Kwa sababu hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imetoa wito kwa Bunge hili kujadili hotuba ya Rais kwa Bunge aliyoitoa tarehe 7 Novemba, 2013 kuhusu mdororo wa mahusiano kwa baadhi ya Nchi Washirika, ili kutoa mapendekezo ambayo yatakuwa sehemu ya suluhisho kwa mgogoro huo baridi ili kunusuru Jumuiya kuvunjika kabla hata ya kufikia lengo la kuunda Shirikisho la kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kupongeza uteuzi wa Baraza jipya Kivuli linaloshirikisha Vyama vya *CUF*, *NCCR* na CHADEMA katika kuisimamia na kuishauri Serikali juu ya masuala mbalimbali ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, napongeza jitihada za ushirikiano wa vyama hivi nje ya Bunge kwa jina la UKAWA kwa kuendelea kuhamasisha na kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuthamini maoni ya wananchi kuhusu Rasimu ya Katiba Mpya ambayo pia itaelekeza utaratibu wa ushiriki wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, umesoma kwa muda unaotakiwa na umesoma vizuri, hongera sana.

**Taarifa ya Kambi ya Upinzani Bungeni Kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Afrika Mashariki Kama Ilivyowasilishwa Mezani**

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHE. JOSEPH ROMAN SELASINI (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFRIKA MASHARIKI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

*(Inatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2013)*

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**
Awali ya yote napenda kumshuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Kwa dhati Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe, kwa kuniteua kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wizara ya hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Nampongeza Mhe. Rukia Kassim Ahmed kwa kuteuliwa kuwa Naibu wangu. Tunaahidi kuchapa kazi kwa kadiri ya uwezo wetu ili kulinda maslahi ya taifa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**
Tanzania imekuwa ikilaumiwa sana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba inakwamisha utekelezaji wa haraka wa kuingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki kwa kuchukua muda mrefu mno wa kufanya uamuzi kuhusu masuala ya Shirikisho. Lawama hizo zilifikia hatua hata baadhi ya nchi za Jumuiya kuanza kushirikiana katika baadhi ya mambo na kuitenga Tanzania katika kile kinachoitwa "*coalition of the willing*".

**Mheshimiwa Spika,**
Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa utafiti ilioufanya na kwa kuzingatia historia ya mahusiano ya nchi za ukanda wa Afrika Mashariki, imebaini kwamba, Tanzania ndio nchi pekee katika Jumuiya hiyo yenye nia ya dhati ya kuwa katika shirikisho la kweli kuliko nchi nyingine ambazo msukumo wao wa kuingia katika Shirikisho kwa kasi, unatokana na maslahi fulani na pengine nje ya maslahi hayo nia ya kuwa katika shirikisho haipo.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwalimu Nyerere, katika kitabu chake cha Freedom and Socialism kilichochapishwa mwaka 1968 aliwahi kusema kwamba: *"It seems that there is nothing we can do in Tanzania, however reasonable and however logical, without being accused of breaking up East African Unity. ...I have often examined the list of our accusers. I am left with the strong impression that it does not consist of people who are, or have been particularly enthusiastic about East African Unity. It consists mainly of foreigners and opportunists who will today be for Federation and tomorrow against it, depending upon their personal interests rather than the interests of East Africa as a whole."*[1]

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa tafsiri isiyo rasmi, Mwalimu alisema, "Inaonekama kwamba hakuna kitu Tanzania inachoweza kufanya hata kama kiwe na maana au mantiki kiasi gani bila kushutumiwa kwamba inataka kuvunja Umoja wa Afrika Mashariki. Nimepitia mara kadhaa orodha ya wanaotushutumu. Nimebaki na ushawishi mkubwa kwamba orodha hiyo haina, wala haijawahi kuwa, na watu wenye shauku na nia ya dhati ya kudumisha Umoja wa Afrika Mashariki. Ina watu ambao wengi wao ni wageni na wasaka-fursa ambao leo wataunga mkono Shirikisho na

kesho watalipinga kulingana na maslahi yao wenyewe kuliko maslahi ya Afrika Mashariki kwa jumla".

**Mheshimiwa Spika,**
Kauli hii ya muasisi wa Taifa letu, inathibitishwa na tamko la Serikali lililotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akilihutubia Bunge tarehe 7 Novemba, 2013 kwamba, Tanzania haitajitoa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Huu ni uthibitisho kwamba Tanzania ina nia ya dhati ya kujenga na kudumisha Ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kamwe kuchelewa kwa Tanzania kuharakisha kuingia katika Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki kusichukuliwe kwamba Tanzania haitaki Shrikisho.

**2. MAUDHUI YA HOTUBA YA RAIS WA TANZANIA KUHUSU JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI.**

**Mheshimiwa Spika**,
Tarehe 7 Novemba, 2013 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alilihutubia Bunge kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo juu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na sintofahamu

iliyokuwa inaendelea. Mara baada ya hotuba hiyo kulipitishwa azimio la kumpongeza Rais na ilitolewa ahadi kwamba hotuba hiyo ingepangiwa ratiba ya kujadiliwa ahadi ambayo mpaka sasa Mwezi Mei 2014, miezi sita baadaye, haijatekelezwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka majibu yatolewe Bungeni na Waziri wa Afrika Mashariki na Spika wa Bunge juu ya sababu za hotuba hiyo kutokujadiliwa na lini hasa hotuba hiyo itajadiliwa.

**Mheshimiwa Spika,**
Kauli hizo ni muhimu zikatolewa kabla ya mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2014/2015 kuendelea kwa kuzingatia kuwa hotuba hiyo iliibua masuala muhimu ambayo ni muhimu yakatafakariwa katika muktadha wa mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Ikiwa majibu hayo hayatatolewa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa wito kwa Wabunge katika kuchangia mjadala wa Hotuba ya Waziri wa Afrika Mashariki warejee pia Hotuba ya Rais juu ya mustakabali wa Jumuiya.

**Mheshimiwa Spika,**
Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana na Hotuba ya Rais kwamba Tanzania imo, itaendelea kuwemo na haina mpango wa kujiondoa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, licha ya tofauti zilizojitokeza baina ya viongozi wetu na viongozi wa nchi za Kenya, Uganda na Rwanda. Hata hivyo, maswali ambayo Rais aliyauliza katika Hotuba yake na kueleza kukosa majibu ya kwamba, namnukuu "wanachukia nchi yetu, wanataka kuunda jumuiya yao au wananichukia mimi mwenyewe?", yanapaswa kutolewa majibu na Waziri wa Afrika Mashariki katika majumuisho ya Hotuba yake kwa kurejea yaliyojiri katika Vikao vya Jumuiya vilivyofuatia baada ya Hotuba ya Rais na mawasiliano mbalimbali ya Kiserikali kuhusu tofauti zilizojitokeza.

**Mheshimiwa Spika;**
Hotuba ya Rais juu ya kwamba viongozi wa nchi tatu walioitwa "Coalition of the Willing" wana madai ya kuwa ushirikiano wa utatu huo ni wa nchi ambazo ziko tayari kuharakisha maendeleo ya Jumuiya hiyo, pamoja na kuitwa na Rais kuwa ni ya uongo yanahitaji kutafakariwa kuiwezesha nchi kufanya maamuzi sahihi.

**Mheshimiwa Spika,**
Itakumbukwa kwamba Rais alilieleza Bunge kwamba "haiwezekani tutumie dola za marekani milioni 12 kila mwaka kuchangia jumuiya hii halafu tuidhoofishe", na kutaja kwamba

kinachoonekana kuwakera viongozi wa nchi zingine ndani ya Jumuiya hiyo, ni msimamo wa Tanzania katika kupinga kuharakisha kuundwa kwa shirikisho, hasa katika eneo la umiliki wa ardhi, uhamiaji na ajira.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana na msimamo wa kujenga Jumuiya hatua kwa hatua kama ilivyoainishwa kwenye mkataba na sio kuruka baadhi ya hatua. Hatua hizo ni Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Umoja wa Fedha na baadaye ndipo kuundwa kwa Shirikisho la Kisiasa kutakakotanguliwa na kura ya maoni ya kupitisha muundo huo wa Shirikisho. Hata hivyo, msimamo huo usitumike kama kivuli cha kuficha udhaifu wa viongozi wa nchi yetu katika kufanya maamuzi thabiti ya ndani katika kuharakisha kutekeleza miradi ya maendeleo yenye tija kwa nchi, wananchi na ukanda wa Afrika Mashariki inayotumika kama kisingizio cha kuashiria udhaifu katika utekelezaji wa utayari huo wa Tanzania katika masuala ya utangamano. Aidha, utofauti wa kimitazamo baina ya viongozi usiweke hatarini mustakabali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuepuka yaliyojitokeza mwaka 1977. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwa wabunge wa Nchi wanachama wa Afrika Mashariki na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kushirikiana kwa karibu kuzisimamia Serikali za nchi wanachama kwa niaba ya wananchi kunusuru na kudumisha uendelevu wa Shirikisho la Afrika ya Mashariki.

**Mheshimiwa Spika;**
Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu kuwa utatu ulivyoanza, Nchi za Kenya, Uganda na Rwanda walifanya vikao vitatu huko Mombasa, Kampala na Kigali ambapo pamoja na mambo mengine viongozi wa nchi za hizo waliamua mambo manane ya msingi kwa kile walichoita ni kuendeleza utangamano wa nchi hizo wanachama wa EAC. Mambo hayo ni kujenga reli ya kisasa kutoka Mombasa hadi Kampala, Kigali na Bujumbura, ujenzi wa bomba la mafuta la kutoka Kenya hadi Uganda na Sudani ya Kusini, kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta nchini Uganda, kuanzisha Himaya Moja ya Ushuru wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutekeleza vipengele vyote.

**Mheshimiwa Spika,**
Mambo Mengine ni kuharakisha Shirikisho la Afrika Mashariki ambapo waliunda kamati ya kuandaa rasimu ya Katiba ya Shirikisho, kuharakisha uanzishwaji wa hati ya pamoja ya kuishi ndani ya nchi hizo tatu, Viza ya pamoja ya utalii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuandaa utaratibu wa kutumia vitambulisho vya taifa kuwa hati ya kusafiria katika nchi zao; na kuongeza uzalishaji na usambazaji wa umeme. Ni wazi orodha hiyo imechanganya mambo ya Jumuiya na yale yasiyo ya Jumuiya; ambapo mambo manne kati ya hayo manane, hayamo kwenye masharti ya kutokufanyika bila ya kuihusisha au kupata ridhaa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,**
Mambo hayo ni uzalishaji na usambazaji wa umeme, ujenzi wa kiwanda cha kusafisha mafuta nchini Uganda, ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Kenya hadi Sudani ya Kusini na Uganda na ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Mombasa – Kampala – Kigali – Bujumbura . Masuala yasiyo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kuwa Tanzania haipaswi kuwa na mzozo nayo katika Jumuiya, lakini Bunge la Jamhuri ya Muungano linapaswa kuyahoji kuisimamia Serikali Wizara zenye dhamana ya masuala hayo zieleze Tanzania inajipangaje kimkakati juu ya masuala hayo na sababu hasa za kucheleweshwa kwa miradi ya ndani katika sekta tajwa ambayo ingeifanya Tanzania kutumia vizuri zaidi fursa yake ya kijiografia na majirani zake mbalimbali katika ukanda wa maziwa makuu.

**Mheshimiwa Spika,**

Itakumbukwa kwamba katika Hotuba yake kwa Bunge Rais alieleza kuwa kuna mambo manne yaliyosalia ambayo yaliamuliwa na kuwekewa utaratibu wake wa utekelezaji na Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo mawili hana maneno nayo. Mambo hayo ni matumizi ya vitambulisho vya taifa kama hati ya kusafiria na Visa ya Pamoja ya Utalii kwani waliamua kwa pamoja kuwa nchi wanachama zilizokuwa tayari waanze. Hata hivyo, Rais alieleza kwamba kwa upande wa kuanzishwa kwa Himaya Moja ya Ushuru wa Forodha na kuharakisha Shirikisho la Afrika Mashariki, masuala hayo makubaliano yaliyofikiwa yalikiuka uamuzi wa pamoja. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni hatua zipi zilichukuliwa toka Hotuba ya Rais mpaka sasa kuhusu ukiukwaji huo wa maamuzi ya pamoja. Kumpongeza Rais pekee kwa Hotuba yake bila kushughulikia udhaifu wa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ndani ya Nchi wanachama na ndani ya nchi yetu hakuwezi kuepusha tofauti zilizojitokeza sasa kujirudia. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka nguvu zielekezwe katika kushughulikia vyanzo vya migogoro badala ya kusubiri mpaka matokeo ya migogoro ili kuwa na utangamano endelevu.

## 3. KUELEKEA SHIRIKISHO LA AFRIKA MASHARIKI

**Mheshimiwa Spika**
Katika mkutano wa wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 30 Aprili 2014 pamoja na mambo mengine, kikao hicho kiliagiza Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki kuandaa Rasimu ya Katiba ya Shirikisho la Afrika ya Mashariki. Aidha Baraza la Mawaziri limeelekezwa pia kutoa mwelekeo kuhusu utungwaji wa Katiba hiyo.[2]

**Mheshimiwa Spika**
Ikumbukwe kuwa suala la uharakishwaji wa kuundwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki lilipata upinzani mkubwa kutoka kwa wananchi wa Tanzania wakati walipoulizwa na Kamati/
Tume ya Profesa Samuel Wangwe. Kwa kuwa nchi yetu kwa

sasa ipo katika mchakato wa kutunga Katiba Mpya ni muhimu kutafakari Mchakato wa Shirikisho la Afrika Mashariki katika muktadha wa Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba, Muundo wa Muungano wetu ili kutoongeza kero nyingine ya Muungano juu ya hadhi, haki na nafasi ya nchi za Tanganyika na Zanzibar katika Shirikisho la Afrika Mashariki pindi Shirikisho hilo litakapokamilika.

**Mheshimiwa Spika**
Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha Uongozi wetu na Hatma ya Tanzania aliandika kwamba *"Nchi mbili zinapoungana na kuwa nchi moja mifumo ya kawaida ya miundo ya katiba ni mbili: Muungano wa serikali moja au shirikisho la serikali tatu.Kwa mfumo wa kwanza kila nchi itafuta serikali yake na nchi mpya inayozaliwa itakuwa ni nchi moja yenye serikali moja. Katika mfumo wa pili kila nchi itajivua madaraka fulani ambayo yatashikwa na serikali ya shirikisho na itakuwa serikali ambayo ina mamlaka juu ya mambo yaliyobaki. Mambo yatakayoshikiliwa na serikali ya shirikisho yatakuwa ni yale ambayo yakibaki katika mamlaka ya nchi zilizoungana, basi kwa kweli nchi zitakuwa hazikuungana kuwa nchi moja ila zinaendelea kuwa nchi mbili zenye ushikiano mkubwa katika mambo fulani fulani. Nchi za Afrika mashariki zilikuwa na hali kama hiyo kabla ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Zilikuwa ni nchi tatu zenye ushirikiano mkubwa. , lakini hazikuwa nchi moja yenye serikali tatu zilizoungana kuwa nchi moja yenye muundo wa shirikisho. Shirikisho halisi la nchi mbili litakuwa ni nchi moja yenye serikali tatu, serikali ya shirikisho, na serikali mbili ya zile nchi mbili za awali zilizoungana kuzaa nchi mpya moja".*

**Mheshimiwa Spika,**

Ni wazi, kwa misingi ya maamuzi ya viongozi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, pamoja na kuwa uharakishaji wa Shirikisho la Kisiasa ulikataliwa na Nchi wanachama; viongozi walishafanya maamuzi kwamba Shirikisho la Afrika Mashariki litaundwa; tofauti ni kuwa utangamano utafanyika hatua kwa hatua.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kuzingatia kwamba mwelekeo ni kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Afrika Mashariki wakati wa majumuisho kulishauri Bunge na Taifa kukubali muundo wa Muungano wa Shirikisho la Tanzania lenye nchi za Tanganyika na Zanzibar ili iwe rahisi kwa nchi hizo mbili kujiunga na Shirikisho la Afrika Mashariki. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba ushauri huo uzingatie maoni ya wananchi waliyoyatoa kwa Tume ya Wangwe juu ya uharakishwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki na maoni ya wananchi yaliyokusanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika,**

Ni muhimu kuzingatia ushauri huu kwa kuwa hata Mwalimu Nyerere katika kitabu hicho hicho cha Uongozi wetu na Hatma ya Tanzania, aliandika, kwamba: "*Labda nivizuri kukumbusha kwamba shabaha ya baadhi yetu ilikuwa kuziunganisha nchi za Afrika Mashariki ziwe nchi moja. Na wakati Zanzibar na Tanganyika zinaungana, Kenya, Uganda na Tanganyika zilikuwa katikati ya mazungumzo ya kutafuta uwezekana wa kuungana. Kama jambo hilo lingetokea, nina hakika kabisa kwamba mfumo wa nchi mpya ambayo ingezaliwa ungekuwa ni wa shirikisho; ama shirikisho la nchi tatu au shirikisho la nchi nne zenye serikali tano. Kwa kweli hata kesho nchi za Afrika ya Mashariki zikiamua kuungana na Tanzania ikawa ni mshiriki naamini kuwa ni rahisi zaidi kushirikisha Tanzania yenye serikali mbili - ya Zanzibar na ya Tanganyika - kuliko Tanzania yenye serikali mbili ya Tanzania na ya Zanzibar*".

**Mheshimiwa Spika,**

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba; Shirikisho la Tanzania, litawezesha watanzania na wananchi wote wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupata uzoefu wa Shirikisho ikiwa ni hatua ya kuelekea Shirikisho la Afrika Mashariki kwa mujibu wa Mkataba wa Jumuiya, itifaki na hatua mbalimbali za utangamano ambazo nchi yetu imeridhia na majadiliano yanayoendelea katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivyo, Kama ambavyo Serikali hii ya CCM imekuwa ikitoa kauli mbiu isemayo ***" Tumethubutu na Tumeweza"*** basi kwa ari hiyohiyo, ithubutu kukubaliana na maoni ya wananchi juu ya Muundo wa Shirikisho la Serikali tatu hapa kwetu ili iweze kuwa mfano wa kuigwa tunapoelekea katika Shirikisho la Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha kuwa kabla uamuzi wa mwisho wa kuunda shirikisho la Afrika Mashariki wananchi wa Tanzania wanashirikishwa kikamilifu kupitia kura ya maoni kwa mujibu wa sheria.

### *3.1. Nafasi ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki*

**Mheshimiwa Spika**

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka wazi kwamba; moja ya kero za Muungano wetu (wa Tanganyika na Zanzibar) ni pamoja na ushiriki wa Zanzibar na manufaa ya ushiriki huo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**
Wizara hii imeahidi miradi mbalimbali inayotakiwa kutekelezwa huko Zanzibar lakini mpaka leo hii, miradi hiyo inasuasua. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na ifuatayo;

i. Miradi ya uchukuzi kama vile upanuzi na ukarabati wa Uwanja wa Ndege Pemba, ujenzi wa Bandari ya Maruhubi , Ujenzi wa Chelezo na kivuko kati ya Bandari ya Zanzibar, Dar es Salaam na Mombasa.

ii. Miradi ya Kilimo ambayo ilihusu kuongeza ubora wa mazao ya kilimo na miundombinu ya uvuvi bora

iii. Mradi wa Nishati kwa ajili ya ufuaji na usambazaji wa Umeme wa Upepo ili kukabiliana na upungufu wa umeme unaotokana na maji.[3]

**Mheshimiwa Spika**
Miradi hii mpaka sasa haina taarifa za rasmi kuhusu utekelezaji wake. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na kuitaka Serikali kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo, vinginevyo miradi hii ya muda mrefu ambayo haitekelezwi inaweza kutafsiriwa kuwa ni kero nyingine ya Muungano. Hii ni kwa sababu baadhi ya miradi inayotakiwa kushughulikiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki inahusu mambo ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**
Hii ni changamoto kubwa hasa kipindi hiki ambacho Jumuiya ya Afrika Mashariki inaelekea kuwa Shirikisho la Kisiasa. Suala muhimu la kujiuliza hapa ni kwamba; nafasi na hadhi ya Zanzibar itakuwaje katika shirikisho hilo?

## 4. MAHAKAMA YA AFRIKA MASHARIKI

**Mheshimiwa Spika**
Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 23 ya Mkataba wa Kuanzishwa kwa Afrika Mashariki wa mwaka 1999. Mahakama hiyo ilianzishwa na kuanza kufanya kazi mwaka 2001.

**Mheshimiwa Spika**
Uteuzi wa Majaji wanaohudumu katika Mahakama hii hufanywa na Mkutano wa wakuu wa nchi wanaounda Jumuiya hiyo kwa mujibu wa ibara ya 24 (2). Muda wa kukaa katika mamlaka za Kijaji kwa Majaji wa Afrika Mashariki ni miaka saba kutokana na muda walioteuliwa toka kuanzishwa kwa Mahakama hii.

[3]Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Afrika Mashariki ya mwaka 2011/2012

**Mheshimiwa Spika**
Pamoja na umuhimu wa Mahakama hii bado kuna changamoto mbalimbali zinazoikabili kama ifuatavyo;
Mosi, Majaji wengi wapya wanaoteuliwa wanatakiwa kupatiwa mafunzo kutokana na utofauti uliopo katika mifumo ya Sheria baina ya nchi washirika wa Afrika Mashariki. Hii ni kwa sababu nchi za Tanzania, Kenya na Uganda zina mfumo sawa wa kisheria tofauti na nchi nyingine washirika kama vile Rwanda na Burundi.

**Mheshimiwa Spika**
Majaji hawa ambao wanateuliwa wanachukua muda mrefu kupata mafunzo na hivyo wakishamaliza mafunzo hutumikia kwa muda mfupi tu katika Mahakama hizi tofauti na jinsi ilivyokuwa imekusudiwa. Hii ni kwa sababu baadhi ya Majaji inabidi wapelekwe katika mafunzo nje ya nchi ambayo wakati mwingine huchukua muda mrefu.

Pili, Majaji katika Mahakama hii hufanya kazi kwa muda mfupi na sio moja kwa moja ofisini kama Majaji wa Mahakama za nchi washirika. Hii ni changamoto kubwa sana kwa uendeshaji wa Mahakama hii, kwa sababu mashauri yanaposajiliwa huwa inakuwa vigumu katika kuwapangia Majaji hao namna ya kusikiliza mashauri hayo bila kwanza kujua ratiba ya Jaji husika.

Tatu, itifaki zote mbili zinazoanzisha Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki pamoja na na Soko la Pamoja zinaanzisha mabaraza/kamati za usuluhishi ambazo zina hadhi sawa na Mahakama ya Afrika ya Mashariki kimamlaka. Hali hii inafanya Mahakama hii kukosa nguvu ya kiutendaji kutoa maamuzi ambayo yataendeleza ushirikiano kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**
Kutokana na mapungufu na Changamoto hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhakikisha kuwa Tanzania kama nchi mshirika, inapeleka mapendekezo katika Kikao cha Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki (Council of Ministers) ili kupendekeza kwa Wakuu wa nchi washirika kufanyia marekebisho Mkataba wa Afrika Mashariki kwa ajili kuzifanyika kazi changamoto hizi.

**Mheshimiwa Spika**
Mahakama ya Afrika Mashariki ina Makao yake Makuu Jijini Arusha Tanzania. Kuna taarifa ambazo sio rasmi kuwa zipo juhudi zinazofanywa na baadhi ya nchi washirika kuhamisha Makao Makuu ya Mahakama hii kwenda Jijini Nairobi nchini Kenya.

**Mheshimiwa Spika**
Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli Bungeni pamoja na msimamo wa Serikali juu ya taarifa hizi za kuhamisha Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Mashariki.

## 5. BUNGE LA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EALA)

**Mheshimiwa Spika**
Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, pamoja na mambo mengine, lina jukumu la kutunga Sheria za Jumuiya katika mambo muhimu yaliyokubaliwa kwa mujibu wa mkataba wa Afrika Mashariki.[4] Bunge hili kwa sasa lina wabunge 45 ambao huchaguliwa na kila Bunge la nchi washirika . Kwa sasa Bunge hilo ni la tatu na lilianza kufanya kazi zake tarehe 5 Juni 2012.

**Mheshimiwa Spika**
Mara kadhaa kwenye uchaguzi wa wabunge wa Afrika Mashariki kumekuwa na malalamiko ya namna unavyoendeshwa na kuwapata wawakilishi hao. Tatizo hili ni kubwa kwa sababu Mkataba wenyewe kupitia ibara ya 50 ndio umeyapa mabunge ya nchi washirika kufanya uchaguzi wa wabunge hao.

**Mheshimiwa Spika**
Kutokana na mifumo mibovu ya uchaguzi katika mabunge ya nchi washirika imepelekea mara kadhaa kwa Mahakama

ya Afrika Mashariki kutakiwa kutoa mwongozo juu ya namna ya kuondoa mapungufu ya kiuchaguzi katika Bunge la Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**
Kambi Rasmi ya Upinzania Bungeni inapendekeza kwa Wizara kufanya mchakato wa kupeleka mapendekezo ya namna ya kufanya uchaguzi wa wabunge wa Afrika Mashariki ili kuwe na ushiriki mpana wa wananchi kuliko ilivyo sasa.

**Mheshimiwa Spika**
Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza uchaguzi wa wabunge wa Afrika Mashariki kufanywa moja kwa moja na wananchi kama mfumo wa kawaida wa kufanya uchaguzi wa Madiwani, Wabunge na Rais.

**Mheshimiwa Spika**
Mfumo huo unaopendekezwa hautakuwa mpya kwa kuwa hata Bunge la Jumuiya ya Ulaya lina mfumo wa uchaguzi ambao wabunge huchaguliwa na wananchi moja kwa moja. Kwa sasa Bunge hilo la Jumuiya ya Ulaya lina wabunge 754 ambao wanachaguliwa na kuwawakilisha wananchi takribani milioni 500[5] kutoka nchi washirika.

**Mheshimiwa Spika**
Kuwa na mfumo wa uchaguzi wa wabunge unaowashirikisha wananchi kutalifanya Bunge la Afrika Mashariki sio tu kuwa na uhalali kwa wananchi wote lakini pia kutawafanya wananchi kuhoji na kuelewa masuala muhimu ya Jumuiya hiyo kuliko ilivyo sasa.

**Mheshimiwa Spika**
Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia kushauri kwamba kuwe na mfumo rasmi ambao utawezesha wabunge wa Afrika Mashariki kutoa mrejesho wa mambo yanayoendelea katika Bunge la Afrika Mashariki na mfumo huo uwe na wigo mpana ili kuwezesha wananchi kupata taarifa hizo kwa

[5]Ruhangisa, J.E (2013) "East African Community Law" - Teaching Materia for LLM Programme, University of Dar es Salaam School of Law.

urahisi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kupitia Wizara kuwataka wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kuleta taarifa ya mara kwa mara ya namna wanavyofanya kazi na pia inaitaka Wizara ieleze ni kwa namna gani wameshiriki katika kuwajengea uwezo wabunge hao katika chombo hiki muhimu na namna wanavyohakikisha kuwa maslahi ya nchi yanazingatiwa katika mijadala.

**Mheshimiwa Spika**
Hivi karibuni kupitia vyombo vya habari umeripotiwa mgogoro katika Bunge la Afrika Mashariki ambapo baadhi ya wabunge wa Bunge hilo wamenuia kupiga kura ya kutokuwa na imani na Spika wa Bunge lao. Hata hivyo, tarehe 09 Mei 2014 Mahakama ya Afrika Mashariki imeamuru mchakato wa kumwondoa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki usimamishwe hadi shauri la msingi lililowasilishwa litakapoamuliwa hapo Mei 29 2014.

**Mheshimiwa Spika**
Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na kwa vyovyote vile na Bunge lako tukufu halijapata kwa undani taarifa juu ya mgogoro huo ambao unaendelea katika Bunge hilo dhidi ya Spika wa Bunge hilo Bi. Margareth Nantongo.

**Mheshimiwa Spika**

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia Bunge hili kutoa taarifa Bungeni kuhusu sakata hili bila kuathiri mwenendo wa kesi iliyopo katika Mahakama ya Afrika ya Mashariki ili Bunge lako tukufu likiwa kama mojawapo ya Jimbo la Uchaguzi liweze kupewa taarifa ya kinachoendelea.

**6. UWIANO WA FURSA ZA KIUCHUMI KATIKA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC) NA USHIRIKIANO WA MAENDELEO YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)**

**Mheshimiwa Spika**
Kutokana na changamoto za kiuchumi na kiusalama, mataifa mbalimbali duniani yanatafuata kuungana ili kukabiliana na changamoto hizo. Bila shaka ni kwa sababu hii, nchi yetu imejiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki na Ushirikiano wa Maendeleo wa Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)

**Mheshimiwa Spika**
Siku za hivi karibuni kumekuwa na taarifa za kutengwa kwa nchi yetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama nilivyoeleza hapo juu na sababu za kutengwa huko haziko bayana sana. Hii ni kwa sababu kauli ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Samwel Sitta wakati akijibu maswali na 25 na 26 ya Waheshimiwa wabunge Rukia Kassim na Johh Damiano Komba kuhusu kutetereka kwa uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki haikuonesha kiini hasa cha mdororo huo wa mahusiano kati ya Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**
Kauli ya Waziri ilionesha kwamba nchi nyingine wanachama wameanza kufanya mambo fulanifulani bila kuishirikisha Tanzania na kwamba Tanzania inasubiri tu kuona mwisho wao kama ambapo tumeonyesha katika taarifa hii. Hata hivyo zipo taarifa kuwa Tanzania inataka kujitoa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuendelea na Ushirikiano wa SADC.

**Mheshimiwa Spika**
Mheshimiwa Spika, wahenga walisema: "*Mshika Mawili Moja Humponyoka*" ni wakati mwafaka sasa kwa Tanzania kuchagua moja; ama kuendelea na Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuachana na SADC ama kuendelea na SADC na kuachana na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**
Katika kuchagua huko, ni lazima kufanya utafiti na kuona ni wapi ambapo Taifa litanufaika zaidi kiuchumi. Kwa taarifa tu ni kwamba mwenendo wa kibiashara wa Tanzania (kwa maana ya kuuza na kununua bidhaa) katika nchi kumi ambazo tunanunua bidhaa duniani, Kenya ni nchi ya 8 na katika nchi kumi za ambazo tunauza bidhaa katika bara la Afrika, Kenya ni nchi ya pili. Takwimu hizi ni kwa mujibu wa Ripoti ya Uchumi ya Benki Kuu ya Tanzania ya 2012. Aidha maingiliano ya kibiashara ya wananchi wa Tanzania katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni makubwa zaidi kuliko maingiliano na nchi za SADC. Hili linatokana na takwimu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zinaonesha kuwa Tanzania inafanya biashara zaidi na nchi za Kenya na Uganda.

**Mheshimiwa Spika**
Utangamano wa Afrika Mashariki umekua tofauti na Ushirikiano na nchi za SADC. Wananchi wa nchi washirika wamekuwa na ushirikiano mkubwa katika nchi zetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kama ambavyo azma yake ilisemwa na Rais ndani ya Bunge lako tukufu kuhakikisha kuwa tofauti za baadhi ya nchi washirika zipate ufumbuzi ili kuendelea kuboresha mahusiano ya nchi hizi.

**Mheshimiwa Spika**
Katika zama hizi za utandawazi na soko huria, kujiweka kando katika ushirikiano hasa wa kibiashara, ni kutafuta ulemavu wa kudumu katika uchumi. Kambi Rasmi ya Upinzania haiamini kama wanadiplomasia wetu na hasa mabalozi wetu wameshindwa kutafuta suluhu ili ushirikiano wetu na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki utengamae na kuleta matunda yaliyokusudiwa. Hata hivyo, kuchelewa sana katika kushughulikia jambo hili hakuwezi kuwa mojawapo ya suluhu maana wenzetu wanazidi kusonga mbele.

**Mheshimiwa Spika**
Wahenga walisema "Fimbo ya Mbali Haiuwi Nyoka" Nina maana kwamba mashirikiano yetu na mataifa makubwa yenye nguvu duniani yasitufanye tudharau ushirikiano na majirani zetu. Ikumbukwe kwamba ushirikiano mzuri na majirani zetu licha tu ya kuleta manufaa ya kiuchumi lakini pia ni nyenzo mojawapo ya kudumisha amani tuliyonayo.

**Mheshimiwa Spika**
Kambi Rasmi ya Upinzania inasisitiza kuwa kama Serikali haitaona umuhimu wa kutafuta chanzo cha mgogoro uliopo kati ya Tanzania na baadhi ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, basi Kambi Rasmi kupitia viongozi wake itachukua jukumu la kuonana na viongozi wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kujua tatizo ni nini ili iweze kuishauri Serikali ipasavyo kwa hatua za kutafuta suluhu.

**7. ULINZI NA USALAMA KATIKA JUMUIYA**

**Mheshimiwa Spika**
Jumuiya Afrika Mashariki inakabiliwa na tishio kubwa sana la ugaidi. Mpaka sasa nchi za Kenya na Uganda zimeathirika kutokana na tatizo hilo. Hivi karibuni tumeshuhudia milipuko mbalimbali nchini Kenya ambapo mara zote imegaharimu maisha ya watu wengi.

**Mheshimiwa Spika**
Kuimarisha Ulinzi na Usalama ndani ya Jumuiya ni jambo muhimu sana kwa sababu hata Tanzania haipo salama kutokana na kuzungukwa kwa na majirani ambao wanapata matatizo makubwa sana.

**Mheshimiwa Spika**
Tatizo la ulinzi na usalama ndani ya Jumuiya linagusa pia tatizo la madawa ya kulevya ambapo nchi yetu limekuwa ni tatizo kubwa sana. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua juhudi zilizofanywa hasa baada a kusaini itifaki ya Ulinzi na Usalama lakini serikali kupitia Wizara ieleze Bunge lako tukufu ni kwa namna gani watashirikiana na nchi washirika chini ya mwavuli wa itifaki hiyo kuondoa tatizo la ugaidi na madawa ya kulevya.

**8. WAHAMIAJI HARAMU KUTOKA KWA NCHI WASHIRIKA**

**Mheshimiwa Spika**
Mwezi Agosti, 2013 Rais alipotembelea Mkoa wa Kagera alitangaza kuwaondoa wahamiaji haramu ambapo zilitolewa wiki mbili kwa ajili ya kuondoka kwa hiari.

**Mheshimiwa Spika**
Kambi Rasmi ya Upinzani haina matatizo na kuwaondoa wahamiaji haramu ndani ya nchi yetu. Wahamiaji haramu wamekuwa kichaka cha kuzagaa kwa silaha za moto, kuvamia maeneo ya nchi yetu kwa ajili ya ufugaji, kugeuza mipaka kuwa sehemu ya kuendesha biashara kwa manufaa ya nchi jirani.

**Mheshimiwa Spika**
Katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tulionyesha jinsi alama za mipaka katika mipaka yetu zilivyong'olewa na hivyo kuwa na ishara ya kuwa na migogoro ya mipaka hapo baadae. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuwa ni lazima serikali ihakikishe mipaka yetu ipo salama na alama hizo zinarejeshwa.

**Mheshimiwa Spika**
Udhaifu wa kulinda mipaka yetu zaidi ya kuwa rahisi kwa wahamiaji haramu kuingia nchini pia kama nchi tunakosa mapato na usalama wa wananchi wa pembezoni unakuwa mashakani. Hata hivyo taarifa zinaonesha kuwa zoezi la kuwaondoa wahamiaji haramu lililopewa jina maarufu la Operesheni Kimbunga liligubikwa na udhaifu wa hali ya juu wa ukiukwaji wa haki za binadamu.

**Mheshimiwa Spika**
Katika zoezi hilo baadhi ya watendaji wa Vijiji na Kata ambao sio waaminifu wanatuhumiwa kuchukua rushwa na hivyo kusababisha watu ambao hawana kipatokuondolewa kama wahamiaji haramu, kuteswa, kupigwa na hata wengine kubakwa. Aidha baadhi ya watanzania walikataliwa nchini Rwanda na Burundi kuwa sio raia na hivyo kusababisha wakose sehemu ya kwenda.

**Mheshimiwa Spika**
Pamoja na rai ya kurudisha alama za mipakani na kuboresha ulinzi na usalama mipakani, Kambi ya Upinzani inaitaka serikali kuharakisha zoezi la kuandikisha vitambulisho vya taifa, kufanya tathmini ya kina ya raia walioingia nchini kabla ya uhuru na au waliongia kabla ya mwaka 1990 na ambao wamethibitika kutii sheria za nchi kupewa uraia wa kudumu. Na pia wale ambao wameingia nchini baada ya 1990 na wanafanya shughuli za kiuchumi pamoja na kutii sheria za nchi wapewe hati ya ukaazi ili kuendelea kulitumikia taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**
Wahamiaji wenye rekodi mbaya ikiwa ni pamoja na tuhuma za makosa ya jinai waondolewe nchini. Matatizo na udhaifu uliojitokeza katika Opersheni Kimbunga yafanyiwe kazi na pia serikali kupitia Wizara hii ihakikishe kuwa kabla ya kutumia nguvu katika masuala ambayo yanaweza kuleta mgogoro kwa nchi washirika itumie msingi wa kusuluhisha migogoro kwa njia ya majadiliano na ujirani mwema kama Mkataba wa Afrika Mashariki unavyotaka.[6]

## 9. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**
Ni dhahiri kwamba ushirikiano wa Afrika Mashariki utaleta manufaa ya kujenga uchumi imara na kuimarisha ulinzi madhubuti katika nchi yetu hasa kwa kipindi hiki ambapo kumekuwa na matukio mengi ya kigaidi na kiharamia katika ukanda wa Afrika Mashariki. Pamoja na umuhimu huo wa kushirikiana, ni vema nchi wanachama wa Jumuiya zikaheshimiana katika kutekeleza azma hiyo ya ushirikiano.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwenendo wa Ushirikiano katika Jumuiya kwa sasa hauleti matumaini sana kwa kuwa kuna dalili za baadhi ya nchi wanachama kudharau au kubeza nafasi ya nchi nyingine katika Jumuiya. Ni kwa sababu hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imetoa wito kwa Bunge hili kujadili hotuba ya Rais kwa Bunge aliyoitoa tarehe 7 Novemba,2013 kuhusu mdororo wa mahusiano

kwa baadhi ya nchi washirika, ili kutoa mapendekezo ambayo yatakuwa sehemu ya suluhisho kwa mgogoro huo baridi ili kunusuru Jumuiya kuvunjika kabla hata ya kufikia lengo la kuunda Shirikisho la kisiasa.

[6]Ibara 6 (b)(c)

**Mheshimiwa Spika,**
Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri pia Serikali kuchagua kujiunga katika Jumuiya moja kati ya SADC na EAC ili kuweza kuwa na tija katika mashirikiano hayo na kunufaika ipasavyo na mashirikiano hayo.

**Mheshimiwa Spika,**
Namalizia kwa kupongeza uteuzi wa Baraza Jipya Kivuli linaloshirikisha vyama vya CUF, NCCR na CHADEMA katika kuisimamia na kuishauri Serikali juu ya masuala mbalimbali ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, napongeza jitihada za ushirikiano wa vyama hivi nje ya Bunge kwa jina la UKAWA kwa kuendelea kuhamasisha na kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuthamini maoni ya wananchi kuhusu Rasimu ya Katiba Mpya ambayo pia itaelekeza utaratibu wa ushiriki wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

Joseph Roman Selasini (Mb)
**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI NA**
**WAZIRI KIVULI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**
22 Mei, 2014

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya wachangiaji. Kwenye Wizara hii wachangiaji siyo wengi sana, kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri mjiandae ku-*wind up* mapema sana.

Mchangiaji wa kwanza ni Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa ajiandae.

**MHE. MOHAMMED SEIF KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia asubuhi ya leo na kuwa mchangiaji wa mwanzo. Pia hii ni Wizara ya kwanza kwangu mimi kuchangia katika Bunge hili la Bajeti. Naunga mkono kwa asilimia mia moja kwa sababu Wizara hii inaendeleza dhamira njema ya viongozi wetu waasisi wa Taifa hili, Abeid Amani Karume na Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inafanya kazi ile ambayo ilianzishwa na vuguvugu la *Pan-Africanism* na vuguvugu la Jumuiya ya *PAFMECA* hapa Tanzania na Afrika Mashariki; kwa sababu hiyo ndiyo maana naunga mkono mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba, madhumuni ya kuwepo kwa *PAFMECA* ilikuwa kwanza kuwaunganisha Waafrika wa nchi wanachama. La pili, kuunda Vyama vya Siasa ambavyo vitasaidia kukomboa nchi zetu. La tatu, kujenga mshikamano wa Vyama vya Siasa vya nchi jirani na nne kuleta muungano baada ya nchi kuwa huru. Kwa hiyo, naamini kwamba mchakato huu utafanikisha hayo ambayo yameanzishwa na *PAFMECA* na pia kuanzishwa na wazee wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe kwamba viongozi wetu *TANU* Julius Kambarage Nyerere na Karume wa *ASP* walishiriki kikamilifu katika shughuli na harakati za kuunda *Pan-Africanism* na kuunda *PAFMECA*. Upo ushahidi wa kutosha kwamba wao walishiriki katika kuunda, kushiriki na kusaidia chombo hiki cha *PAFMECA* ambacho ndicho kilichokuwa muhimu sana wakati ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mikutano mingi ya *PAFMECA* katika Afrika Mashariki. Wa kwanza ulifanyika Mwanza, Mei mwaka 58. Wa pili ulifanyika Zanzibar Aprili mwaka 57. Wa tatu ulifanyika Mbale, Uganda mwaka 57. Wa nne ulifanyika Moshi mwaka 1960. Kwa hiyo mikutano yote hii ilikuwa inashirikisha viongozi wetu wa *TANU* na *ASP* na Abeid Amani Karume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu ninukuu maelezo ya Thabit Kombo mmoja wa waasisi hao kuhusu mkutano wa Mwanza kwamba *ASP* ilialikwa na *TANU* na Kambarage Nyerere. Mimi mwenyewe nilipokea mwaliko kutoka kwa Mwalimu Nyerere, nilipata barua kuomba *Afro Shiraz Party* kuhudhuria mkutano huo mwaka huo, mkutano wa mwanzo wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye mkutano wa Zanzibar, Thabit Kombo anasema hivi, kutoka Tanganyika alikuja Mwalimu Nyerere, Jeremia Bagabenja na Edward Barongo. Kwa hiyo, kwa ushahidi huu ni kwamba, kulikuwa na ushirikiano wa karibu sana wa Vyama vya *TANU* na *ASP* na viongozi wetu wakubwa wa Taifa letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niseme kwamba Mkutano uliofanyika kule Ghana mwaka 58, mkutano muhimu sana huo wa nchi za Kiafrika, ulihudhuriwa na viongozi wa *TANU* na *ASP* na kiongozi wa *ASP*, Abeid Amani Karume alihudhuria. Aliporejea kutoka Ghana mwaka 58 alifanya mkutano kwenye Jimbo langu ambalo linaitwa Ghana kwa sababu jina hili lilipewa na yeye mwenyewe, ukaimbwa wimbo Abeid Amani karudi Ghana kavaa pakacha mchana. Kwa hiyo ni wazi kwamba kulikuwa na ushirikiano wa karibu sana sana kati ya Watanganyika na Wazanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi CCM tunakubaliana na mawazo ya *TANU* na *ASP*, lakini *TANU* na *ASP* ndio waliokuwa mfano mzuri wa kufanya kazi ya kuunganisha Waafrika wa nchi zao na pia Waafrika wa Afrika Mashariki. Mwaka 57 kule Zanzibar kuliundwa Chama cha *ASP*, chama hiki kiliunganisha watu wa Tanganyika na watu wa Zanzibar wanaoishi Zanzibar. Huo ulikuwa ni muungano wa kwanza wa Watanganyika na Wazanzibari ndani ya Zanzibar yenyewe; lakini bahati nzuri wakati chama hiki kinaundwa Kambarage Nyerere alikuwepo, alishuhudia mchakato huo wa pole pole wa kukamilisha ile *Pan-Africanism* na pia *PAFMECA* kuunganisha Waafrika wa Tanganyika na Zanzibar.

Mwaka 1964, Mapinduzi ya Zanzibar yalifanywa na Watanganyika na Wazanzibar wanaoishi Zanzibar. Mwaka 1964, Muungano umeletwa na Watanganyika na Wazanzibari; lakini pia mwaka 1977 Chama cha *ASP* na TANU waliunda CCM kuunganisha Watanganyika na Wazanzibari. Mwaka 1992 kulipoanzishwa Vyama vingi vya Siasa viliwalazimisha lazima Vyama vya Siasa viwe na uongozi bara na visiwani. Kwa hiyo, yote haya ni kwamba wanatekeleza azma ya *Pan-Africanism* na Azma ya *PAFMECA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nini ujumbe wangu. Karume na Nyerere hawajakutana barabarani, walikutana katika harakati za kudai uhuru kwa miaka nenda miaka rudi. La pili, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar haukuja kwa bahati, ulikuwa na malengo na dhamira ya *Pan-Africanism* na *PAFMECA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, ajiandae Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi kuchangia katika Wizara hii muhimu sana katika nchi yetu. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na matatizo mengi wanayokabiliana nayo. Kwa kweli wanaibeba vizuri sana Bendera ya nchi yetu katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze mambo machache. Kwanza, nataka nizungumze suala zima la biashara katika Afrika Mashariki. Ni vizuri basi tukaelezwa hapa, toka tumeanza huu ushuru wa forodha kuwa ni mmoja mpaka hatua hii tuliyonayo nchi yetu imeweza kuuza bidhaa kiasi gani katika soko hili la Afrika ya Mashariki, kwa maana ukitazama nje nje unaona labda sisi wenyewe ndio tunakuwa soko la wenzetu kama Kenya na wengine, lakini je sisi katika soko hilo tumeuza nini, Watanzania wameshiriki vipi, ni vizuri wakaelezwa kwa sababu vinginevyo inaweza ikachukuliwa kijuu juu tu watu wasijue nini kinafanyika. Ningeomba watakapokuja watueleze hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni suala la miradi. Miradi ipo mingi na inakabiliwa na changamoto nyingi. Nimewahi kusikia, hasa ile miradi inayokuja kule kwetu Zanzibar, kuna vitu ambavyo wakati mwingine vinakwamisha kwa sababu inawezekana mradi unatoka nje, lakini unatakiwa kuwa angalau *feasibility study* ichangiwe na Serikali husika. Sasa kwa uchache wa fedha na mambo mengine utakuta miradi hii inakwama. Hata hivyo, ninaloomba, angalau basi wangechagua miradi ambayo italeta *impact* kubwa katika maisha ya watu. Labda niseme mfano hai ni mradi wa Bandari ambao nimekuwa nikiuomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Pemba, ni vizuri sana kama Mheshimiwa Wazri na wenzake wote wakasaidia ile Bandari ya Wete kupata mfadhili na kujengwa, kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza pale Wete ni karibu sana na Kenya, ni rahisi kama bandari ile itakuwa kubwa, meli kuja pale na kuweza kuchukua bidhaa na kuzipeleka Kenya. Watu wa Pemba wanazalisha bidhaa nyingi sana, viungo mbalimbali, bidhaa za kilimo na mambo mengine ambayo nina hakika wenzetu wanayahitaji katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mradi huu wa Bandari ya Wete waupiganie kwa sababu tumeshausemea sana, lakini mpaka sasa Serikali iko kimya. Inawezekana kuna masuala ya kiufundi wanahitaji basi kutuambia ili tuchukue hatua na bandari hii ijengwe. Si tu iweze kuwasaidia watu wanaoishi katika Kisiwa cha Pemba, lakini pia itaweza kuonesha au kujenga uhusiano mzuri wa kibiashara baina ya sisi na majirani zetu hasa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ningependa nizungumzie suala la bajeti. Wizara hii inasikitisha sana kwa sababu ukiitazama unahisi ni Wizara ambayo ina majukumu makubwa ya kuwaunganisha watu wa Afrika ya Mashariki kwa upande wetu, yaani wanapaswa kufanya mambo mengi, lakini fedha wanazopewa, kwanza ni kidogo sana, lakini hata ule mgawo wenyewe wa kufika katika Wizara yao kama zilivyo Wizara nyingine bado kuna tatizo. Sasa napenda niulize, leo Watanzania wali wengi sana hawaelewi ni nini kinafanyika katika Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu hawa wangekuwa na jukumu basi kama wangekuwa wamewezeshwa kifedha angalau kufanya semina mbalimbali katika mikoa, katika Bunge, katika Baraza la Wawakilishi na katika maeneo mbalimbali ambayo wananchi wangeweza kuelezwa hatua mbalimbali zinazoendelea katika suala zima la ushirikiano wa Afrika Mashariki,

lakini ukienda huko nje watu wanakuuliza nini kinafanyika hawajui. Hawajui kwa sababu Wizara yenye jukumu la kuwajulisha na kuwaelimisha hawapewi uwezo wa kifedha na Serikali. Sasa, unapompa mtu jukumu halafu humwezeshi inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, hata hizo *OC* ambazo walipaswa wapewe kwa wakati hazifiki kwa wakati na hawa wana majukumu mengi. Wanatakiwa washiriki kwenye Bunge lenyewe, wanatakiwa kwenye ziara mbalimbali. Pamoja na hizo shughuli za Kibunge labda zinagharamiwa kwa pamoja lakini kama watendaji wetu, kama mabalozi wetu kwenye Jumuiya hii wanahitaji kufanya kazi nyingi ambazo zote zinahitaji fedha. Nadhani bilioni ishirini, bilioni thelathini kwa Wizara kama hii ambayo ni Wizara nzima pesa hizo ni *sub-component* tu ya baadhi ya Wizara nyingine. Sasa tunaundaje Wizara, lakini kumbe hatujawa tayari kuiwezesha! Hili ni jambo linalosikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wenzangu wengi wameshasema katika hotuba mbalimbali zilizopita. Sisi kama Zanzibar, nahisi tunahitaji kushirikishwa sana katika jambo hili, kwa sababu kuna mambo ambayo naamini ni ya Zanzibar peke yake si ya Muungano. Sasa yale Zanzibar yenyewe inashiriki vipi katika jumuiya hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Naibu Waziri anatoka Zanzibar, lakini pale akiwapo yeye ni Naibu Waziri wa Afrika ya Mashariki, lakini je Serikali ya Zanzibar yenyewe inashirikishwa vipi? Ni vizuri wenzetu hawa wakija hapa wakatoa maelezo kwa sababu hii inaweza kusaidia kufuta fikra za watu za kuona kuwa labda Zanzibar haishirikishwi, pengine hata mimi nina wasiwasi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana mkatupa maelezo ambayo watu wataweza kuelewa Serikali ya Zanzibar au Wazanzibari wanashirikishwa vipi katika suala zima la muungano huu wa Afrika ya Mashariki. Vinginevyo, tutaendelea kuona kuwa labda kuna tatizo, lakini pengine halipo na kama lipo litakuwa lipo, basi ni vizuri mkatoa ufafanuzi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nataka nizungumzie, kidogo nitaje tu; nimeona leo Wabunge wa Afrika ya Mashariki, wapo hapa. Unajua sisi Wabunge wa Majimbo tukienda kwetu wanasema jamaa huyu hajapita miaka miwili hapa, pengine ulipita miezi miwili tu iliyopita, basi na wao si vibaya wakawa wanakuja kwenye Jimbo lao, angalau kwa kusalimiana tu pale kwenye chai basi wanaondoka, wala si lazima wafanye kitu kikubwa, lakini wanakaa hawaonekani mpaka leo kwenye bajeti. Nawaomba waje kwa sababu hili si ndilo Jimbo lenyewe, ndio wapiga kura sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, amelisema hapa mwakilishi wa Kambi ya Upinzani. Tunahitaji, nafikiri lazima iandaliwe *mode* ya namna gani mrejesho wa kazi zinazofanyika katika Bunge la Afrika ya Mashariki zitafika angalau hapa Bungeni watu wakaelewa, lakini mfumo tulionao sasa, ambao inabidi Wabunge wale au Wizara itoe *briefing* kwenye Kamati ya Mambo ya Nje kwa uchache tu, Wabunge hawana nafasi kubwa ya kuelewa kwa sababu Bunge lile ni *Legislative*, linatunga sheria mbalimbali, je Wabunge hawa na wananchi wanajua ni sheria gani imetungwa? Hawajui kwa urahisi.

Sasa ni vizuri ikaandaliwa namna ambapo Bunge litakuwa linapata mrejesho wa kazi zinazofanyika angalau mara mbili kwa mwaka; hii itasaidia kujenga weledi wa Waheshimiwa Wabunge juu ya kazi zinazofanyika katika Bunge la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nafikiri Wabunge wa Afrika Mashariki mmesikiliza na Mwenyekiti wenu, Mheshimiwa Kimbisa; basi mje mpite pite hasa kipindi cha chai pale ili tukumbuke tuko na ninyi. Sasa namwita Mheshimiwa Raya na ajiandae Mheshimiwa Anastazia.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Wizara hii ya Afrika ya Mashariki. Katika mchango wangu nisingekuwa na mengi ya kueleza zaidi ya mengi ya kutaka ufafanuzi na maelekezo ambayo Wizara inayashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ningependa kuipongeza hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo imesomwa na Mheshimiwa Selasini, kwa kweli ina mambo mazito na tunaomba Wizara iyafanyie kazi na katika majibu ituridhishe tuone ni jinsi gani Wizara hii inafanya kazi na Watanzania wajue nini kinaendelea katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia suala zima la ushirikishwaji wa Wazanzibari katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ambavyo kwa utangulizi Mheshimiwa Khalifa amelizungumzia, lakini pia ningependa kulielezea zaidi. Mfano, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Zanzibar inashirikishwa vipi ama inahusishwa vipi katika mambo ambayo si ya kimuungano, hususan katika Wizara ambazo si za kimuungano, mfano, Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye mambo ya biashara na viwanda Zanzibar kama Zanzibar suala hili halipo katika mambo ya Muungano. Kwa hiyo, tungependa Mheshimiwa Waziri akija ku-*wind-up* hapa atuambie ni kwa namna gani ama kwa kiasi gani Wazanzibari ama Serikali ya Zanzibar inashirikishwa katika Shirikisho la Afrika Mashariki kuhusiana na Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa kuzungumzia kutoka katika Wizara ya Chakula na Kilimo kwa upande wa Zanzibar. Tunajua kwamba zao kuu la Zanzibar ni karafuu, na tunajua kwamba Waunguja na Wapemba kwa ujumla wanalima sana karafuu na wanapata pato kubwa kutokana na zao hili, lakini pia katika biashara yake ama uuzwaji wake karafuu inauzwa sana Kenya. Tunataka kujua wananufaika vipi kutoka katika Jumuiya, faida zinazotokana na zao hili la karafuu hususan kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula kutoka katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa kuzungumzia vikwazo vya kibiashara. Vikwazo vilivyopo katika biashara ndani ya Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, tunaona kwamba kuna vikwazo vingi vinavyowapata wafanyabiashara hususan wanavyotoa na kuingiza ndani ya nchi yetu. Yaani kutokana na vikwazo hivi, aidha mipakani ama hata barabarani ukiwa ndani ya nchi, Jumuiya moja unakwenda katika nchi nyingine ya Jumuiya kuna vikwazo vingi barabarani ambavyo vinapelekea ku-*delay* ama kudorora kwa uchumi kutokana na zile biashara ama mizigo ambayo inategemewa kwenda upande mwingine kutofika kwa wakati wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ningependa kutoa ushauri, ningependa Wizara izingatie ushauri wangu. Ni kwamba, kwa nini sasa kila nchi katika Jumuiya ambayo tunajua inatoa biashara upande mmoja kwenda upande mwingine, kuwe kuna kituo kimoja ambapo mzigo ule unapotoka katika kituo cha nchi ile ukaguliwe mara moja na uruhusiwe kupita. Aidha, labda mpaka mpakani pale ukaguliwe tena ama na Nchi Mwanachama nyingine ambapo unakwenda, ukaguliwe tena kwa mara nyingine. Nadhani njia hii itarahisisha zaidi kutokuchukua muda mrefu kwa bidhaa zikiwa barabarani kuliko huu utaratibu ambao tunaufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile pia mipakani waangaliwe sana hawa watu ambao wanapeleka uchumi nchi nyingine ama wanatoa biashara na ambao wanaingiza biashara; wenzetu wanaita *importation and exportation* watazamwe zaidi kwa ajili ya shughuli za uingizaji na utoaji wa kibiashara.

Masuala tu ya ufahamu ambapo tungependa kujua. Kwenye hotuba ya Kambi imezungumziwa, *issue* ya Spika wa Bunge la Afrika Mashariki. Tunaona tu kwenye vyombo vya habari, tunasikia na baadhi ya wengine nadhani hata hawajasikia au hawajaona, kwamba *issue* ya Spika, Bunge kuahirishwa kwa muda ambao hautajulikana. Tunataka tujue, nini kinaendelea, Wizara itujulishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri haya yanatokea ni kwa kutokana na kutokuwa na mrejesho wa nini kinafanyika katika Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambalo hatuletewi mrejesho kama Wabunge, hatujui nini kinaendelea, zaidi tu ya kusikia kwenye vyombo vya habari ama usikie kwa watu wengine huko. Wabunge kama Wabunge ambao ndio Jimbo na Bunge kwa ujumla, ndilo Jimbo la Wabunge wetu wa Afrika ya Mashariki, wanakwenda kutuwakilisha katika nchi za Jumuiya za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasikitika kwamba tunapata tu taarifa; tunasikia, anatokea tu mtu anakuuliza unashindwa kutoa ufafanuzi mzuri ni nini kinaendelea kuhusiana na Bunge letu la Afrika ya Mashariki. Kwa hiyo, tungependa kujua nini kinachoendelea katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna suala lingine la mgongano ama mgogoro kati ya Rais wetu na Rais Kagame. Tunataka kujua, ni hatua gani Jumuiya imechukua, ama Tanzania imechukua kutokana na migogoro ya viongozi hawa katika masuala mazima ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara mtufahamishe, Waziri ukija ku-*wind up* atufahamishe ni hatua gani, ni mambo gani kama Tanzania tumefanya katika huu mgogoro kati ya Kagame na Rais Kikwete ambao unaendelea. Tunataka kujua nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa kujua lini Tanzania, yaani katika hilo suala la Kagame na Mheshimiwa Kikwete, Tanzania lini imepeleka hoja, ama ina utaratibu gani, imefanya nini, ama hoja na ni kitu gani, ambacho kimepelekwa kwenye Bunge la Afrika ya Mashariki hoja yoyote, kuhusiana na hili suala la kuundwa kwa Jumuiya ndani ya Jumuiya. Tunaona kwamba Tanzania inaelekea kutengwa. Kwa hiyo kuna utaratibu ambao unafanyika, wanaunda Jumuiya ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, tungependa kujua Tanzania kama Tanzania, inasema nini na imechukua hatua gani katika suala hili kuona kwamba tuimarishe na kudumisha zaidi ushirikiano, yaani ushirikiano ambao tuko nao wa Nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anastazia Wambura, ajiandae Mheshimiwa Waride Bakari Jabu!

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niwe miongoni mwa wachangiaji wachache katika Wizara hii ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai ambayo amenijali. Pia niwapongeze sana viongozi wa nchi za Afrika ya Mashariki, kwa

kutuunga mkono katika maadhimisho ya miaka hamsini ya Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi hawa wameonesha moyo wa mshikamano, lakini pia naomba wawe ni mfano wa kuigwa karika Bara la Afrika, kwa sababu wametekeleza vizuri sana hii kauli yetu mbiu ya *One People, One Destiny*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau nianze tena kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Napenda niipongeze sana nchi yetu ya Tanzania kwa kufanya vizuri katika *export* kwa mwaka 2005 – 2010. Hii inajionesha wazi katika tathmini ya mpango wa maendeleo wa Afrika ya Mashariki wa 2005/2006 na 2010/2011. Kwamba katika mwaka 2005 *Export Share per GDP* ziliongezeka kutoka asilimia 11.9 hadi asilimia 18.4 mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tathimini hii tunaambiwa bado upo uwezo mkubwa sana wa kuongeza hizi *export shares.* Tutaongeza kama tutaimarisha sera ya uongezaji thamani na vile vile kama tutawekeza katika sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Watanzania wenzangu tuwekeze sana katika sayansi na teknolojia. Nitoe mfano mdogo tu kwamba, Tanzania inasemwa sana kwamba ina-*export* chumvi katika nchi za Afrika ya Mashariki, hasa hasa katika Kenya, lakini utakuta kwamba chumvi tunayotumia nyingi inatoka Mombasa na nyingine inatoka katika nchi nyingine. Huu ni udhaifu mkubwa ambao unajitokeza katika uongezaji wa thamani ya bidhaa zetu. Naamini kabisa kwamba tukiongeza thamani katika chumvi yetu tunaweza tukaongeza *export shares* katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie utafiti katika Wizara hii. Suala la Utafiti ni la msingi sana katika utekelezaji wa mambo mengi, au katika utekelezaji wa mpango mzima wa maendeleo ya Afrika Mashariki. Wizara imetuambia kwamba imeshapeleka maombi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui ni kengele.

**MWENYEKITI:** *(Hakusikika)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi ili kusudi kupata kibali cha uanzishwaji wa Idara ya Utafiti. Naomba lifanyike hilo. Naiomba sana Ofisi hii ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ilifanyie kazi suala hili, itoe kibali mapema ili kuiwezesha Wizara hii, ianzishe Idara ya Utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu tathimini ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Afrika Mashariki, inasema kwamba utafiti mdogo ikiwa ni pamoja na utafiti usiounganifu, ni moja ya changamoto katika sekta ya utalii na sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu inategemea sana *export* za mazao ya kilimo. Nadhani na naamini kabisa ikianzishwa Idara ya Utafiti, itasaidia sana katika maeneo ya kilimo. Eneo la kwanza ambalo linaweza likasaidia, tunaambiwa kwamba nchi ya Kenya, ina tija katika mazao ya mbogamboga na matunda mara kumi zaidi ya Tanzania. Sasa je, ni kwa nini tija hii iwe mara kumi zaidi ya nchi yetu. Inaweza ikatusaidia sana ili na sisi tuweze kuongeza tija. Ukiangalia pia tunasafirisha sana mahindi nje. Tunapeleka Kenya na nchi nyingine za Afrika Mashariki, lakini je, tunaweza tukaongeza tija hii mara kumi au zaidi? Vile vile tuna fursa za *SAGCOT,* je, tunaweza tukatumia vipi fursa hii ya *SAGCOT,* katika soko la Afrika ya Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ajira pia. Utafiti ufanyike kujua ni vijana wangapi wa Tanzania ambao wanaajiriwa katika Soko la Afrika Mashariki. Je, utendaji wao ukoje na wale wenye sifa ambao hawakuajiriwa, ni kwa nini hawaajiriwi katika soko la Afrika ya Mashariki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja pia kwenye suala la biashara, wanalalamika sana wafanyabiashara wetu kuna *non-tariff barriers*. Utafiti ufanyike wa kina kwamba hizi *non-tariff barriers* ni zipi na ni nani yuko *genuine,* je, ni wale wanaoziweka au ni wafanyabiashara wetu wanaojisababishia *barriers?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo ningependa kuongelea ni suala la fedha. Naomba sana, huu mtindo wa kutoa fedha nusu nusu uachwe. Fedha zitakazoidhinishwa katika Bajeti hii ya Afrika Mashariki, naomba zitolewe zote. Zitolewe zote na hasa kwa kuzingatia kwamba kuna mpango wa nne wa Maendeleo 2011/2012 hadi 2015/2016. Hii Wizara inahitajika ifuate Mpango huu wa Maendeleo katika kutekeleza mambo yake ipasavyo. Itakuwa ni aibu sana kama sisi ndiyo tutakaokuwa kikwazo katika utekelezaji wa mpango huu kutokana na uhaba wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie sasa kwa kuipongeza Wizara kwa mambo mazuri inayoyafanya. Huwa tunaona mara nyingi habari kwenye *TV* matangazo mengi ya kuitangaza Afrika ya Mashariki, lakini naamini kwamba uhaba wa fedha ndiyo unasababisha habari hizi hazifiki maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, naomba fedha zitolewe za kutosha ili kusudi wananchi wa vijijini nao waweze kupata manufaa na kupata uelewa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga tena mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Waride Bakari Jabu na ajiandae Mheshimiwa Kombo Khamis!

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mikmi kwanza ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijali afya na uzima, lakini pia nataka kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kuipongeza tena Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa kuimarisha utangamano tulionao ndani ya nchi zetu za Afrika ya Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utengamano huu kwa kweli una faida kubwa ndani ya nchi zetu. Tumekuwa tunaona tunapata ajira, biashara zetu kwa pamoja, biashara ya kati, biashara ndogo ndogo. Tumeona wananchi wetu wanaofaidika katika soko lile la Jua Kali kule Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumekuwa tunafaidika katika nyanja ya kielimu, Watanzania wanasoma Kenya na Uganda, lakini wa Kenya na Uganda pia nao wanakuja Tanzania nao kupata elimu. Pia katika miradi ya kimaendeleo tuko pamoja kwenye reli, maji kama kule *Lake Victoria* vile vile umeme yote haya kwa ajili ya utangamano huu tulionao wa Afrika ya Mashariki. Nawaasa sana Watanzania wenzangu, tuudumishe huu Muungano tuliokuwa nao. Kwani hapa tumesikia historia tuliyoambiwa na Mheshimwia Mohamed Seif Khatib kwamba, utangamano huu umeenziwa kutokana na Muungano wetu wa Tanzania Bara na Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia, nimemsikia Mheshimiwa Waziri, akizungumzia kuhusu Sera ya Afrika Mashariki, inayohusiana na Wanawake, Vijana na Walemavu. Nataka kujua Sera hii imefikia wapi? Kwani naamini Sera hii, kama alivyotueleza Mheshimiwa Waziri ina mambo mengi na mambo muhimu, yakiwemo kupatiwa uwezo wa wanawake wetu, vijana na Walemavu, lakini pia kusomeshwa na kuwa na mikakati ya pamoja ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuiuliza Wizara je, imeshirikishwaje katika kuandaa Sera hii, ambayo tumeambiwa hapa na Mheshimiwa Waziri, kwani nasi Watanzania tusiwe nyuma katika kutengeneza hizi sera zinazotuhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia pia kuna *Visa* moja ya Utalii na wenzetu, Kenya, Uganda na Rwanda, wameshaungana na wanashirikiana kwa pamoja. Nataka kujua sisi Tanzania, kwa nini tunasitasita na sababu gani ambazo zimetufanya tusiingie humo katika hiyo *Visa* moja ya Utalii? Nahisi hili ni jambo jema, lakini kwa kweli tulifanyie kwanza utafiti na uchambuzi mzuri kabla hatujaingia, isije kuwa tunaingia katika hiyo *Visa* moja ikawa wenzetu huko wanafaidi fedha, sisi kwetu wanakuja kuangalia Mbuga katika Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuzungumzia suala hili. Kumpongeza kwa kweli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maamuzi ya Serikali aliyoyatoa ya kuendeleza mikakati ya ushuru wa pamoja. Kwa kweli hili jambo ni zuri nalo, lakini nawaomba sana Watendaji wetu na hasa Wabunge wetu wa Afrika Mashariki, wanapokwenda kwenye majadiliano wahakikishe Tanzania kwanza, kwa sababu ushuru huu, tunaosema ndiyo moyo wetu Watanzania na ndiyo kila kitu kinatokana na huu ushuru wa pamoja. Kwa hiyo, nawaomba sana watendaji wanapokwenda katika meza ya majadiliano na Wabunge wetu hili walione kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekti, pia nataka kuzungumzia kuhusu Wabunge wetu wa Afrika Mashariki. Nimeona hapa Wabunge wengi, hata katika Taarifa ya Kambi ya Upinzani na Kamati inayohusika na mambo ya Afrika Mashariki, imekuwa ikiwajadili au inalalamika kutopata taarifa husika kutokana na hawa Wabunge wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wajue kwa kuwa, Wabunge tuliomo humu ndani ndiyo Wapiga Kura wao. Kwa hiyo, tunahitaji kusikia yale ambayo wanakwenda kuyajadili huko au yaliyotokezea. Kama hivi tunasikia hilo la Spika, kuondolewa au tunasikia sasa hivi kuna mzunguko wa kufanya vikao; Mara Burundi, mara Arusha, hatuelewi kulikoni, lakini kama watakuwa wanatupa taarifa za uhakika na usahihi tutakuwa hatuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanywe utaratibu kabisa wa kuwa hawa Wabunge wawe wanakuja katika Kamati husika kutoa taarifa kwa hayo, yanayotendeka kule. Pia kuna mambo ambayo kama Wabunge katika Kamati zetu yanahusiana na Mambo ya Afrika Mashariki, waje kukaa na zile Kamati husika, waambiwe mikakati, mipango na mengineyo ili waweze kwenda kuyajadili huko wanakokwenda katika Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumalizia kwa hii Miradi ya Zanzibar iliyowasililshwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kweli nimekisoma hiki kijarida na kwa kweli kama tunavyosema *business as usual,* haya mambo toka tumeanza Bunge hili tunasikia upembuzi yakinifu, itafanywa hivi, itafanywa hivi, lakini kwa kweli namwomba sana Mheshimiwa Waziri atueleze, kuna kitu gani ambacho kinakwamisha hii Miradi ya Zanzibar katika ufadhili wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni Wizara yenyewe au Wizara ya Miundombinu Zanzibar au Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Hata hivyo, nilikuwa nikimwona sana Mheshimiwa Waziri alikuwa anakwenda sana Zanzibar. Sasa nataka kujua alikuwa akienda huko kufuatilia Miradi hii au alikuwa akienda huko kufuatilia shughuli za UKAWA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, jina hilo kwa kweli tumekubaliana lisitajwe tajwe humu ndani na sijambo zuri kwenda kinyume na *ruling* za Spika. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Kombo Khamis ajiandae Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi na tutamalizia na Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nami nishukuru kupata nafasi hii, lakini kwanza nichukulie kauli aliyoimaliza Mheshimiwa pale, niseme kwamba kauli zake alizozisemea juu ya hii miradi ni sawasawa na mtu kuwa na harusi yake, lakini mwenye harusi akaalikwa kwenda kula wali kwenye jamvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar ambayo ilikuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kabla ya kuvunjwa kwake na kuundwa upya ilikuwa na wajumbe sawa na Tanganyika. Leo hii Zanzibar imepewa nafasi mbili za kuwa na Wabunge ndani ya Jumuiya kama hisani. Niseme kwamba suala hili ni miongoni mwa masuala ambayo yanawapa wasiwasi Wazanzibari juu ya Muungano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Jumuiya ambayo Tanzania inaingia kama Jamhuri ya Muungano kuna mambo 17, lakini mambo manne tu ndiyo ambayo ni ya Muungano. Tujiulize haya mambo 13 yanawakilishwa na nani. Wakati Watanganyika wanawakilisha mambo yale, kwa kutumia Jamhuri ya Muungano, haya mambo 13 ambayo siyo ya Muungano yanawakilishwa na nani ndani ya Jumuiya? Kwa nini basi, Wazanzibari wasipewe fursa ya kuweza kusimamia mambo haya wenyewe ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki? Wakati ni mambo manne tu ya Muungano ambayo yanashughulikiwa na Waziri na Naibu Waziri, yapi mengi kati ya haya 13 na haya manne? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naomba kusema kwamba, kufunguliwa kwa Taasisi ya Kiswahili Zanzibar ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, bado haijawa suluhisho la Zanzibar kudai nafasi yake ya kutetea masuala yake ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ni hili suala la migogoro ambalo wenzangu wengi wamelieleza. Migogoro baina ya Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya. Mheshimiwa Raya kalieleza, lakini tunataka tupewe kauli ya Serikali, hii migogoro ambayo imetokea baina ya Viongozi Wakuu Wanachama wa Jumuiya, kuna Tume yoyote ambayo imeundwa ya Usuluhishi kuweza kuleta suluhu juu ya migogoro hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna Tume ambayo imeundwa ya kuweza kuleta suluhisho, tutaamini vipi nchi zetu kama ziko salama wakati tuna migogoro hii, ni nini hatma ya nchi zetu? Ikiwa vichwa vya nchi zetu ni vigonjwa, basi hatuwezi kufika kokote kuzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna suala ambalo limeamuliwa kuanzishwa Jumuiya ya walio tayari kati ya Kenya, Uganda na Rwanda. Je, ni lini Tanzania ilitoa tamko la kwamba haiko tayari? Ni lini? Tayari Tanzania imeshatoa kauli hii? Kuna nchi ambazo zimeunda Jumuiya ya walio tayari ikiongozwa na Museven. Je, Tanzania tayari imeshatoa kauli kama hii kwamba haiko tayari?

Halafu, kuna tatizo la vizuizi ambalo wenzangu wengi wameshalizungumza. Nashukuru Mheshimiwa Waziri mwenyewe kalizungumza. Lakini tuangalie pale Tunduma, mizigo inaweza kukaa siku 20 wakati tayari mizigo hiyo hiyo imeshafanyiwa uchunguzi sehemu moja. Kwa nini mizigo ile isipatiwe fursa ya kuingia katika nchi jirani? Je, huku siyo kujijengea uhasama baina ya sisi na nchi jirani?

Tunaomba masuala haya yapatiwe ufumbuzi wa haraka sana ili migogoro hii iweze kuondoka na nchi yetu iweze kurejesha heshima na hadhi yake kwa nchi jirani. Leo tunaonekana Tanzania ni kikwazo kikubwa kinachozuia bidhaa kuingia nchi nyingine. Hatujijengei, bali tunajivunjia!

Sasa kwa sababu Waziri ametoa kauli kwamba masuala haya yatapatiwa, ufumbuzi basi yapatiwe ufumbuzi wa haraka sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Lissu.

**MHE. FATUMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba hotuba ya wenzetu wa Kambi ya Upinzani imezungumzia sana masuala ya Serikali mbili na Serikali tatu. Nataka niseme kwamba masuala ya Serikali mbili au tatu ni ya kwetu Tanzania na hayahusiani na Afrika Mashariki. Naomba wenzetu wa Afrika Mashariki mtuachie mambo yetu, hayo achaneni nayo, msije mkachanganyikiwa mkasema kwamba Tanzania wametuambia hili, la hasha! Mambo ya Serikali tatu au mbili mtuachie wenyewe Watanzania. Tutayashughulikia wenyewe Watanzania na tutapata ufumbuzi wake. Ninyi achaneni nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka nianze kuchangia suala hili la Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afrika Mashariki imebeba mambo yote ya Wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Elimu, Afya, Mawasiliano, Ujenzi, Utalii, Uchukuzi, Michezo; Wizara zote zilizopo Tanzania, basi zimo katika Afrika Mashariki. Ni juu yetu sisi wenyewe tuchambue ipi yenye uzito zaidi na tushirikiane na wenzetu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba Tanzania ni Cinderella ya Afrika Mashariki. Cinderella ni neno la Kiingereza na Kifaransa. Maana yake ni kitu kilichotengwa na wenzi wake. Kwa nini nimesema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwa kweli tumetengwa na mambo mengi na wenzetu wa Afrika Mashariki. Lazima twende mbio, twende kwa kasi, tufuatilie kwa jitihada zote kuhakikisha kwamba mambo yote yaliyomo katika Afrika Mashariki na sisi tunakwenda nayo sambamba bila kuachwa popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hilo na sababu ninayo. Nina sababu moja, na kwenye bajeti iliyopita niliuliza kwamba nchi hizi za Tanzania ambazo ni kongwe zinasaidiwaje na Jumuiya za Madola kama *UNICEF* na kadhalika? Zinasaidiwaje? Nilisema kwamba sisi Watanzania tuna Miji mikongwe ambayo ni Miji ya zamani kabisa! Wanasema nchi za Ano Domino, baada ya kuzaliwa Yesu Kristo. Nchi hizo zilikuwepo sita, sisi Tanzania ni mojawapo. Wapo Mombasa, Kenya, wapo Lamu, Kenya, Mogadishu Somalia, Sofala Msumbiji, Tanzania tupo Kilwa; Zanzibar, Tanzania. Miji hii ya Ano Domino ya mwaka 1700 ilikuwa na biashara zake ustaarabu wake, zilikuwa na fedha za kwao zilikuwa ni kiunganishi kati ya nchi hizo zote, ilikuwa na heshima yake na walikuwa wanatembeleana kimichezo na hata Lindi walikuwa wanafika wakati ule wanakwenda Kilwa wanakuja Lindi kucheza mechi. Uwanja wa Lindi ulikuwa na taa wakati ule, enzi hizo! Walikuwa wanacheza michezo, watu walikuwa wanatoka Mombasa kuja Lindi kwenda Kilwa.

Sasa swali langu likoje? Swali langu lipo hivi, kwamba je, sisi Watanzania Kilwa na Zanzibar tunasaidiwaje katika mkakati huu wa kuendeleza hizi nchi kongwe za Afrika Mashariki ambazo ni mbili, big, yaani Kilwa na Zanzibar, tunasaidiwaje? Kwa sababu hawa wenzetu niliowasema hapa: Mombasa, Lamu, Mogadishu na Sofala wanasaidiwa na *UNICEF,* Marekani, Japan, Uingereza na Ujerumani. Je, sisi Watanzania tunasaidiwaje katika hizi nchi kongwe au Miji mikongwe ya Afrika Mashariki? Ndiyo nilipomalizia hapa kwa suala hili la Miji mikongwe ya Afrika Mashariki, tunataka na sisi tujue tunasaidiwaje katika mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afrika Mashariki Wizara hii inahusika na mambo yote katika Wizara mbalimbali kama nilivyoanza hapo mwanzo.

Sasa nije katika suala la utalii. Naomba sana Wizara hii itusaidie kutangaza utalii wa Tanzania. Tuna mambo mengi sana ya utalii Tanzania. Pamoja na wao wenyewe Wizara ya Utalii wanatangaza mambo mbalimbali, lakini na sisi kama Jumuiya ya Afrika Mashariki tunao wajibu wa kuitangaza Tanzania katika Jumuiya yetu na nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mambo mengi, hapa nikiyataja tutakesha. Haya ya Lindi peke yake ni tishio. Sisi Lindi tusaidiwe kutangaza utalii, kwani tuna *Seleou Game Reserve*, Lindi, Kilwa na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mikidadi, mchango ni mzuri sana, uendeleze kwa maandishi ili upewe majibu sahihi.

Sasa namwita Mheshimiwa Lissu, ambaye ni mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia na ahsante sana.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Kwa vile muda siyo mrefu sana naomba nizungumzie suala moja au mawili yanayohusu ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alikuja ndani ya Bunge hili Novemba, 2013 na akazungumza kwa uchungu sana juu ya mahusiano yanayoelekea kuwa siyo mazuri kati ya nchi yetu na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *namely* Kenya, Uganda na Rwanda. Tulitegemea kwamba suala hili kwa vile Rais alikuja akalizungumzia Bungeni tulitazamia kwamba katika hotuba ya mwaka ya Waziri anayehusika na ushirikiano wa Afrika Mashariki lingepatiwa angalau sentensi moja kama siyo *paragraph* au siyo *chapter* kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri angetueleza kama hali aliyoieleza Mheshimiwa Rais mwaka 2013, bado imeendelea kuwa vile vile au kama kumekuwa na nafuu katika mahusiano yetu na majirani zetu. Nimejaribu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijaona mahali popote ambapo amezungumzia hii inayoelekea kuwa *diplomatic crisis* kati yetu na wanachama wenzetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Itakuwa vizuri Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako hali ikoje sasa hivi *specifically* kwa sababu Mkuu wa Nchi alikuja akalalamika sana humu ndani. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwamba kwa vyovyote vile, kwa kuangalia jiografia ya nchi yetu, nchi yetu ndiyo moyo wa *arrangement,* yoyote na mahusiano yoyote katika Afrika Mashariki na ya Kati, sisi ndiyo tunatakwa tuwe lango kuu la kuingilia katika nchi nyingine za Afrika Mashariki na ya kati. Sisi tupo karibu zaidi na Uganda kuliko Kenya. Tupo karibu na Rwanda, tupo karibu zaidi na Burundi, tupo karibu zaidi na Congo, tupo karibu na nchi nyingine zote za Afrika Mashariki na Kati ukilinganisha na Kenya. Kenya nazungumzia langu kuu la Mombasa. Kwa hiyo, *by visual geographical location* peke yake sisi tunatakiwa tuwe ndiyo waendeshaji wa huu ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa sababu tu ya *geographical location* ukiacha *advantage* nyingine za raslimali ambazo tunazo, lakini kwa hali tu ya kijiografia sisi tunatakiwa tuwe ndio wafaidikaji wakubwa wa utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu na pengine itatusaidia Mheshimiwa Waziri akitueleza, leo sisi ndio tunaopiga kelele kwamba tunaachwa nyuma, *we are being isolated,* leo Wakenya, Waganda na Wanyarwanda wanazungumza kujenga reli ya kutoka Mombasa kwenda Uganda na Rwanda; wakati ingekuwa rahisi zaidi na gharama nafuu zaidi kujenga reli kutoka Dar es Salaam au Tanga kwenda Kigali au Kampala au Uganda kwa ujumla. Ni kitu gani hasa, ni sababu zipi ambazo zinaifanya nchi yetu licha ya hiyo *geographical advantage* iliyonayo inaachwa nyuma, tunawekwa pembeni na watu ambao wanatakiwa wawe wametukumbatia? Tumekosa nini? Serikali yetu imekosea wapi? Kwa nini hawa ambao hawana *geographical advantage* tulizonazo sisi, kwa nini wanatuacha nyuma? Kwa nini wanafikiria kwamba sisi ndio wakwamishaji? Maana yake tunaachwa kwa sababu wanatuona *we are obstructers!* Tunakwamisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hilo, Waziri atusaidie kwa sababu Wakenya na hiyo *coalition of the willing* wanatakaka kujenga hiyo reli na baadaye waende *South Sudan* au Sudani ya Kusini. Itakuwa na madhara gani kwetu kiuchumi? Kwa sababu ni lazima kuwe na madhara kiuchumi. Anayefikiria kwamba tunaweza kuwa *isolated* na tukabaki sawasawa tu atakuwa anajidanganya kama hatudanganyi na sisi. Huu ugomvi wa kidiplomasia unaoelekea kuwa ugomvi wa kiuchumi, utakuwa na madhara gani kwa nchi yetu? Tutapoteza kiasi gani kiuchumi? Tutapoteza kiasi gani kibiashara? Tutapoteza kiasi gani katika uwekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona takwimu hapa kwamba kwa mwaka uliopita uwekezaji kutoka nchi wanachama kuja kwetu ni Dola milioni tisa. Dola milioni tisa ni *loose change*. Dola milioni tisa ni vijisenti kutumia msemo wa mtu fulani humu ndani. Inawezekanaje nchi ambayo ina *advantage* kama hizi ikapokea vijisenti katika uwekezaji? Tumekosea wapi?

Kuna hisia kwamba tunakwamisha mambo. Hizi hisia Mheshimiwa Waziri naomba utueleze, ni kiasi gani hisi hisia kwamba sisi ndio tunawazuia wenzetu kusonga mbele kwenye *Regional Integration* ni za kweli kiasi gani? Wanatuambia siyo taarifa rasmi sana, lakini wanasema kwamba *protocols* mbalimbali zikija kwenye Serikali yetu zinakaliwa, hakuna taarifa, hatusemi hapana wala hatusemi ndiyo, hatufanyi maamuzi. Hii ndiyo sababu inayowafanya wanatutenga au ni sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwa sababu muda hautoshi tuyazungumze haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa sekunde chache zilizobaki, nimeangalia takwimu za kiuchumi kati yetu na nchi wanachama wa *EAC* na kwa mwaka 2013 tu inaelekea biashara yetu imepanda kwa kiasi kikubwa sana ukilinganisha na miaka ya nyuma. Itakuwa vizuri tukapata takwimu halisi, maana yake hizi ni *only provision data.* Ni kitu gani kimetokea kufanya hii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, lipo tatizo ambalo vilevile Serikali inatakiwa ilishughulikie nalo ni suala la vitendea kazi vya Wabunge wetu wa Afrika Mashariki. Ni suala ambalo Serikali inalikwepa na hatujui inalikwepa kwa sababu ya nini. Labda Serikali ingejaribu kutuambia ni nani hasa anayehusika na vitendea kazi vya Wabunge wa Afrika Mashariki na hasa kwenye masuala ya usafiri? Wananunua magari kwa pesa zao na wengine sasa hivi wapo hoi, mpaka tumeanza kupigana mizinga Mitaani. Hali zao ni duni. Haina sababu ya wao kukosa fursa ambazo zinatakiwa ziwepo. Kama zinatakiwa ngazi za juu ndiyo ziwe na taarifa, basi tuambiwe, ni nani anayehusika ili taarifa ziwafikie ili waweze na wao kujaliwa.

Mfano mdogo tu Mheshimiwa Waziri, na ninyi mnajua, ukitazama nchi ya Uganda *package* ambayo Wabunge wao wanapewa; nchi ya Kenya na hata Rwanda. Kwa hiyo, kuna umuhimu na hawa wakienda pale wasijione ni yatima wakati wanatoka kwenye Taifa kubwa lenye uwezo mkubwa na wao wakajiona ni sehemu ya Taifa lao na watakuwa na moyo na ari kubwa kabisa ya kutetea maslahi ya Taifa wakiona na wao maslahi yao yanalindwa.

Waheshimiwa Wabunge, jioni tuna mchangiaji mmoja tu, Mheshimiwa Freeman Mbowe na baada ya hapo Wizara mtaanza ku-*wind up* na kumaliza hoja yenu.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 6.58 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuna mchangiaji mmoja tu ndiye aliyebakia, na baada ya hapo Waziri wa Afrika Mashariki atahitimisha. Sasa namwita Mheshimiwa Freeman Mbowe awe mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii na wa mwisho. Karibu!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza mchana wa leo na ya mwisho nichangie katika hoja ya Bajeti ya Wizara ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza katika maeneo machache sana ambayo nina hakika yataweza kutupa pengine msingi wa namna tunavyostahili twende mbele katika ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo ningependa wenzetu katika Serikali na la kipekee, Wizara ielewe ni kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi haionekani kuwa na dhamira ya kutosha ya kuwa sehemu ya Afrika Mashariki. Wanaweza wakawa wanasema kwamba tunapenda Utangamano wa Afrika Mashariki, lakini vitendo vya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kauli za Serikali ya Chama cha Mapinduzi haziashirii kwamba tuna dhamira ya kweli kama Taifa kushiriki na wenzetu wa nchi za jirani katika kuunda Utangamano wenye faida za kiuchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ambayo inajiita sikivu ni Serikali ya watu waoga sana, hasa inapokuwa inahusisha Mataifa yanayotuzunguka, tunazi uoga bila sababu ya msingi. Leo ni miaka 14 tangu tumesaini Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ile *treaty,* Tangu mwaka 1999 tumesaini *treaty*. Kwa miaka 19 tumeshindwa kutengeneza sera *(policy)* ya mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hatuna sera inayotuongoza kama Taifa, hatuna *strategic engagement* katika *partnership* na wenzetu wa Afrika Mashariki. Yaani ina maana kama Taifa hatujui tunahitaji nini Kenya; kama Taifa hatujui tunahitaji nini Uganda; tunahitaji nini Rwanda wala Burundi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo Wizara ambayo tunaambiwa ndiyo inasimamia zoezi la mtangamano wa Afrika Mashariki ilikuwa ni kaidara kadogo tu katika Wizara nzima ya Mambo ya Nje. Wizara yenye bajeti ya Shilingi bilioni 23 kwa matumizi yote, unategemea ndiyo itaweza kuliandaa Taifa na kuliingiza katika mtengamano wa Afrika Mashariki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu unasikia leo Wabunge wetu wa Afrika Mashariki wanalalamika. Wabunge wa Afrika Mashariki ambao ni Wawakilishi wetu katika *EALA* hawana Ofisi, hawajui wanaripoti kwa nani. Hawajui wanaripoti kwa Bunge au kwa Wizara ya Afrika Mashariki na ya Kati. Wakienda kwenye vikao vya Jumuiya, wakitoka kwenye vikao vya *EALA* wakirudi nchini hawajui wanakwenda wapi? Wanafanyia wapi kazi? Wanapatikana wapi? Wanaripoti kwa nani? Mambo yote haya yako wazi, halafu tunasema tuko *serious* katika kujenga mtengamano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ndiyo jambo la msingi sana ambalo lingetupeleka katika mambo yote ya mtangamano, lakini hatuna *economic policy* katika *integration*. Hatuna *social policy* wala *political policy* katika mambo ya *integration*. Tunakwenda tu kama mzobe mzobe, kinachojitokeza ni ajali, tunasaini *protocols* mbalimbali hatuna mkakati wa kuzitekeleza, hatuna kitengo cha utafiti katika Wizara hii, kitu ambacho kingekuwa cha msingi mno kutuandalia sera ambayo ingetuwezesha kujua tunafaidi nini kama Taifa katika mtangamano huu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu za fedha za biashara; katika mwaka wa fedha 2011 Tanzania tuliuza katika nchi za wenzetu bidhaa za thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 409. Mwaka 2012 tuliuza bidhaa za Dola za Kimarekani bilioni 613 na mwaka 2013 tuliuza bidhaa za thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 1.120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni fedha nyingi sana. Katika mazingira ya kawaida ni fedha nyingi sana. Lakini katika kipindi hiki hiki cha miaka mitatu haya Mataifa mengine yote manne

yaliyotuzunguka kati ya mwaka 2011 mpaka 2013 yalifanya *direct investment* katika nchi yetu yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni tisa ambazo ni fedha kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maana ya hoja ninayotaka kuijenga mahali hapa? Kama nchi, tunaweza kuuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1,000 kwa nchi nyingine, ni lazima masuala ya nchi hizo zinazotuzunguka, tuyaheshimu na tushirikiane vizuri sana. Hatuwezi tukapuuza soko ambalo tunaweza kuuza mali ya thamani ya Dola bilioni moja kwa mwaka kama nchi.

Kukiwa kuna *instability* ya njia yoyote Kenya, *whether* hali ya kiusalama au ni Al-Shabab nchini Kenya, inatuhusu sana Watanzania kwa sababu hii *cross border trade,* kama usalama katika *zone* nzima ya Afrika Mashariki utaathiriwa kwa sababu nyingine yoyote ile, ina maana sisi kama nchi tunakosa soko la Dola bilioni moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni fedha nyingi sana ambayo inatupasa tujitafakari kama Taifa, tumekuwa ni sehemu gani ya kuongeza *stability* ya Kenya? Sisi tunakuwa sehemu gani ya kuongeza *stability* ya Uganda? Tunakuwa sehemu gani ya kuongeza *stability* ya Burundi na Rwanda! Kwa sababu hawa ni *partner states*; kama wakishambuliwa ama tukawa na mahusiano ambayo siyo mema, ina maana tuko tayari kupoteza soko la zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni moja jambo amblo nafikiri ni la hatari sana na hatustahili kabisa kuliendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri alizungumza kwamba, eti tayari walishakutana Kampala na katika kikao kile walikubaliana kwamba waandae Katiba ya nchi za Jumuia. Sasa ni jambo la ajabu kidogo kwamba wanakubaliana na wako katika mchakato wa kuandika Rasimu ya Katiba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, wakati humu ndani hatuijui. Bunge hili kwanza halijaletewa hiyo *protocol* tukakubaliana. Yako mambo ya msingi ambayo tungetegemea tuwe tumeshakubaliana kabla wakubwa wenzetu hawajaenda kukaa Kampala na kukubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya ndiyo mambo ya kufanya mambo kienyeji. Ndiyo nasema, haya mambo mengine pamoja na kwamba tunataka masuala ya Jumuiya yawe *fast tracked*, lakini kwa kweli kwa matendo yetu kama Watanzania tunafanya mambo bila dhamira njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika misingi hiyo, nikirudi kwa Wabunge wa Afrika Mashariki, kama tunachagua Wabunge, tunawataka wakaingie katika Bunge la Afrika Mashariki, wakashindane na Wabunge wa nchi nyingine, ni lazima tuwaandae. Kama hatuko tayari kuwawezesha Wabunge wetu, hawana Ofisi, hawana Wasaidizi, hawana vitendea kazi, hakuna bajeti ya kuwahudumia, halafu tunategemea wakashindane na wenzao wa Uganda, wenzao wa Kenya, na wenzao wa Rwanda na Burundi kwenye kutetea *interests* za Tanzania, hakika wale watu hawawezi kwa sababu kwanza *confidence* hawana kwa sababu ya mazingira yao ya utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kama tunahitaji kweli kuendelea kupanua hili soko letu la Afrika Mashariki ambapo sisi tuko *positioned strategically* kabisa, tunatengeneza zaidi ya nusu, *actually* ni asilimia 60 ya eneo lote la ardhi la Afrika Mashariki, lakini tumekuwa ni watu waoga, tumeshindwa kujenga reli, tumeshindwa ku-*connect* na hizi nchi, tumeshindwa ku-*take advantage* ambazo wenzetu wanatushangaa, hivi Watanzania mna akili timamu kweli kweli nyie? *(Makofi)*

Mheshimiwa Lukuvi ananianglia sana; Mheshimiwa Lukuvi hivi Serikali yetu inasikia kweli hii? Mmeshindwa kuona kabisa *advantages* ambazo ziko wazi, ziko nje za kuona! Hamwoni, ham-*take advantage,* mpo tu!

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha k*
*wa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbowe nakushukuru sana, utapata nafasi kwenye mshahara wa Waziri, utasema tena.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, huyu ni mchangiaji wetu wa mwisho. Hivi sasa namwita Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na baadaye atakuja Waziri kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kwa maana kubwa ya kutimiza wajibu wangu katika Taifa hili juu ya kazi hii niliyopewa ya kusimamia Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Pili, nimshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Mauungano wa Tanzania kwa kutuongoza kwa umahiri na weledi mkubwa kama ilivyoonekana wakati alipokuja kuhutubia Bunge letu hili.

Kwa kweli, yeye kwa upande wa Wizara yetu tunamhesabu kama ni *mentor* mzuri, mwelekezi mzuri na Jemadari wa kuaminika. Pia natoa shukrani kwa Viongozi wote wa Kisekta, Makatibu Wakuu, Watendaji na Maofisa. Kama inavyotambulika kwamba Wizara yetu ni mtambuka, kwa kweli wao kwa ajili ya kuweka heshima ya Taifa letu, wameshirikiana na sisi kwa hali na mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, sitakuwa mwingi wa hisani kama sitatoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Samweli Sitta kwa kuwa kiongozi, Mwalimu na mwelekezi mzuri sana na Mungu amzidishie subra na kipaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashukuru familia yangu ya Mzee Sadalla na wapiga kura wangu wa Jimbo la Raha Leo na ninawaambia kwamba, mbele kwa mbele na mwenendo ni mwendo mdundo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea michango mingi ya hoja nyingi sana za kimaandishi na nyingine za kauli, lakini tunasema tu kwamba, wakubali hoja zetu hizi na sisi zile ambazo tutashindwa kuzijibu, tutazileta kimaandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika hoja zilizotolewa ni ushauri juu ya kutoa elimu kwa Umma kwa ajili ya Mtangamano wa Afrika Mashariki. Hoja hii imetoka mara nyingi na Wizara yetu inajitahidi sana. Pamoja na kuwa na mkakati juu ya Mtangamano wa Afrika Mashariki na kuweza kutoa elimu kwa Umma, tumetoa elimu kwa Umma katika Vyuo, mipakani na kila tunapofanya ziara huwa tunatoa elimu kwa Umma.

Vilevile kuna vijarida, kuna televisheni na kuna waraka mkubwa sana wa kuonesha ni namna gani tumetoa elimu kwa Umma. Tunafurahi sana kwamba kwa kiasi fulani elimu kwa Umma imefahamika kwa wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hatutaishia hapo, katika mpango mkakati wetu wa Wizara tumekusudia sasa tutoe elimu kwa Umma kwa *SMEs* (Wajasiriamali wa Kati na Wadogo),

na vilevile kushusha elimu kwa Umma tuache katika *Northern Corridor* au tuendelee katika katika *Southern Corridor* ili wananchi nao kule waweze kufaidika na kujua ni namna gani wanaweza kutumia fursa za Mtangamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wametoa hoja zao juu ya miradi hasa ya Zanzibar. Mara hii Wizara imeamua kutoa kipeperushi maalum ili kuelezea hatua za kutekelezwa miradi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunzia, kuna mradi wa uwanja wa ndege wa Pemba. Taarifa za Maafisa wetu na za vikao ambavyo tunaingia, zinasema ifuatavyo:

Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliahidi kutoa Shilingi milioni 500 kwa ajili ya mshauri mwelekezi ili baada ya kupatikana ripoti hiyo ndiyo yule mshauri mwelekezi na Serikali watatuarifu kwamba *African Development Bank* iingie kati kwa ufadhili wa hatua zinazofuata mpaka kuuzwa kwa mradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tulizokuwa nazo mpaka hivi sasa ni kwamba, bado hali hiyo inaendelea na upembuzi yakinifu *(feasibility study)* inaendelea na hadi hivi sasa SMZ hawajatupa ripoti yoyote. Kwa hiyo, hapo ndipo tulipokwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bandari ya Maruhubi; SMZ tumejua na tuliripoti kama mara tatu hapa kwamba, tumepata taarifa kwa kuambiwa na vikao vya SMT/SMZ kwamba, wameshamaliza upembuzi yakinifu, lakini Wizara yetu haijapata mmeng'enyuo na uchambuzi halisi ambao tunaita kwa Kiingereza *project un-pack* ambayo ingetufanya sisi tuweze kuchukua zile ripoti na tukazikabidhi kwa ajili ya kufanya utafiti wa fedha.

Ushauri wangu, pamoja na kwamba najua wapo Wabunge wengi ambao tumeshirikiana katika suala hili, lakini SMZ itupatie tu kile tunachoita *dossier* ya *project* ili tuweze kwenda katika Mikutano na kuweza kutetea na wao wenyewe wakiwepo itakuwa ni busara zaidi kwa sababu watakuwa weledi wa kuona suala lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme wazi tu kwamba miradi hii yote ambayo nimeieleza hapa ni miradi ambayo tumepata *concept paper* yake na imeishapitishwa kwamba ni miradi ya kipaumbele katika Afrika Mashariki.

Kadhalika kuna mradi huu wa RORO, kama nilivyosema kuna Wabunge wengi walikuwa wanataka kujua kuhusu jambo hilo. Halikadhalika ni kwamba, mpaka hivi sasa hatujapata andiko au *dossier* juu ya *project* hii ya kuweza kutetewa katika vikao vya kutafuta fedha baina ya wafadhili na *stake holders* ndani ya Afrika Mashariki. Kwa maana ya hapa *stake holders* ni Tanzania juu ya *project* hii. Lakini tunayo *project* ambapo Mombasa na Lamu waliishaanza mradi huu na hapa kama inavyojulikana kwamba, Bandari ya Dar es Salaam pamoja na uchimbaji wa njia na kuchimbua bath Na 1 - 7 na hii *issue* ya RORO nayo pia imo katika uendelezaji wa suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mapendekezo tu ya kusema kwamba Zanzibar ingetuletea sasa kwa kile kipande chake cha baina ya Unguja na Pemba, ambayo ni Mkoani au Fukuchani; ingekuja ile *project* nzima tukaitetea nayo pamoja na wao kuja katika vikao vya pamoja vya wadau au tukawakabidhi Viongozi wetu wanapokwenda kuomba *project* nao wapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nzima juu ya kutengeneza Katiba ya Afrika Mashariki na hata sasa hivi Mheshimiwa Mbowe ameizungumza.

Ningependa kuwaelewesha wananchi kwamba kilichoamuliwa na Viongozi wetu ni kwamba, wakati hatua za Mtangamano zinaendelea, Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Sarafu ya Pamoja na ambayo tunasema hatimaye kutakuwa na *political federation*, wakati haya yanaendelea limetoka agizo ambalo liko katika *Community* linasema kwamba, uanze utaratibu wa kuweza kutathmini mangapi na mambo yanaenda vipi ndani ya utekelezaji huu wa Mtangamano? Hilo ni la mwanzo. Faida na hasara zake. Itengenezwe njia ambayo inaitwa *road worthy* ya namna gani tutakwenda katika kutengeneza *constitution,* lakini vilevile muundo wa *constitution* wenyewe ukoje? Ufanyiwe tathimini na Sheria za nchi zetu nazo vilevile zitakuwaje?

Kwa hiyo, kilichoamuliwa hapa, siyo kwamba tunakwenda kutengeneza *constitution*. Hapa hapana *big bang* lakini ni kutengenezea kuanzia *road map* na kutathimini ni hatua gani. Kwasababu sisi Tanzania na Watendaji wetu wanaamioni kwamba yale ambayo yatakuwa yamejitokeza, tunasema yame-*chip in* katika utengenezaji kwa faida ambayo tunasema, *verifying indicators* lazima ziwepo. Zile *verifying indicators* ndizo zitatusaidia sisi kuwa kama nyenzo za kutia chumvi ndani ya utengenezaji wa ile rasimu ya Katiba.

Kwa hiyo, kuna mchakato mkubwa sana. Ukitazama juu juu tu, ikiwa mpaka *Monetary Union* imo ndani ya suala hili, basi angalau siyo chini ya miaka kumi ndiyo tutaanza kufikiria, yapi na namna gani tutaingia kwenye uandishi wa hiyo Rasimu ya Katiba. Kwa hiyo, siyo jambo jepesi kama lilivyokuwa linafikiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala juu ya mwenendo wa watu na wafanyakazi. Ni kweli kabisa kwamba nchi tatu; Kenya, Uganda na Rwanda zimeamua wananchi wawe wanavuka kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine kwa vitambulisho. Lakini vitambulisho vingine, kuna vya mpiga kura, kuna vitambulisho vya shule ambavyo ni *laminated* vile, kuna vitambulisho vya wafanyakazi, kwa upande wa Tanzania, wataalamu na kwa maamuzi ya Serikali ni kwamba sisi hatutakubaliana na msimamo wa kutembea kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine kwa vitambulisho vya *laminated* vya shule au vya Katiba.

Tumeweka bayana kabisa kwamba lazima kuwe na matumizi ya *passport* ya kusafiria na kwasababu ndiyo yenye vielelezo vya kiusalama na ambavyo tumekubaliana Kimataifa kwamba tutaweza kusafiri kwa njia hii.

Kuna wazo kubwa ambalo limetolewa na sisi tunalitafakari lakini bado hatujalifanyia uchambuzi yakinifu kwamba tuwe tunatumia vitambulisho vyetu vya Kitaifa. Ni kweli kwamba vitambulisho vya Kitaifa vinaweza kutumika, hata katika *EU* vitambulisho vya Kitaifa vinatumika lakini sasa vitambulisho vile: Je, tumeshavifanyia tathimini ambayo nilizungumza awali ya kiusalama? Tumeshafanya utafiti kama nilivyosema awali juu ya utambulisho wa Kimataifa. Kwa hiyo, hiki ni kitu ambacho hakikuwa na uhakika mpaka sasa hivi na sisi hatutakuwa tayari.

Uamuzi wetu sisi tumesema kwamba walioamua kwenda na vitambulisho hivi, acha waende, sisi tutajiunga nao baadaye wakishakuwa na vitambulisho vya Kitaifa. Kwa taarifa tu ni kwamba Tanzania tumepiga hatua. Pamoja na kwamba wao wazo walitoa mapema, lakini Tanzania tumepiga hatua kubwa sana kuwa na vitambulisho vya Kitaifa ambavyo vinasomeka kimashine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine hapa ambayo ilizungumzwa juu ya masuala ya Bunge la Afrika ya Mashariki. Ni kweli kumefanyika maamuzi ya kuwa na vikao vya mzunguko na hili wazo limetolewa ndani ya Bunge la Afrika Mashariki, na maamuzi yalitolewa

ndani ya Bunge la Afrika Mashariki na kwa hiyo, utekelezaji tunautegemea kutokea ndani ya Bunge la Afrika Mashariki. Mwaka 2013 kidogo kulikuwa na tatizo la kalenda kuwa ni nani aanze na nani asianze, lakini tunaamini mwaka huu tutakwenda vizuri, katika *rotation* zile zile za vikao viwili ambavyo tuna cha *Audit* na cha Bajeti kufanyika Arusha na kimoja kitakuwa kinazunguka katika nchi husika.

Mzunguko, kwa kweli Tanzania kidogo tulikuwa ni wagumu kwa kulikubali hili, lakini ilibidi tufanye *win win situation* kwa sababu nchi nyingine zilikuwa zinahitaji kuwa na *exposure* na kuonekana katika hali hii ya Afrika Mashariki.

Kulikuwa na suala hili ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Pereira juu ya *Single Tourist Visa.* Ndani ya Afrika ya Mashariki kuna wazo lilitokezea la *Single Tourist Visa* na hili ni Visa moja ya Utalii na hili pia limezungumzwa baina ya nchi tatu; Kenya, Uganda na Rwanda na wao sasa hivi wanatumia hii *Single Tourist Visa.* Ushauri ambao umefanywa ndani ya Sekretarieti ya Afrika Mashariki hilo ni la mwanzo, lakini ushauri mwingine ambao umefanywa na utafiti wa Tanzania tumeona kwamba kwa hivi sasa Tanzania isiwe tayari kujiunga katika *Single Tuorist Visa* kwasababu zifuatazo:-

Kwanza, mgawanyo wa kimapato wa hizi *visa* haukuwa bayana na mpaka hivi sasa hauko bayana mpaka karibu mwezi uliopita wameanza kuweka *ratios* ambazo hawajazifanyia *verification.*

Kwa kuwa hilo halikufanyika, sisi tumeona kwamba tusikubaliane nalo. Vilevile tumesema kwamba unapokuwa na *Single Tourist Visa* unatakiwa lazima kujua ni nani anatoa na Balozi gani na anaingia kwenye mpaka gani?

Kwa hiyo, kama hatukuwa na mtandao wa kimaelewano wa kikompyuta yaani *ICT* katika Balozi zetu, na katika mipaka yetu, vilevile tumesema kwamba hili tusilikubali. Lakini kubwa zaidi linahusiana na mambo ya Kiusalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujakaa kitako kuamua nani kafanya nini. Tunatoa mfano mmoja mzuri tu, inawezekana mtu mmoja ambaye ni *sympathizer* wa kundi fulani la Kigaidi akachukua *Visa* nchi fulani, akapitia labda Tanzania kwenda katika nchi nyingine, akafanya jambo na akarudi kiwepesi kabisa kama ni mtalii. Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo limetufanya sisi tusikubali.

Baada ya muda, hizi *logistics* zote pamoja na za *operation logistics* za haya mambo zikishakuwa tayari tunasema sisi tunaweza kujinga nao na hatuna matatizo. Kwa hiyo, ile kauli ya kwamba Tanzania haitaki kujiunga au ni *Road Block* kwa mambo haya, siyo! Isipokuwa tu tumesema kwamba ni lazima tukae kitako tuainishiane haya mambo ambayo sisi tuna wasiwasi nao halafu tuendelee kujiunga nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine ambayo inazungumza juu ya ushirikishwaji wa SMZ ndani ya SMT. Hapa ningependa nieleze suala moja; ni kweli kuna masuala mawili yale ambayo ni ya Muungano yanashughulikiwa vipi? Yale ambayo siyo ya Muungano yanashughulikiwa vipi? Masuala yaliyokuwa ya Muungano moja kwa moja pamoja na Wizara ambazo zinahusiana moja kwa moja na Muungano katika SMZ tunakaa nao pamoja na tunakwenda kupeleka hoja kuanzia *level* ya Watendaji wadogo mpaka katika *Sectral Council* na kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa yale ambayo siyo ya Muungano vilevile, inapokuja hoja tunawaarifu *SMZ*; narejea tena, tunawaarifu *SMZ* kupitia katika Ofisi ya Rais ambayo baadaye

wao huchagua, ile sekta ni sekta gani, tunakaa nao pamoja katika *level* ya Watendaji wadogo, ushauri wao unaotoka mpaka katika *Sectral Council.*

Tena kwa taarifa tu niseme kwamba unatokea wakati unamkuta Waziri anayetoka kule ambaye hayuko katika Sekta ya Muungano kutokana na *protocol* zilivyo, yeye ndiye anashika bendera pale na anaendelea kuzungumza na anaingia kwenye *dialogue* akiongoza wengine.

Kwa hiyo ushirikiano na ushirikishwaji uko vizuri, umetulia na utamaduni huo unaendelea. Kama utaniuliza utamaduni huo utaendelea mpaka lini? Mheshimiwa Rajab na wewe uliuliza suala hili, nami nasema utamaduni huu utaendelea mpaka hapo tutakapoamua kihalisia ndani ya Katiba nini kifanyike juu ya ushirikishwaji wa Zanzibar katika masuala ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuja suala la biashara ya Karafuu. Hili suala ni la zamani na tulishughulikia tangu miaka ya 1900 na 2000. Kuna kitengo katika Afrika Mashariki kinaitwa *Inter State Security* kilishughulikia suala hili, Wabunge wa Tanzania tuliwashirikisha na mimi mwenyewe nilifanya ziara kwenda Shimoni ili kutazama ni namna gani tunaweza kuliondoa hili suala kwasababu Zanzibar Karafuu ni suala ambalo ni *item* ambayo imeenziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana SMZ na Wizara yetu ya Afrika ya Mashariki suala hili liliondoka kabisa, karafuu ikawa haisafiri, uharamia ukawa haupo, wavuvi wakawa hawana matatizo, lakini nikiri kwamba karibu miezi miwili, mitatu iliyokuwepo imeanza kuibuka tena hili suala.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri tu ndugu zangu Wabunge na sisi kama Serikali tutachukua jitihada kwa vyovyote kwa mara ya pili tena kuweza kupunguza uharamia huu wa kusafirisha karafuu katika hali ambayo siyo halali. Kulikuwa kuna suala lingine ambalo na Mheshimiwa Mbowe alilizungumza vilevile, suala la taarifa baina ya Watendaji na *EALA*. Ni lazima tueleze ukweli kwamba kabla ya awamu hii ya uongozi haijaingia kulikuwa kuna malalamiko baina ya Wabunge wa *EALA* na namna gani wanaweza kuwasilisha utendaji wao, na shida zao katika Bunge la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu kwanza iliamua kukaa nao katika kabla ya kila kikao na pengine wakati wowote ambao wao wanatuhitaji sisi tunakaa nao na tunazungumza juu ya kipi wanachokihitaji? Elimu gani wanaitaka? Mwongozo gani wanautaka? Au suala gani la Kisera wanalolihitaji ili na wao waweze kwenda kuchangia. Hili limesaidia sana, nami kwa kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Wizara kwa kuwapongeza kwa kuwa wepesi wa kutukubalia na wao wamekuwa wepesi katika kueleza Sera za nchi ndani ya Bunge la Afrika Mashariki. Lakini halitaishia hapo, ni wazi kwamba imebidi sasa wao wanapotekeleza ndani ya Bunge la Afrika ya Mashariki, kuna masuala kadhaa wa kadha, kuna maamuzi ya Sera, maamuzi ya *protocols,* maamuzi ya Sheria yale yanafika vipi ndani ya Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taratibu za Kisheria ambazo zipo baina ya Bunge la Afrika Mashariki na Bunge letu na liko ndani ya *treat* na *rules of regulations* za Afrika Mashariki kwamba Katibu wa kule kila tukio linalotokea ni lazima amwarifu Katibu wa huku wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Siyo wajibu wa Wizara, hayo ni mahusiano baina Bunge na Bunge.

Kwa taarifa tulizonazo mpaka hivi sasa, *Commission* ikikutana inaleta majibu, Bunge likikutana kila baada ya Bunge taarifa imeletwa huku.

Mheshimiwa Mnyika naye alishauri suala hili na Mheshimiwa Masauni kwamba: Je, zinakuwa *tabled*? Kamati zetu zinapata hizi taarifa?

Kwa kweli niseme kwama inawezekana kuna udhaifu juu ya suala hilo na Wizara na Wabunge tutakaa nao pamoja ili tuweze kuwashawishi na kuwahimiza utendaji ndani ya Bunge kuwa utendaji huu na ripoti hizi zipatikane kwa sababu ni kweli, baadhi ya ripoti zinakiuwa ziko *very sensitive* na zina umuhimu mkubwa sana wa kujadiliwa na kupata mrejesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja fulani ambayo ilizungumzwa na Mheshimiwa Tundu Lissu na Mheshimiwa Kombo Khamis kwamba: Je, kuna sababu gani zinazosababisha baadhi ya nchi wanachama kuunda Jumuiya ndani ya Jumuiya? Juu ya suala hili hatuwezi kusema kwamba kuna Jumuiya ndani ya Jumuiya, lakini Mheshimiwa Rais katika hotuba yake amelielezea vizuri sana, ameliainisha vizuri sana na sidhani kama kuna ziada kuzungumza zaidi ya pale kuliko ile shule ambayo Mheshimiwa ametupa.

Kwa hiyo, ni imani yetu kwamba maadamu masuala yanaendelea na hasa ukifikiria juu ya mpango wa *Single Custom Territory* na juu ya *Political Federation* kwamba ni maamuzi ambayo wamekaa kitako wao wenyewe na wakatupa sisi na yameendana na uratibu ambao kabla, ulikuwepo ndani ya Afrika Mashariki *proper* ile ambayo sisi tumejadiliana. Ni yale yale ambayo yalichukuliwa na kuamuliwa na viongozi juu ya *Political Federation,* wakati huo huo juu ya *Single Custom Territory.* Kwa hiyo, tunahisi kwamba maelewano yamepatikana na sisi hatuna *objection* yoyote na nisingependa sana kuzungumza zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Wambura naye alizungumza juu ya suala hilo na ametoa pongezi nyingi na Mheshimiwa Waride pia alizungumza juu ya suala hilo na ameuliza swali ambalo siwezi kulijibu, Mheshimiwa Sitta atakuja kujibu yeye mwenyewe. Lakini ni lazima nieleze kwamba alikuwa na wasiwasi kuhusiana na usalama ambapo vilevile kuna Waheshimiwa Wabunge wengi walizungumza kama hili.

Waheshimiwa Wabunge, ni lazima lizungumzwe kwamba wasiwasi ni lazima uwepo juu ya usalama wa nchi yetu. Ni kweli tumezungukwa na nchi ambazo zina matatizo na nyingine zimekuwa na matatizo kiasi ambacho silaha nyingi za moto zimekuwa *free,* zinaachiliwa tu hivi kiholela. Tena nichukue nafasi hii kuwapongeza Askari Polisi, walikuwa na mkakati wa nguvu tena wa nguvu kweli kwa muda wa miaka mitatu juu ya kusajili, kuziweka hizi silaha katika sehemu nzuri na kuwagundua nani anayo na nani hanayo katika mradi unaoitwa *Small Disarmament Project,* nayo pia ilikuwa imesimamiwa na Afrika ya Mashariki.

Vilevile nitoe taarifa kwamba kuna mahusiano ya karibu juu ya kuzuia maharamia; *Alhamdulilah!* Kwa hiyo, nazungumzia juu ya usalama. Kwa hiyo, uko ukaribu mkubwa sana na ndiyo maana unaona kwamba kupeana habari baina ya nchi zetu hizi ni mzuri na Askari wetu wako makini na raia wema nao vilevile wawe katika msimamo wa busara wa kutuletea taarifa hizi ili Askari wetu wazifanyie kazi. Tumshukuru Mungu kwamba yanayotokea huko nje mpaka hivi sasa hayajatokezea kwetu na Mungu aepushe mbali yasitokee.

Mheshimiwa Kombo pia aliulizia juu ya suala la Serikali kwamba inatoa kauli gani kuhusu msongamano katika mipaka ya Tanzania na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki? Ni lazima tukubaliane kuwa kulikuwa na msongamano mkubwa sana wa bidhaa, wa magari na hata abiria baina ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Kombo kwamba kwa upande wa bidhaa, uharaka wa kuvuka tumepunguza katika *levels* mbili. *Level* ya kwanza bidhaa zote katika mfumo wa *Single Custom Territory* zinapoingia Bandarini, basi zinakuwa na hatua tatu tu za kupimwa hasa mizigo mikubwa katika mfumo wa *Single Custom Territory.* Malipo hayatalipwa Dar es Salaam, yanakwenda kulipwa kule mzigo unapokwenda kupakuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi sasa utaratibu upo vituo vimekuwa ni vitatu badala ya 15. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo linarahisisha biashara. Lakini pia Kituo cha kwanza ambacho kitakuwepo pale Kibaha kwa mbele ambacho kinajengwa, kitakuwa na *way in motion,* yaani hata magari pale yatakuwa hayasimami. Kwa hiyo, hii ni moja katika taratibu ya kuondoa msongamano wa magari katika njia zetu.

Vile vile hata mipakani kuna kitu kinaitwa *One Stop Boarder Post;* hivi ni vituo ambavyo uhakiki wa bidhaa unafanywa katika sehemu moja, Maafisa wawili kutoka Tanzania na wengine kutoka nchi yoyote katika nchi jirani. Faida yake imeonekana na hivi vituo viko katika mipaka kuanzia Holili, Sirari, vinazunguka Rusumo; na Desemba, mwisho wa mwaka huu, 2014 imekusudiwa kwamba vituo vyote hivi vitano vifunguliwe kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo Wizara imetushauri, na Wabunge wengi wameshauri kwamba ndani ya Muundo wa Wizara kuwe na kitengo cha Utafiti. Siyo jambo baya na kusema kweli Wizara imeshakaa kitako na imeshatoa muundo ambao baada ya kujadiliana na wadau wengi ambao wanatakiwa, tumeshapeleka utumishi. Kwa hiyo, hivi sasa tunasubiri kauli ya Utumishi watasaidia vipi.  Lakini je, swali, tulale tu tusubiri Utumishi? Hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho sasa hivi tumekifanya ndani ya Wizara ni kwamba tumeamua chini ya Kitengo cha Mipango kwamba tafiti zote ambazo ni muhimu tunashirikiana na *BOT*, Wizara ya Fedha, Kitengo cha Takwimu *(statistics)* na tunashirikiana na Wizara ya Viwanda juu ya tafiti tofauti na kwa kweli tunashukuru kwa hawa wenzetu kutukubalia, tunawa-*outsource* na wanakuja wanafanya *consultancy* kwa tafiti ambazo zipo kwake.

Kwa hiyo, siyo kwamba tunakuwa tumelala tu. Pindi itakapohitajika, basi tunaweza tuka-*outsource research* kwenye Taasisi nyingine husika ambazo zinaweza kutupa matokeo. Kwa hiyo, siyo kwamba tumelala. Lakini ukitazama kiuhalisia, hata hawa ambao tungekuwa nao pale isingekuwa rahisi kwamba wangeweza kuingia katika nyanja zote, isipokuwa ni kitengo ambacho kinasimamia tafiti. Kwa sababu unaweza kusema kwamba sasa hivi kuna tatizo la kijeshi, lakini mtafiti uliyekuwanaye ni ya *economical diplomacy*. Kwa hiyo, ni suala ambalo linahitaji kuingiliana katika masuala ya kutatua matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Tanzania katika makubaliano yote tutakayoingia; kuna hoja nyingi ambazo zimekuja kimaandishi kwamba katika makubaliano yote ambayo tumeingia, Tanzania ihakikishe inalinda ardhi. Hilo ni suala ambalo halina mbadala, ni jambo ambalo limeshajadiliwa na limeshaamuliwa ndani ya *common market protocol* na ndiyo tunaloendelea nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sera kama hii ya mtangamano tuliyozungumza, kuna Waheshimiwa Wabunge walisema vile vile zisambazwe. Niseme tu kwamba hizi sera bado ziko katika *stage* ya mwisho ya kukutana na wadau, lakini ikishatoka kwa wadau tu, siyo kitu cha kukificha, kinaweza kuja, kitakuwa bayana, kitatazamwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwa uwazi juu ya Sera ya Mtangamano wa Kikanda, tayari Rasimu yake imeshapatikana, ipo katika *level* ya kujadiliwa na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja moja tunaulizwa; katika kutengeneza mikakati ya Kitaifa: Je, Wizara inafuata taratibu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kabisa ifahamike kwamba Wizara yetu pamoja na Wizara nyingine zote za kisekta, katukatu hatuwezi kwenda kwenye majadiliano pasipokuwa na uchambuzi, majadiliano yakinifu na mwisho wake kuwa na mkakati wa pamoja wa kinchi, na tunapofika pale tunasema tunakwenda pale katika mkakati wa nchi ambao umewekwa.

Kwa hiyo, naamini kwamba Wabunge na wananchi wataamini hilo kwa sababu Wizara yetu sisi ni Wizara ambayo inafanya *coordination* na *coordination* hiyo tutaamini mpaka sasa hivi inakaaje. Ndiyo maana wakati mwingine unaweza kuambiwa kwamba Tanzania tuna *leg behind,* lakini Mbunge mmoja alisema kwamba Tanzania vile vile ndiyo keki. Sasa unajua kwamba mti ambao una matunda mazuri hauachwi kupopolewa kwa kila hila!

Kwa hiyo, wakati mwingine sisi inabidi tukae, tupime na tujadiliane tena kwa kina, mara moja, mara mbili ama mara tatu kabla hatujatoa nchi kuipeleka katika maamuzi ambayo yana uhakika wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yapo mengi sana lakini kulikuwa na hili suala ambalo ni dogo tu, kuna mtu alisema Wabunge wa *EALA* waje Jimboni. Mimi sio msemaji wao, lakini naamini kwamba ni jambo ambalo wanalizungumza, mimi nakaa nao sana na wanataka kuja Jimboni na ndiyo sehemu ambayo wao wanaamini kwamba watakuwa na maingiliano mazuri sana kwa niaba ya wananchi na siyo kwa niaba ya *executive arm*, ili waweze kuwakilisha kiuhalisia na naamini kwamba wakifika Bungeni watatoa mawazo na maingiliano yataongezeka.

Kuna suala lilikuja kwamba tunaulizwa kwamba tupo katika ngazi gani kwenye *monetary union*?

Waheshimiwa Wabunge, lazima niseme kwamba *monetary union protocol* yake imeshajazwa. Kufikiwa kwake inabidi, lazima yale ambayo tumeyataja katika kitabu yakamilike. Kwa hiyo, hivi sasa siyo rahisi kusema kwamba Tanzania imeshakamilisha mangapi? Kama kuna Mbunge fulani alivyouliza lakini ni wazi kwamba Tanzania kwa kukopeshwa tunaweza kukopesheka, ndani ya Afrika Mashariki kuna nchi ambazo haziwezi kukopesheka; *deficit* yetu na *inflations* zetu, sisi ziko nzuri kuliko baadhi ya nchi nyingine. Kuna wakati tunashindwa kutoa hizi takwimu lakini Mheshimiwa aliyeuliza tutamjibu kimaandishi.

Kulikuwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi aliulizia suala la zile mali za Afrika Mashariki ya kabla ziko wapi? Zile zilikuwa zinarudishwa katika vitengo husika, havikukabidhia kwetu sisi.

Mheshimiwa Selasini yeye aliulizia vilevile kuhusu mambo ya msongamano lakini ni kama nilivyojibu kwamba msongamano katika mipaka mpaka sasa hivi umepungua sana. Vilevile alizungumzia kuhusu namna gani tunaweza kuimarisha mienendo ya wananchi mipakani.

Kwanza, nimpongeze yeye mwenyewe jinsi alivyoshughulika. Alishughulika sana wakati tunaenda kufanya ziara pale. Lakini vilevile aliibua jambo ambalo limeonyesha kwamba kidogo lilikuwa na msingi mzuri kwamba aliwatakiwa mpaka upande wa pili kule, upande wa Holili kuwe na Benki ya *CRDB* na taarifa hizi tutazipeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hapo nilipofika, mambo ni mengi sana, nisingeweza kuyamaliza, lakini nilijaribu ku-*highlight* yale ambayo yalikuwa ni muhimu na *controversial* na *contentious* lakini Mungu akipenda wakati wa kupitisha vifungu vyetu, pindi kama itahitajika basi tutakiwa tayari kuwajibu Waheshimiwa Wabunge na imani kwamba hawatakuwa wagumu sana kwa sababu Wizara hii ni mtambuka na tunategemea kwamba inawakilisha Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuna utaratibu wa kuwa na wageni asubuhi na jioni na orodha ni ndefu, naona bora niisome kabisa. Wageni waliopo Bungeni jioni hii, wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wageni wa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda kutoka *Alliance Club International* ambao ni Bwana Wilson Ndesanjo, *Governor* wa *Club* Tanzania na Uganda. Ahsante, karibu! Dkt. Hussein Hassa, Mwenyekiti wa *Clouds* wa Kanda. Bwana Said Abdul Hai Kadri, Mjumbe; Bwana Emo Bakari, Mjumbe. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mbunge na Waziri wa Maendeleo ya Uvuvi ambao ni Dkt. Charles Nyamrunda, Katibu Mkuu; Dkt. Yohana Bedeba, Naibu Katibu Mkuu, karibu sana. Magdalena Mawaka Mlengeya, ni mke wake, karibu sana. Wenyeviti wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mandeleo ya Mifugo na Uvuvi, karibuni sana. Wakurugenzi wa Idara, Vitengo na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Uvuvi. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ni kama wafuatao:-

Viongozi na Watendaji wanane kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Busega, wakiongozwa na Ndugu Paul Mzindakaya, Mkuu wa Wilaya ya Busega. Ndugu John Charles Lukale, Mwenyekiti wa Halmashauri, Wafugaji watatu kutoka Chama cha Wafugaji Kanda ya Ziwa ambaye ni Hamisi Bitego, Johansein Kabuzi na Richard Mzuka. Karibuni sana. *(Makofi)*

Viongozi 13 kutoka Chama cha Wavuvi Tanzania, wakiongozwa na Ndugu Thomas Minyaro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wanne kutoka Tanzania *Commercil Policy Association* wakiongozwa na Ndugu Lameck Chavon Msaidizi wa Katibu *TCPA*. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Viongozi 21 ambao ni wanachama wa Chama cha Wafugaji Tanzania. Karibuni sana. Kuna wageni 15 wa Mheshimiwa Mwigulu Lameck Mchemba, Mbunge na Naibu Waziri wa Fedha kutoka matawi ya CCM wakiongozwa na Ndugu Charles Selemani. Karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Rose Kamili, Mbunge ambaye ni Ndugu Ignas Winboard (Mtoto wake). Karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kujaribu kujibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wameziongea kuhusu Wizara yangu ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Nawashukuru sana, Wabunge wote 21; tisa kwa kauli na 12 kwa maandishi ambao kwa kuwa sio wengi naomba unisamehe niwataje. Mheshimiwa Mohamed Seif Khatibu, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Raya Khamis, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Kombo Khamis, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi na Mheshimiwa Tundu Lissu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulisema mambo fulani ambayo nayo lazima nikutambue na Mheshimiwa Mbowe. Kwa maandishi Mheshimiwa Khatibu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ungeendelea tu, uache wengine.

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vizuri. Sasa labda kwa heshima labda nianze na hili lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulisema kwamba Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki hawaelekei kuhudumia vyema ambayo ni kweli. Tatizo letu limekuwa ni utaratibu upi utumike ili huduma stahili kama nyenzo, Ofisi, magari na kadhalika wapate.

Suala hili limechukua muda kuanzia mwaka wa fedha wa juzi mpaka mwaka wa fedha huu tunaoumaliza, ndiyo tumeweza kuelewana kwa misingi ya Kikatiba kwamba Wabunge hawawezi kuhudumiwa kupitia Wizara kwa sababu ni sehemu moja ya kutunga Sheria.

Sehemu zote, utaratibu bora ni kwamba Bunge la nchi husika linahusika na Wabunge wake wanaokwenda katika Mabunge hayo mengine. Kwa hiyo, mwishoni mwa mwaka 2013 tumewekeana sahihi utaratibu na Mheshimiwa Spika ambapo sasa *vote* au fungu hili maalum la Bunge ndiyo linatakiwa lifanye kazi ya kuwahudumia Wabunge wetu.

Natumaini katika makadirio ya mwaka huu, hili litakuwa limefanyika na kwa hiyo, haya mengi yaliyokuwa yanazungumzwa kama vile kupatiwa Ofisi na sisi tulipendekeza wapatiwe Ofisi Dar es Salaam kwa sababu Wabunge wa *East Africa* wanakutana zaidi na watu kutoka Mataifa mbalimbali ambao ni rahisi zaidi kuwa Dar es Salaam.

Naelewa kwamba Mheshimiwa Spika na timu yake wanafanya juhudi kuweza kuwapatia Ofisi Wabunge wa *EALA* na mimi nadhani hata yale mambo ya kupata nyenzo kama magari, vifaa vya Ofisi na kadhalika, yatashughulikia kwa mtindo huo. Kwa hiyo, tunatumaini sasa kuanzia mwaka huu wa fedha 2014/2015 suala hili haliwezi tena likajirudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo yamejirudia hapa. La kwanza ambalo Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman mbowe amezungumzia, la msingi tu; ni je, kuna utayari kweli wa Tanzania kuingia katika huu mtangamano kwa nguvu moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania haina nia yoyote ya kuwa ni kikwazo katika kuendeleza ushirikiano wa Kikanda hususan Afrika Mashariki ambapo ndilo eneo letu rasmi kabisa. Tunazungumza lugha moja, Kiswahili; jiografia imetuweka pamoja na hususan nchi hizi tatu; Kenya, Tanzania na Uganda.

Tumefurahi wenzetu hawa wawili, Burundi na Rwanda wamekuja na hatimaye tunategemea Sudan ya Kusini na baadaye hata Somalia itakaporejea katika hali ya amani nayo inaunga vizuri sana eneo la Afrika Mashariki kuwa moja.

Tatizo linalotufanya Tanzania tuonekane kama vile tuko baridi kidogo, ni fundisho tulilolipata mwaka 1977. Jamani Jumuiya hii ilipovunjika mwaka 1977 athari kwa Tanzania ilikuwa ni kubwa sana. Tulipoteza kabisa Shirika la Ndege, Makao Makuu ya Bandari yalikuwa Mombasa, Shirika la Posta na Simu lilikuwa Kampala.

Baada ya yote haya, tukajikuta sasa tuna miaka kumi ya kuhangaishana, kutokuelewana, mpaka ukafungwa, biashara na Kenya ikasimama hadi hapo alipokuja yule Mswiss, msuluhishi Prof. Umbridge ndio akatusaidia tukagawana baadhi ya mali.

Kwa hiyo, tunapoanza upya, tukumbuke Waheshimiwa Wabunge kwamba Tanzania ni asilimia 52 ya eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa ukubwa huo kama ilivyo kwa kitu chochote katika mwanguko, ukiwa mkubwa zaidi ukianguka, athari inakuwa kubwa. Mtu mwepesi hivi akianguka, hasara yake ni ndogo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunakwenda kwa uangalifu sana katika mambo mengi. Huu mwelekeo wa kuonekana sisi ni waangalifu ndiyo unatuponza tueleweke eti kana kwamba hatutaki kushiriki vizuri katika Jumuiya, lakini siyo kweli, tuna tahadhari nyingi za kuchukua mathlani kuhusu Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tu wakulima na wafugaji wetu wanapambana. Leo tungefungulia tu mipaka wenzetu Wanyarwanda, Warundi, eneo zima la nchi ya Rwanda kwa mfano ni kilometa za mraba 26,000,000, kwa huku bara ni kama Wilaya moja. Lakini idadi ya watu ni milioni 10. Wana wingi wa watu, yaani ukisema *density,* ni zaidi ya watu 600 kwa kilometa ya mraba moja, ukilinganisha na Tanzania watu 43 kwa kilometa ya mraba moja.

Kwa hiyo, mambo haya ukiyafungua tu hovyo hovyo uonekane tu mzuri unapenda kushirikiana, sasa watakula kwako. Maana wote hawa wakija kwa uzito uliopo; na ndio maana mikataba mingi inayosema kuna haki ya mtu anaitwa Mwaafrika Mashariki; sisi Tanzania tunaikataa, kwa sababu hatujampata raia wa Afrika Mashariki. Ukishasema ni raia, maana yake apate haki sawa. Haki sawa ni pamoja na haki za ardhi na haki nyingine.

Kwa hiyo, tunakwenda kwa uangalifu na mara nyingi misimamo yetu inakuja hatimaye kukubalika kwa sababu imechujwa vizuri sana.

La pili, linalohusiana na hilo ni Umoja wa Utatu ambalo vyombo vya habari limeuita *coalition of the willing*. Hili siyo jina rasmi, wamejiita wenyewe tu. Waandishi wa Habari wamewaita wao eti ndio *willing.* Sijui *willing* kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichopo hapa ni kwamba Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaruhusu nchi zozote zinapokuwa tayari kushirikiana katika mambo ambayo yanawagusa ndani ya mfumo wa Afrika Mashariki kuendelea na jambo hilo. Mathalani, katika Afrika Mashariki tunazo kanda mbili za usafirishaji, Kaskazini ambayo tunaita *Northern Corridor* inawagusa Rwanda, Uganda na Kenya, Kusini tuna *Southern Corridor* ambayo wengine wanaita *Central Corridor* inagusa nchi ambayo siyo mwanachama nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi na sisi, wanatakiwa kupitia *Central line*. Kwa hiyo, kilichofanyika hapa ni kwamba wenzetu wanakutana kupata ufumbuzi wa miundombinu ya *corridor* ya Kaskazini. Mwaka huu na sisi tutakuwa na mkutano pamoja na Burundi na tunawakaribisha Jamhuri ya Demokrasia ya Congo tuhangaike na *central corridor.* Hatuwaaliki Sudan wala siyo lazima Uganda waje, tutawapa taarifa tu lakini *Central Corridor* inawahusu zaidi DRC, Burundi na Tanzania, kwa sababu ndiyo njia ya mkato kufikia bandari ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, haya mambo ni ya kawaida tu, ni mambo ya ushirikiano ambayo yanahusu kuharakisha kile ambacho kipo karibu yetu kwa manufaa ya wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Uganda tunawavutia kwa kuunadi mradi wa reli kutoka Musoma kwenda Arusha na Arusha bandari itakayotumika iwe ni Tanga. Tutakapokuwa tunalizungumza hilo, tuna hiari ya kuwakaribisha Uganda na Rwanda pengine na Burundi ingawa Burundi wanatumia zaidi *corridor* ya katikati. Tutakapokuwa tunafanya hivyo ieleweke

tu kwamba ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha ushirikiano wa Afrika Mashariki lakini kwa mambo ambayo yanazigusa nchi chache zaidi kuliko nchi zote tano zilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati tukiwa hapahapa Bungeni alimwakilisha Mheshimiwa Rais katika mkutano wa hao mnaowaita *Coalition of the Willing* kutazama mambo ya kuweza kupanga mitaji ya kuendesha shughuli za mafuta ambayo yamepatikana kwa wenzetu Kenya na Uganda. Je, tujenge mabomba au itakuwaje na sisi pia tunanadi miradi ya gesi. Kwa hiyo, ushirikiano huo usimpe mtu yeyote wasiwasi wala sisi hatuna wasiwasi hata kidogo wanapokutana Kenya, Uganda na Rwanda. Mambo mengine jamani yanakuzwa tu na vyombo vya habari yaonekane ni mambo ya ajabu, mngeshuhudia katika mikutano yetu tunavyokaa sisi ni marafiki, tunatambuana kwamba ni ndugu na tunaishi vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa kuhusu miradi ya Zanzibar. Kumekuwa na shauku iliyo dhahiri kwa wenzetu Wabunge kutoka Zanzibar kwamba pengine Zanzibar haipati msisitizo katika miradi yake, hii siyo kweli. Kwanza, kuna mambo mawili, kuna mambo ya Muungano ambayo yanatuhusu kwa pamoja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki halafu yapo mambo ambayo siyo ya Muungano. La kwanza, kwa yote mawili, mfumo wetu ambao nadhani haujaeleweka vizuri ni kwamba ipo Idara chini ya Rais wa Zanzibar inaongozwa na Waziri, Mheshimiwa Mwinyihaji Makame ambayo ndiyo mahali ambapo kuna uratibu wa shughuli zote zinazohusu Zanzibar ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, liwe ni la Muungano lisiwe la Muungano kama vile miradi yote yanashirikisha Ofisi ya Rais wa Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge, niwaambieni jamani hakuna mwaliko wowote tunaokwenda katika Jumuiya ambapo sisi hatuna wenzetu wa Zanzibar, hata mkutano mmoja ingekuwa ni jambo la ajabu. Kwa sababu utaona basi kama jambo linahusu Wizara mathalani ya Mawasiliano, Mheshimiwa Waziri Makame anawaarifu wale Mawaziri wa SMZ wanaohusika na tunakwenda kama *delegation* moja, msafara wetu unakuwa ni mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapotoa taarifa hapa kuhusu miradi ya Zanzibar ambayo siyo ya Muungano ni wajibu wetu tu kufanya hivyo lakini kwa kweli Baraza la Wawakilishi lina kila haki ya kuwahoji Mawaziri wa SMZ kuhusu sekta zote ambazo si za Muungano kwa sababu wao Mawaziri wanashiriki katika miradi hiyo. Kwa mfano, unapozungumzia uwanja wa ndege wa Pemba, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri hapa au bandari ya Zanzibar na kadhalika, hata ule ushirikiano na Sekretarieti unakuwa wa moja kwa moja na sisi wanatupa taarifa katika miradi hiyo. Ndiyo maana hatua mbalimbali, upembuzi yakinifu, *full engineering study* ya miradi hi imefikia hatua hiyo na kupitia *ADB* kwa sisi Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushirikiana. Kwa hiyo, hakuna lililoachwa au kusema kwamba limepuuzwa kwa sababu labda ni la Zanzibar hapana! Ila utengano huo ni lazima kuuzingatia kwa sababu sisi hatuwajibiki hapa Bungeni kwa masuala ambayo siyo ya Muungano. SMZ inao Mawaziri, wanashiriki kwenye vikao vya Afrika Mashariki na wanastahili kuhojiwa kwa yale ambayo siyo ya Muungano, wanastahili kuhojiwa ndani ya Baraza la Wawakilishi. Mnapoyachanganya haya mawili ndiyo tunaona tunapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuchelewa kwa upembuzi yakinifu wa uwanja wa ndege Pemba, kuchelewa huku hakuwezi kulalamikiwa kwa Serikali ya Muungano kwa sababu upembuzi yakinifu wa uwanja wa ndege Pemba unafanywa na Serikali ya Mapinduzi na ndivyo hata mkataba tulionao unasema hivyo. Kwa hiyo, ukiyachukua yote kwa pamoja, ya Muungano, yasiyo ya Muungano ukayauliza yote kwa Waziri wa Afrika Mashariki nadhani mkakati huo unakuwa kidogo mgumu kwa sababu hatuendi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushiriki wa Wabunge wa *EALA* katika kuleta taarifa zao na kadhalika, kama nilivyosema awali, mambo haya nayo yote yamekabidhiwa Ofisi ya Spika. Inatakiwa Katibu wa Bunge kwa kuwasiliana na Katibu wa *EALA* taarifa za kila robo mwaka zitufikie hapa kupitia Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ili hayo inapoonekana kwa mujibu wa Kamati kwamba yanahitaji mjadala humu ndani basi yanaweza kuletwa. Kazi yetu sisi kama Wizara ni uratibu wa hayo mambo lakini hatuwezi kuleta hapa na kuomba kwenye *Order Paper* iwekwe ajenda ambayo inahusu *East Africa Legislative Assembly* kwa sababu hilo ni suala ambalo litashughulikiwa Kibunge kupitia kwa Kamati inayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka mwaka juzi nadhani kidogo tufanikiwe kupata Kamati ya masuala ya Afrika Mashariki lakini ikaonekana siyo busara ndiyo maana ikaunganishwa na Kamati ya Mambo ya Nje baada ya kutenganisha ile Kamati ya Ulinzi na ile ya Mambo ya Nje. Kwa hiyo, huo ndiyo mkondo ambao ulitakiwa upite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nigusie kidogo suala la Mheshimiwa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki, suala hili lipo Mahakamani hivi sasa, Spika mwenyewe amelipeleka Mahakamani, Waheshimiwa Wabunge wa *EALA* walikuwa wanataka kung'ang'ania kumng'oa, hatujui litaishia wapi. Kwa sababu liko Mahakamani, kilichotokea ni kwamba sasa Mahakama imezuia huyu Spika asijadiliwe lakini shughuli za *EALA* zisisimame, hiyo ndiyo amri ya mwanzo ya Mahakama. Mambo ya Bunge yataendelea na wiki ijayo kuna kikao Arusha ambapo Bunge la Afrika Mashariki litaendelea na kikao chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matendo ya Mbunge mmoja mmoja wengine wanagoma, hayo yanayotokea katika Mabunge yetu pia, kwa hiyo hatuwajibiki kujua tena sababu zao ni nini na kadhalika kwa sababu ni uhuru wa kila Mbunge kufanya analoweza kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeulizwa pia juu ya mikakati ya kujiimarisha ili jiografia itupe tija. Hili ni kweli kabisa, sisi tupo pazuri, tuna bandari kubwa tatu, Tanga, Dar es Salaam na Mtwara na zote hizi zinatupa tija kubwa katika kuhudumia mizigo, abiria na hata kuendeleza masuala ya utalii kama alivyosema Mheshimiwa Fatma Mikidadi kule Lindi na kadhalika kuna historia kubwa sana ya Mji wa Kale wa Kilwa. Yote hayo ni mambo ambayo yanaipa Tanzania tija na ni lazima tuitumie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ni mingi, sisi katika nchi hii tumekwishafanya utafiti wa kujenga *standard gauge line* kuibadili kabisa kuanzia Dar es Salaam hadi Kigoma na ndiyo maana reli mpya tunayoipanga ya kutoka Uvinza kwenda Msongati ni *standard gauge* kwa sababu hatimaye reli zetu zote hata ile ya kwenda Tanga, Ruvu Mnyusi na kadhalika zitakuwa katika mfumo wa *standard gauge*. Maelezo zaidi nadhani Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi ataweza kuwapatia pale ambapo atakuwa anatoa maelezo ya bajeti yake ni mikakati gani ameipanga lakini sisi kama Waratibu tunaelewa kwamba mikakati hiyo ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza usafiri wa anga kwenda Bunjumbura kutumia Air Tanzania, tunazungumza na Kenya kuhusu kampuni zetu za ndege kwenda Nairobi mara nyingi zaidi kuliko ambavyo tunafanya sasa. Ni suala la kukuza tu uwezo wenyewe. Tunaelewa kwamba kuna kazi kubwa inafanywa ya kuendeleza bandari zetu, Tanga Mwambani, Dar es Salaam kwa yale magati mapya ambayo yatajengwa pamoja na kukarabati yale magati namba moja mpaka saba, yote hii ni namna yetu ya kujaribu kuhakikisha kwamba tunachukua sehemu kubwa ya biashara ambayo jiografia imetuweka vizuri kuweza kuipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa kifupi tu nimalizie ushauri ambao tumepewa, namshukuru sana Mheshimiwa John Mnyika ametupa ushauri mzuri sana kuhusu mambo mbalimbali katika mchango wake wa maandishi. Moja hili alilolitolea ushauri kwamba ni vizuri

maandalizi ya sera mbalimbali ambayo kwa upande wetu sisi yanaratibiwa na Wizara ya Mambo ya Nje, ni muhimu sana rasimu ya sera hiyo ikatolewa maoni na wadau, hiyo ndiyo hatua inayofuata. Rasimu sasa tunayo ya Sera ya Mtangamano wa Afrika Mashariki, tutaifikisha kwa wadau mara baada ya muda wa Bunge hili (mara baada ya June 30th). Tukishapata maoni ya wadau na hapa tunakusudia zaidi wafanyabiashara kwa sababu wao ndiyo injini itakayotusaidia kwenda mbele, kushindana kibiashara na wawekezaji wa viwanda ili tuweze kuwa na ushindani mzuri.

Mheshimiwa Mnyika pia alipendekeza juu ya Wabunge wa *EALA* kuweza kutoa taarifa zao, hilo nalo tumelizingatia.

Mheshimiwa Akunaay amesema bajeti yetu ni ndogo, ni kweli lakini tumejitahidi katika bajeti hiyo ndogo kufanya mambo mengi, tunachoomba mwaka huu kwa kushirikiana na Wizara ya Utumishi tuunde ile Idara ya Utafiti kwa sababu mambo haya ya ushindani katika biashara bila kuwa na Kitengo au Idara ya Utafiti itakuwa ni vigumu sana kuweza kushindana. Kuna mambo mengi yanatokea yanahitaji kufanyiwa utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Amina Abdallah Amour amesema shirikisho halina haraka, ni kweli na hapa nigusie alichosema Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu kuonekana tunaharakisha shirikisho. Hatuharakishi shirikisho, ila shauku, ilipotumwa ile Tume ya Profesa Wangwe, raia wa Afrika Mashariki walikuwa na shauku ya kujua hivi shirikisho litaonekanaje kabla hata hujalifikia. Watu wajue unazungumzia shirikisho la kuunda nchi moja au vipi, *decentralized model* na kadhalika. Tunahangaika na hilo hivi sasa ili tunachokinadi kiwe kinajulikana. Kwa hiyo, siyo kwamba tunaunda ili tuungane kesho, tunatengeneza rasimu tuitazame, ipate maoni ya wananchi ili hatimaye wao watakapokuja kupiga kura maana yake mkataba wa Afrika Mashariki unasema ili kufikia hitimisho la kuwa na shirikisho ni lazima tushirikishe wananchi wote wa Afrika Mashariki kwa kura ya maoni. Natumai wakati huo, tumejifunza safari yetu ya kutengeneza Katiba hapa imekuwa ni ngumu, hivyo ni lazima twende kwa uangalifu kidogo. Kuna wenzetu wanakuwa kidogo wepesi wa kukasirika na kuonyesha hisia zao, ndiyo siasa ilivyo. Sisi wenye ngozi ngumu siyo wengi sana, mimi ukinikwaruza hapa hupati lolote lakini wengine wanataka kupigana, wengine ukianza tu hoja wanatoka nje, aaah! Ni mambo ambayo ni lazima tuvumiliane. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,, sasa hii tu ni nchi mbili, leo hii nchi tano au ikiingia na Sudan nchi ya sita, ikiingia na Somalia nchi ya saba itakuwa balaa kubwa kabisa! Mimi nadhani kuna pendekezo hapa eti kwamba kama tumeshindwa kuelewana na wenzetu hawa, tunakwaruzana sijui na nini, basi tuwapeleke wapinzani. Mimi nashangaa kweli pendekezo hili, kwamba ili tupatanishwe na wanachoona wao kwamba tunagombana nao, tuwatume wao, wakisusa je? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja hiyo imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, leo matangazo ni mengi lakini hili ni tangazo muhimu sana kwa Wabunge wetu. Kesho Ijumaa tarehe 23 Mei, 2014 kutakuwa na hafla fupi ya kuwaapisha Wahandisi wote waliosajiliwa waliopo Dodoma na maeneo jirani katika ukumbi wa *African Dream Area* D, Dodoma. Awamu hii ya uapishaji ni mwendelezo wa zoezi la utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Bunge ya Bodi ya Usajili wa Wahandisi Tanzania, Sura ya 63 ya mwaka

2007, ambayo inahusu Wahandisi watalaam (*Professional Engineers)* wote waliosajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Wahandisi wafuatao ambao ni Waheshimiwa Wabunge wanashauriwa kutenga muda ili washiriki kula kiapo kitakachofanyika mbele ya Kamishna wa Viapo na kushuhudiwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Mbunge na Waziri wa Ujenzi. Tukio hilo litafanyika kuanzia saa tatu hadi saa tano asubuhi. Wahandisi hao ni *Engineer Prof*. Mark James Mwandosya, Namba ya Usajili PE715; *Engineer* Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Namba ya Usajili PE2900; *Engineer* Christopher Kajoro Chiza, Namba ya Usajili PE1529; *Engineer* Gerson Hosea Lwenge, Namba ya Usajili PE552; *Engineer* Dkt. Charles John Tizeba, Namba ya Usajili PE1446; *Engineer* Stella Martin Manyanya, Namba ya Usajili PE1656; *Engineer* Ramo Matala Makani, Namba ya Usajili PE2236; *Engineer* Omar Rashid Nundu, Namba ya Usajili PE495 na *Engineer* Hamad Yussuf Masauni, Namba ya Usajili PE2939. *(Makofi)*

Kwa niaba ya Mheshimiwa Spika, nawapongeza wote waliopata usajili huu na ambao kesho wanakwenda kula kiapo, Katibu!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 97 – Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Kif. 1001 – *Administration and*
*HR Management*……… ............Tshs.4,898,202,000/=

**MWENYEKITI:** Haya tuna mshahara wa Waziri, mlichelewa lakini na mkichelewa mnaondoka tu. Subirini basi, mbona mna mumkari.

Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida tuna majina ambayo tayari tumeshapewa na vyama husika. Naanza na Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, umo humo, kama unataka kujifuta, jifute tu.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Atazungumza Mheshimiwa Wenje.

**MWENYEKITI:** *Okay,* tunakwenda kwa Mheshimiwa Michael Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama kwa sababu nataka ufafanuzi kwa sababu mimi nahusika sana, niko mpakani, kwa hiyo, nilitaka sana ufafanuzi kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbowe kwamba ni kama sisi Watanzania hatujajiandaa. Pale mpakani tunayaona majengo yanajengwa, ni kama mradi wa mwekezaji ambao hautuhusu sisi. Hakuna semina wala elimu inayotolewa kwa wananchi ili wafahamu kwamba nini kinaendelea. Wenzetu wamejiandaa vizuri. Upande wa Kenya wana Ofisi na mtaalam yuko pale ambaye yeye ndiye anatoa elimu, yeye ndiye Afisa Mahusiano, kama kuna jambo lolote ambalo liko upande wetu ambalo halieleweki, yeye ndiye anayewaeleza wa Kenya, yeye ndiye Mshauri Mkuu wa Wakenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka ufafanuzi kwa sababu kwa hili nasema nitatoa shilingi kama sikupata ufafanuzi kwamba kwa nini Serikali yetu imekaa kimya bila kuwapa Watanzania elimu katika jambo hili ambalo ni muhimu sana katika nchi hii. Jumuiya hii ni ya wananchi, siyo ya mwekezaji, Shirikisho hili linawahusu sana wananchi hasa walioko mpakani, nataka nipate ufafanuzi.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tumepata kulizungumza na Mheshimiwa Mbunge. Tatizo hapa ni kwamba sisi kama Wizara tuliomba Halmashauri zote nchini zilete majina mahsusi ya Maafisa waliopo katika kila Halmashauri bila kujali yuko Kaskazini, Kusini inapakana na Afrika Mashariki au vipi, kutoa tu elimu. Mtu huyo tumemwita *focal person* kwa maana ya kwamba yeye ndiyo atakuwa ni mahali ambapo unaweza kupata taarifa zote kuhusu mambo ya mtangamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Wilaya ya Longido tunaye na jina tunaweza kumpatia Mheshimiwa Mbunge kwa sababu hili siyo jambo la ajabu, wamefanyiwa semina. Tunataka kutafuta kupitia *TMEA - Trade Mark East Africa,* tunatafuta vifaa waweze kuwa na *computer* ili waweze kuwa wanawasiliana kwa urahisi kabisa na Makao Makuu kupata taarifa zote za kisasa ambazo zinahusu mtangamano wa Afrika Mashariki, fursa za biashara, uwekezaji, masuala ya kisheria na taratibu. Tunalo jina, nadhani wataalam wangu hapa wanaweza kunipatia kwa sababu nisingeweza kuwa na majina ya *focal persons* wa Wilaya zote za Tanzania kichwani lakini tunao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa sana katika Jumuiya hii kwa sababu wenzetu wanaweka vikwazo vingi sana kwa wafanyabiashara wetu wanapokwenda kupeleka biashara huko Kenya. Hatufahamu kwamba ni nani …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer kipindi hiki nafasi yako ni kusema sasa natoa shilingi na sasa nachangia.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Natoa shilingi na nachangia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Pia naomba Wabunge wenzangu waniunge mkono kwa sababu sisi tuna vituo vingi sana vya mpakani. Tuna karibu vituo sita, tuna Holili, Sirari, Mtukula, Horohoro, Rusumo na Namanga. Katika nchi zote hizi hakuna nchi yenye vituo kama Tanzania lakini sisi Watanzania ndiyo tunazembea kuliko watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa wafanyabiashara wa Tanzania wakibughudhiwa kule Kenya lakini Wakenya wanafanya biashara huku *free*. Wenzetu wametusoma, niliwahi kusema hapa tujengewe soko kubwa pale Namanga, kwa sababu wenzetu wanataka nao kujenga soko lakini sisi tuanze…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer hoja yako ya kwanza ilikuwa ni elimu na wenzetu Kenya wanao watu wanaotoa elimu lakini kwetu hakuna. Mheshimiwa Waziri amekujibu kwamba mtoaji elimu yupo na hivi sasa anasubiri jina liletwe na wataalam wake ili akupatie. Sasa kesho uende ukamfuate huyo anayetoa elimu umhoji kwa nini hatoi elimu.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa hapo naomba usiisaidie Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Subiri Mheshimiwa Laizer, wewe ndiye mwenye hoja umeisema hiyo sasa unaisema hoja nyingine ya biashara na vituo unaongeza tena *it is not fair*. Ukipata nafasi ya kusimama unasimama kuchangia hoja yako ileile moja ya elimu. Sasa unaweza ukaipanua vile

ambavyo unaona wewe ambapo baadaye ita-*engage* hivyo vitu vingine. Ukienda hivyo itakuwa ile shilingi yako sasa unataka milioni siyo shilingi tena.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nimetoa shilingi, kwanza muda wangu bado haujaisha ila ukumbuke jana lilipoguswa suala la Wamachinga ukasahau kwamba wewe ndiye unayeongoza kikao ukaanza kuchangia kwa sababu wameguswa wapiga kura wako. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer, twende *specific* kwenye hoja yako.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Naomba na mimi unipe nafasi.

**MWENYEKITI:** Aah, aah, kwa utaratibu, hata mimi nilifuata utaratibu. Ulitaka kuhusu elimu basi shilingi yako iwe ni kuhusu elimu, sasa ukishaingia kwenye vituo na vitu vingine sio utaratibu. Nakubaliana na hoja yako ya msingi na wananchi wako wanakusikiliza saa hizi lakini sasa ziko Kanuni hapa inabidi nizisimamie.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumzia Kituo kimoja cha Namanga lakini vituo ni vingi na vyote vinafanana kwa sababu ni vituo vya Tanzania na hao watu hawako katika vituo vyote na hili suala sanasana litagusa wafanyabiashara, siyo kila Mtanzania atahusika na hii biashara na wafanyabiashara wa Jimbo langu ndiyo wanaumia zaidi kuliko walioko Kenya, Wakenya wanafanya biashara *free*. Kwa hiyo, naomba kwa hili naomba nipate maelezo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hoja yako wewe hawa watano waliokuwepo hawatoshi, vituo ni vingi, elimu haiendi kwa wananchi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Hata wafanyabiashara wanaofanya biashara hawana elimu yoyote wala hawana mtu wa kukimbilia kumwambia matatizo yao kama Wakenya walivyokuwa na mtu wao wa kushughulikia matatizo yao.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama kumuunga mkono Mheshimiwa Laizer kwa sababu ni kweli kabisa wananchi hawana uelewa wa kutosha juu ya fursa za Shirikisho la Afrika Mashariki na hasa sisi ambao tunatoka mipakani na hizi nchi ambazo tumeungana nazo. Nikizungumzia *with reference* na Sirari ni kweli kabisa wafanyabiashara wa Sirari au wa Tarime au Watanzania wote wanaokuja kufanya biashara kandokando pale wanapata adha kubwa sana ukilinganisha na wenzetu wa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ni juzi tu wakati wanawakilisha hapa Wizara ya Viwanda na Biashara wakasema kuna soko ndiyo limekamilika sasa hivi Sirari. Wenzetu wa Kenya miaka mingi walikuwa wameshajenga soko kule. Leo Waziri wa Afrika Mashariki pia ameonyesha jengo kwamba wanaenda kulifunga sijui mwezi wa ngapi. Hii ina-*cement* kwamba ni jinsi gani Watanzania hatupo tayari na hatu-*take* hizo *opportunity*. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna mtu ambaye ni *focal person*, huyo mtu pale Sirari mfano anafanya nini maana wananchi wa Tarime hawapo *aware* kabisa na fursa za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Laizer. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rajab.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Laizer ya kuondoa shilingi katika suala zima la utoaji wa elimu kuhusiana na masuala haya mtambuka ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imeonekana dhahiri hata wakati Mheshimiwa Waziri alipokuwa anafanya majumuisho yake hususani kuhusiana na mambo ya Muungano. Maelezo aliyokuwa anayatoa kwa kweli sisi wengine tulianza kuweka vidole mdomoni, hayafanani hata na umri wake, nafasi yake na yeye mwenyewe alivyo na majibu aliyokuwa anayatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kwamba masuala haya mengine ambayo yako kwenye Jumiya ya Afrika Mashariki yakaulizwe ndani ya Baraza la Wawakilishi, sioni kama ni sahihi. Nasema hivyo kwa sababu Wizara ya Afrika Mashariki bajeti yake inapangwa humu Bungeni, mambo yake yote yanashughulikiwa humu Bungeni, kama ni Wabunge kutoka Zanzibar wamo humu ndani lakini hata hao Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanachaguliwa humu ndani, hakuna anayechaguliwa kutoka ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kwa kweli inaonekana kwamba elimu inahitajika. Hata Waziri mwenyewe naye anahitaji elimu katika haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nchambi.

**MHE. SULEIMAN M.N SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili husema mchuma janga hula na wa kwao. Kwa hivyo, mimi nilitaka niunge mkono hoja ya Mzee wangu pale lakini nitoe angalizo kwamba watu walio mipakani ndiyo wanaotakiwa kunufaika sana na elimu, soko na kadhalika. Nilitaka niseme Kishapu pia na maeneo mengine, niunge hoja hiyo yenye mashiko, bila kutoa elimu ya kutosha maana kila mtu hulipwa kwa ujira wa palizi aliyoifanya, ukipalia heka moja basi utalipwa ujira wa heka moja. Kama elimu imetoka asilimia mbili na wenzetu wa nchi nyingine wametoa kwa asilimia 100, ni wazi kabisa mwenye palizi kubwa ndiye atakayelipwa ujira mkubwa kwa tafsiri rahisi wa eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Mzee wangu marehemu Mzee Salim, Baba yangu mkubwa, Mungu amrehemu alikuwa na ile *Passport* ya *East African*, ninayo nimeitunza sana na vitambulisho vingine. Tunajaribu kuangalia sisi Serikali yetu imekuwa na utaratibu, maana tukiwa tunasafiri kwenda Morogoro, tunajua daraja limebomoka ni lazima wakati tunaanza safari tujenge daraja. Elimu kwenye jambo hili ni muhimu, naomba sana kama mimi Kishapu sina Maafisa wa *Passport,* kwa hiyo naunga mkono hoja ya mzee hapo na ashikilie shilingi tutamuunga mkono mpaka mwisho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nchambi ahsante, Mheshimiwa Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni-*declare interest,* mimi nimefanya kazi Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa muda wa miaka tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikuwa na maeneo mengi ya kuhakikisha kwamba wanafanya *sensitization* katika nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili wananchi waweze kujua Afrika Mashariki pamoja na fursa zilizopo. Wakati niko pale kupitia Bunge la Afrika Mashariki tulikuwa na utarartibu wa kuhakikisha kwamba Bunge la Afrika Mashariki linazunguka kufanya mikutano yake kwenye nchi wanachama na mojawapo ya *activity* ambayo walikuwa wakiifanya ilikuwa ni kupeleka elimu kwa wananchi ambako wanafanyia Bunge kwa wakati huo. Nakumbuka kuna wakati tumetembea kwenye maeneo yote ya mipaka, mpaka kule Rusahunga, tunawauliza wafanyabiashara na wananchi wa kawaida namna gani ambavyo wanapata matatizo kuhusiana na kutopata *certificate of*

*origin* katika ku-*declare* vitu ambavyo vimezalishwa ndani ya nchi wanachama. Kukawa na matatizo ambayo walikuwa wanaeleweshwa hata kuvusha kreti moja ya soda kwa wananchi ambao wameoana majirani wakawa wanaona kwamba ni matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naamini kwamba kama Jumuiya ya Afrika Mashariki itaendelea na utaratibu wa *sensitization* kwa kutumia Bunge la Afrika Mashariki elimu hii itakwenda lakini nakiri kwamba bado kuna matatizo makubwa kwenye mipaka na nakiri bado kuna nchi wanachama hususani Wakenya pamoja na Waganda wanaendelea kunyanyasa wananchi wetu mipakani. Ndiyo sababu hata juzi juzi Mtukula Askari Polisi wa Uganda ameingia mpaka ndani ya nchi ya Tanzania na kupiga risasi wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwamba elimu bado inahitajika. Juhudi zinahitajika, Mheshimiwa Sitta nakuheshimu sana, jambo hili ni la muhimu Wabunge wetu muwatumie ili waweze kueneza elimu hii kwenye mipaka pamoja na wananchi ambao wako ndani ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye hili la Mheshimiwa Laizer alivyolipanua kuhusu elimu, kwanza mimi kama Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, tumetembelea maeneo yote ya vituo vya mpakani tukiwa na Waziri wa nchi jirani na Maafisa wao, tunafanya mikutano ya hadhara pale mipakani watu wengi tu wanakuwepo kwa pande zote mbili za mpaka na hatufanyi mara moja, tunafanya mara kadhaa. Elimu tunayoitoa pale ni ya moja kwa moja, tunaacha na vipeperushi na kama nilivyosema tumetatua matatizo mengi kwa njia hiyo. Isitoshe kwenye kila mpaka tumewashirikisha Wakuu wa Wilaya ili wawasiliane na upande wa pili na tumewaomba wao waunde Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Namanga, Mheshimiwa Laizer anafahamu, upande mmoja tuna *DC,* upande wa pili kwa utaratibu wao wanao ma-*Chief.* Hapa nimepata jina la *focal point* wa Longido anaitwa Mr. Nanyaro Mchumu; yuko pale Longido, Wilayani kwenye Halmashauri na kila Halmashauri ina mtu wa namna hii. Inawezekana nyenzo hazijatosha tukaweza kuelimisha wote lakini mkumbuke mpango huu sasa ni miaka miwili tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mashaka na jambo moja tunachanganya pia. Kuchangamkia biashara ni hulka ya mtu mwenyewe. Kama una kitu cha kwenda kuuza Kenya, hivi kweli unahitaji Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki akusukume, akupe motisha, ndio uende Kenya? Mbona tunao watu mbalimbali ambao tayari wanafanya biashara na nchi hizo? Tunao watu wana zabuni hivi sasa kuuza unga wa mahindi Sudan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wala sisi wenyewe Wabunge tusijiweke nje ya hili kwa sababu elimu hii sio suala la Wizara. Hii ni elimu ya sisi Viongozi wote, maana ya kuwapeni vipeperushi vyote hivi Waheshimiwa Wabunge sio kwamba mvifungie, mvisome, mtoe hiyo elimu. Kwa sababu kuwaambia watu wa Jimbo lako wakapate fursa mahali fulani sio jambo ambalo linahitaji nyenzo nyingi za kusema ni Wizara tu itatoa taarifa, itatoa elimu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther Matiko tumekuja Sirari, tumefanya hivyohivyo. Jengo lenyewe ambalo ni *One Stop Border Post* ni utaratibu mpya kwamba Maafisa Forodha na Maafisa Uhamiaji na Polisi wa pande zote mbili watafanya kazi katika jengo moja ili isilazimike mfanyabiashara kukaguliwa mara mbili. Utaratibu huu jamani unaanza mwezi

Novemba, tumekwishasema katika hotuba. Ni utaratibu mpya na sisi tunadhani utarahisisha sana biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea kwa Wakuu wa Wilaya wote wa mipakani, tumetoa utaratibu kwamba ndani ya eneo la kilometa 20 katika mipaka yetu, tumekubaliana na wenzetu Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, kwa yale masoko ya kawaida ya raia ya kununua ndizi, kuuza matunda, wasiwabughudhi watu badala yake waunde Kamati za mpakani ambazo zitakuwa zinatoa vibali kwa kupitia pale kwa Mtendaji wa Kata au Mtendaji wa Kijiji. Anapiga mhuri, mtu anavuka kama anataka kwenda kununua *aspirin* Namanga ya Kenya, habughudhiwi, haombwi *Passport,* haombwi kitu chochote kingine. Pale Horohoro kuna matatizo mbalimbali lakini tumewakuta Watanzania wanaingia Kenya kwa sababu wengi ni watu ambao wanahusiana. Kwa hiyo, mimi nasema bado mambo hayajakaa vizuri hakika, lakini juhudi tunazozifanya ndani ya uwezo wa bajeti tunayopewa kwa upande wetu tunajitahidi sana ili mambo haya yaweze kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila baada ya miezi mitatu nazungumza kwenye *TV, program* ambayo ni *interactive,* watu wanauliza maswali na kadhalika. Naibu Waziri na mimi pia, tunatembea Mikoani kutoa elimu hiihii katika ziara zetu za kazi. Kwa hiyo, ni kazi kubwa lakini nadhani tuwahimize Watanzania wenzetu kwamba ujasiriamali hauishii tu ndani ya mipaka yetu, waendelee na wafanye shughuli zao kokote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rajab amesema Waziri naye anahitaji elimu, sawa, elimu haina mwisho, mimi ni mtu mzima pengine yeye ana akili sana atanielimisha. Mimi huwa nayapokea tu haya kwa sababu, sio kama yeye, yeye ningemsemesha maneno haya yasiyo na adabu sijui kama tungekaa hapa lakini mimi nayapokea tu kwa sababu mimi ni Mwanasiasa niliyekomaa. Siwezi kukereka na maneno ya ajabuajabu haya ambayo mwenzangu anayatoa. Mimi na yeye sijui nani anahitaji elimu? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lisilo la Muungano likahojiwe katika Baraza la Wawakilishi, huu ndio utaratibu wa nchi; leo unasema habari gani hapa? Suala la mawasiliano uje uulize humu na ujibiwe, Bunge hili haliwezi kuwajibika kwa mambo ambayo si ya Muungano, ama mmegeuka sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo Wizara hapa sio maana yake inajibu kila kitu, haiwezekani! Sasa ndio maana kuna shida huko basi, maana hata *feasibility* zinachukua muda mrefu unakuja kuuliza humu, *feasibility study* inafanyika Zanzibar na inafanywa na Serikali ya Mapinduzi. Ukiniuliza mimi unanionea tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Nchambi anasema na yeye hana Afisa Habari; nadhani kesho asubuhi tutasambaza orodha ya majina yote ya Maafisa Habari wanaohusika na Jumuiya, *Focal Point Persons,* kwa Wilaya zote tutazigawa kesho asubuhi; kama wao wanazembea basi ni suala lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lugola amesisitiza kuhusu elimu kwa wananchi kwa kutumia Bunge la Afrika Mashariki. Ni kweli, ndio maana Bunge hivi sasa 50% ya vikao vyake vinafanyika Arusha, 50% vinafanyika kwa mzunguko ili kuleta lile joto, watu kuelewa kwamba kuna kitu ambacho kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Laizer, wewe ni *Senator* humu ndani, umemsikia Waziri.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema kwamba, sio vizuri watu wazima wakibishana. Nadhani wapiga kura wangu wa Namanga wanasikia na nadhani wananiunga mkono kwamba hakuna kikao kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu ninarudisha shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba hawa Maafisa waliopatikana leo, kwa sababu naanza kusikia jina leo kama amekwenda amekwenda tukiwa hapa Bungeni, wawe na Ofisi kule mipakani katika Vituo vilivyojengwa, wasiende Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudisha shilingi, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Kwa kurudisha shilingi Mheshimiwa Laizer, hoja yako sasa ni *valid,* unaweza ukaifuatilia, iko hewani wala haijakufa. Kwa hiyo, sasa wewe na Waziri huyu ni *zero* beneti, Mheshimiwa Kombo!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia na wakati Mheshimiwa Waziri alipokuwa akitoa maelezo yake, mimi binafsi majibu yake hayakunifurahisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza kwamba masuala ya Tanganyika ambayo si ya Muungano yanawasilishwa ndani ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa kutumia Jamhuri ya Muungano. Yale masuala ambayo si ya Muungano kutoka upande wa pili wa Muungano yanawasilishwa na nani na kwa Sheria ipi? Mheshimiwa Waziri wakati akitoa maelezo yake alisema kwamba masuala ambayo hayahusiani na Muungano twende tukayaulize kwenye Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Wizara hii ni ya Muungano. Ndipo mara nyingi tunaposema kwamba Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Wazanzibari wapewe nafasi washirikishwe kama wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa sababu hizi kwamba, kuna mambo ambayo si ya Muungano, hayahusiani na Muungano, katika mambo 17 mambo manne tu ndio ya Muungano mambo 13 si ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba jawabu na ufafanuzi wa kina, vinginevyo nakusudia kuzuia shilingi ya Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumjibu Mheshimiwa Kombo suala ambalo ameliuliza. Kwa kiasi kikubwa mimi na Mheshimiwa Waziri tumeliainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee tena kuzungumza kwamba, masuala ya *SMZ* kwa maana ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yaliyokuwa si ya Muungano yanawakilishwa na *SMZ* na Wajumbe wao kupitia Wizara ya Afrika Mashariki, hali ya kwamba na wao wapo wanatetea na vikao wanahudhuria na nilisema kwamba unatokea wakati mimi nafsi yangu nikiwa kama ni Naibu Waziri Mheshimiwa Mazrui alishashika bendera, Mheshimiwa Mwinyihaji Makame alishashika bendera, Mheshimiwa Jihad Hassan alishashika bendera, atetee katika

masuala ya pale. Nina sehemu, nina ushahidi na katika masuala ambayo wakati tumekaa katika Meza moja yaliyokuwa yakija ya Muungano anasema sasa Mheshimiwa yeyote aliyekuwepo pale au pamoja na mimi mwenyewe tunashughulikia mambo ya Muungano lakini tuko pamoja na huu ndio utamaduni ambao upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ikiwa libadilike sawa lakini kutokana na Katiba ya sasa hivi hili haliwezi kubadilika. Mwongozo na Busara za Viongozi upo, sasa kama kulibadilisha tulibadilishe mbele ya safari lakini huu ndio utamaduni na tunakwenda vizuri na mambo mengi sana yanakwenda vizuri na hayana tatizo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tumeshalizungumza na hakuna maelezo mengine. Kama Mheshimiwa Mbunge utakuwa hajatuelewa, tutazidi kueleweshana.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kushika shilingi. Kwa sababu…

**MWENYEKITI:** Sasa unaitoa, sema sasa ndio naitoa, unachangia na kama kuna mtu atachangia hoja yako wataruhusiwa kuchangia.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawasawa. Niseme kwamba Mheshimiwa Mazrui, Mwinyihaji Makame na Mheshimiwa Jihad ambao wanaalikwa, wanakwenda kule kama nani wao?

**MBUNGE FULANI:** Waalikwa, si utamaduni.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nchi haiendi kwa utamaduni, tunakwenda kwa Sheria na wao wanakwenda kwa Sheria ipi? Wao wanapofika kwenye vikao hivyo wana kura gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni waalikwa tu, bado haijawa sababu ya kusema kwamba Zanzibar inashirikishwa katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono juu ya hoja hii ili iweze kuchangiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa hoja yako mahsusi ni ipi? Maana umezungumza mengi hapa? Umezungumza Sheria, umezungumza anakwenda vipi, anabeba nini, hoja yako ni ipi?

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kujua wanakwenda kule kisheria?

**MWENYEKITI:** Basi?

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** *Yes.*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Rukia!

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naunga mkono hoja ya Maalim Kombo kwa sababu Zanzibar kuwe kuna *coordinator* kati yake na Waziri. Leo mambo ya Tanganyika yanafanyika, ya Zanzibar anatuambia hakuna mchanganuo mpaka lini wakati Zanzibar ilikuwa ipewe nafasi yake. Zanzibar iwe moja kwa moja Wajumbe wa kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na wachaguliwe basi na Baraza la Wawakilishi, kwa nini hilo halikufanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaingia katika mwavuli huu lakini matokeo yake Zanzibar hakuna kinachotendeka. Bandari ya Mpigaduru tangu siku iliyoanza Jumuiya hii tunaambiwa itajengwa na mpaka leo tunaambiwa hakuna *feasibility study,* sijui kwa sababu hakuna mchanganuo, mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *airport* ya Pemba hakuna taa, ikifika saa 12.00 ndege haziwezi kutua, huu ni usumbufu. Mambo yanayohusu Tanganyika mbona yanafanywa? Kwa sababu, kule tunaambiwa kule hakuna mchanganuo, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wete kuna kituo, watu kutoka Mombasa wanaingia Pemba. Kwa nini vituo vimejengwa, Pemba hakukujengwa kituo na wakati Pemba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nini haikufanywa hivyo? Au kwa sababu Waziri huyu yupo huku tu kwenye Jamhuri ya Muungano kule hakuna?

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kuwe na *coordinator* basi tumjue wa kumkamata.

**MWENYEKITI:** Haya, yule Sheria, wewe *coordinator.* Mheshimiwa Nchambi?

**MHE. SULEIMAN M.N. SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hatuna hoja. Hatuna Katiba inayoongelea nchi tatu, hapa tuna Tanzania, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayowakilisha *East Africa. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama utaendelea kuwaruhusu washike shilingi kwa hoja ambayo haina mashiko, hakuna Zanzibar hapa…

**MWENYEKITI:** Aah, Mheshimiwa Nchambi kaa chini. Wewe huwezi kunifundisha mimi kazi yangu hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Msigwa!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikuomba, alikuwa ameomba Mheshimiwa Raya.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kombo kwamba sawa Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kwamba tunaenda kwa utamaduni na itaendelea kuwa hivyo *unless* kama kutakuwa na mabadiliko mengineyo. Hata hivyo, ningependa kujua huu utamaduni, kama Wizara, hatuoni ipo haja ya kwamba iwepo Sheria Maalum ama iwepo Sera ama utaratibu wowote ambao utakuwa *identified* katika *document* ambazo ni *official* itajulikana kwamba hiki kitu ni lazima kiwepo hivyo? Kwa sababu tukisema utamaduni ama mazoea kwa kweli nchi kama hivi ama Wizara kama hii ambayo inaitwa yenye viwango kusema kwamba tunaendesha mambo kiutamaduni au mambo kwa namna fulani kwa kweli tunakuwa bado hatujaelewa. Tungependa kwamba iwepo Sheria maalum ama kuwe kuna Sera maalum au utaratibu maalum ambao unajulikana katika Wizara na hata katika sehemu nyingine kuwe kuna *document* zina-*identify* Sheria hiyo ambayo itatumika. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze na Mheshimiwa Raya, Mheshimiwa Raya mimi nipenda kukukumbusha tu kwamba mambo ya Afrika Mashariki ni mambo ya nchi za nje. Sera ya Mambo ya Nchi za Nje Tanzania ipo, tena ya zamani, wala haikumbushwi na msimamo wa Muungano juu ya Mambo ya Nchi za Nje upo ndani ya Sera na Ndani ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio tuliposema kwamba pakitokea sintofahamu ndogo tunatengeneza Mwongozo ambao unatuongoza kutokana na Sera zile. Katika Sheria za kiutawala hili jambo lipo; kuna nchi zinaongozwa na kauli za wazee tu. *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Uingereza kauli za wazee zinaongoza, Katiba haikuandikwa Uingereza; samahani mimi naomba tuingie kwenye *issue*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mimi nafikiri hapa ikiwa tunataka manufaa ya Zanzibar kama mnavyoongea ninyi, mmeuliza *coordinator;* Mheshimiwa Waziri kamzungumza, Mheshimiwa Mwinyihaji yupo pale kama *coordinator.* Wizara yetu, ninyi wenyewe ndio mliopiga kelele Wizara iwe na ofisi Zanzibar, tukapeleka Ofisi Zanzibar na wafanyakazi wapo na vitendea kazi na bajeti yake ipo. Huyo pia ni *coordinator* wa pili huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rukia ulizungumza jambo ambalo mimi limeni-*touch* kidogo, nilitumwa na Mheshimiwa Waziri ziara Pemba, nimekwenda mpaka Micheweni. Mheshimiwa Khatib umeshaniletea barua sana kunipongeza; mimi nafsi yangu ndio niliyesema Wete kuwe na kituo katika *principle* ya *One Stop Border Post* kwa sababu haiwezekani kujenga *One Stop Border Post* kwenye bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaiuza hoja hiyo kwa *CEO* wa *TMEA* na nina barua hapa tano za kukumbusha, *DC* ana habari, Mkurugenzi wa bandari ana habari, Katibu Mkuu ana habari, Waziri ana habari hatujapata maandiko, sasa tunaonekana sisi hatufanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nahisi la kufanya hapa mimi na ninyi tuwe na mahusiano mazuri na wawakilishi wetu, tuzungumze katika Baraza la Wawakilishi na zile hoja sisi tuzisimamie huku ili Zanzibar iweze kwenda na kufaidika na msimamo huu wa Tanzania, hilo ndiyo nafikiri la kushawishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuombeni sana yaani ukitoa shilingi hapa mimi utakuwa unanionea maana raha leo kule ndiyo kama jana alivyozungumza mwenzangu hatuna chochote sisi tunauza papa, ng'onda, nguru. Kwa hiyo, mimi naomba tushirikiane pamoja twende mbele, tuzungumze *issues* tusizungumze watu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo, nafikiri Waziri amejieleza vizuri bado kuna umuhimu tu wa kufanya *engagement* ili mpate ukweli na uhalali wa mambo yenu na maslahi ya hayo mnayoyatetea, wewe mrudishie tu shilingi yake.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narejesha shilingi ya Waziri kwa kauli ya kwamba tukae pamoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka ufafanuzi kuhusiana na utekelezaji wa mwongozo ambao umetolewa na Serikali. Kama utakumbuka wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) na hata Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, walizungumzia kuhusiana na mwongozo ambao umetoka kuhusiana na suala zima la ajira kwamba sasa katika maeneo ya Muungano ajira Zanzibar itakuwa ni asilimia 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka nijue tu utekelezaji wa jambo hilo kwenye hii Wizara ya Afrika Mashariki umefikia wapi? Haya mambo mengine haya yaliyopita nafikiri hapa siyo mahali pake pazuri pa kuweza kurekebisha mambo haya ilikuwa ni kwenye Bunge la Katiba na wenzetu hawa wamekimbia lakini hili la mwongozo niipongeze sana Serikali kwamba imelisimamia vizuri, nataka nijue utekelezaji wake katika Wizara ya Afrika Mashariki ukoje, ni hilo tu.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika hotuba hizo mbili alizozitamka Mheshimiwa Masauni, Mbunge wa Kikwajuni, Serikali ilikaa kitako katika masuala ya kuondoa kero za Muungano kwamba kuwe na asilimia 21 ya waajiriwa katika vyombo vya Muungano kutoka Tanzania Zanzibar na bakaa iliyobaki kwa Tanzania Bara. Msimamo huo upo na azimio limeshatoka ndani ya Serikali na bahati nzuri tu hapa nyuma kuna Mheshimiwa Celina Kombani ambaye pia ni Waziri amenihakikishia hilo, kwa hiyo, tunakuhakikishia kwamba utekelezaji wake umeshaanza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Wenje.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. KEISSY A. MOHAMED:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, tafadhali kaa. *(Kicheko)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika *winding up* ya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu *Political Federation,* Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba katika *communiqué* ambayo ninayo hapa kwamba wameagizwa sasa ndiyo mchakato uanze wa kutengeneza Rasimu ya Katiba ya *federation* itakuwaje. Mheshimiwa Waziri pia amesema kwamba sasa ndiyo wameanza kukaa kuangalia muundo utakuwaje na masuala kadhaa yatakayohusu *political federation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri na maelezo waliyotoa walivyokuwa wanafanya *winding up* ni vitu viwili tofauti. Katika hotuba yake, ukurasa wa 18, naomba ni-*quote* kidogo amesema, katika hotuba yangu ya mwaka 2013/2014 nilitoa taarifa kuwa nchi wanachama zilitakiwa kutoa maoni kuhusu Rasimu ya Mpango Kazi na *model* ya Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara iliwasilisha maoni ya Tanzania kuhusu suala hili katika mkutano wa ishirini nane wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hapa maana yake ni kwamba tayari kuna maoni ya Tanzania na ukisema Tanzania maana yake ni kwamba hakuna Tanzania bila Watanzania. Kwa hiyo, kimsingi Mheshimiwa Waziri anajaribu kusema kwamba kuna maoni ya Watanzania ambayo tayari yalishawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa maana ya *Ministerial Council* ya *East Africa Community.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, unapochukua nchi ya watu unaenda kuunganisha na nchi nyingine huu mchakato lazima uanze na wananchi wenyewe. Sasa kama leo tunaambiwa kwamba aidha mchakato huu ulishaanza na kuna vitu vilishawasilishwa au kama wanavyosema leo lugha nyingine kwamba ndiyo wanataka kuanza mchakato, sasa ni lini Watanzania watashirikishwa? Kwa sababu ni haki ya wananchi kushirikishwa katika hii *process* hii na kutengeneza Katiba lazima Rasimu itokane na wananchi, hauwezi ukachukua Rasimu yako ndiyo ukaleta kwa wananchi yaani lazima mawazo ya *structure* ya muundo huo itoke kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *process* hii yote hakuna kitu kinachotoka kwa wananchi. Kwa hiyo, mimi nataka kujua ni lini sasa Serikali itaanza mchakato wa kuhusisha Watanzania katika huu mchakato wa kutengeneza Katiba ya *Political Federation* kabla hawajatengeneza hiyo Rasimu wanayosema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna mchanganyiko tu wa dhana na maneno. Ikiwa nchi zinajadiliana huwa kuna mawazo ya awali ndiyo maana linatumika neno *model.* Kwa mfano kwenye hili niwaambie kabisa, Uganda tayari wana mawazo kwamba tuwe na Shirikisho ambalo linakaribiana kuwa kama nchi moja, sisi tuna mawazo tofauti ya awali tu, tunaijua nchi yetu kwa hiyo hatuwezi kuwa Serikali ambayo kila ikiulizwa inasema ngoja tukaulize wananchi, utazungumza na nani duniani sasa. Kwa hiyo, wamesema hebu tupeni sura Muungano au Shirikisho liweje, hilo ni swali la kawaida kabisa katika majadiliano kwa hiyo tumetoa sisi *model* tunaita *decentralized model* lakini hayo siyo maoni ya Watanzania kwa maana ya Rasimu yenyewe, hakuna Rasimu hapa, tunazungumza ili tuje tuwe na mawazo ya awali yapitie katika ngazi husika na hatimaye tutakapofikia ngazi ya Rasimu tutayapitisha kama mkataba wenyewe unavyosema wananchi wa Afrika Mashariki, wote wenye uwezo, umri na sifa za kupiga kura ndiyo watakaoamua kuhusu hiyo Rasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kilichofanyika sasa ni mawazo ya awali ili tuanze kuzungumza na yawezeshe sasa baada ya wataalam na nikumbushe tu pengine hakuisoma yote ile ya mwaka jana, mwaka juzi waliteuliwa wataalam watatu, watatu kutoka kila nchi. Wametembea na ni wataalam waliobobea, kwa upande wetu alikuwepo pia Profesa Kabudi, ni mmoja wa *think tank* waliopo wanaojaribu kuelezea aina mbalimbali za mashirikisho na miungano ya nchi. Katika hatua hiyo, bado hatujawa tayari kuweza kuwauliza Watanzania kwa sababu ni mambo ya nchi tano hayajakaa katika kiwango ambacho yameiva na yakaitwa ndiyo maoni. Kwa hiyo, tukifika hapo, kama kawaida utafanyika utaratibu wa Kikatiba wa kupata maoni ya Wanaafrika Mashariki ikiwa ni pamoja na Watanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Huvisa.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wenje tunafuata Kanuni, hukuwa na nia, hukusema habari ya shilingi, umechelewa Mheshimiwa Wenje.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** *With due respect* Mheshimiwa Wenje umechelewa kaa chini. Ulikuwa na hoja kubwa sana sasa ndiyo umechelewa ndiyo Kanuni zinavyosema.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wote hapa wamepata…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wenje, mimi siyo kocha ni *referee,* umechelewa Mheshimiwa Wenje kaa chini.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa Wenje hukutoa shilingi na hata Mheshimiwa Mbowe yuko hapo alikuwa anakusikia…

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Walikuwa wanakupigia debe utoe shilingi hukutoa.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi inatolewa kwenye *second argument*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wenje, *please* kaa chini.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi inatolewa kwenye *argument* ya pili.

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana, kaa chini Mheshimiwa Dokta Huvisa.

**MHE. DKT. TEREZYA P.L. HUVISA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Mimi naomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu Sera ya Takwimu za hali ya hewa iliyoko ukurasa namba nane. Wote tunajua kwamba athari za mabadiliko ya tabia nchi ni pamoja na kutokuwa na uhakika wa utabiri wa hali ya hewa. Je, ni kwa namna gani Sera hii imeweza kuhusisha mabadiliko ya tabia nchi hususan kwenye mambo ya *Disaster Risk Management* yaani mkakati wa kujiandaa na maafa? Ni namna gani Sera hiyo imeweza kuhusisha mambo hayo muhimu ili kunusuru maisha ya Watanzania pamoja na maisha ya wananchi wote wa Jumuiya ya Afrika Mashariki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba hoja ya tabia nchi ilijadiliwa kwa kina na Wakuu wa Nchi Arusha na wakatoa kauli ya kwamba itengenezwe Sera ya pamoja kwa sababu tabia nchi haichagui sehemu, sasa hivi wataalam kutoka katika nchi zote, wamekaa kitako wanatia utaalam wao pamoja na kuainisha Sera za *individual partner state.* Kwa hiyo, Sera hii bado haijawa tayari lakini itahusisha masuala yote ya kisera juu ya tabia nchi, ahsante.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* …............ Tsh.412,346,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 – *Policy and Planning* … ...........Tshs.14,849,860,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kasma 270200, *current grant to International Organizations,* kasma hii ni kwa ajili ya kulipia ada ya Tanzania katika

Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwaka wa fedha uliopita kilitengewa shilingi bilioni 12.4, mwaka huu kiwango kimeongezeka mpaka shilingi bilioni 13.7. Kwenye taarifa ya Kamati ya Bunge, ukurasa wa kumi na nane, Kamati ya Bunge inasema kwamba, ilipokuwa inazungumzia Wizara hii inatengewa pesa kidogo, katika hali hiyo, Kamati yangu inaishauri Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhamisha fedha zote za michango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuziweka moja kwa moja chini ya Wizara ya Fedha - Hazina ambayo italipia gharama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Wizara na iwapo sitaridhika, nitaomba walau katika hili kuondoa shilingi. Jukumu la kuhamisha hiki kifungu, ombi la Kamati ni kazi hii kwenda kufanywa na Kamati ya Bajeti lakini sisi hapa sasa hivi ndiyo tunapitisha bajeti ya Wizara. Kwa kuwa makadirio haya yameletwa na Waziri, je, Waziri yuko tayari kukubaliana na pendekezo hili la Kamati ili fungu hili hapa lisipitishwe katika eneo hili lipitishwe katika hatua tutakayofikia ya Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa kurejea vilevile Kanuni ya 102 ambayo inaweza kuruhusu kuhamisha kifungu au mafungu. Nasema hivi kwa sababu sasa hivi tunaweza tukadhani tunapitisha bajeti ya Wizara ya shilingi bilioni 23 kumbe ukweli ni kwamba bajeti ya Wizara hii ni shilingi bilioni 10 peke yake ndiyo ya kazi ya Wizara, fedha nyingine yote inakwenda kulipia ada tu ya Jumuiya ya Afrka Mashariki. Wizara hii ikikubali, ukweli ukajulikana kwamba bajeti ya Wizara iliyoko mbele yetu ni shilingi bilioni kumi peke yake maana yake Bunge litaona Wizara hii ni karibu sawa na Idara tu ya Serikali, tutafanya uamuzi wa kutekeleza pendekezo la pili la Kamati kwamba Kamati vilevile inashauri Kamati ya Bunge ya Bajeti kuitengea fedha za miradi ya maendeleo Wizara itakayolenga kuimarisha uchumi kutokana na fursa za mtangamano na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa sasa Wizara hii ni kati ya Wizara chache ambazo hazina kabisa fungu la bajeti ya maendeleo, kwenye kitabu cha bajeti ya maendeleo hakuna kabisa fungu la Wizara hii. Kwa hiyo, Wizara hii kama itakuwa hivi ilivyo ni afadhali tusiwe na hii Wizara kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri akubaliane na rai hii ili fedha za Jumuiya zitoke hapa zipelekwe kwingine ili tuone kabisa kwamba bajeti ya Wizara hii kimsingi ni ndogo ili ufanyike uamuzi wa Kibunge wa kuitengea Wizara hii bajeti ya maendeleo kwa ajili ya miradi muhimu ya maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo Wabunge mbalimbali wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jibu la Waziri na endepo sitaridhika nitaomba kuondoa shilingi ili jambo hili lijadiliwe na Wabunge wote, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tunaloombwa hapa halimo ndani ya mamlaka yetu hata kidogo. Hili ni suala la Hazina ndiyo wanaopanga mipangilio yote hii. Sisi kwa miaka miwili mfululizo tumekuwa tukikubaliana tu na wazo hili lakini kuhamisha ni suala la *Paymaster General,* ndiyo taratibu za Serikali zilivyo. Kwa hiyo, hatuwezi sisi tukasimama hapa tuseme tumekubali halafu hata akitazama kwenye Kanuni uhamishaji wa mafungu ni ndani, Bunge linahamisha ndani ya fungu lenyewe lakini siyo kuhamisha kutoka Wizara moja kupeleka nyingine, hali hiyo ikibidi iwe hivyo inabidi turejee tena kwenye Kamati ili hilo liweze kufanyika na pia twende kwenye Kamati ya bajeti na kwa muda huu wa Kamati ya matumizi ombi kama hili halitekelezeki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika subiri kwanza, hoja yako ni ya msingi na Kamati imejaribu kulipigania hili miaka yote lakini mwaka huu vilevile imekuja tena vilevile na hoja hii sisi tuna *audience* na Kamati ya Bajeti kesho kuzungumzia suala hili na masuala mengine. Sasa

mimi nilikuwa nakuomba, Waziri amezungumza, *is quite right* na wewe unajua Kanuni zetu zilivyo, unaweza ukabadilisha vifungu ndani ya kifungu cha humu humu ndani ukitoe hapa, ukipeleke kirudi Hazina kwa kipindi hiki, haiwezekani. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nakuomba tu ukubali na mimi ndio tuko kwenye Kamati hii tunajaribu kuli-*sort out,* tutashirikiana na Wabunge ili kulishughulikia. Ndiyo kama nilivyosema hata kwa suala la Mheshimiwa Laizer, wewe umesema fedha nyingi kabisa shilingi bilioni kumi ni shilingi bilioni nane na nusu tu wanapewa hawa na zimeongezeka *this time for five billion,* mwaka jana walipata shilingi bilioni tatu, *you can imagine pressure* ya Wizara ambayo wanayo na *pressure* ya Wabunge kutafuta walimu kwenye vituo vya Longido, vituo vya Kiembesamaki, vituo vya wapi, kote huko wanakuwa hawawezi kutokana na uhaba wa fedha.

Kwa hiyo, mimi nikushauri hoja yako ni *valid,* Kamati imeiona, sisi tunaichukua na kesho tuna *audience* na Kamati ya Bunge saa tano ilikuwa twende leo bahati mbaya tupo hapa juu. Kwa hiyo, mimi nikubaliane na wewe mrudishie shilingi yake tuli-*carry* pamoja ili sasa lionekane uzito wake kuwa Bunge limeliona na Serikali walione, Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa hata sijaondoa shilingi bado, nilikuwa nimeomba ufafanuzi iwapo sitaridhika na ufafanuzi niweze kuondoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kuondoa shilingi iko kwenye Kanuni ya 103(3) ya Bunge ambayo inasema madhumuni ya hoja ya aina hiyo ni kumwezesha Mbunge aliyetoa hoja aweze kueleza kutoridhika kwake na utekelezaji wa jambo fulani mahsusi ambalo ni dhahiri linahusika na kifungu hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo hili la kuhamisha kifungu hiki, jambo hili la kuhakikisha Wizara hii inatengewa fedha zaidi ya fedha za kawaida kuwa na fedha za maendeleo, tumelihoji kwenye Mkutano wa Bunge mwaka jana na mwaka umepita, *Paymaster General* hajafanya hicho ambacho Mheshimiwa Waziri anakisema sasa, Serikali haijatekeleza, tukipewa fursa ya kuondoa shilingi hapa tutapewa nafasi ya kueleza kutoridhika juu ya utekelezaji wa kifungu hiki na sasa haitakuwa wazo tu la Kamati yako ambayo wewe ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati litakuwa ni wazo la Bunge kwa umoja wetu na jambo hili Serikali italazimishwa kulitekeleza.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa kama ni hivyo, kama unatoa shilingi toa uanze kujadili.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya kuondoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Sasa changia.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kwa sababu naamini Serikali ipo mbele yetu ikiwakilishwa na Wizara ya Afrika Mashariki, lakini pia ikiliwasilishwa na benchi la Waziri Mkuu ambaye hayupo, naamini wako wengine kwa niaba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kwenye Vikao vya Baraza la Mawaziri, Wizara ya Fedha na Serikali, haichukulii uzito kikamilifu kauli ambazo Wabunge tumezitoa mkutano uliopita, kauli ambazo Kamati imesema, kauli ambazo Wizara imesema. Kwa hiyo, naomba kutoa shilingi na Wabunge wenzangu waniunge mkono kwamba, tuitake Wizara ya Fedha, ambayo mlipaji mkuu wa fedha za Serikali iko chini yake, itoe kauli hapa Bungeni kama iko tayari sasa kutekeleza ushauri huu wa toka miaka iliyopita wa kuhakikisha Wizara ya Afrika Mashariki inatengewa bajeti ya maendeleo, kuhakikisha fedha za Uachama kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki zinalipwa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tusijidanganye kwamba, bajeti yetu ni kubwa, tutenge rasilimali za kutosha kwenye suala muhimu la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kama Wizara ya Fedha haiko tayari kutoa kauli hapa, basi Waziri Mkuu atoe kauli, kwa sababu ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali kwamba sasa Serikali inakwenda kutekeleza wazo hili. Kwa hiyo, naomba kutoa shilingi na naomba Waheshimiwa wenzangu ambao wanaunga mkono kwamba, Wizara hii inatakiwa ipewe uzito kuhakikisha michakato ya utengamano ya Afrika Mashariki inapewa uzito unaostahili, waweze kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa kwamba, nchi yetu inaingia kwenye Shirikisho. Ukisoma Hotuba ya Waziri ina pande mbili; upande wa kwanza ulikuwa ni Baraza la Mawaziri *(Council of Ministers),* wamekubaliana kwamba watengeneze hiyo *model* ya Shirikisho ambayo ameizungumza Mheshimiwa Wenje. Upande wa pili, baada ya kupitisha ile *model* ya Shirikisho walipeleka kwenye *Summit,* Mkutano wa Wakuu wa Nchi na mimi ninayo hapa Maazimio yaliyosainiwa na Mheshimiwa Rais Kikwete, Mheshimiwa Kaguta, Mheshimiwa Kenyatta, Waziri Mkuu wa Rwanda na Makamu wa Rais wa Burundi. Wamekubaliana rasmi sasa Mawaziri wamepewa agizo la kwenda kuandaa Katiba ya Shirikisho la Afrika Mashariki. Hatuzungumzii utangamano wa kiuchumi tu, mpaka utangamano wa kisiasa, Wizara inayotakiwa kuiongoza nchi katika mambo haya makubwa kwa mustakabali wa Wananchi, haina hata bajeti ya maendeleo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono. Ahsante sana.

**MHE. FREEMAN E. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kila sababu ya kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika, kwa sababu ya umuhimu wa Wizara hii. Nitazungumza kwa kifupi sana, katika mchango wangu wa msingi nilionesha namna ambavyo pengine hatujatoa msukumo wa kutosha kuweza ku-*take advantage* ya Tanzania *strategically* ilivyo, *geographically*, kuweza kufaidi uchumi na mahusiano na nchi majirani zetu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka vilevile katika mchango wa Mheshimiwa Naibu Waziri, alizungumzia hoja kwamba, sisi hatuko tayari kuruhusu *free movement* ya raia wa nchi zetu za Afrika Mashariki. Kwamba, wenzetu wamekubaliana kuweza kuingilia kiurahisi, lakini sisi tumesisitiza kwamba lazima tutumie *passport*. Sasa hili ni Taifa la watu milioni 45, ambapo Watanzania ambao leo wana *passport* za kuwawezesha kusafiri kiurahisi bila vikwazo nina uhakika hawafiki laki tatu, lakini tunasisitiza kwamba, namna ya ku-*move* katika Afrika Mashariki lazima tuendelee kutumia *passport! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi, tunaweza tukawa tunaangalia tu upande mmoja wa faida ambazo wenzetu watazipata kwa kuja Tanzania, lakini hatuoni vilevile fursa ambazo tunawanyima Watanzania wenzetu kwenda katika nchi za jirani katika misingi ambayo ni ya urahisi. Kwa hiyo, mimi naunga mkono sana hoja hii kwa sababu moja tu msingi, Serikali itoe uzito wa kutosha kwa Wizara ya Afrika Mashariki. Kuna fursa nyingi sana za kiuchumi, kisiasa na kijamii ambazo hatutaki kuzitumia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mbowe. Mheshimiwa Mbowe akishazungumza ndiyo bosi wenu ninyi mtasema nini zaidi yake tena? Mheshimiwa Lukuvi! (Kicheko)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hoja nzuri sana ya Mheshimiwa Mnyika, nataka kumwambia kwamba, utaratibu huu wa mafungu ya kila Wizara kutengewa fedha kulipia ada kwa Taasisi na Mashirika ya nje yanayosimamiwa na kuratibiwa na Wizara, siyo kwa Wizara hii peke yake. Leo ameyaona haya shilingi bilioni 13 kwa East Africa, juzi ungesoma Wizara ya Kilimo ungekuta

kuna *WFP, FAO,* tayari tumeshalipa huko. Ukija kesho kutwa kwenye Wizara ya Mambo ya Nje, utaona. Kila Wizara, hata kwangu Waziri Mkuu sina hela nyingi, lakini nina Glare kule Makao Makuu Rwanda, masuala ya UKIMWI, ninalipa kidogo japo dola mia tano. Kwa hiyo, Wizara inawajibika kusimamia na fedha zinatengwa kwenye Fungu la Wizara kwa ajili ya kulipia ada ya Masharika ambayo inaungana nao.

Tunayo ndege ya kunyunyizia dawa hapa Airport ya Dodoma, Makao Makuu yake yako Addis Ababa. Sisi ni *members.* Inakuja kutoka Addis kuja kunyunyizia kwereakwerea hapa kwa sababu Waziri wa Kilimo ametengewa fedha za kulipia ada kwenye Shirika lile ili kuiwezesha Serikali ya Tanzania kutumia ile fursa. *(Makofi)*

Haiwezekani Hazina ukakusanya mapesa yote ya Serikali nzima wakawa wanafanya jambo hilo. Huu ni utaratibu mzuri wa *management* ya fedha za Serikali. Kwa hiyo, ndiyo maana Mheshimiwa Waziri kwa Fungu lake, Serikali inampa yeye fedha za kugharamia ada zote katika Fungu lake kwa ajili ya hilo.

Sasa hili lisichanganywe na ufinyu wa bajeti ya maendeleo. Hili ni suala moja kwamba, lazima utaratibu ufuatwe, lakini suala la uhaba wa fedha za maendeleo tunalijua. Ninyi wenyewe Wabunge hivi sasa mnajua, tulipokuwa kwenye Kamati ya Uongozi, Mheshimiwa Mnyika ulimwakilisha Mheshimiwa Mbowe, tumekubaliana tuahirishe Wizara mbili; kwa nini tumeahirisha Wizara ya Nishati na Maji kuja mwisho kwa sababu tuliliona hili. Sasa muamue tu kwamba, waende bajeti kule wakafute hela za maji, wakafute hela za wapi, tukajenge *Boarder Post* ya East Africa; kupanga ni kuchagua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lukuvi, umejieleza vya kutosha nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Sitta.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani jibu limepatikana, sisi kama Wizara tunakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mnyika na wengine. Mheshimiwa Mbowe, namshukuru sana, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Malipo ya ada kwa Wizara ndiyo yanachukua sehemu kama asilimia 60 ya bajeti nzima. (Makofi)

Kwa hiyo, hoja ilikuwa hapo hapo kwamba, kama ni hivyo basi inaifanya tu ionekane zipo shilingi bilioni 20, 23, lakini kumbe ni 13. Ukumbuke kadiri dola inavyopanda kwa thamani ndivyo malipo kwa shilingi nayo yanaongezeka. Kwa hiyo, kidogo inaleta shida. Kwa kuwa ni nje ya utaratibu na utaratibu wenyewe unasimamiwa Kitaifa, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Lukuvi, sasa katika hatua hii ya Kamati ya Matumizi tukilizungumza sana hili, nadhani wenzetu waridhike kwamba, limezungumzwa, Serikali imesikia, kesho Kamati yako Mheshimiwa Mwenyekiti tunakwenda kwenye Kamati ya Bajeti, tutalizungumza tena. Nadhani kwa maana ya Kamati hii ya Matumizi limefika pazuri tu, tuendelee halafu tutaona siku zijazo nini kitatokea. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika umeli-*broadcast* vizuri, limekaa vizuri na mimi nakuomba vilevile subiri basi mimi ndiyo ninayesema. Mimi nikisema wewe unasubiri halafu wewe ndiyo unapata haki yako, kaa basi kwanza. *(Kicheko)*

Umelisema vizuri na hata Mheshimiwa Mbowe kalisema vizuri na hii ndiyo *concern* ya Kamati, lakini hapa nao wamebanwa, ziko kanuni na taratibu ambazo ndiyo tunajaribu sasa kuzifukia hizi *hurdles,* ili sasa tuendane hoja yetu na yako iwe moja. Sasa sisemi kama hutoi shilingi, najua kwa nafsi yako utairudisha shilingi, lakini nilikuwa nasema tu *in case* ukiamua

kuitoa, hii hoja inakufa humu ndani *and then* inakuwa na sisi inakuwa haitupi nguvu ya kwenda nayo. Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza, nishukuru kwa majibu ya Waziri wa Afrika Mashiriki, Mheshimiwa Sitta, lakini nasikitishwa sana na majibu ya Waziri wa Ofisi ya Nchi (Sera, Uratibu na Bunge); kwa sababu amesema mambo mawili ambayo kama Bunge lisipoyafahamu, hata mtakapokwenda kujadiliana mtakwenda kukwama.

Kwanza, ametumia kisingizio cha kwamba kwa kuwa kuna vifungu vingine vya ulipaji wa ada kwenye Wizara nyingine, basi haiwezekani kwa kifungu cha kulipa kwenye Mashirika ya Kitaifa kuwa chini ya Mfuko wa Hazina au kuwa Hazina, jambo ambalo siyo sahihi kwa sababu kuna ada zingine ambazo ziko kwenye Mfuko wa Hazina na zinalipwa na Serikali. Tafsiri ya jibu la Mheshimiwa Lukuvi ni kwamba, Kamati yenu ambayo wewe ni Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Lowassa ni Mwenyekiti na Wajumbe wote hapa akina Mheshimiwa Seleman Jafo, Mheshimiwa Khalfa, Mheshimiwa Susan Lyimo, orodha ndefu kweli, mliotoa pendekezo hili la kwamba kifungu hiki kihamishiwe Hazina, mlitoa pendekezo lisilokuwa na maana ndiyo tafsiri yake. Mimi siamini kama mlitoa pendekezo lisilokuwa na maana. Kwa hiyo, hili jibu la Mheshimiwa Lukuvi lisikubalike, bado pendekezo lenu libaki ili majadiliano yaendelee. *(Makofi)*

La pili, Mheshimiwa Lukuvi, amefanya propaganda kwamba, kama vile kuamua kutenga fedha za maendeleo Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kufanya sasa tupunguze fedha za maji na umeme ili kila mtu aone aah, kwa sababu Wananchi wataumia, tusitenge fedha za maendeleo kwenye Bajeti ya Afrika Mashariki. Mheshimiwa Lukuvi, amesahau kwamba, kwenye Afrika Mashariki kuna Miradi ya Kikanda ya Maji, kuna Miradi ya Kikanda ya Umeme, kuna Miradi ya Kikanda ya Barabara na leo tuna mgogoro kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu ya udhaifu wa upande kwenye Miradi ya Kikanda. *(Makofi)*

Kwa hiyo, narudisha shilingi lakini mkirudi huko kwenye Kamati ya Bajeti, haya maelezo ya Mheshimiwa Lukuvi yasikubalike, badala yake mapendekezo ya Kamati na Majadiliano ya Bunge ndiyo yaongoze majadiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, kifungu hiki kinakubalika?

**MBUNGE FULANI:** Bado Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Bado nani?

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa nina shida kwenye *subvote* 1003.

**MWENYEKITI:** Haya *okay,* Mheshimiwa Lugola!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye Kasma 270200, inayohusiana na mchango wetu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Naliongelea hili bahati nzuri Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wananisikia, fedha ambazo tumekuwa tukizitenga …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola, *issue* yoyote ikitolewa maamuzi haijadiliwi tena.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Siyo hiyo.

**MWENYEKITI:** Kifungu chako kipi?

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Kifungu hicho lakini kifungu hiki siyo mambo ya Mnyika ni mambo yangu na Kanuni zinaruhusu …

**MWENYEKITI:** Haya sema basi tuyasikilize mambo yako.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha ambazo tumekuwa tukichangia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna fedha zingine ambazo zinaenda kwenye *Lake Victoria Basin Commission* na kuna fedha zingine ambazo zinaenda kwenye Miradi ya Hifadhi ya Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria *(LIVEMP)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Mara na hususan Wilaya ya Bunda, fedha hizi zimekuwa hazifiki kwa ajili ya kupambana na magugu maji, ambayo ni tatizo kubwa katika Ziwa Victoria hususan Wilaya ya Bunda. Matokeo yake magugu maji sasa yamekwenda mpaka kilomita tano, yamevamia Vijiji vya Kabainja ambavyo vina mabwawa yenye maji yanayotumiwa na Wananchi kwa matumizi ya majumbani. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anaitembelea Wilaya ya Bunda na sisi tukiwa tunamsubiri Kabainja Jimbo la Mwibara, hakuweza kufika kwa ajili ya kujiridhisha namna ya kupambana na haya magugu maji.

Sasa mimi nilitaka *commitment* ya Wizara, sina nia ya kukamata shilingi; kwa nini fedha hizi na hata katika Hotuba yake wametaja Miradi katika Mkoa wa Mwanza, Simiyu, pamoja na Geita; lakini sasa hivi wanakuja na mradi mwingine tena mpya unaitwa *prepared* ambao ulikuwa uanze 2012 mpaka sasa haujaanza. Sasa Mheshimiwa Waziri, ninakuheshimu sana; ni lini utafuatana na mimi ili tuone kwamba fedha hizi ambazo tunazichangia kwenye Jumuiya ya Afrika hata Wanabunda nao wana shida hizi hizi ili tukaangalie namna ya kuondoa magugu maji kwenye Bwawa la Wananchi wa Kabainja? Ninahitaji tu *commitment*.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba, tutakwenda kwenye hiyo sehemu.

**MWENYEKITI:** Inaotosha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 – *Trade, Finance and Investment* … … Sh. 742,631,000

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu cha 1004, Item 221100 - *Travel Out of Country*. Tunaona kuna ongezeko; mwaka juzi ailikuwa shilingi milioni 297, mwaka jana ikapungua kuja milioni 224 na mwaka imeongezeka zaidi mpaka shilingi milioni 375.

**MWENYEKITI:** Samahani kifungu kipi?

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 221100, chini kabisa. Idara hii ya *Trade, Finance* na *Investment* ndiyo inahusika na mambo yote ya biashara na uwekezaji. Moja ya kazi ambayo watafanya mwaka huu ni kwenda kuandaa Itifaki ya Utalii na Wanyamapori. Vilevile mojawapo ya masuala ambayo tunajua yanakwenda kujadiliwa ni suala la kutaka kufungua ile gati ya watalii ya kutoka Kenya kuingia mpaka Serengeti. Kwa hiyo, maana nyingine ni kwamba, tuna hofu sisi watu ambao tunatokea Ukanda wa Arusha na ambao tunahusika sana na biashara ya utalii, kwamba, pengine nchi yetu tunaweza tukapunguza fursa za kupata mapato kwa sababu watalii wana uwezo wa kuvuka moja kwa moja kutoka Masai Mara kuingia Serengeti na kurudi bila kupita kwetu.

Sasa nilitaka kupata maelekezo kwamba, hizi fedha zimeongezeka na maana yake ni hizi safari pamoja na kazi ya kwenda kuandaa Itifaki ya Utalii ambayo tayari rasimu imekwishakutengenezwa na pamoja kwamba haijaletwa kwa wadau. Tukihakikishiwa kwamba hizi fedha nyingi zimeongezeka zisije zikaenda kutumika vibaya hususan kwenye kuandaa hiyo itifaki tukajikuta tunapoteza badala ya kupata. Kwa hiyo, ningependa kupata maelezo ya Waziri.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Nassari, fedha hizi hazihusiani hata kidogo na hilo analolisema la kuingia Kilimanjaro kupitia Lango la Borogonja. Fedha hizi zinaombwa kwa sababu Idara hii sasa kutokana na kuongezeka kwa shughuli, baada ya kuingia majadiliano yanayohusu soko la pamoja lililoanza mwaka 2010 na kwenda kwenye majadiliano kuhusu kuunganisha sarafu tuwe na sarafu moja, Idara hii itakuwa na kazi kubwa ya kufanya hizo kazi. Kwa sababu kumeongezeka bajeti kidogo zaidi, ndiyo tumeona tuimarishe ili wafanye hilo.

Hilo lingine la Borogonja wala halihusiani hapa na wala sisi kama Wizara ya Uratibu haturuhusiwi kulitolea uamuzi wowote, ni suala la maliasili.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 – *Economic and Social*
*Infrastructure* … … … … … … … … … … … … Sh. 720,142,00

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Sina dhamira ya kuondoa shilingi kwenye kifungu hiki, ninachoomba ni ufafanuzi kutoka kwa Waziri na *commitment* kwenye Kasma 229900 - *Other Operating Expenses,* matumizi mengineyo. Hii Idara ni ya miundombinu ya kiuchumi na huduma za kijamii na Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake ya safari hii, amesema kwamba, wamepitisha kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sera ya Jumuiya ya Vijana na Sera ya Watu Wenye Mahitaji Maalum. Sasa kwenye Kasma hii kuna milioni 20.3 ambazo zimewekwa na mwaka jana hakukuwa kumetengwa pesa zozote, fedha hizi ni kwa ajili ya kuwapa Washauri Waelekezi.

Ningependa nipate ufafanuzi tu, kwa awamu hii wamedhamiria kulipa Washauri Waelekezi katika maeneo yapi na kama upo uwezekano katika usambazaji na utekelezaji wa hii Sera ya Afrika Mashariki kwa upande wa nchi yetu ya vijana kama jambo hili nalo watalipa kipaumbele katika kutafakari wanapotoa huduma za Washauri Waelekezi wa hizi kazi zinavyokwenda? Ningependa kupata ufafanuzi tu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHIRIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya Mheshimiwa Mnyika ni nzuri na ya kufanyiwa kazi, lakini hizi fedha sasa hivi zitatumika katika kutafuta Mshauri Mwelekezi wa kutathmini shughuli za Idara hii juu ya masuala ya usafiri, kwa sababu tangu *Common Market* ianze haijawahi kufanyiwa tathmini yoyote. Kwa hiyo, hizi ni kwa ajili ya kwa hao Washauri Waelekezi na utendaji kazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 - *Political, Defense and Security* … … … Sh. 472,835,000
Kif. 1007 - *Procurement Management Unit* … … Sh. 232,986,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1008 - *Government Communication Unit* … Sh. 483,683,000

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hiki kifungu kinahusu Idara ya Mawasiliano ya Serikali na utoaji taarifa. Kasma hii ya 221200 - *Communication and Information,* ambayo mwaka jana ilikuwa na shilingi milioni 59.7, mwaka huu imeongezewa mpaka shilingi milioni 99.5. Kwa hiyo, angalau kuna fedha kidogo imeongezeka. Nashukuru kwamba, Mheshimiwa Waziri kila mwaka huwa anatuletea kifurushi cha baadhi ya vipeperushi na taarifa nyingine za utangamano; nyingine zikichapishwa na Jumuiya. Sasa kuna mambo ambayo niliomba; kwamba, kwa kuwa fedha za machapisho zimeongezwa na kwa kuwa Wizara kila mwaka huwa katika mambo muhimu sana inatuletea orodha tu lakini hatuletewi nakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Wizara imepitisha Azimio la kuzitaka nchi wanachama kuwapatia wasichana vifaa vya afya mashuleni. Wizara imepitisha Azimio la kutaka, kwa maana ya Bunge, iwepo mikakati ya kuboresha makazi ya watu duni mijini *(slums)* na kuzuia kujengwa kwa makazi holela ya aina hiyo. Wizara imepitisha Muswaada wa Sheria wa Jumuiya juu ya Utoaji wa Elimu ya Mtangamano Afrika Mashariki. Wizara imepitisha Muswada wa Huduma za Kisheria kwa nchi wanachama na kadhalika. Kwa hiyo, kuna Miswada mingi muhimu sana inapitishwa.

Sasa naelewa kwenye ufafanuzi wamesema kuna mambo ambayo yanapitishwa kupitia kwa Katibu wa Bunge. Ninaamini Wizara kama inavyotuletea vipeperushi vingine, ingeweza kabisa kwa nyongeza hii ya pesa ya mawasiliano, kutuletea nakala ya nyaraka hizi muhimu ambazo Bunge letu linaweza kufuatilia utekelezaji kwa nchi yetu na tukawasaidia Wananchi.

Kwa hiyo, ningependa kupata *commitment* ya Waziri kwamba, katika nyaraka ambazo wao Wizara wanaona ni muhimu sana kwetu Wabunge, zile zinazopitia kwa Katibu wa Bunge zipitie, lakini zile wanazoweza kuchapisha wakatuletea, watumie hii nyongeza ya fedha kuchapisha na kutuletea.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru umeeleweka, Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndivyo haswa tunavyokusudia; kwa sababu kama unavyoona kifungu hiki kilikuwa na fedha kidogo, sasa imeongezeka. Tutaendelea katika lile jukumu letu la kutoa taarifa kwa wingi kwa makundi mbalimbali pamoja na Bunge Tukufu ili kuweza kuwa na vipeperushi, taarifa mbalimbali, kutumia teknolojia ya kisasa kusambaza habari. Yote yamo katika sehemu hii na utaona tofauti katika mwaka huu wa fedha.

Nakuomba Mheshimiwa Mnyika, uendeleze hii kazi nzuri ya kuitetea sana Wizara hii iongezewe fedha. Ahsante sana. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko* yoyote)

Kif. 1009 - *Management Information System* … Sh. 444,604,000
Kif. 1010 - *Internal Audit Unit* … … … … … … Sh. 227,271,000
Kif. 1011 - *Legal Service Unit* … … … … ..... … Sh. 300,686,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko* yoyote)

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Bunge hili likikaa kama Kamati ya Matumizi, limepitia Makadirio ya Matumizi na Mapato ya Fungu Namba 97 la Wizara yangu ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kupitia kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Makadirio hayo yapitishwe na Bunge hili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka 2014/2015 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nawapongeza sana Wizara ya Afrika Mashariki; Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu, Wataalam na Wabunge wote wa *EALA,* kwa kazi nzuri mnayofanya. Katibu, hatua inayofuata!

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**

**Hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo Kama Ilivyosomwa Bungeni**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha taarifa ya mapitio ya kazi za Wizara kwa mwaka 2013/2014 na mwelekeo wa kazi za Wizara kwa mwaka 2014/15. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilali, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zao za kuongoza, kusimamia na kuendeleza amani, utulivu, mshikamano na uchumi wa nchi yetu. Pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa uamuzi wake wa kuanzisha mchakato wa kupata Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile napenda kuwapongeza Wajumbe wa Bunge Maaalum la Katiba, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushiriki katika mchakato wa kupata Katiba. Tuna imani kuwa mchakato huu utatuwezesha kupata Katiba itakayofaa kwa kipindi kijacho. Aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuniteua mimi na Naibu Waziri, Mheshimiwa Kaika Saning'o Ole-Telele,

Mbunge wa Ngorongoro, kuongoza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na tunaahidi kutumia uwezo wetu wote katika kutekeleza majukumu tuliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri, kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais katika nafasi zao mpya. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya, waliojiunga na Bunge lako Tukufu kufuatia chaguzi ndogo zilizofanyika katika Jimbo la Chambani, Mheshimiwa Yusuf Salum Hussein, Jimbo la Kalenga, Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa na Jimbo la Chalinze, Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kiketwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Hayati Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa aliyekuwa Mbunge wa Kalenga na Hayati Said Ramadhani Bwanamdogo aliyekuwa Mbunge wa Chalinze. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu, ndugu na Wananchi wa Majimbo waliyokuwa wanayawakilisha. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwakumbuka Wananchi wenzetu waliopoteza maisha kutokana na mafuriko, ajali na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo na Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushauri, maoni, maelekezo na ushirikiano waliotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maandalizi ya bajeti hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri, mapendekezo na maoni ya Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi, kwa Hotuba yake nzuri, yenye kutoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi za Serikali kwa mwaka 2014/2015. Aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote waliotoa Hotuba zao ambazo zimeainisha maeneo mbalimbali tunayoshirikiana nao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini. Vilevile, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao kuhusu masuala ya maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi kupitia Hotuba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya Sekta za Mifugo na Uvuvi na Changamoto Zilizopo. Katika mwaka 2013, Sekta ya Mifugo ilikua kwa asilimia 3.8 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2012 na kuchangia asilimia 4.4 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2012. Aidha, idadi ya mifugo nchini inakadiriwa kuwa ng'ombe milioni 22.8, mbuzi milioni 15.6 na kondoo milioni 7.0. Pia, wapo kuku wa asili milioni 35.5, kuku wa kisasa milioni 24.5 na nguruwe milioni 2.01. Viwango vya ulaji wa mazao ya mifugo kwa sasa ni wastani wa kilo 12 za nyama, lita 45 za maziwa na mayai 75 kwa mtu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi yetu ina ukanda wa Pwani wa Bahari wenye urefu wa kilometa 1,424 ambao umegawanyika katika eneo la Maji ya Kitaifa lenye ukubwa wa kilometa za mraba 64,000 na eneo la Bahari Kuu kilometa za mraba 223,000. Eneo la maji baridi linajumuisha Maziwa Makuu matatu ambayo ni Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, Maziwa ya Kati na Madogo 29, Mito na maeneo oevu.

Katika mwaka 2013, Sekta ya Uvuvi ilikua kwa asilimia 2.2 ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2012. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kumechangiwa na kupungua kwa mauzo ya samaki

na mazao yake nje ya nchi. Aidha, mchango wa Sekta hii kwa Pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia 1.4 kwa mwaka 2013. Vilevile, idadi ya wavuvi wadogo imeongezeka kutoka wavuvi 182,741 mwaka 2012/2013 hadi wavuvi 183,341 mwaka 2013/2014 na Wananchi zaidi ya milioni 4.0 wameendelea kutegemea shughuli za uvuvi, ikiwemo biashara ya samaki, uchakataji wa mazao ya uvuvi, utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi na biashara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 zimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zilizoainishwa katika aya ya 10 ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2013/2014 na Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka 2014/2015. Mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2013/2014 kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli na matumizi ya fedha yamefafanuliwa kwa ufasaha kuanzia aya ya 12 hadi aya ya 14 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu, kupitia na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mikakati na programu mbalimbali za kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini. Katika mwaka 2013/2014, Sera na Sheria za Sekta za Mifugo na Uvuvi zimeendelea kupitiwa na Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuboresha mazingira ya kibiashara kama ilivyoainishwa katika aya ya 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa Sekta ya Mifugo. Zao la Maziwa: Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa asilimia 3.5 kutoka lita bilioni 1.9 mwaka 2012/2013 hadi lita bilioni 2.0. Aidha, maziwa yanayosindikwa kwa siku yameongezeka kutoka lita 135,300 mwaka 2012/2013 hadi lita 139,800 mwaka 2013/2014. Pia, Wizara imeendelea kuboresha Mashamba ya Uzalishaji Mifugo ili kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo ya asili ambapo katika mwaka 2013/2014, jumla ya mitamba 681 ilizalishwa katika mashamba ya Wizara na kusambazwa kwa wafugaji mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji kama njia yenye tija ya kuzalisha mifugo bora. Katika mwaka 2013/2014, Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji – NAIC Usa River pamoja na Vituo vya Kanda vya Uhimilishaji vya Kibaha, Dodoma, Lindi, Mwanza na Uyole – Mbeya vimeimarishwa. Jumla ya dozi 58,210 za mbegu bora zimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji. Pia, ng'ombe 90,300 wamehimilishwa katika mikoa mbalimbali.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha uhimilishaji nchini kwa kuzalisha dozi 190,000 za mbegu, kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha Sao Hill, kuimarisha Kituo cha Uhimilishaji cha Taifa cha NAIC – Usa River na Vituo sita vya Kanda vya Uhimilishaji. Aidha, Wizara itaendeleza teknolojia ya uhawilishaji kiinitete kwa kukamilisha ujenzi wa Maabara ya TALIRI - Mpwapwa na kuitumia teknolojia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyama: Katika mwaka 2013/2014, uzalishaji wa nyama umeongezeka kutoka tani 553,455 mwaka 2012/2013 hadi tani 563,086 mwaka 2012/2013. Aidha, wadau wameendelea kuhamasishwa kutumia mfumo wa unenepeshaji mifugo ambapo ng'ombe walionenepeshwa wameongezeka kwa asilimia 11 kutoka ng'ombe 155,206 mwaka 2012/2013 hadi ng'ombe 175,000 mwaka 2013/2014. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuhamasisha uzalishaji, usindikaji wa nyama, kuweka mazingira mazuri ili sekta binafsi iwekeze zaidi. Pia, Serikali itaendelea kuhamasisha unenepeshaji ili kufikia idadi ya ng'ombe 200,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeimarisha minada ya Pugu, Lumecha (Songea), Meserani (Arusha) na Nyamatala (Misungwi). Aidha, Mnada wa Upili wa Nyamatala umezinduliwa rasmi tarehe 8 Aprili, 2014. Minada ya Kirumi (Butiama) na Longido inaendelea kujengwa. Vilevile, wafanyabiashara 340 walipatiwa mafunzo kuhusu biashara, matumizi ya mizani na umuhimu wa kulipa mapato ya Serikali kwenye minada ya upili na ya mipakani. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea na ujenzi wa Minada ya Longido na Kirumi na kukarabati Minada ya Pugu, Weruweru, Sekenke, Kizota, Meserani na Igunga. Aidha, Serikali itaendelea kuratibu uuzaji wa mifugo katika minada na kuhamasisha matumizi ya mizani ya kupimia uzito wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, jumla ya ng'ombe 1,215,541, mbuzi 960,199 na kondoo 209,292 wenye thamani ya shilingi bilioni 989.3 waliuzwa minadani. Katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika ujenzi wa viwanda na biashara ya mifugo na mazao yake ili kuongeza mauzo ya nyama ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NARCO* imeendelea kuzalisha, kunenepesha, kuuza mifugo kwa ajili ya nyama na kuendesha machinjio ya Dodoma kwa ubia na Kampuni ya *NICOL*. Aidha, Kampuni imeendelea kutoa huduma za ushauri kwa wafugaji wanaozunguka ranchi 10 za mfano za Kagoma, Kalambo, Kikulula, Kongwa, Mabale, Missenyi, Mkata, Mzeri, Ruvu na West Kilimanjaro. Katika mwaka 2014/2015, *NARCO* itaendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Ruvu na kununua ng'ombe wazazi 1,200 ili kuongeza idadi ya ng'ombe katika ranchi zake. Aidha, jumla ya ndama 4,050 wanategemea kuzaliwa kutokana na ng'ombe wazazi 5,786. Pia, Kampuni itaendelea na jitihada za kuongeza uzalishaji kwa kutafuta mitaji mipya na kuvutia wawekezaji kwa ubia katika ranchi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, jumla ya vifaranga milioni 61 vya kuku wa nyama na mayai vilizalishwa nchini, ikilinganishwa na vifaranga milioni 52 mwaka 2012/2013. Pia, mayai 348,000 ya kuku wazazi na mayai 6,240,000 ya kutotolesha vifaranga yaliingizwa nchini. Vilevile, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka bilioni 3.7 mwaka 2012/2013 hadi mayai bilioni 3.9 mwaka 2013/2014. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika ufugaji wa kuku kibiashara na kushirikiana na wadau kuandaa maonesho yatakayowezesha wadau kuzalisha mazao bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, uzalishaji wa nyama ya nguruwe umeongezeka kwa asilimia 35 kutoka tani 50,814 mwaka 2012/2013 hadi tani 79,174 mwaka 2013/2014. Ili kuimarisha ufugaji wa nguruwe nchini, Wizara imenunua nguruwe wa mbegu 24 mbali ya *Large White* na *Duroc* na kuwapeleka katika Shamba la Ngerengere ili kuwazalisha na kusambaza mbegu bora kwa wafugaji. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha uzalishaji wa nguruwe nchini kwa kuongeza nguruwe wazazi katika Shamba la Ngerengere. Aidha, Wizara itashirikiana na Halmashauri kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ufugaji wa nguruwe wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, ngozi zilizosindikwa na kuuzwa nje ya nchi ziliongezeka kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe 969,060 vyenye thamani ya shilingi bilioni 32.3 na vipande vya ngozi za mbuzi na kondoo 2,582,525 vyenye thamani ya shilingi bilioni 18.6 katika mwaka 2012/2013 hadi kufikia vipande vya ngozi za ng'ombe 1,060,777 vyenye thamani ya shilingi bilioni 39.4 na vipande vya ngozi za mbuzi na kondoo 2,715,436 vyenye thamani ya shilingi bilioni 19.6 katika mwaka 2013/2014. Aidha, vipande vya ngozi za ng'ombe 250,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 12.5 vilisindikwa hadi hatua ya mwisho na kutumika kutengeneza bidhaa za ngozi hapa nchini ikilinganishwa na vipande vya ngozi za ng'ombe 212,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 15.0 katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Viwanda na Biashara, Halmashauri 75 na Chama cha Wadau wa Ngozi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo, imewajengea uwezo Wataalam 40 wa Halmashauri. Aidha, imewezesha uimarishaji wa Chama cha Wazalishaji wa Ngozi cha Kitaifa na ukamilishaji wa taratibu za uanzishwaji wa Chama cha Wazalishaji wa Ngozi nchini, ambacho kitasimamia masilahi ya wazalishaji wa ngozi wakiwemo wafugaji, wachinjaji na wakusanyaji wa ngozi katika Halmashauri zote nchini. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi katika Halmashauri 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Rasilimali za Ardhi, Maji na Malisho kwa Mifugo na Utatuzi wa Migogoro. Katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuhimiza Halmashauri kuandaa Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi na kutenga maeneo ya ufugaji kwa ajili ya kuendeleza malisho ya mifugo katika Halmashauri zote nchini. Upatikanaji wa maeneo ya malisho utaepusha migogoro ya mara kwa mara kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Hadi sasa, vijiji 589 katika Wilaya 80 ndani ya Mikoa 22 vimepimwa kutenga maeneo kwa ajili ya ufugaji na kufanya jumla ya eneo lililopimwa kufikia hekta milioni 1.51. Katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri itaainisha na kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya maendeleo endelevu ya rasilimali za mifugo katika Wilaya za Busega, Kiteto, Kilosa, Ngorongoro, Mvomero, Kilindi, Igunga, Iramba na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inakemea tabia inayozidi kujengeka ya kutesa mifugo kwa kuinyima chakula na maji, kuipiga risasi au kuikata mapanga, kwa kisingizio cha migogoro ya ardhi, kwani huko ni kuvunja Sheria ya Ustawi wa Wanyama Namba 19 ya Mwaka 2008. Kosa haliwezi kurekebishwa kwa kutenda kosa. Aidha, wafugaji wanasisitizwa kuheshimu shughuli za watumiaji wengine wa ardhi kwani jamii zote zinategemeana. Wizara itaendelea kuhamasisha jamii ya wafugaji kuanza kumiliki ardhi na kuiendeleza, kufuga kibiashara na kuachana na ufugaji wa kuhamahama kwani siyo endelevu. *(Makofi)*

Katika mwaka 2014/15 Serikali itaangalia upya maeneo yaliyobinafsishwa na kushindwa kuendelezwa ikiwa ni pamoja na maeneo ya Ranchi za Taifa na maeneo ya hifadhi yaliyopoteza sifa ili yatumike kwa shughuli za ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mbegu za malisho ya Vikuge (Kibaha), Sao Hill (Mufindi), Langwira (Mbeya), Mabuki (Misungwi) na Kizota (Dodoma). Mashamba hayo yamezalisha mbegu za malisho tani 48.2 na marobota ya hei 497,620. Pia, sekta binafsi imezalisha marobota 425,000 ya hei. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora za malisho na kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa malisho na mbegu bora za malisho. Pia, Serikali itawezesha uchimbaji wa kisima kirefu cha maji ya mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Same, kujenga malambo na majosho katika Wilaya za Chemba, Handeni, Kiteto, Kilwa, Chunya, Kilindi na Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa zoezi la kutoa kifuta machozi kwa wafugaji waliopoteza mifugo yao yote katika Wilaya za Longido, Monduli na Ngorongoro kutokana na ukame uliotokea mwaka 2008/2009, umeendelea kutekelezwa. Hadi sasa ng'ombe 17,214 na mbuzi 6,190 wenye thamani ya shilingi bilioni 7.4 waligawiwa kwa wafugaji, sawa na asilimia 70 ya malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo cha Kanda ya Kusini Magharibi, Mjini Sumbawanga, kwa kukipatia vitendea kazi na Wataalam. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha eneo huru la magonjwa ya mifugo kwa kukarabati Jengo la Ofisi la Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo cha Kanda ya Kusini Magharibi, kuwajengea uwezo wataalam na kukipatia vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia kampeni za chanjo ya Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo katika mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro na Kagera, ambapo jumla ya mbuzi na kondoo 1,163,451 walichanjwa dhidi ya ugonjwa huo. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itanunua dozi 1,000,000 za chanjo ya Sotoka ya Mbuzi na Kondoo na kuzisambaza katika Mikoa ya Arusha, Tanga, Mara na Tabora, iliyo katika hatari ya kuwa na mlipuko wa ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kufuatilia mwenendo wa Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege hapa nchini na nje ya nchi. Ufuatiliaji huu umebaini kuwa ugonjwa huo haujaingia hapa nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, imeendelea kutoa tahadhari ili kuhakikisha kuwa virusi vya ugonjwa huo haviingii hapa nchini. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huu. Aidha, Wizara itaendelea kushirikisha wadau wengine ikiwa ni pamoja na *AU-IBAR,* kufuatilia mwenendo wa ugonjwa ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kufuatilia Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe nchini kwa kuchanja ng'ombe 290,000 katika Mikoa ya Pwani, Kagera, Manyara na Tanga. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itanunua dozi 3,000,000 za chanjo kwa ajili ya kuendeleza uchanjaji katika mikoa yenye matukio ya ugonjwa ikiwemo Mikoa ya Kagera, Geita na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau wengine kudhibiti kupe na magonjwa yanayoenezwa na kupe. Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza mpango wa ruzuku ya asilimia 40 kwa dawa za kuogesha mifugo, ambapo lita 10,736 zenye kiini cha pareto zilinunuliwa kwa thamani ya shilingi milioni 181.8 na kusambazwa katika mikoa 24. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea kuhamasisha matumizi ya chanjo dhidi ya Ugonjwa hatari wa Ndigana Kali ambapo jumla ya ng'ombe 113,955 walichanjwa dhidi ya ugonjwa huo katika Mikoa ya Arusha, Manyara, Tanga, Kilimanjaro, Dodoma, Tabora, Kagera na Pwani. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea

kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine, kuhamasisha matumizi ya chanjo hii, ujenzi na ukarabati wa majosho pamoja na matumizi sahihi ya dawa za kuogesha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara ilishirikiana na wadau mbalimbali kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Mbung'o na Nagana. Katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Programu ya *Pan African Tsetse and Trypanosomiasis Eradication Campaign (PATTEC),* itaendelea kudhibiti Mbung'o na Nagana kwa kutekeleza miradi ya kuangamiza mbung'o kwa ajili ya Mikoa ya Mara, Ikolojia ya Serengeti, Kigoma, Tabora, Rukwa na Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magonjwa ya Mifugo yanayoambukiza Binadamu. Katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Mradi wa Kutokomeza Kichaa cha Mbwa, unaofadhiliwa na Taasisi ya *Bill & Melinda Gates Foundation,* kwa uratibu wa Shirika la Afya Ulimwenguni, imeendelea kudhibiti Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Morogoro, Mtwara na Pwani kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na wadau mbalimbali.

Jumla ya dozi 200,000 zimesambazwa katika Halmashauri 24 zinazotekeleza Mradi huu. Udhibiti wa magonjwa mengine ya mifugo yanayoambukiza binadamu ni pamoja na Homa ya Bonde la Ufa, Ugonjwa wa Kutupa Mimba na Kifua Kikuu kama ilivyoainishwa katika Aya ya 43 na 44 ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, jumla ya ng'ombe 987,172, mbuzi 885,061, kondoo 275,197, nguruwe 440,000 na kuku 1,632,000 walikaguliwa na wataalam katika machinjio mbalimbali. Aidha, Wizara imeendesha mafunzo rejea kwa Wakaguzi wa Nyama 12 kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na wadau 34 kutoka machinjio ya Vingunguti. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kufuatilia usalama wa mazao yatokanayo na mifugo kwa kukagua mifugo na mazao yake ili kukuza biashara ya mifugo na kulinda afya za walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo. Wizara imeendelea kuimarisha Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo kwa kutoa mafunzo kuhusu stadi za utambuzi wa mifugo na ukusanyaji takwimu. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa mfumo wa kielektroniki wa utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo kwa kutoa mafunzo kwa wataalam wa mifugo 75 kuhusu mfumo huo na kuhamasisha umma ili kuwezesha utambuzi wa mifugo 45,000 katika makundi ya wafugaji wa ng'ombe wa asili na kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imetoa elimu ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi unaozingatia mfumo wa ikolojia na mazingira kwa wavuvi 641 kutoka Halmashauri za Bagamoyo, Kinondoni, Temeke na Mkuranga. Aidha, Maafisa Uvuvi 16 wa Wilaya, Wavuvi 16 na Wawakilishi wa Vikundi vya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi *(BMUs)* 16 kutoka Halmashauri 16 za Ukanda wa Pwani, walipatiwa mafunzo kuhusu usimamizi endelevu wa rasilimali ya Jodari na samaki wanaopatikana katika tabaka la juu la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvu ya uvuvi nchini imeongezeka kutoka wavuvi 182,741 na vyombo vya uvuvi 56,985 mwaka 2012/2013 hadi wavuvi 183,431 wanaotumia vyombo vya uvuvi 57,385 mwaka 2013/2014. Kutokana na nguvu hiyo ya uvuvi, jumla ya tani 375,158 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 1.4 zilivunwa ambapo kati ya hizo, tani 52,846 ni kutoka ukanda wa maji chumvi na tani 147,020 maji baridi, ikilinganishwa na tani 365,023.38 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 1.3 zilizovunwa mwaka 2012/2013.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu, kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na kufanya sensa za uvuvi katika Bahari, Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa, Rukwa, Bwawa la Nyumba ya Mungu na Mto Rufiji, kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji, uchambuzi na uhifadhi wa takwimu za uvuvi na kuhamasisha jamii za wavuvi kusimamia, kuendeleza na kulinda rasilimali za uvuvi kwa kuzingatia mfumo wa ikolojia na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwezeshaji Wavuvi Wadogo: Katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Programu ya *SmartFish* na *United Nations University Iceland* imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia sahihi kwa ajili ya uandaaji, uchakataji na usambazaji wa mazao ya uvuvi kwa wavuvi 735 katika Mikoa ya Kigoma, Kagera, Mara, Mwanza na Pwani na kuwezesha ujenzi wa vichanja vya kisasa 40 vya kukaushia samaki na majiko sanifu manne katika Halmashauri ya Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *WWF*, iliwawezesha wavuvi kutoka Halmashauri za Kilwa, Lindi, Mtwara, Pangani na Mafia kuhudhuria mafunzo ya uchakataji wa samaki aina ya Jodari na utunzaji wa samaki wa mapambo; usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kupitia *BMUs* na uendeshaji wa Miradi. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu fursa za uwekezaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kutengeneza boti hasa za *fibre* na zana za uvuvi zinazokubalika kisheria. Vilevile, itaendelea kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kukamilisha ujenzi wa mialo minne katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika, ujenzi wa karakana ya kutengeneza boti katika Ukanda wa Ziwa Nyasa pale *Mbamba Bay* na kuendeleza mchakato wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuzaji wa viumbe kwenye maji: Katika mwaka 2013/2014, jumla ya vifaranga 2,295,032 vimezalishwa na kusambazwa ambapo vifaranga 19,692 vimezalishwa katika Vituo vya Serikali na 2,275,340 katika vituo vya sekta binafsi. Aidha, Wananchi 2,604 wamehamasishwa kwa kupatiwa elimu ya ufugaji samaki na kutokana na uhamasishaji huo, mabwawa ya kufugia samaki yameongezeka kutoka 20,134 mwaka 2012/2013 hadi 20,493 mwaka 2013/2014 yenye uwezo wa kuzalisha tani 3,546 za samaki. Pia, tani 320 za kambamiti zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.56 zimevunwa katika mabwawa ya Kampuni ya *Alphakrust* katika Wilaya ya Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuimarisha Vituo vya Utafiti vya *TALIRI* vya Kongwa, Mabuki, Mpwapwa, Naliendele, Tanga, Uyole na West Kilimanjaro kwa kuvipatia vitendea kazi na kukarabati miundombinu. Aidha, Taasisi imeendelea kutekeleza miradi ya utafiti wa mifugo ya kuboresha uzalishaji wa ng'ombe wa nyama na maziwa, nguruwe, kuku, malisho na masoko ya mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, *TALIRI* imetathmini na kusambaza ng'ombe 143 aina ya Mpwapwa kwa wafugaji katika Manispaa za Dodoma na Tanga na Halmashauri za Chamwino, Kilindi, Kisarawe na Bagamoyo. Aidha, Taasisi imesambaza jumla ya madume 32 aina ya *Friesian* katika Wilaya za Bagamoyo, Muheza, Mufindi na Njombe na Mbuzi aina ya Malya 65 katika maeneo ya Mikoa ya Dodoma na Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia fedha za maendeleo chini ya *COSTECH*, *TALIRI* imekamilisha ujenzi wa jengo la maabara ya nyama, nyumba tatu za watumishi katika Kituo cha Mabuki na ukarabati wa jengo la maabara ya viini tete Mpwapwa. Pia, inaendelea na ukarabati wa jengo la maabara ya maziwa Uyole, Ofisi ya Tanga na mabanda ya mbuzi West Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, jumla ya aina 39 za malisho ya asili zimekusanywa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini vituoni. Vilevile, jumla ya marobota 44,347 ya malisho yalivunwa katika vituo vya Mpwapwa, Uyole na Kongwa. Katika mwaka 2014/2015, *TALIRI* itaimarisha miundombinu ya utafiti kwa kununua vifaa vya maabara, kemikali na samani katika maabara ya sayansi ya nyama ya Mabuki, Uhawilishaji Viinitete (Mpwapwa), maabara ya teknolojia ya maziwa (Uyole), maabara za lishe ya mifugo (Mpwapwa, Tanga, Naliendele na West Kilimanjaro).

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* katika mwaka 2013/2014, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)* imekarabati Ofisi ya Utawala ya Kituo cha Kyela na kujenga uzio katika kituo cha Dar es Salaam, matangi tisa katika kituo cha Dar es Salaam kwa ajili ya utafiti wa majaribio ya vyakula vya samaki kutokana na malighafi asili. Pia, imechimba mabwawa ya vifaranga bora vya samaki katika Kituo cha Mwanza na kuimarisha utafiti katika vituo vya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Kyela na kituo kidogo cha Sota (Rorya). Aidha, *TAFIRI* imebaini kuwa wingi wa samaki aina ya Sangara katika Ziwa Victoria umeshuka kutoka mavuno ya kilo 296 kwa saa mwaka 2008 hadi kufikia kilo 185 kwa saa mwaka 2013.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara ikishirikiana na wadau wengine wa uvuvi, itaendelea kuiwezesha *TAFIRI* kuendelea na tafiti za uvuvi na mazingira katika Bahari ya Hindi, Maziwa, Mito na Mabwawa ili kubaini uwingi, mtawanyiko na ikolojia ya rasilimali kwa ajili ya kuweka menejimenti ya uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi *(Fisheries Education and Training Agency – FETA),* katika mwaka 2013/14 imekarabati Kituo cha Kigoma na kupata usajili wa kudumu kutoka *NACTE.* Udahiri wa wanafunzi umeongezeka kutoka wanachuo 943 mwaka 2012/2013 hadi wanachuo 1073 mwaka 2013/2014. Aidha, Wakala umeendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam 54 kutoka nchi za SADC. Katika mwaka 2014/15, Wizara itaendelea kuiwezesha Wakala kutekeleza majukumu yake ya kuongeza udahiri wa wanafunzi kutoka 1,073 hadi 1,500. Aidha, *FETA* itaendelea kujenga Kituo cha Gabomori Rorya na kukarabati Kituo cha Mikindani Mtwara.

Mhheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo *(Livestock Training Agency - LITA)*, katika mwaka 2013/2014 imeongeza udahili wa wanafunzi kutoka 949 mwaka 2012/2013 hadi 2215, wakiwemo 655 wa stashahada na 1560 wa stashahada za afya mifugo na uzalishaji. Vilevile Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na vyuo binafsi vya Visere Mpwapwa na Kaole Bagamoyo vimedahili jumla ya wanafunzi 492 wa Stashahada na Astashahada.

Katika mwaka 2014/2015 Wizara itaendelea kuiwezesha Wakala kutekeleza majukumu yake na kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 2,215 hadi 2,500. Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha vyuo na kuongeza udahili kufikia lengo la wanafunzi 5,000 kwa mwaka ili kupunguza pengo la maafisa ugani na kuwezesha mafunzo ya ufugaji kibiashara kwa vijana *(Emerging Young Commercial Farmers)* ili waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/14 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau, imeendelea kutoa elimu na kusambaza teknolojia za kisasa kuhusu uvuvi endelevu, ukuzaji bora wa viumbe kwenye maji na ufugaji bora wa mifugo. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha utoaji huduma za ugani katika Sekta ya Uvuvi kwa kutoa mafunzo elekezi ya ufugaji wa samaki kwa wataalam kumi na moja na wadau wa uvuvi 256 katika Mikoa ya Tanga, Iringa na Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/14, Wizara kupitia Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania *(Tanzania Veterinary Laboratory Agency – TVLA),* ilitekeleza kazi za utambuzi,

uchunguzi na utafiti wa magonjwa ya mifugo, uhakiki wa vyakula vya mifugo na madawa ya kuogeshea mifugo katika Maabara zake za Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Tabora, Mpwapwa, Tanga, Kigoma, Iringa na Mtwara. Aidha, *TVLA* kwa kushirikiana na Idara ya Wanyamapori, imetengeneza vitambaa 300 na kuviweka katika maeneo ya Pori la Akiba la Selous ili kudhibiti mbung'o.

Katika mwaka 2014/2015, *TVLA* itaendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuendelea kufanya utambuzi wa magonjwa mbalimbali ya mifugo, kuendeleza tafiti za magonjwa ya mifugo, kuzalisha dozi milioni mia moja za chanzo ya mdondo, dozi laki tano za chanjo ya chambavu, dozi laki tano za chanjo ya kimeta na dozi laki mbili na elfu hamsini za chanjo ya ugonjwa wa kutupa mimba kwa ng'ombe na Maabara Kuu ya Mifugo Temeke kukamilisha taratibu za kupata Ithibati ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa ubora wa mazao na huduma za mifugo na uvuvi. Katika mwaka 2013/2014 Wizara imeendelea kuiimarisha Bodi ya Nyama Tanzania kwa kuipatia wataalam na vitendeakazi. Aidha, Bodi imeandaa maelezo ya Sheria ya Nyama, Sura 421, katika Lugha ya Kiswahili na kutoa elimu kwa wadau kupitia vipindi vya redio 14 na kusambaza nakala 800 za vipeperushi. Vilevile Bodi imehamasisha wadau wa tasnia ya nyama katika Mikoa ya Simiyu, Mwanza, Geita, Dar es Salaam, Arusha, Iringa na Pwani kusajili ambapo wadau 116 wamesajiliwa na wadau wengine 50 wameunganishwa na soko la mifugo na nyama.

Katika mwaka 2014/15, Bodi ya Nyama Tanzania itaendelea kuiimarisha Sekretarieti ya Bodi kwa kuajiri watumishi sita na kutambua na kusajili wadau 200 wa tasnia ya nyama na vyama vyao. Vilevile Bodi itaendelea kuimarisha Vyama vya Wadau vya Wafanyabiashara wa Mifugo na Nyama Tanzania *(TARIMETA),* Wasindikadi wa Nyama Tanzania *(TAMEPA)* na Wafugaji Tanzania *(CCWT)*, kwa kushauri, kutoa mafunzo na kuratibu maendeleo ya vyama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 Wizara imeendelea kuimarisha Bodi ya Maziwa Tanzania iliyoundwa kwa Sheria ya Maziwa, Sura 262. Aidha, Bodi imeelimisha wadau 100 wa maziwa kuhusu Sheria ya Maziwa katika Mkoa wa Njombe. Katika mwaka 2014/2015, Bodi itaendelea kuelimisha wadau wa maziwa kuhusu Sheria ya Maziwa, Sura 262 na kuisimamia, kuwajengea uwezo wakaguzi 50 wa maziwa kutoka Halmashauri za Mikoa ya Iringa, Njombe na Mara na kuhamasisha Halmashauri kutekeleza mpango wa unywaji wa maziwa shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Veterinari Tanzania katika mwaka 2013/2014 limeimarisha ukaguzi katika ngazi za Kanda, Mikoa na Halmashauri ambapo wakaguzi wapya 200 wameteuliwa. Pia imesajili madaktari wa mifugo 37, wataalamu wasaidizi wa afya ya mifugo 221 na vituo 106 vya kutolea huduma za afya ya mifugo. Katika mwaka 2014/2015, Baraza litasajili madaktari wa mifugo 40, vituo vya huduma za mifugo 200, kuorodhesha na kuandikisha wataalamu wasaidizi 700, kutoa leseni kwa wataalamu wasaidizi 110 na kufanya ukaguzi wa maadili kwa kushirikiana na Halmashauri 156 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi na Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi Nyegezi, imeendelea kuratibu na kusimamia ubora, viwango na usalama wa mazao ya uvuvi pamoja na huduma za kitaalam, ikiwepo kufanya kaguzi mbalimbali za kuhakiki ubora wa mazo ya uvuvi katika viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, mialo, masoko na kwenye magari na boti zinazosafirisha mazao ya uvuvi.

Mheshimwia Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuimarisha Vituo vya Udhibiti Ubora wa Mazao ya Uvuvi vya Bukoba, Dar es Salaam, Kigoma, Kilwa, Mafia, Musoma, Mwanza na Tanga,

pamoja na Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi Nyegezi, kwa kuvipatia watumishi na vitendeakazi. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya sampuli 1,318 za samaki, maji, vyakula na samaki za udongo zilifanyiwa uchunguzi. Kati ya hizo, 966 zilichunguzwa kubaini uwepo wa vimelea vya magonjwa na 352 kubaini mabaki ya viuatilifu, madini tembo na kemikali. Matokeo ya uchunguzi wa sampuli hizi ulionesha kukidhi viwango. Katika mwaka 2014/2015 Wizara itaendelea kuimarisha Vituo vya Ubora na Udhibiti wa Mazao ya Uvuvi na Maabara za Uvuvi Nyegezi kwa kuvipatia vitendea kazi na mafunzo kwa wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na Halmashauri, imeendelea kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi kwa kudhibiti uvuvi haramu na utoroshaji wa samaki na mazao ya uvuvi mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeanzisha Kituo cha Doria cha Buhingu Uvinza na kufanya vituo vya doria kufikia 23. Pia doria zenye siku kazi 6201 zimefanyika na kuwezesha kukamata nyavu mbalimbali 33,861, vyandarua 123, mabomu 73, tambi za kulipulia mabomu 15, mitungi ya gesi 48, viatu vya kuzamia jozi 35, miwani ya kuogelea jozi 11, mitumbwi 194, injini za boti 10, magari 12 na pikipiki 12. Vilevile watuhumiwa 319 walikamatwa kwa kujihusisha na uvuvi na biashara haramu ya mazao uvuvi ambapo kesi 48 zilifunguliwa mahakamani.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea kuratibu na kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi na kudhibiti biashara haramu ya mazao ya uvuvi, kwa kufanya doria zenye siku kazi 6,000 katika maeneo ya maji baridi, Bahari ya Kitaifa na maeneo ya mipakani. Aidha, itaendelea kuwezesha uanzishwaji wa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi *(BMUs)* na kuimarisha vikundi vilivyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, inaendelea kufanya utafiti kuhusu matumizi sahihi ya vifaa vya kuvutia samaki *(Fish Aggregating Devices - FADs)*. Pia mamlaka imeendelea kuandaa mazingira rafiki ambayo yatawawezesha Watanzania kuingia ubia na wageni ili waweze kuwekeza kwenye uvuvi katika Bahari Kuu. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na nchi wanachama wa *Indian Ocean Tuna Commission (IOTC)* za Comoro, Madagascar, Seychelles, Reunion na Mauritius, ilifanya doria za pamoja za siku nane kukagua meli nane zilizovua katika Bahari Kuu ya Tanzania. Pia ukaguzi ulifanyika kwa meli 25 za uvuvi wa *purse seine* na *long liner* zenye Bendera ya Hispania, Taiwan na China katika Bandari za Dar es Salaam na Zanzibar, Mombasa, Mahe Victoria (Ushelisheli), Madagascar na Mauritius. Katika ukaguzi huo meli husika zilionekana kukidhi masharti ya leseni. Vilevile leseni za uvuvi wa Bahari Kuu 68 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 1,472,153, sawa na Shilingi 2,400,000,000, zilitolewa kwa meli kutoka Mataifa ya Hispania, Ufaransa, Ushelisheli, Taiwan, Japan Oman na China.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaiwezesha Mamlaka kukamilisha marekebisho ya Sheria na Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu, kuendesha doria na kufanya tathmini ya utendaji wa *FADs*. Pia kuendelea kuhamasisha Wavuvi wa Tanzania na wawekezaji wengine kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu na kusindika mazao ya uvuvi. Vilevile kuendelea kutoa mafunzo ya uvuvi wa Bahari Kuu kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia maendeleo ya rasilimali za uvuvi katika maeneo yaliyohifadhiwa kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu *(MPRU)*, ambapo doria zenye siku kazi 800 zilifanyika, zilizowezesha kukamata vifaa mbalimbali

yakiwemo mabomu 21 na tambi zake, chupa za mbolea ya urea inayotumika kutengeneza mabomu na makokoro matano.

Katika mwaka 2014/2015, kitengo kitafanya doria zanye siku kazi 416 katika eneo la kilometa za mraba 2000, kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu kwenye hifadhi za bahari na maeneo tengefu na pia kuvutia uwekezaji wa utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 Wizara imeajiri watumishi 124 wakiwemo 71 wa kada za mifugo, 43 kada za uvuvi na 10 kada mtambuka. Aidha, Maafisa Mifugo na Uvuvi 853 wameajiriwa na kupelekwa katika Sekretarieti za Mikoa 17 na Halmashauri 103 nchini kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Vilevile watumishi wamepandishwa vyeo, wamebadilishwa kazi kulingana na kanuni za utumishi.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara inatarajia kuajiri watumishi 214 wakiwemo wa mifugo 62, uvuvi 86 na mtambuka 66, kupandisha vyeo watumishi 223, kuthibitisha kazini watumishi 125 na watumishi 312 watahudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Mheshimia Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, vipindi vitano kuhusu mafanikio ya Sekta za Mifugo na Uvuvi na makala moja ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 vilitangazwa kupitia runinga na magazeti. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha Dawati la Malalamiko na Maktaba na kutoa mafunzo kwa maafisa habari wawili. Aidha, itatoa mafunzo kwa maafisa kutoka vituo vya nje kuhusu mawasiliano kwa umma na kuchapisha na kusambaza kwa wadau nakala 1,000 za kalenda.

Katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kusimamia masuala mengine mtambuka ya Utawala Bora, Jinsia, UKIMWI, TEHAMA na Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi kama yalivyoainishwa katika aya ya 110 hadi 115 ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wafugaji, Wavuvi, Wasindikaji, Wafanyabiashara na Wadau wengine, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini. Wizara inaomba waendeleze shughuli hizo na inaahidi kuendelea kushirikiana nao kuleta Mapinduzi ya Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini. Aidha, napenda kuzitambua na kuzishukuru nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Nchi za Ulaya, Serikali za Australia, Austria, Brazil, Canada, Jamhuri ya Czech, Hispania, Iceland, Ireland, Japan, Jamhuri ya Watu wa China, Israel, Korea Kusini, Marekani, Misri, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswizi pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *FAO, IAEA, Unicef, UNPD, UNIDO* na *WHO* na Mifuko ya Kimataifa ya *GEF* na *IFAD*, kwa kuchangia katika maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nazishukuru Taasisi za Kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la *JICA,* Shirika la *KOICA,* Shirika la Misaada la Ireland, *USAID,* Shirika la Misaada la Australia, *DfID,* Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika *(AU-IBAR),* Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE),* Shirika la Maendeleo ya Uswizi, Shirika la Ushirikiano wa Ujerumani *(GTZ), United Nations University,* Shirika la Maendeleo la Denmark na Shirika la Maendeleo la Sweden, kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi. Pia kwa namna ya pekee, nayashukuru Mashirika na Taasisi za Hiari za *Bill and Melinda Gates Foundation, ASARECA, NEPAD, International Livestock Research Institute, World Wide Fund for Nature, Indian Ocean Tuna Commission, South West Indian Ocean Fisheries Commission, Heifer Project International, Overseas Fisheries Cooperation Foundation of Japan, Vetaid, Care International, OXFAM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities, World Society for Protection of*

*Animals, Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine, Institute for Security Studies, International Land Coalition, British Gas International, Sea Sense, Indian Ocean Tuna Commission, International Whaling Commission, SmartFish na Marine Stewardship Council.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Kaika Saning'o Ole Telele, Mbunge wa Ngorongoro na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa msaada wake wa katibu katika kusimamia kazi za Wizara. Aidha, pia napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu, Dkt. Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Yohana Budeba, Wakuu wa Idara na Vitengo, Taasisi na Watumishi wote wa Wizara, kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa na kufanikisha maandalizi ya bajeti hii.

Vilevile napenda kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Busega, kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipatia na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu, wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya, ndugu yangu Pascal Mzindakaya, ambaye yuko hapa pamoja nasi. Pia naishukuru familia yangu kwa dhati, kwa kuendelea kunitia moyo ninapotekeleza majukumu yangu ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya Shilingi 66,142,627,000 kama ifuatavyo:-

Shilingi 40,952,022,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya hizo, Shilingi 22,968,188,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na Shilingi 17,984,834,000 ni kwa ajili ya matumizi mengine au *OC*. Shilingi 25,190,605,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi 23,000,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 2,190,605,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.mifugouvuvi.go.tz.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Hotuba hii, nimeambatisha Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo Kama Ilivyowasilishwa Mezani**

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI, MHESHIMIWA DK. TITUS MLENGEYA KAMANI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015**

**1.0 UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, iliyochambua bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2013/2014 na mwelekeo wa kazi za Wizara kwa mwaka 2014/2015. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

**2. Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt Mohamed Gharib Bilal**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda**, Mbunge wa Katavi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zao za kuongoza, kusimamia na kuendeleza amani, utulivu, mshikamano na uchumi wa nchi yetu. Pia, napenda kumpongeza **Mheshimiwa Rais** kwa uamuzi wake wa kuanzisha mchakato wa kupata katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, napenda kuwapongeza Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba kwa kuteuliwa na **Mheshimiwa Rais** kushiriki katika mchakato wa kupata katiba. Tuna imani kuwa mchakato huo utatuwezesha kupata Katiba itakayofaa kwa kipindi kijacho. Aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Rais** kwa kuniteua mimi na Naibu Waziri, Mheshimiwa **Kaika Saning'o Ole Telele** Mbunge wa Ngorongoro kuongoza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na tunaahidi kutumia uwezo wetu katika kutekeleza majukumu tuliyopewa.

**3. Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kwao na **Mheshimiwa Rais** katika nafasi zao mpya. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako tukufu kufuatia chaguzi ndogo zilizofanyika katika Jimbo la Chambani **Mheshimiwa Yusuf Salim Hussein,** Jimbo la Kalenga **Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa** na Jimbo la Chalinze **Mheshimiwa Ridhiwan Jakaya Kikwete**.

**4. Mheshimiwa *Spika,*** Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu; Hayati **Mhe. Dkt. William Augustao Mgimwa** aliyekuwa mbunge wa Kalenga na Hayati **Said Ramadhani Bwanamdogo** aliyekuwa Mbunge wa Chalinze. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salaam za rambirambi kwa familia za marehemu, ndugu na wananchi wa majimbo waliokuwa wanayawakilisha. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwakumbuka wananchi wenzetu waliopoteza maisha kutokana na mafuriko, ajali na sababu mbalimbali.

**5. Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kumshukuru **Mhe. Profesa Peter Mahamudu Msolla,** Mbunge wa Kilolo na **Mhe. Said Juma Nkumba**, Mbunge wa Sikonge pamoja na wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushauri, maoni, maelekezo na ushirikiano waliotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maandalizi ya bajeti hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri, mapendekezo na maoni ya Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu.

**6.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, **Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda**, Mbunge wa Katavi kwa hotuba yake nzuri yenye kutoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi za Serikali kwa mwaka 2013/2014. Aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote waliotoa hotuba zao ambazo zimeainisha maeneo mbalimbali tunayoshirikiana katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Vilevile, nawashukuru waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao kuhusu masuala ya maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi kupitia hotuba hizo.

## *2.0 HALI YA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI NA CHANGAMOTO ZILIZOPO*

### *Sekta ya Mifugo*

**7.** **Mheshimiwa Spika**, sekta ya mifugo ina umuhimu mkubwa katika kuwapatia wananchi lishe bora, ajira na kipato hivyo kuchangia katika kumwondolea mwananchi umaskini. Mifugo hutoa ajira, lishe, nishati, mbolea na hutumika kama wanyamakazi na benki hai. Kulingana na takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2013, sekta ya mifugo ilikua kwa asilimia **3.8** ikilinganishwa na asilimia **3.1** mwaka 2012 na kuchangia asilimia **4.4** katika pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia **4.6** mwaka 2012. Kulingana na takwimu zilizopo, idadi ya mifugo nchini inakadiriwa kuwa ng'ombe **milioni 22.8**, mbuzi **milioni 15.6** na kondoo **milioni 7.0.** Pia, wapo kuku wa asili **milioni 35.5,** kuku wa kisasa **milioni 24.5** na nguruwe **milioni 2.01.**

Aidha, ulaji wa mazao ya mifugo kulingana na viwango vya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO, 2011) ni kilo **50** za nyama, lita **200** za maziwa na mayai **300** kwa mtu kwa mwaka. Kwa upande wa nchi yetu viwango vya ulaji wa mazao hayo kwa sasa ni wastani wa kilo **12** za nyama, lita **45** za maziwa na mayai **75** kwa mtu kwa mwaka.

### *Hali ya Sekta ya Uvuvi*

**8.** **Mheshimiwa Spika,** shughuli za uvuvi hufanyika katika maeneo ya maji chumvi na maji baridi. Nchi yetu ina ukanda wa pwani wa bahari wenye urefu wa kilometa **1,424** ambao umegawanyika katika eneo la Maji ya Kitaifa (Territorial Sea) lenye ukubwa wa kilometa za mraba **64,000** na eneo la Bahari Kuu lenye ukubwa wa kilometa za mraba **223,000**. Eneo la maji baridi linajumuisha maziwa makuu matatu ambayo ni; Ziwa Victoria (kilometa za mraba **35,088**), Ziwa Tanganyika (kilometa za mraba **13,489**) na Ziwa Nyasa (kilometa za mraba **5,700**), maziwa ya kati na madogo **29**, mito na maeneo oevu.

**9.** **Mheshimiwa Spika,** sekta ya uvuvi huchangia katika upatikanaji wa lishe bora, ajira, kipato kwa wananchi, pato la Taifa na hivyo kuchangia katika kuondoa umaskini. Sekta hii imekua kwa asilimia **2.2** mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia **2.9** mwaka 2012. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kumechangiwa na kupungua kwa mauzo ya samaki na mazao yake nje ya nchi. Aidha, mchango wa sekta hii kwa pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia **1.4** kwa mwaka 2013. Vilevile, katika mwaka 2013/2014, idadi ya wavuvi wadogo imeongezeka kufikia **183,341** ikilinganishwa na wavuvi **182,741** mwaka 2012/2013 na zaidi ya wananchi **milioni 4.0** wameendelea kutegemea shughuli za uvuvi ikiwemo biashara ya samaki, uchakataji wa mazao ya uvuvi, utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi na biashara nyingine katika kujipatia kipato.

***Changamoto***

**10. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 sekta za mifugo na uvuvi zimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kutopata fedha za kutosha na kwa wakati ili kutekeleza majukumu yaliyoainishwa kwenye mpango kazi.

(ii) Uwekezaji mdogo katika sekta za mifugo na uvuvi hasa katika usindikaji wa mazao ya mifugo na uvuvi na katika Bahari Kuu kunaathiri mchango wa sekta katika pato la Taifa;

(iii) Kasi ndogo katika kumilikisha maeneo ya ufugaji kunachangia kuhamahama kwa mifugo na kusababisha migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, uharibifu wa mazingira na ueneaji wa magonjwa ya mifugo;

(iv) Kuenea kwa magonjwa ya mifugo, hususan ya milipuko, yasiyo na mipaka na yaenezwayo na kupe na mbung'o;

(v) Kutopatikana kwa mikopo ya kutosha na yenye masharti nafuu kwa wafugaji na wavuvi;

(vi) Kupanda kwa gharama za pembejeo na zana kwa ajili ya ufugaji na uvuvi;

(vii) Uhaba wa Maafisa ugani wa mifugo na uvuvi ikilinganishwa na mahitaji;

(viii) Upungufu wa mbegu bora za mifugo na samaki, pembejeo na huduma hafifu ya uhimilishaji;

(ix) Ukosefu wa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi hususan maeneo ya vijijini;

(x) Ushiriki mdogo wa wadau katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi; na

(xi) Elimu duni ya ufugaji bora, ufugaji usio wa kibiashara na matumizi duni ya teknolojia za kisasa kwa wafugaji na wavuvi.

**11. Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na changamoto hizi, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

(i) Wizara kuendelea kuhimiza Serikali kutenga fedha za kutosha ili kuweza kukidhi mahitaji ya sekta.

(ii) Kuhamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika sekta za mifugo na uvuvi kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji. Aidha, vijitabu vyenye kuonyesha fursa za uwekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi vimeandaliwa na kusambazwa kwa wadau na kutangazwa kwenye tovuti ya Wizara na kupitia ofisi za Ubalozi.

(iii) Kushirikiana na Mamlaka husika kuhimiza uainishaji, upimaji, umilikishaji na uendelezaji wa maeneo ya ufugaji ili yawe endelevu kwa lengo la kudhibiti uhamaji holela wa mifugo ili kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na hivyo kupunguza uharibifu wa mazingira na kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo. Aidha, Serikali imeanza kupima upya baadhi ya ranchi zake kwa lengo la kupunguza migogoro kati ya ranchi na wafugaji.

(iv) Kuimarisha huduma za afya ya mifugo kwa kudhibiti magonjwa ya mifugo hususan ya milipuko ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa ruzuku ya madawa ya kuogeshea mifugo na chanjo. Aidha, Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) unaendelea kuimarishwa kwa ajili ya kuboresha huduma za kimaabara ikiwemo uzalishaji wa chanjo za mifugo.

(v) Kuhamasisha taasisi za fedha kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa ufugaji na uvuvi. Aidha, kuhamasisha wafugaji na wavuvi kuunda vyama vya ushirika vya akiba na mikopo ili kuwawezesha kupata pembejeo na zana kwa ajili ya ufugaji na uvuvi.

(vi) Kuendelea kuimarisha Wakala za Mafunzo ya Mifugo na Elimu na Mafunzo ya Uvuvi ili kuongeza udahili kutoka **1,720** hadi **2,500** (mifugo) na **1,150** hadi **1,500** (uvuvi) kuimarisha huduma za mafunzo na kuongeza idadi ya maafisa ugani wa mifugo na uvuvi katika Halmashauri nchini. Aidha, kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika mafunzo ya mifugo na uvuvi. Hadi sasa kuna vyuo vya mifugo vitatu vya mifugo Visele (Mpwapwa), Kaole (Bagamoyo) na SUA ambavyo vimedahili wanafunzi 375. Vilevile Wizara kuendelea kushawishi Serikali kuendelea kuajiri wataalam mbalimbali wa mifugo na uvuvi ili kukidhi mahitaji ya huduma za ugani.

(vii) Kuanzisha na kuimarisha vituo vya kuzalisha mbegu na pembejeo bora za mifugo na samaki pamoja na kuimarisha huduma ya uhimilishaji (artificial insemination); ufugaji wa samaki na ukuzaji wa viumbe wengine kwenye maji (aquaculture).

(viii) Kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi kuimarisha na kujenga miundombinu muhimu ya mifugo na uvuvi ikiwemo minada, masoko na mialo na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao mifugo na uvuvi.

(ix) Kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya uvuvi kwa kuhimiza na kuimarisha ushirikishwaji wa jamii na wadau wengine katika ulinzi, usimamizi na matumizi endelevu ya raslimali za uvuvi. Aidha, vituo vya doria, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu (DSFA) na vikundi vya kusimamia rasilimali za uvuvi (BMUs) vinaimarishwa. Vilevile, Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kitaimarishwa ili kiweze kuanzisha na kuendeleza maeneo tengefu kwenye maziwa makuu hususan Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa.

(x) Kuhimiza wafugaji na wavuvi kutumia kanuni bora za ufugaji na uvuvi kwa kutoa mafunzo kupitia vyombo vya habari, semina, shamba darasa, machapisho, na mafunzo mbalimbali. Aidha, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) zinaimarishwa ili kuendeleza huduma za utafiti wa mifugo na uvuvi ikiwa ni pamoja na kukarabati miundombinu, kuwajengea uwezo watafiti na kuwapatia vitendea kazi muhimu.

### *3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2013/2014 NA MWELEKEO WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015*

#### *3.1 UKUSANYAJI WA MAPATO*

**12.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi **19,317,830,050.00.** Kati ya hizo, shilingi **8,981,727,050.00 (46.5%)** ni kutoka Sekta ya Mifugo

na shilingi **10,336,103,000.00 (53.5%)** ni kutoka Sekta ya Uvuvi. Hadi kufikia 30 Aprili, 2014, kiasi cha shilingi **13,265,344,132.96** kimekusanywa na Wizara ikiwa ni sawa na asilimia **68** ya lengo la makusanyo. Kati ya hizo, shilingi **5,093,839,662.00** zimekusanywa kutoka sekta ya mifugo (asilimia **56.7** ya lengo) na shilingi **8,171,504,470.96** zimekusanywa kutoka sekta ya uvuvi (asilimia **79** ya lengo). Katika mwaka 2014/2015, Wizara inatarajia kukusanya shilingi **32,889,362,437.00**. Kati ya hizo, shilingi **24,401,371,000.00** zitakusanywa na Wizara na shilingi **8,487,991,437.00** zitakusanywa na Taasisi, Wakala na Bodi zilizo chini ya Wizara ambazo zitatumiwa na Taasisi, Wakala na Bodi hizo kutekeleza majukumu yake.

### *3.2 MATUMIZI YA FEDHA*

**13. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi **67,180,225,000.00** ikihusisha shilingi **bilioni 20** zilizoongezwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya kiasi hiki, shilingi **38,206,909,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **28,973,316,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi **21,867,642,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC) na shilingi **16,339,267,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara. Vilevile, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo, shilingi **23,488,270,000.00** (**81.1%)** ni fedha za ndani na shilingi **5,485,046,000.00 (18.9%)** ni fedha za nje.

**14. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Aprili 2014, jumla ya shilingi **23,681,299,494.86** zimetolewa, sawa na asilimia **62** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi **16,021,023,638** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Wizara (PE) na shilingi **7,660,275,856.86** ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC). Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi **23,435,217,537.55** (asilimia **98.9**) zimetumika. Aidha, jumla ya shilingi **3,881,376,828.00** (asilimia **13.4**) zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo jumla ya shilingi **2,555,975,110.25** (asilimia **65.9**) zimetumika. Kati ya fedha za maendeleo zilizotolewa, shilingi **2,229,376,828.00** ni fedha za ndani na shilingi **1,652,000,000** ni fedha za nje.

### *3.3 UBUNIFU NA UTEKELEZAJI WA SERA NA SHERIA ZA SEKTA*

**15. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu, kupitia na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mikakati na programu mbalimbali za kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Katika mwaka 2013/2014, Wizara imesambaza nakala **500** za Sera ya Taifa ya Mifugo na nakala **200** za Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake ya mwaka 1997 na kutoa elimu ya sera hizo kwa wadau mbalimbali hapa nchini. Aidha, imesambaza nakala **200** za Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo Nchini (LSDS), nakala **300** za Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo Nchini, nakala **150** za Programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi Nchini na nakala **400** za Fursa za Uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo imeendelea kushiriki katika maandalizi ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini Awamu ya Pili (ASDP II) na Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDS II).

**16. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, sera na sheria za sekta za mifugo na uvuvi zimeendelea kupitiwa na Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuboresha mazingira ya kibiashara. Kazi zilizofanyika ni pamoja na:-

(i) Kuandaa na kujadiliwa mapendekezo ya Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2014 na mikakati yake katika ngazi ya Makatibu Wakuu;

(ii) Kuandaa na kujadiliwa mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania ya mwaka 2014 katika ngazi ya Makatibu Wakuu;

(iii) Kuandaa na kujadiliwa mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu ya mwaka 2014 katika ngazi ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;

(iv) Kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri wa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Mbari Bora za Wanyama (Animal Breeding Act);

(v) Kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (The Deep Sea Fishing Authority Act) SURA 388 kwa ajili ya kupata maoni ya wadau;

(vi) Kuainisha maeneo yanayohitaji marekebisho katika Sheria ya Uvuvi (The Fisheries Act) SURA 279 kwa ajili ya kujadiliwa na wadau;

(vii) Kuandaa Waraka wa Taarifa ya Utekelezaji wa Maamuzi ya Baraza la Mawaziri Na. 2/2002 kuhusu Mapendekezo ya Mkataba wa Ubinafsishaji wa Mashamba ya Mifugo na Ranchi za Taifa na kujadiliwa katika ngazi ya Sekretariati ya Baraza la Mawaziri.

(viii) Kuandaa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali notisi za uteuzi wa Wakaguzi wa Mifugo na mazao yake chini ya Sheria ya Magonjwa ya Wanyama SURA 156 na Sheria ya Veterinari SURA 319 na kupatiwa Namba zifuatazo:

- Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Notisi ya (Ukaguzi) Tangazo la Serikali Na. 390/2013;
- Sheria ya Veterinari, Notisi ya (Uteuzi wa Wakaguzi wa Veterinari) Tangazo la Serikali Na. 386/2013;
- Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Notisi ya (Uteuzi wa Wakaguzi wa Mifugo na mazao yake) Tangazo la Serikali Na. 387/2013; na
- Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Notisi ya (Madaktari wa Mifugo wa Wilaya) Tangazo la Serikali Na. 389/ 2013.

(ix) Kutafsiri katika lugha ya Kiswahili Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 toleo la Tangazo la Serikali Na. 308 la mwaka 2009 na kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili aweze kuzipitia kabla ya kuchapishwa.

Aidha, marekebisho ya Kanuni zifuatazo yameandaliwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali:-

(i) Kanuni za Magonjwa ya Wanyama (Udhibiti wa Usafirishaji wa Wanyama na Mazao yatokanayo na Wanyama ya 2013) The Animal Diseases (Animal and Animal Products

Movements Control) (Amendment) Regulations, 2013, Tangazo la Serikali Na. 225 la mwaka 2013;

(ii) Kanuni za Biashara ya Ngozi "The Hides, Skins and Leather (Trading in Hides, Skins and Leather) (Amendment) Regulations, 2014" Tangazo la Serikali Na. 46 la mwaka 2014; na

(iii) Kanuni za Veterinari (Viwango vya Mafunzo vya Usajili, Uorodheshaji na Uandikishaji) "The Veterinary (Training Standards for Registration, Enrolment and Enlistment) (Amendment) Regulations, 2014, Tangazo la Serikali Na. 45 la mwaka 2014.

**17. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu sera, sheria na kanuni za sekta za mifugo na uvuvi ili zizingatie mfumo wa ugatuaji madaraka (D by D). Pia, itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake (1997) na Mkakati wa utekelezaji. Aidha, Wizara itakamilisha mapendekezo ya Sheria za Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Sura 146 na Sheria ya Mbari Bora za Wanyama (Animal Breeding Act).

### *3.4 UENDELEZAJI WA SEKTA YA MIFUGO*

#### *Uzalishaji na Biashara ya Mifugo na Mazao yake Zao la Maziwa*

**18. Mheshimiwa Spika,** tasnia ya maziwa imeendelea kukua kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji, ukusanyaji na usindikaji wa maziwa. Uzalishaji wa maziwa umeongezeka na kufikia lita **bilioni 2.0** mwaka 2013/2014 ikilinganishwa na lita **bilioni 1.9** kwa mwaka 2012/2013 **(Jedwali Na.1)** sawa na ongezeko la asilimia **3.5.** Aidha, usindikaji wa maziwa kwa siku umeongezeka kutoka lita **135,300** mwaka 2012/2013 hadi lita **139,800** mwaka 2013/2014 sawa na ongezeko la asilimia **3.2** (**Jedwali Na.2**). Ongezeko hilo limetokana na kuanzishwa kwa viwanda vipya vya kusindika maziwa vikiwemo vya Milk com (Dar es Salaam), Prince Food Technologies na Grand Denam (Arusha) na kufanya idadi ya viwanda vya kusindika maziwa nchini kuwa **74**.

Katika juhudi za kuhamasisha ukusanyaji na usindikaji wa maziwa nchini, Wizara imevipatia Vyama vya Wafugaji Njombe (NJOLIFA) na Siha (kijiji cha Kishisha) matenki ya kupoza maziwa ambapo uzinduzi rasmi ulifanyika katika kijiji cha Wangama – Njombe.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuimarisha ukusanyaji na usindikaji wa maziwa ili kuongeza usindikaji kufikia lita **165,000** kwa siku.

**19. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 jumla ya mitamba **681** ilizalishwa katika mashamba ya Wizara na kusambazwa kwa wafugaji mbalimbali nchini. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha mashamba ya kuzalisha mifugo ili kuongeza upatikanaji wa mitamba kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kununua ng'ombe wazazi **67** kwa ajili ya mashamba ya Ngerengere (**25**), Sao Hill (**25**) na Mabuki (**17**);

(ii) Kuunganisha umeme katika nyumba za wafanyakazi na ofisi za shamba la Nangaramo;

(iii) Kutengeneza makinga moto kilometa **28** kwenye maeneo ya malisho katika mashamba ya Mabuki **(10),** Sao Hill **(5),** Nangaramo **(5)** na Ngerengere **(8)**;

(iv) Kukarabati barabara kilomita **12** kwenye mashamba ya Mabuki **(10)** na Ngerengere (**2**);

(v) Kufyeka vichaka hekta **60** katika mashamba ya Mabuki (**50**) na Nangaramo (**10**); na

(vi) Kuendeleza malisho hekta **42** katika mashamba ya Mabuki (**23**), Sao Hill (**8**), Kitulo (**7**) na Ngerengere (**4**).

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kusimamia, kuboresha mashamba na kuzalisha mitamba kwa kutumia teknolojia ya uhimilishaji na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mitamba bora. Aidha, katika kuimarisha mashamba, Wizara itafanya yafuatayo:-

(i) Kununua ng'ombe wazazi **300** kwa ajili ya mashamba ya Mabuki (**150**), Nangaramo (**100**) na Ngerengere (**50**);

(ii) Kununua trekta moja kwa ajili ya shamba la Mabuki na magari mawili (**2**) kwa ajili ya Mabuki na Nangaramo;

(iii) Kukarabati nyumba za watumishi wa shamba la Kitulo; na

(iv) Kuweka makinga moto na uzio kwenye maeneo ya malisho katika mashamba yote ya kuzalisha mitamba.

**20.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji kama njia yenye tija ya kuzalisha mifugo bora. Katika mwaka 2013/2014, Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji – NAIC Usa River kimeimarishwa kwa kupatiwa vifaa vya maabara ili kuongeza ubora wa mbegu. Aidha, Vituo vitano **(5)** vya Kanda vya Uhimilishaji vya Kibaha (Pwani), Dodoma, Lindi, ZVC Mwanza na Uyole (Mbeya) vimeimarishwa kwa kukarabati mitambo na kupatiwa vitendea kazi. Vilevile, katika juhudi ya kuendeleza teknolojia ya uhimilishaji yafuatayo yamefanyika:-

(i) Jumla ya dozi **58,210** za mbegu bora zimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji;

(ii) Jumla ya ng'ombe **90,300** wamehimilishwa yakiwemo maeneo ya mifugo ya asili ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wataalam **136** wa uhimilishaji kutoka kwenye maeneo mbalimbali nchini;

(iv) Kuendelea na ujenzi wa Kituo kipya cha Uhimilishaji cha Sao Hill na kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Uhimilishaji cha Kanda cha Katavi, ambapo mitambo ya kutengeneza kimiminika cha naitrojeni imesimikwa katika vituo hivyo;

(v) Kutumia huduma ya uhimilishaji katika Mashamba ya Kuzalisha Mifugo, ambapo jumla ya ng'ombe **440** walihimilishwa; Mabuki **(97),** SaoHill **(52),** Kitulo **(183**) na Ngerengere (**108);** na

(vi) Kuendeleza teknolojia ya uhawilishaji kiinitete (*embryo transfer*) kwa kujenga maabara TALIRI-Mpwapwa.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha uhimilishaji nchini kwa kuzalisha dozi **190,000** za mbegu, kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha Sao Hill, kuimarisha Kituo cha Uhimilishaji cha Taifa NAIC – Usa River na Vituo sita **(6)** vya Kanda vya Uhimilishaji. Aidha, Wizara itaendeleza teknolojia ya uhawilishaji kiinitete kwa kukamilisha ujenzi wa maabara ya TALIRI-Mpwapwa na kuitumia teknolojia hiyo katika mashamba ya mifugo ya Mzeri, Mpwapwa, Mivumoni na Sao Hill.

**Nyama - Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo, Nguruwe na Kuku**

**21. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, uzalishaji wa nyama umeongezeka kutoka tani **553,455** mwaka 2012/2013 hadi tani **563,086** (ng'ombe tani **309,353,** mbuzi na kondoo tani **120,199** nguruwe tani **79,174** na kuku tani **54,360**) mwaka 2012/2013 **(Jedwali Na. 1)**. Aidha, wadau wameendelea kuhamasishwa kutumia mfumo wa unenepeshaji mifugo ambapo ng'ombe walionenepeshwa wameongezeka kwa asilimia **11** kutoka ng'ombe **155,206** mwaka 2012/2013 hadi ng'ombe **175,000** mwaka 2013/2014 katika mikoa ya Kanda ya Ziwa **115,300**; Kati **22,270**; Kaskazini **27,430**; Nyanda za Juu Kusini **1,500** na NARCO **8,500 (Jedwali Na. 3).** Aidha, nakala **500** za Mwongozo wa Unenepesheji zimesambazwa kwa wadau mbalimbali. Katika juhudi za kusaidia upatikanaji wa soko la mifugo iliyonenepeshwa, Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ili kuvutia wawekezaji kuwekeza katika ujenzi na ukarabati wa machinjio za kisasa na viwanda vya kusindika nyama, ambapo katika mwaka 2013/2014 yafuatayo yamefanyika:-

(i) Manispaa ya Iringa kwa kushirikiana na UNIDO inajenga machinjio yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe **200** na mbuzi/kondoo **200** kwa siku;

(ii) Kampuni ya Chobo inajenga machinjio katika Jiji la Mwanza itakayokuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **160** na mbuzi/kondoo **400** kwa siku;

(iii) Kampuni ya Triple S inaendelea kukarabati Kiwanda cha Kusindika Nyama cha Shinyanga kitakachokuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **500** kwa siku;

(iv) Machinjio ya Dodoma imeboreshwa kwa kuongeza sehemu ya kukata nyama ili kuongeza thamani ambapo imeweza kufikia uwezo wa kuchinja ng'ombe **450** badala ya **200** na Mbuzi/Kondoo **200** kwa siku; na

(v) Machinjio nyingine zilizokamilika hivi karibuni na zinafanya kazi ni machinjio ya Kampuni ya Tandan iliyopo Mkuranga yenye uwezo wa kuchinja na kusindika nguruwe **200** kwa siku; Machinjio ya Kampuni ya Kiliagro iliyopo Jijini Arusha yenye uwezo wa kuchinja na kusindika kuku **4,000** kwa siku; Machinjio ya Kampuni ya Mtanga Foods Ltd iliyopo katika Halmashauri ya Kilolo yenye uwezo wa kuchinja na kusindika ng'ombe **80** kwa siku; kiwanda/machinjio ya Kampuni ya Alpha Choice iliyopo Magu yenye uwezo wa kuchinja na kusindika ng'ombe **80** na Machinjio ya Aman (Endanahai) iliyoko Babati yenye uwezo wa kuchinja na kusindika kuku **4,000** kwa siku.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuhamasisha uzalishaji, usindikaji wa nyama, kuweka mazingira mazuri ili sekta binafsi iwekeze zaidi na kuhimiza matumizi ya sheria na kanuni ili kuinua viwango vya nyama na bidhaa zitokanazo na nyama. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha unenepeshaji ili kufikia idadi ya ng'ombe **200,000** kwa mwaka.

**22. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya masoko ya mifugo kwa lengo la kukuza biashara ya mifugo katika minada ya upili na ya mipakani. Katika mwaka wa 2013/2014, Wizara imeimarisha minada ya Pugu (Dar es Salaam), Lumecha (Songea), Meserani (Arusha) na Nyamatala (Misungwi). Aidha, mnada wa upili wa Nyamatala umezinduliwa rasmi tarehe 8 Aprili, 2014. Minada ya Kirumi (Butiama) na Longido inaendelea kujengwa. Vilevile, wafanyabiashara **340** walipatiwa mafunzo kuhusu biashara, matumizi ya mizani na umuhimu wa kulipa mapato ya Serikali kwenye minada ya upili na ya mipakani.
Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea na ujenzi wa minada miwili (**2)** ya Longido na Kirumi na kukarabati minada sita **(6**) ya Pugu, Weruweru, Sekenke, Kizota, Meserani na Igunga. Aidha, Serikali itaendelea kuratibu uuzaji wa mifugo katika minada na kuhamasisha matumizi ya mizani ya kupimia uzito wa mifugo.

**23. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya ng'ombe **1,215,541** mbuzi **960,199** na kondoo **209,292** wenye thamani ya shilingi **bilioni 989.3** waliuzwa minadani. Hata hivyo, idadi ya mifugo iliyouzwa nje ya nchi imepungua kutoka ng'ombe **1,705**, mbuzi na kondoo **1,003** wenye thamani ya shilingi **bilioni 2.16** mwaka 2012/2013 hadi ng'ombe **1,123** na mbuzi **517** wenye thamani ya shilingi **bilioni 1.78** mwaka 2013/2014. Aidha, jumla ya **tani 2.8** za nyama ya ng'ombe, tani **1,048.85** za nyama ya mbuzi na tani **58.97** za nyama ya kondoo zenye thamani ya shilingi **bilioni 36.17** mwaka 2013/2014 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na mauzo ya nyama ya ng'ombe tani **126,** mbuzi tani **667.8** na kondoo tani **88.4** zenye thamani ya shilingi **bilioni 28.8** mwaka 2012/2013.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika ujenzi wa viwanda na biashara ya mifugo na mazao yake ili kuongeza mauzo ya nyama ndani na nje ya nchi.

**Uzalishaji wa Nyama katika Kampuni ya Ranchi za Taifa (National Ranching Company - NARCO)**

**24. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imeendelea kuzalisha, kunenepesha, kuuza mifugo kwa ajili ya nyama na kuendesha machinjio ya Dodoma kwa ubia na Kampuni ya NICOL. Aidha, Kampuni imeendelea kutoa huduma za ushauri kwa wafugaji wanaozunguka ranchi **10** za mfano za Kagoma, Kalambo, Kikulula, Kongwa, Mabale, Missenyi, Mkata, Mzeri, Ruvu na West Kilimanjaro. NARCO ina jumla ya hekta **230,384** zenye uwezo wa kuweka ng'ombe kati ya **80,000** na **90,000**. Kwa sasa Kampuni ina jumla ya ng'ombe **14,618**, kondoo na mbuzi **1,520**, farasi **41** na punda **43.**

Katika mwaka wa 2013/2014, NARCO imefanya yafuatayo:-

(i) Kuzalisha ndama **4,372** kutokana na ng'ombe wazazi **6,428**;

(ii) Kunenepesha ng'ombe **3,000** kutoka kwa wafugaji na kuuza ng'ombe **5,600** wenye thamani ya shilingi **bilioni 3.1**;

(iii) Kutoa hati miliki ndogo (sub-lease) kwa vitalu **13** katika Ranchi ya Kalambo na kufikisha idadi ya hati miliki ndogo **96** kati ya **105** zinazotakiwa kutolewa;

(iv) Kutoa ushauri na mafunzo ya kusimamia ufugaji wa kisasa kwa wawekezaji watanzania **50** ambao wamemilikishwa vitalu ndani ya Ranchi za Taifa pamoja na wafugaji

wanaozunguka ranchi hizo. Vitalu hivyo vimewekeza ng'ombe **36,820**, mbuzi na kondoo **8,612**; na

(v) Kumpata Mshauri Mwelekezi ili ashauri jinsi ya kuendeleza ujenzi wa machinjio ya Ruvu. Aidha, taratibu za kumpata mkandarasi wa kuendeleza ujenzi wa machinjio hiyo zinaendelea baada ya mkataba wa awali kuvunjwa.

Katika mwaka 2014/2015, NARCO itaendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Ruvu na kununua ng'ombe wazazi **1,200** ili kuongeza idadi ya ng'ombe katika ranchi zake. Aidha, jumla ya ndama **4,050** wanategemea kuzaliwa kutokana na ng'ombe wazazi **5,786**. Pia, Kampuni itaendelea na jitihada za kuongeza uzalishaji kwa kutafuta mitaji mipya na kuvutia wawekezaji kwa ubia katika ranchi zake.

**Kuku**

**25.** **Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji wa kuku na mayai nchini. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya vifaranga **milioni 61** vya kuku wa nyama na mayai vilizalishwa nchini ikilinganishwa na vifaranga **milioni 52** mwaka 2012/2013. Pia, mayai **348,000** ya kuku wazazi na mayai **6,240,000** ya kutotolesha vifaranga yaliingizwa nchini. Vilevile, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka **bilioni 3.7** mwaka 2012/2013 hadi mayai **bilioni 3.9** mwaka 2013/2014. Aidha, Wizara imeshirikiana na Kampuni ya Black Mark kufanya maonesho ya tasnia ya kuku katika ukumbi wa Mlimani City mwezi Oktoba, 2013 yaliyoshirikisha pia kampuni tano **(5)** kutoka nchi za Mauritius, Malawi, Misri, Zambia na Ufaransa. Vilevile, Wizara imefanya mkutano wa wadau wa tasnia ya kuku kujadili hali ya tasnia ikiwa ni pamoja na namna ya kutumia fursa zilizopo na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika ufugaji wa kuku kibiashara na kushirikiana na wadau kuandaa maonesho yatakayowezesha wadau kuzalisha mazao bora.

**Nguruwe**

**26.** **Mheshimiwa Spika,** ufugaji wa nguruwe nchini umeendelea kukua kutokana na kuongezeka kwa mahitaji. Katika mwaka 2013/2014, uzalishaji wa nyama ya nguruwe umeongezeka kwa asilimia **35** kutoka tani **50,814** mwaka 2012/2013 hadi tani **79,174** mwaka 2013/2014. Ili kuimarisha ufugaji wa nguruwe nchini, Wizara imenunua nguruwe wa mbegu **24** (majike **20** na madume **4)** mbari ya *Large White* na *Duroc* na kuwapeleka katika shamba la Ngerengere ili kuwazalisha na kusambaza mbegu bora kwa wafugaji.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha uzalishaji wa nguruwe nchini kwa kuendeleza shamba la Ngerengere kwa kuongeza nguruwe wazazi. Aidha, Wizara itashirikiana na Halmashauri kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ufugaji wa nguruwe wa kisasa.

**Ngozi**

**27.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, ngozi zilizosindikwa na kuuzwa nje ya nchi ziliongezeka kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe **969,060** vyenye thamani ya shilingi **bilioni**

**32.3** na vipande vya ngozi za mbuzi na kondoo **2,582,525** vyenye thamani ya shilingi **bilioni 18.6** katika mwaka 2012/2013 hadi kufikia vipande vya ngozi za ng'ombe **1,060,777** vyenye thamani ya shilingi **bilioni 39.4** na vipande vya ngozi za mbuzi na kondoo **2,715,436** vyenye thamani ya shilingi **bilioni 19.6** katika mwaka 2013/2014, sawa na ongezeko la asilimia **16**. Aidha, vipande vya ngozi za ng'ombe **250,000** vyenye thamani ya shilingi **bilioni 12.5** vilisindikwa hadi hatua ya mwisho na kutumika kutengeneza bidhaa za ngozi hapa nchini ikilinganishwa na vipande vya ngozi za ng'ombe **212,000** vyenye thamani ya shilingi **bilioni 15.0** katika mwaka 2012/2013.

**28. Mheshimiwa Spika,** kuongezeka kwa ushuru wa ngozi ghafi zinazouzwa nje ya nchi wa asilimia **90** au shilingi **900** kwa kilo kutegemea ipi ni kubwa kumehamasisha uwekezaji katika usindikaji. Kwa mfano, kiwanda kipya cha ngozi cha Xinghua Investment cha Shinyanga chenye uwezo wa kusindika ngozi za ng'ombe **900,000** na vipande vya ngozi za mbuzi na kondoo **milioni 2.1** kwa mwaka kimekamilika kujengwa na kuanza kazi mwezi Machi, 2014. Kiwanda kipya cha Meru (Arusha) chenye uwezo wa kusindika ngozi za ng'ombe **624,000** na vipande vya ngozi za mbuzi na kondoo **milioni 1.5** kwa mwaka kitaanza kazi katika mwezi Julai, 2014. Viwanda hivi vitaongeza uwezo wa usindikaji wa ngozi nchini na hivyo kuondoa kilio cha wazalishaji wa ngozi kukosa soko la uhakika la ngozi zao.

**29. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara ya Viwanda na Biashara, Halmashauri **75** na Chama cha Wadau wa Ngozi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (Livestock Development Fund) imefanya yafuatayo:-

(i) Kuwajengea uwezo wataalam **40** wa Halmashauri ambazo haziko kwenye mpango wa kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta ya Viwanda vya Ngozi;

(ii) Kuwezesha uimarishaji wa Chama cha Wazalishaji wa Ngozi cha Kitaifa;

(iii) Kuwezesha Mkutano wa wadau wa tasnia ya ngozi ili kuainisha fursa na changamoto na kuweka mikakati ya pamoja ya kuendeleza tasnia hii;

(iv) Kuwezesha vikao vya kisheria vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ngozi na Kamati ya Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo; na

(v) Kukamilishwa taratibu za uanzishwaji wa Chama cha Wazalishaji wa Ngozi nchini ambacho kitasimamia maslahi ya wazalishaji wa ngozi wakiwemo wafugaji, wachinjaji na wakusanyaji wa ngozi katika Halmashauri zote nchini.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi katika Halmashauri **75** kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuhamasisha matumizi ya mfumo wa ufuatiliaji wa uzalishaji na biashara ya ngozi toka machinjioni hadi viwandani ili kuzuia utoroshwaji wa ngozi nje ya nchi;

(ii) Kuwezesha uendeshaji wa vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ngozi na Kamati ya Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo ili kutekeleza majukumu yake;

(iii) Kuwajengea uwezo wataalam **130** wa Halmashauri **65** zisizotekeleza Mkakati wa Kufufua na kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi nchini kuhusu uzalishaji, uhifadhi na usindikaji wa ngozi unaozingatia hifadhi ya mazingira; na

(iv) Kuwezesha mikutano mitatu **(3**) ya wadau itakayojadili maendeleo ya tasnia ya ngozi nchini.

**Matumizi ya Rasilimali za Ardhi, Maji na Malisho kwa Mifugo na Utatuzi wa Migogoro**

**30. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuhimiza Halmashauri kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi na kutenga maeneo ya ufugaji, kwa ajili ya kuendeleza malisho ya mifugo katika Halmashauri zote nchini. Aidha, upatikanaji wa maeneo ya malisho utaepusha migogoro ya mara kwa mara kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Hadi sasa, vijiji **589** katika wilaya **80** ndani ya mikoa **22** iliyopimwa na kutenga maeneo kwa ajili ya ufugaji na kufikia jumla ya hekta **milioni 1.51** (**Jedwali Na. 4**)

Katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri itaainisha na kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya maendeleo endelevu ya rasilimali za mifugo katika Wilaya tisa (**9)** za Busega, Kiteto, Kilosa, Ngorogoro, Mvomero, Kilindi, Igunga, Iramba na Lindi.

**31. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mbegu za malisho ya Vikuge (Kibaha), Sao Hill (Mufindi), Langwira (Mbeya), Mabuki (Misungwi) na Kizota (Dodoma) kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kununua vitendea kazi na pembejeo vikiwemo reki ya trekta, tela, mowa, mifuko **10** ya mbolea na kilo **100** za mbegu za malisho kwa ajili ya shamba la Vikuge;

(ii) Kununua trekta moja (**1)** na vifaa vyake, mbolea mifuko **5** na mbegu kilo **50** na kukarabati ofisi na miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Langwira;

(iii) Kufyeka vichaka hekta **50** katika shamba la mifugo la Mabuki; na

(iv) Kuendeleza malisho hekta **31** katika mashamba ya Mabuki (**23**) na Sao Hill (**8)**.

Aidha, mashamba hayo kwa pamoja yameweza kuzalisha mbegu za malisho tani **48.2** na marobota ya hei **497,620** (**Jedwali Na. 5).** Pia, sekta binafsi imezalisha marobota **425,000** ya hei. Vilevile, Wizara imeendelea kusimamia uzalishaji na usindikaji wa vyakula bora vya mifugo nchini katika viwanda **80** ambapo tani **915,000** zimezalishwa na kuuzwa.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora za malisho kwa kuyapatia vitendea kazi na kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa malisho na mbegu bora za malisho. Vilevile, Wizara itakamilisha uteuzi wa wakaguzi wa vyakula vya mifugo watakaosimamia viwango vya ubora.

**32. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kusimamia ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mifugo kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) inayotekelezwa na Halmashauri mbalimbali hapa nchini. Aidha, katika mwaka 2013/2014 malambo mapya **15** yamejengwa na malambo **4** yamekarabatiwa **(Jedwali Na. 6).**

Katika mwaka 2014/2015, Serikali itawezesha uchimbaji wa kisima kirefu cha maji ya mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Same, kujenga malambo na majosho katika Wilaya saba **(7)** za Chemba, Handeni, Kiteto, Kilwa, Chunya, Kilindi na Ngorongoro .

**Utoaji wa Kifuta Machozi kwa Wafugaji**

**33. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa zoezi la kutoa kifuta machozi kwa wafugaji waliopoteza mifugo yao yote katika wilaya za Longido (kaya **2,852**), Monduli (kaya **1,484**) na Ngorongoro (kaya **1,791)** kutokana na ukame uliotokea mwaka 2008/2009 umeendelea kutekelezwa. Hadi sasa ng'ombe **17,214** (mitamba **17,202** na madume bora **12**), mbuzi, **6,190** wenye thamani ya shilingi bilioni **7.4** waligawiwa kwa wafugaji sawa na asilimia 70 ya malengo.

### *3.5 UDHIBITI WA MAGONJWA YA MIFUGO*

**Maeneo Huru ya Magonjwa ya Mifugo**

**34. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo cha Kanda ya Kusini Magharibi kilichopo mjini Sumbawanga kwa kukipatia vitendea kazi ikiwa ni pamoja na gari **1** na kutoa mafunzo kwa wataalam **4** watakaoshughulikia udhibiti wa magonjwa katika maeneo huru ya magonjwa ya mifugo.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha Eneo huru la Magonjwa ya Mifugo kwa kukarabati jengo la ofisi za Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo cha Kanda ya Kusini Magharibi, kuwajengea uwezo wataalam na kukipatia vitendea kazi kituo cha Sumbawanga.

**Magonjwa ya Mlipuko**

**35. Mheshimiwa Spika***,* katika mwaka 2013/2014, Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia kampeni za chanjo ya ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo katika mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro na Kagera ambapo jumla ya mbuzi na kondoo **1,163,451** walichanjwa dhidi ya ugonjwa huo.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itanunua dozi **1,000,000** za chanjo ya Sotoka ya Mbuzi na Kondoo na kuzisambaza katika mikoa ya Arusha, Tanga, Mara na Tabora yenye hatari ya kuwa na mlipuko wa ugonjwa.

**36. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia mradi ambao umemalizika wa SADC-TADs ilikamilisha taratibu za ununuzi wa Biological safety cabinets **8** zenye thamani ya **USD 101,000** na vifaa vya maabara vyenye thamani ya **USD 416,572.15** vilinunuliwa kwa ajili ya Maabara Kuu ya Mifugo. Aidha, mradi uliwezesha uchukuaji wa sampuli kwa ajili ya utafiti wa Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD) kwenye nyati na ng'ombe katika mapori ya akiba ya Selous, Moyowosi na Kigosi ambapo jumla ya sampuli **25** za nyati na **210** za ng'ombe zilichukuliwa na virusi vya FMD aina ya *O, SAT 1* na *SAT 2* vilibainika.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kutoa mafunzo ya wataalam, ununuzi wa vitendea kazi vya maabara na kufanya utambuzi wa aina ya chanjo itakayofaa kutoa kinga dhidi ya ugonjwa huo.

**37.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kufuatilia mwenendo wa Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege (HPAI-H5N1) hapa nchini na nje ya nchi. Ufuatiliaji huu umebaini kuwa ugonjwa huo haujaingia hapa nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kutoa tahadhari ili kuhakikisha kuwa virusi vya ugonjwa huo (HPAI-H5N1) pamoja na H7N9 haviingii hapa nchini.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huu. Aidha, Wizara itaendelea kushirikisha wadau wengine ikiwa ni pamoja na AU-IBAR kufuatilia mwenendo wa Ugonjwa ndani na nje ya nchi.

**38.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kufuatilia Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe nchini kwa kuchanja ng'ombe **290,000** katika mikoa ya Pwani (**5,000**), Kagera(**20,000**), Manyara (**180,000**) na Tanga (**85,000**)

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itanunua dozi **3,000,000** za chanjo kwa ajili ya kuendeleza uchanjaji katika mikoa yenye matukio ya ugonjwa ikiwemo mikoa ya Kagera, Geita na Shinyanga.

**Magonjwa yanayoenezwa na Wadudu (Kupe na Mbung'o)**

**(i) Udhibiti wa Kupe na Magonjwa Wayaenezayo**

**39.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau wengine kudhibiti kupe na magonjwa yanayoenezwa na kupe. Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza mpango wa ruzuku ya asilimia **40** kwa dawa za kuogesha mifugo ambapo lita **10,736** zenye kiini cha pareto zilinunuliwa kwa thamani ya shilingi **milioni 181.8** na kusambazwa katika mikoa **24**. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea kuhamasisha matumizi ya chanjo dhidi ya ugonjwa hatari wa Ndigana kali ambapo jumla ya ng'ombe **113,955** walichanjwa dhidi ya ugonjwa huo katika mikoa ya Arusha, Manyara, Tanga, Kilimanjaro, Dodoma, Tabora, Kagera na Pwani.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine kuhamasisha matumizi ya chanjo hii, ujenzi na ukarabati wa majosho pamoja na matumizi sahihi ya dawa za uogeshaji wa mifugo.

**(ii) Udhibiti wa Mbung'o na Nagana**

**40.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara ilishirikiana na wadau mbalimbali kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Mbung'o na Nagana. Aidha, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Baraza la Sayansi la Kimataifa la Utafiti na Udhibiti wa Ndorobo (ISCTRC) uliofanyika Khartoum Sudan na kuhudhuriwa na wajumbe **9** kutoka taasisi zinazotekeleza shughuli za udhibiti wa mbung'o na ndorobo. Katika mkutano huu, maandiko mawili ya Udhibiti wa Mbung'o na Nagana toka Tanzania yalipitishwa kwa ajili ya utekelezaji na taratibu za kupata mkopo kutoka *Arab Bank for Economic Development in Africa* -BADEA zinaendelea kukamilishwa.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Program ya Pan African Tsetse and Trypanosomiasis Eradication Campaign (PATTEC) itaendelea kudhibiti Mbung'o na Nagana kwa kutekeleza

miradi ya kuangamiza mbung'o kwa ajili ya mikoa ya Mara - Ikolojia ya Serengeti, Kigoma, Tabora, Rukwa na Katavi ambayo imepata kibali cha kupata fedha kiasi cha Dola za Kimarekani milioni **29** kutoka BADEA kwa kipindi cha miaka mitano (**5**).

**Magonjwa ya Mifugo yanayoambukiza Binadamu**

**Kichaa cha Mbwa**

**41. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Mradi wa Kutokomeza Kichaa cha Mbwa unaofadhiliwa na Taasisi ya *Bill & Melinda Gates Foundation* na kuratibiwa na Shirika la Afya Duniani imeendelea kudhibiti Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Morogoro, Mtwara na Pwani kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na wadau mbalimbali. Aidha, jumla ya dozi **271,000** za chanjo na vifaa vya kuchanja vilinunuliwa na dozi **200,000** zimesambazwa katika Halmashauri **24** zinazotekeleza mradi wa Kichaa cha Mbwa za Rufiji, Mkuranga, Kisarawe, Kibaha (Mji), Kibaha (W), Kilwa, Liwale, Lindi (W), Ruangwa, Nachingwea, Masasi, Nanyumbu, Newala, Tandahimba, Mtwara (W), Morogoro (W), Kilombero, Ulanga na Manispaa za Mtwara, Lindi, Temeke, Ilala, Kinondoni na Morogoro ambapo mbwa **107,400** na paka **2,120** wamechanjwa. Pia, dozi **71,000** zimesambazwa katika mikoa iliyo nje ya mradi ya Dodoma, Singida, Iringa, Njombe, Mbeya, Ruvuma, Rukwa na Katavi. Halmashauri zinahimizwa kununua chanjo zaidi kwa kutumia vyanzo vyake vya mapato kwa vile chanjo inayonunuliwa na Wizara ni kidogo na haiwezi kutosheleza mahitaji. Vilevile, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa na siku ya Wanyama Duniani.
Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kudhibiti Kichaa cha Mbwa kwa kununua chanjo dozi 100,000 kwa ajili ya kuchanja mbwa na paka kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na sekta binafsi. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha jamii kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huu.

**Homa ya Bonde la Ufa**

**42. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kufuatilia viashiria na mwenendo wa Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa (Rift Valley Fever-RVF). Aidha, ipo hatari ya ugonjwa huu kutokea wakati wowote ikizingatiwa kuwa viashiria vya ugonjwa huu ambavyo ni pamoja na mafuriko na maji kutuama kwenye mabonde kwa muda mrefu vimeanza kujitokeza katika baadhi ya maeneo hapa nchini. Ili kukabiliana na hali hiyo, Wizara inaendelea na taratibu za kununua dozi **150,000** za chanjo ya Homa ya Bonde la Ufa kwa ajili ya kusambazwa na kuchanja ng'ombe katika maeneo hatarishi ya mikoa ya Dodoma, Arusha, Manyara, Kagera, Simiyu, Geita, Mara, Mwanza na Shinyanga.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kufuatilia mwenendo wa ugonjwa huo na kuchukua hatua stahiki. Aidha, Serikali itanunua dozi **1,000,000** za chanjo ya ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa kwa ajili ya mikoa ya Arusha, Tanga, Tabora na baadhi ya mikoa katika Kanda Ziwa.

**Ukaguzi wa Mifugo na Mazao yake**

**43. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kushirikiana na Halmashauri kukagua mifugo na mazao yake ili kulinda afya ya jamii na kudhibiti kuenea kwa magonjwa yanayoambukiza binadamu kutoka kwa mifugo. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya ng'ombe **987,172** mbuzi

**885,061**, kondoo **275,197**, nguruwe **440,000** na kuku **1,632,000** walikaguliwa na wataalam katika machinjio mbalimbali. Aidha, Wizara imeendesha mafunzo rejea kwa Wakaguzi wa Nyama **12** kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na wadau **34** kutoka machinjio ya Vingunguti. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kufuatilia usalama wa mazao yatokanayo na mifugo kwa kukagua mifugo na mazao yake ili kukuza biashara ya mifugo na kulinda afya za walaji.

**Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo**

**44. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuimarisha Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo *(*Tanzania Livestock Identification and Traceability System- TANLITS*)* kwa kutoa mafunzo kuhusu stadi za utambuzi wa mifugo na ukusanyaji takwimu kwa ajili ya *database* ya TANLITS kwa wataalam **125** kutoka Halmashauri **4** za Wilaya za Kibaha, Bagamoyo, Muheza na Mji wa Kibaha. Aidha, kupitia ufadhili wa FAO ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa Utambuzi na Ufuatiliaji Mifugo umekamilika na unafanyiwa majaribio katika Halmashauri hizo. Pia, kupitia Mradi wa EAAPP, vifaa vya utambuzi ikiwa ni pamoja na hereni za elektroniki (RFID Ear Tag) **15,000** na *applicators* **100** vimenunuliwa na kusambazwa. Vilevile, ng'ombe **82,000** walitambuliwa kwa njia ya chapa ya moto katika Wilaya za Karagwe na Ngara; na ng'ombe **5,500** wametambuliwa kwa njia ya hereni za elektroniki katika Halmashauri za Wilaya za Muheza, Bagamoyo na Kibaha.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa mfumo wa elektroniki wa Utambuzi na Ufuatiliaji wa mifugo kwa kutoa mafunzo kwa wataalam wa mifugo **75** kuhusu mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo na kuhamasisha umma ili kuwezesha utambuzi wa mifugo **45,000** katika makundi ya wafugaji wa ng'ombe wa asili na kisasa.

***3.6 UENDELEZAJI WA SEKTA YA UVUVI***

**Uvunaji wa Samaki na Uuzaji wa Mazao ya Uvuvi**

**45. Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua umuhimu wa sekta ya uvuvi katika kukuza uchumi, uhakika wa chakula, kuongeza kipato, ajira na kupunguza umaskini, Wizara imeendelea kuhamasisha wavuvi na wadau wengine wa uvuvi kuhusu njia endelevu za uvunaji wa rasilimali za uvuvi kupitia mafunzo, maonesho na mikutano mbalimbali.

**46. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara imetoa elimu kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi unaozingatia mfumo wa ikolojia na mazingira (Ecosystem Approach to Fisheries Management –EAF) kwa wavuvi **641** kutoka Halmashauri za Bagamoyo (**288**), Kinondoni (**130**), Temeke (**130**) na Mkuranga (**93**). Aidha, Maafisa Uvuvi **16** wa Wilaya**,** Wavuvi **16** na Wawakilishi wa BMUs **16** kutoka Halmashauri **16** za Ukanda wa Pwani walipatiwa mafunzo kuhusu usimamizi endelevu wa rasilimali ya Jodari na samaki wanaopatikana katika tabaka la juu la maji (Pelagic fish species). Pia, nakala **1,000** za Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Samaki aina ya Jodari na **1,000** za Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji zimeandaliwa na kusambazwa kwa wadau. Vilevile, kupitia maonesho ya kitaifa ya Siku ya Mvuvi Duniani, Nane Nane, Siku ya Chakula Duniani na Wiki ya Usalama wa Chakula, jumla ya wadau **508** walipatiwa elimu ya usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

**47. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia ukusanyaji, uchambuzi na uhifadhi wa takwimu za uvuvi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara imefanya sensa mbili (**2**) za uvuvi Mto Kilombero katika Wilaya za Ulanga na Kilombero na Bwawa la Mtera katika maeneo ya Halmashauri za Iringa, Chamwino na Mpwapwa. Matokeo yanaonesha kuwepo kwa wavuvi **1,759**, vyombo vya uvuvi **1,598**, zana za uvuvi **16,870** na mialo **50** katika Mto Kilombero na mialo **29** yenye wavuvi wapatao **2,081** wanaotumia vyombo vya uvuvi **1,223** na zana za uvuvi **1,236** katika Bwawa la Mtera. Pia, mafunzo kuhusu mfumo mpya wa takwimu za kusafirisha na kuingiza nchini mazao ya uvuvi kwa maafisa uvuvi **10** kutoka Mikoa ya Mwanza (**4**), Mara (**3**) na Kagera (**3**) yalitolewa.

**48. Mheshimiwa Spika,** nguvu ya uvuvi nchini (fishing effort) imeongezeka kutoka wavuvi **182,741** na vyombo vya uvuvi **56,985** mwaka 2012/2013 hadi wavuvi **183,431** wanaotumia vyombo vya uvuvi **57,385** mwaka 2013/2014. Kutokana na nguvu hiyo ya uvuvi, jumla ya tani **375,158** za samaki zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi **trilioni 1.4** zilivunwa ambapo kati ya hizo, tani **52,846** ni kutoka ukanda wa maji chumvi na tani **147,020** maji baridi ikilinganishwa na tani **365,023.38** za samaki zenye thamani ya shilingi **trilioni 1.3** zilizovunwa mwaka 2012/2013 (**Jedwali Na. 7a na 7b**).

Aidha, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia uuzaji wa samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi ambapo jumla ya tani **38,574** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **44,260** zimeuzwa na kuiingizia Serikali mapato ya shilingi **bilioni 6.1** ikilinganishwa na tani **41,394** na samaki hai wa mapambo **45,550** zilizouzwa mwaka 2012/2013 na kuiingizia Serikali kiasi cha shilingi bilioni **6.8** (**Jedwali Na. 8a na 8b**).

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu, kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi. Pia, itafanya sensa **7** za uvuvi katika maji bahari, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Bwawa la Nyumba ya Mungu na Mto Rufiji kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji, uchambuzi na uhifadhi wa takwimu za uvuvi na kuhamasisha jamii za wavuvi kusimamia, kuendeleza na kulinda rasilimali za uvuvi kwa kuzingatia mfumo wa ikolojia na mazingira.

**Uwezeshaji Wavuvi Wadogo**

**49. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta binafsi imeendelea kuratibu upatikanaji wa matumizi ya teknolojia na miundombinu sahihi kwa ajili ya uandaaji, uchakataji, usambazaji na uuzaji wa samaki na mazao yake ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia programu ya SmartFish na United Nations University (UNU) Iceland imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia sahihi kwa ajili ya uandaaji, uchakataji na usambazaji wa mazao ya uvuvi kwa wavuvi **735** katika mikoa ya Kigoma (**140)**, Kagera (**180**), Mara (**150**), Mwanza (**240)** na Pwani (**25)** na kuwezesha ujenzi wa vichanja vya kisasa **40** vya kukaushia samaki na majiko sanifu manne (**4**) katika Halmashauri ya Uvinza.

**50. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na WWF, iliwawezesha wavuvi watano (**5**) kutoka Halmashauri za Kilwa (**1**), Lindi (**1**), Mtwara (**1**), Pangani (**1**) na Mafia (**1**) kuhudhuria mafunzo ya uchakataji wa samaki aina ya Jodari na utunzaji wa samaki wa mapambo; usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kupitia BMUs na uendeshaji wa miradi midogo. Aidha, kupitia Programu ya SmartFish, wavuvi **9** kutoka mikoa ya Kagera (**1**), Pwani (**1**), Mara (**1**), Mwanza (**4**) na Tanga (**2**) waliwezeshwa kuhudhuria maonesho ya kikanda ya mazao ya uvuvi yaliyofanyika Entebbe Uganda ambapo walipata fursa ya kujifunza mbinu mbalimbali za uhifadhi wa mazao ya uvuvi.

**51. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwemo kukamilisha ujenzi na kuzindua rasmi matumizi ya mialo mitatu (**3**) ya Masoko-Pwani (Kilwa), Kilindoni (Mafia) na Nyamisati (Rufiji) katika Ukanda wa Pwani na kuendelea na ujenzi wa mialo minne (**4**) ya Kibirizi (Kigoma-Ujiji), Muyobozi (Uvinza), Ikola (Mpanda) na Kirando (Nkasi) katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango; Wizara za Viwanda na Biashara; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ujenzi na Mamlaka ya Bandari, imeandaa Andiko la Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi (Fishing Port Construction Concept Note). Bandari hii itawezesha kukuza sekta ya uvuvi kwa kuvutia uwekezaji, kukuza ajira, kipato cha wavuvi pamoja na pato la Taifa. Pia, maandalizi ya Mradi wa *Southwest Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Programme -SWIOFish* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia yanaendelea.

**52. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa elimu ya uanzishwaji wa vyama vya ushirika vya wavuvi na kuandaa mwongozo na kutoa taarifa kwa umma kuhusu mpango wa ruzuku kwa wavuvi wadogo kwa ajili ya ununuzi wa boti, injini za boti, nyavu na mishipi. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha wadau kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta ya uvuvi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na kusambaza nakala **200** za Kitabu cha Fursa za Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi kwa wadau.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu fursa za uwekezaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kutengeneza boti hasa za *fibre* na zana za uvuvi zinazokubalika kisheria. Aidha, itaendelea kuhamasisha jamii za wavuvi kuanzisha vyama vya ushirika vya wavuvi na kuwezesha wavuvi wadogo kupata zana na pembejeo za uvuvi ikiwemo boti, nyavu, injini na viambata vyake kupitia mpango wa ruzuku. Pia, Wizara itahamasisha wadau **400** wa uvuvi kuhusu uchakataji wa samaki na mazao yake na kuwezesha ujenzi wa chanja za kuanikia samaki katika mikoa ya Kigoma, Mwanza, Rukwa, Mara, Ruvuma na Lindi. Vilevile, itaendelea kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kukamilisha ujenzi wa mialo **minne** katika ukanda wa Ziwa Tanganyika, ujenzi wa karakana ya kutengeneza boti katika Ukanda wa Ziwa Nyasa (Mbamba Bay) na kuendeleza mchakato wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi.

**Ukuzaji wa Viumbe kwenye Maji**

**53. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu shughuli za ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa samaki, ajira, kipato na kupunguza nguvu ya uvuvi katika maji ya asili. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya vifaranga **2,295,032** vimezalishwa na kusambazwa ambapo vifaranga **19,692** vimezalishwa katika vituo vya Serikali na **2,275,340** katika sekta binafsi.

**54. Mheshimiwa Spika,** mwaka 2013/2014, jumla ya wananchi **2,604** wamehamasishwa kwa kupatiwa elimu ya ufugaji samaki ambapo kutokana na uhamasishaji huo mabwawa ya kufugia samaki yameongezeka kutoka **20,134** mwaka 2012/2013 hadi **20,493** mwaka 2013/2014 yenye uwezo wa kuzalisha tani **3,546** za samaki. Aidha, tani **179.3** za mwani zenye thamani ya Shilingi **84,370,000/=** zimevunwa na wakulima katika Wilaya za Mkinga na Pangani. Pia, tani **320** za kambamiti zenye thamani ya Shilingi **bilioni 2.56** zimevunwa katika mabwawa ya kampuni ya Alphakrust katika Wilaya ya Mafia. Vilevile, vituo vya kuzalisha vifaranga kwa wingi kwa kutumia teknolojia sahihi ya kitotolishi cha ndani (indoor hatchery) vimeongezeka kutoka kituo kimoja mwaka 2012/2013 hadi vituo saba (**7**) mwaka 2013/2014 kati ya hivyo, vituo vinne (**4**) ni vya Serikali na vitatu (**3**) ni vya Makampuni binafsi **(Jedwali Na. 9).**

**55.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha vituo vyake kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa vifaranga vya samaki kwa wananchi ambapo katika Kituo cha Mwamapuli kimejengwa kitotolishi cha ndani, mabwawa ya kusakafia mawili (**2**) ya kutunzia samaki wazazi na ukusanyaji wa mbegu. Pia, mabwawa mawili **(2**) ya kufugia samaki yameandaliwa na kupandikizwa samaki aina ya kambale katika uanzishaji wa kilimo mseto cha mpunga pamoja na ufugaji wa samaki (Rice cum Fish) ambalo linatumika kama shamba darasa kwa jamii inayozunguka eneo hilo.

**56.** **Mheshimiwa Spika,** katika Kituo cha Kingolwira, jengo moja (**1**) limekarabatiwa kwa ajili ya kuweka kitotolishi cha ndani, matangi **17** yamekarabatiwa na mabwawa mawili (**2**) mapya yamejengwa. Vilevile, Kituo cha Luhira kimeimarishwa kwa kujenga kitotolishi cha ndani na kuweka mfumo wa maji. Pia, matangi manne (**4**) ya kukuzia vifaranga yamejengwa. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja kutathmini hali ya kituo cha Hombolo – Dodoma kinachomilikiwa na Kanisa la Anglikana na kituo cha Kilimo Mseto – Bacho Dareda kinachomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania kwa lengo la kuzalisha vifaranga vya samaki na samaki kwa mfumo wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Matokeo ya tathmini yanaonesha vituo hivi vinafaa iwapo vitaboreshwa. Vilevile, vifaranga **22,000** vya samaki aina ya perege vimepandikizwa katika bwawa la Bulenya lililoko Igunga na vifaranga ….. katika bwawa la Namtumbo Songea kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa samaki.

**57.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeimarisha vituo vya ukuzaji viumbe kwenye maji bahari ambapo matangi sita (**6**) yenye ujazo wa lita **8,000** kila moja yamejengwa na kuzungushiwa uzio kwa ajili ya kuzalishia vifaranga vya samaki katika kituo cha Machui Tanga. Aidha, kituo cha Mbegani kimeimarishwa kwa kukarabati jengo la ofisi na kujenga bwawa moja (**1**) la kukuzia samaki.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendeleza ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa kuimarisha vituo viwili (**2**) vya Dareda Manyara na Hombolo Dodoma, kuanzisha kituo cha Kibirizi Kigoma na kuimarisha vituo tisa (**9**) vya ufugaji wa samaki wa maji baridi kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki**.** Aidha, Wizara itaanzisha kituo kimoja **(1)** cha Mtwara na kuimarisha vituo viwili (**2**) vya Machui Tanga na Mbegani Bagamoyo kwa ajili ya kuzalisha vifaranga vya samaki wa maji bahari. Pia, itaandaa miongozo ya ukuzaji viumbe kwenye maji na kupitia Mpango Mkakati wa Taifa wa Ukuzaji Viumbe Kwenye Maji Tanzania.

### *3.7 UTAFITI, MAFUNZO NA UGANI WA MIFUGO NA UVUVI*

**58.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara na Taasisi zilizo chini yake na kushirikiana na wadau wengine wa ndani na nje iliendelea kuimarisha, kuratibu, kusimamia na kuendesha utafiti, mafunzo na utoaji wa huduma za ugani za mifugo na uvuvi nchini kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija katika ufugaji, uvuvi na ukuzaji viumbe kwenye maji. Aidha, Wizara ilifanya tathmini ya miradi ya utafiti ya ZARDEF katika kanda saba (**7**) iliyofanyika chini ya programu ya ASDP pamoja na miradi iliyoratibiwa na COSTECH. Matokeo ya tathmini hizi yanaonesha kuwa asilimia **70** ya tafiti za ZARDEF zimekamilika na matokeo yake kupelekwa kwa wadau ambapo tafiti zinazoratibiwa na COSTECH bado zinaendelea. Vilevile, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa tafiti **5** za Mifugo chini ya Mradi wa Kuongeza Tija wa Nchi za Kanda ya Mashariki ya Afrika (Eastern Africa Agricultural Productivity Programme- EAAPP).

**59.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu na kutathmini utafiti na huduma za utafiti na maendeleo ya ufugaji na uvuvi kulingana na programu zake zinazofadhiliwa na Serikali na Wafadhili mbalimbali kama EAAPP, ASARECA, Bill & Melinda Gates Foundation, IFAD na Benki ya Dunia. Aidha, kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini ya Wizara na

vituo vyake TALIRI (7), TAFIRI (5), TVLA (11), FETA (5) na LITA (6), Wizara itaandaa mikakati ya kutathmini, kuibua miradi mipya na kuboresha kiwango cha upatikanaji na usambazji wa matokeo ya tafiti za mifugo na uvuvi kwa wadau.

**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)**

**60. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kwa kuboresha miundombinu, kuipatia vitendea kazi na rasilimali watu. Katika mwaka 2013/2014, Taasisi iliendelea kukamilisha maandalizi ya Nyaraka na Miongozo mbalimbali ikiwemo Mpango Mkakati wa Miaka Mitano 2013/2014 - 2017/2018 na Muundo wa Taasisi (*Organization Structure*). Aidha, Muundo wa Utumishi wa TALIRI (*Scheme of Service*), Kanuni za Utumishi, Kanuni za Fedha na Mkataba wa Huduma kwa Wateja imeendelea kukamilishwa ili kuboresha utendaji wa Taasisi kwa mujibu wa Sheria iliyoiunda.

**61. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 TALIRI iliendelea kutekeleza miradi **54** ya utafiti kupitia vituo vyake **saba** vya Mpwapwa, Tanga, Uyole, West Kilimanjaro, Kongwa, Mabuki na Naliendele. Kati ya miradi hiyo, **13** ni ya utafiti wa uendelezaji wa tasnia ya maziwa na uzalishaji wa ng'ombe husika, **11** ni ya uzalishaji na uendelezaji wa nyama, **6** ni ya utafiti wa wanyama wadogo wanaocheua (mbuzi na kondoo), **15** ni ya uendelezaji wa malisho na **9** ni ya wanyama wasiocheua yaani kuku na nguruwe.

**62. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya ng'ombe **1,820,** waliendelea kutunzwa katika vituo kwa ajili ya utafiti kwa lengo la kuzalisha na kusambaza matokeo ya tafiti hizo ikiwa ni pamoja na mifugo bora kwa wadau mbalimbali. Hadi kufikia mwezi April mwaka 2014, TALIRI imesambaza jumla ya ng'ombe **143** aina ya Mpwapwa wakiwemo madume **110** na majike **33** katika Wilaya za Chamwino (madume **4**), Mwanza Mabuki (madume 19), Manyoni (madume 60), Dodoma Manispaa (madume **19**,majike **8**), Tanga (dume 1, majike **16**), Kilindi (dume **1**), Kisarawe (dume **1**, majike **4**) na Bagamoyo (madume **5**, majike **5**). Aidha, Taasisi imesambaza jumla ya madume **32** aina Friesian katika Wilaya za Bagamoyo (**10**), Muheza (**10**), Mufindi (**6**) na Njombe (**6**). Vilevile, taasisi imesambaza jumla ya Mbuzi aina ya Malya **65** katika maeneo ya Dodoma (**43**) na Pwani (**22**). Pia, nguruwe **60** wa mbegu wamepelekwa Mbeya (Mbozi na Mbeya Vijijini) kwa wafugaji kwa ajili ya kuongeza tija ya uzalishaji ambapo tathimini ya kiwango cha ukuaji wa nguruwe kwa siku katika mazingira ya wafugaji (on-farm) ulikuwa ni kati ya gramu **170** hadi **450** ikiwa ni wastani wa gramu **250** kwa siku katika maeneo tajwa.

**63. Mheshimiwa Spika,** watafiti wa TALIRI kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI) waliendesha mafunzo juu ya uendelezaji wa malisho katika vijiji **8** vya mikoa ya Morogoro na Tanga ambapo jumla ya washiriki **37** katika mkoa wa Tanga (**17**) na Morogoro (**20**) walishiriki. Pia, wafugaji **86** kutoka mikoa ya Singida na Simiyu walipatiwa mafunzo juu ya unenepeshaji wa ng'ombe.

**64. Mheshimiwa Spika,** TALIRI imekamilisha ujenzi wa jengo la maabara ya nyama, nyumba tatu (**3**) za watumishi katika kituo cha Mabuki na ukarabati wa jengo la maabara ya viini tete Mpwapwa. Aidha, TALIRI inaendelea na ukarabati wa jengo la maabara ya maziwa Uyole, ofisi ya Tanga na mabanda ya mbuzi West Kilimanjaro. Kazi hizi zimegharimiwa kwa fedha za maendeleo za ndani, COSTECH na wafadhili mbalimbali kama vile Benki ya Dunia, IFAD na ASARECA.

**65. Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na uhaba wa watumishi, Wizara imeajiri watafiti **4** na mtunza kumbukumbu mmoja (**1**). Aidha, jumla ya watafiti wanane **(8)** wamepata shahada za uzamili katika nyanja za taaluma mbalimbali za utafiti wa mifugo. Pia, TALIRI inaendelea

kusomesha watumishi ambapo jumla ya watafiti **18** wanaendelea na masomo ya Shahada za Uzamivu (**8**), Uzamili (**8**) na Shahada ya Kwanza (**2**).

**Utafiti wa malisho ya Mifugo**

**66.** **Mheshimiwa Spika**, tathmini ya uzalishaji wa malisho ya asili ilifanyika na kubaini kuwa uzalishaji wa malisho ulikuwa kati ya tani **2.95-8.10/ha** na tani **0.4-2.2/ha** kwa miti malisho. *Cenchrus ciliaris, Bothriochloa insclupta* na *Eragrostis superba* zilikuwa na uzani mkubwa (biomass) katika majani yaliyo vunwa ikilinganishwa na aina nyingine ya majani. Aidha, majani ya mikunde aina ya *Leucaena pallida* yalikuwa na mavuno ya kutosha ikilinganishwa na aina nyingine za miti ya malisho. Jumla ya wafugaji **140** katika Wilaya za Kilwa na Maswa wamepewa mafunzo juu ya utunzaji na uboreshaji wa malisho ya asili, hifadhi na utunzaji.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, jumla ya aina **39** za malisho ya asili zimekusanywa kwa ajili ya kufanyiwa tahimini vituoni. Aidha, sampuli za kila jani zilichukuliwa kwa ajili ya kuangalia ubora wake. Vilevile, jumla ya marobota **44,347** ya malisho yalivunwa kama ifuatavyo; TALIRI Mpwapwa (**29,254**), TALIRI Uyole (**11,000**) na TALIRI Kongwa (**4,093**) kwa ajili ya kulishia mifugo pamoja na kuuza kwa wafugaji waliohitaji. Pia, jumla ya marobota **2,220** ya masalia ya mazao ya shayiri, ngano na maharage yalikusanywa katika kituo cha TALIRI West Kilimanjaro na kuuzwa kwa wafugaji.

**68.** **Mheshimiwa Spika**, matokeo ya utafiti yaliendelea kusambazwa kwa wadau kupitia ziara za mafunzo kwa wafugaji waliotembelea vituo vya TALIRI, Taasisi kushiriki maonesho ya wakulima na wafugaji (Nane nane), wafugaji kushiriki katika mikutano na majukwaa ya wadau, watafiti kushiriki mikutano na makongamano na kwa watafiti kuchapisha matokeo ya tafiti zao katika majarida ya kisayansi.

Katika mwaka 2014/2015, TALIRI itaimarisha miundombinu ya utafiti kwa kununua vifaa vya maabara, kemikali na samani katika maabara ya sayansi ya nyama (Mabuki), Uhawilishaji Viinitete (Mpwapwa), maabara ya teknolojia ya maziwa (Uyole), maabara za lishe ya mifugo (Mpwapwa, Tanga, Naliendele na West Kilimanjaro). Aidha, TALIRI itaendelea kukarabati ofisi, nyumba za watumishi na miundombinu ya mashamba ya mifugo. Vilevile, Taasisi itaibua na kutekeleza miradi ya uendelezaji wa teknolojia mbalimbali za mifugo kwa lengo la kuongeza tija na ubora wa mazao ya mifugo.

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)**

**69.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu na rasilimali watu kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) ili kuboresha matokeo ya tafiti za uvuvi nchini. Katika mwaka 2013/2014, Taasisi imekarabati ofisi ya Utawala ya Kituo cha Kyela na kujenga uzio wa seng'enge katika kituo cha Dar es Salaam; imejenga matangi **9** katika kituo cha Dar es Salaam kwa ajili ya utafiti wa majaribio ya vyakula vya samaki kutokana na malighafi asili; imechimba mabwawa **2** katika kituo cha Mwanza kwa ajili ya kuzalisha vifaranga bora vya samaki hivyo kuwa na jumla ya mabwawa **10**; imenunua vitendea kazi vikiwemo boti **5** za utafiti, vifaa vya maabara, kompyuta (**10**) na mashine za kudurufu kwa vituo vya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Kyela, kituo kidogo cha Sota (Rorya) na Makao Makuu. Pia, Taasisi imewawezesha watumishi **23** kuhudhuria mafunzo katika ngazi ya shahada ya kwanza (**1),** uzamili (**7)** na uzamivu (**15)** kwa ufadhili wa COSTECH na wafadhili wa nje. Aidha, Taasisi imeandaa Mpango Mkakati kwa kipindi cha 2013/2014 - 2017/2018 na kuboresha Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa Taasisi wa mwaka 2009.

**70. Mheshimiwa Spika,** TAFIRI imeendelea kufanya utafiti na kuishauri Serikali na wadau wa uvuvi kuhusu hali ya rasilimali za uvuvi na jinsi ya kuzivuna kwa uendelevu. Ushauri huo umetolewa kupitia tafiti mbalimbali, ikiwemo tathmini ya uwingi wa samaki aina ya sangara (fish stock assessment survey) katika Ziwa Victoria ambapo matokeo yamebaini wingi wa samaki hawa unaendelea kushuka kutoka mavuno ya Kg **296** kwa saa (2008) hadi kufikia mavuno ya Kg **185** kwa saa (2013); utafiti wa maeneo yenye mawe katika Ziwa Victoria ambao ulibaini maeneo haya kuwa na bioanuwai kubwa na hivyo yanahitaji kuhifadhiwa na; Utafiti wa kuangalia vinasaba vya samaki na bioanuwai katika mabwawa ya Mtera, Hombolo, Mindu na Kidatu na mito ya Ruaha na Wami umebaini maeneo haya kuwa na bioanuwai kubwa.

**71. Mheshimiwa Spika**, TAFIRI imeandaa Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Ziwa Tanganyika ukilenga maeneo muhimu ya mazalia, makulia na malisho ya samaki (critical habitats) yaliyoainishwa baada ya utafiti katika ziwa hilo upande wa Tanzania. Matokeo yameonesha maeneo haya kuwa na bioanuwai kubwa ya samaki. Aidha, Taasisi imefanya utafiti wa samaki wa mapambo katika Ziwa Tanganyika na matokeo ya awali yanaonesha kuna aina **84** za samaki hao ambao bioanuwai na uwingi wao unaongezeka kuelekea kusini mwa ziwa.

**72. Mheshimiwa Spika,** naomba kuarifu Bunge lako Tukufu kuwa, aina nne za samaki wa mapambo ambao ni *Trophius dunoisi*, *T. maswa*, *Neolaomprogus lelouki* na *Frutosa* spp. black wapo katika hatari ya kutoweka kwa sababu wanavuliwa kwa wingi kutokana na bei yao kuwa juu (dola 300-400 kwa samaki). Aidha, samaki aina ya *Frutosa* spp. blue amepotea upande wa Tanzania na anapatikana upande wa DRC.

**73. Mheshimiwa Spika,** TAFIRI imeendelea kufanya utafiti kwa kushirikiana na wafugaji wa samaki ili wapate ujuzi na kuboresha ufugaji wao uwe wa tija. Utafiti huo kwa kushirikiana na wafugaji wa samaki ulihusu utengenezaji wa vyakula bora vya samaki kwa kutumia malighafi zipatikanazo karibu na wafugaji, uzalishaji mbegu (vifaranga) bora vya samaki na ufugaji wa mfumo wa mseto unaojumuisha samaki, kilimo cha mbogamboga na kuku. Tafiti hizi zilifanyika kwa malighafi kutoka Mikoa ya Morogoro, Mwanza, Mara, Arusha, Iringa na Dar es Salaam. Pia, Taasisi imendelea kufanya utafiti wa majaribio ya kifaa cha kukaushia samaki kinachotumia mionzi ya jua kwa kushirikiana na wavuvi wa Ziwa Nyasa ili kupunguza uharibifu wa mazao ya samaki baada ya uvunaji ambalo ni tatizo kubwa linaloshusha mapato ya wavuvi.

**74. Mheshimiwa Spika,** TAFIRI imetoa matokeo ya tafiti zake kwa Serikali na wadau wa uvuvi kupitia makongamano, mikutano, warsha, vyombo vya habari kama vile luninga na magazeti, vipeperushi, machapisho katika majarida ya kisayansi, sikukuu za kitaifa kama Nane Nane, Siku ya Mvuvi Duniani na Wiki ya Utumishi wa Umma.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara ikishirikiana na wadau wengine wa uvuvi itaendelea kuiwezesha TAFIRI kuendelea na tafiti za uvuvi na mazingira katika Bahari ya Hindi, maziwa, mito na mabwawa ili kubaini uwingi, mtawanyiko na ikolojia ya rasilimali kwa ajili ya kuweka menejimenti ya uvuvi endelevu. Aidha, Taasisi itaendelea kufanya utafiti wa ufugaji wa samaki ili kubaini teknolojia sahihi ya uzalishaji, upatikanaji wa mbegu bora na chakula bora vya samaki. Vilevile, Taasisi itafanya utafiti wa kupunguza upotevu wa mazao ya samaki baada ya uvunaji; kuimarisha miundombinu ya Taasisi kwa kujenga ofisi na maabara ya kituo cha Dar es Salaam na Sota; kukarabati na kununua vitendea kazi vya kitafiti pamoja na vifaa vya maabara kwa vituo vya TAFIRI. Pia, Taasisi itaendelea na tafiti na kwa kushirikiana na wadau itatoa muongozo wa uvuvi wa samaki wa mapambo ili kulinda rasilimali hii muhimu iwe kwa uvuvi endelevu.

**Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (Fisheries Education and Training Agency - FETA)**

**75. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) ili kukidhi mahitaji ya wataalam katika Sekta ya uvuvi. Katika mwaka 2013/2014, ukarabati wa Kituo cha Kigoma ulikamilika na kupata usajili wa kudumu kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Aidha, ukarabati wa kituo cha Mwanza South kilicho chini ya kampasi ya Nyegezi umefanyika na kuwezesha udahili wa wanachuo **20** wa masomo ya ufugaji wa viumbe kwenye maji. Vilevile, kituo cha Gabimori (Rorya) kimeendelea kujengwa ambapo nyumba mbili (**2**) za watumishi zimejengwa. Pia, udahili wa wanafunzi umeongezeka kutoka wanachuo **943** mwaka 2012/2013 hadi wanachuo **1,073** mwaka 2013/2014 katika Kampasi za Mbegani **(433**), Nyegezi **(611**) na Kigoma **(29**). Aidha, Wakala umeendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam **54** kutoka nchi za SADC.

**76. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Ushauri ya FETA imewezeshwa kufanya vikao viwili (**2**) na Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa mwaka 2013/2014 umeandaliwa na kupitishwa na Baraza la Wafanyakazi Mwezi Januari, 2014.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuiwezesha Wakala kutekeleza majukumu yake na kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka **1,073** hadi **1,500.** Aidha, FETA itaendelea kujenga kituo cha Gabimori (Rolya) na Mikindani Mtwara kwa kukikarabati.

**Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (Livestock Training Agency - LITA)**

**77. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuimarisha Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) ili kukidhi mahitaji ya wataalam katika sekta ya mifugo. Aidha, LITA imefungua Kampasi ya Kikulula ambayo imedahili wanafunzi **32** wa mwaka wa kwanza ngazi ya astashahada katika mwaka huu wa fedha 2013/2014. LITA imeongeza udahili wa wanafunzi kutoka **949** mwaka 2012/2013 hadi **2,215** mwaka 2013/2014 wakiwemo **655** wa Stashahada na **1,560** wa Astashahada za Afya ya Mifugo na Uzalishaji. Katika mwaka 2013/2014 wanafunzi **949** wanatarajiwa kuhitimu mafunzo yao mwezi Juni 2014 wakiwemo **198** wa Stashahada na **751** wa Astashahada. Vilevile, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na vyuo binafsi vya Visele (Mpwapwa) na Kaole (Bagamoyo) vimedahili jumla ya wanafunzi **492** wa Stashahada na Astashahada.

**78. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha na kusimamia utendaji, LITA imeandaa Mpango wa Biashara wa mwaka 2013/2014 – 2017/2018. Aidha, Wakala umeendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji na wadau wengine **587** kuhusu Afya ya Mifugo (**30)**, Ufugaji Bora wa Ng'ombe wa Maziwa (**339)**, Usindikaji wa Maziwa (**125)** na Ufugaji Bora wa Nguruwe na kuku wa kienyeji (**93)**.

**79. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zilizotekelezwa na LITA ni pamoja na:

(i) Kukarabati darasa moja katika kila Kampasi za Tengeru, Buhuri, Temeke na Kikulula; ukumbi wa mitihani katika Kampasi ya Mpwapwa na mabweni matatu katika Kampasi za Madaba (**1**) na Kikulula (**2**);

(ii) Kununua madawati **24** na viti **24** Kampasi ya Morogoro, madawati **30,** meza **30**, magodoro **30,** *Printer* (**1**) na *Photocopier* **1** kwa Kituo cha Kikulula, S*olar power panels* **14** Kituo cha Mabuki na Kompyuta mbili (**2**), *lap top* **moja** na *printer* **moja** kwa ajili ya Makao Makuu; na

(iii) Kuendeleza Wakufunzi **27** kupata mafunzo katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu (**3**); Uzamili **(11)** na Shahada ya Kwanza **(13).** Aidha, mtumishi mmoja (**1**) anaendelea na mafunzo ya stashahada na watatu **(3)** wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi ya utawala bora.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuiwezesha Wakala kutekeleza majukumu yake na kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka **2,215** hadi **2,500;** kuhamasisha Sekta binafsi kuanzisha vyuo na kuongeza udahili kufikia lengo la wanafunzi **5,000** kwa mwaka ili kupunguza pengo la maafisa ugani na kuwezesha mafunzo ya ufugaji kibiashara kwa vijana (Emerging Young Commercial Farmers) ili waweze kujiajiri.

**Huduma za Ugani**

**80.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau imeendelea kutoa elimu na kusambaza teknolojia za kisasa kuhusu uvuvi endelevu, ukuzaji bora wa viumbe kwenye maji na ufugaji bora wa mifugo. Katika kipindi hiki, vipindi **52** vya redio na **12** vya luninga vilivyohusu ufugaji bora wa mifugo na uvuvi viliandaliwa na kurushwa hewani. Aidha, jumla ya teknolojia **55** za uzalishaji maziwa ziliainishwa kutoka vituo vya Utafiti vya Tanga, Uyole, Seliani (Arusha), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Kituo Mahiri cha Uzalishaji wa Maziwa Kenya ambapo teknolojia **18** zimesambazwa kwa wadau katika maeneo ya Kanda za Mashariki na Nyanda za Juu Kusini. Vilevile, Wataalam **53** wa ugani wamepatiwa mafunzo kuhusu uzalishaji na uhifadhi wa malisho, usafi na utunzaji wa maziwa.

**81.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia mradi wa EAAPP unaotekelezwa katika Halmashauri **11** za Kanda ya Mashariki na Nyanda za Juu Kusini imepeleka wafugaji **10** Naivasha Kenya kwa ziara ya mafunzo ya uzalishaji wa zao la maziwa. Pia, jumla ya wafugaji **325** kutoka eneo la mradi walipata mafunzo ya mnyororo wa thamani katika zao la maziwa, uzalishaji na uhifadhi wa malisho (**205**) na usindikaji na masoko ya maziwa (**120)** katika Kampasi ya Buhuri. Aidha, mabango matatu (**3)** na vipeperushi **8,500** kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa yalisambazwa kwa wafugaji.

**82.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuboresha utoaji huduma za ugani katika sekta ya uvuvi kwa kutoa mafunzo elekezi ya ufugaji wa samaki kwa wataalam **11** na wadau wa uvuvi **256** katika mikoa ya Tanga, Iringa na Morogoro. Aidha, mwongozo wa utekelezaji wa huduma za ugani katika sekta ya uvuvi umekamilika ambapo makala **1,000** zimechapishwa.

Katika mwaka 2014/2015 Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake katika eneo la utafiti, mafunzo na ugani itatekeleza yafuatayo:

(i) Kujenga uwezo kwa watafiti waandamizi **40** na wa ngazi ya kati na waajiriwa wapya **60** kwa kutoa mafunzo ya kuibua na kuandika tungo za utafiti na machapisho yanayokubaliwa katika majarida ya kimataifa;

(ii) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, utunzaji na usambazaji wa taarifa za matokeo ya tafiti za mifugo na Uvuvi nchini (data base);

(iii) Kuendelea kushirikiana na Nchi za Afrika Mashariki na Kati kutekeleza Mradi wa Kuongeza Tija katika Kilimo – zao la maziwa (EAAPP);

(iv) Kuendelea kuimarisha TALIRI na TAFIRI katika kuendeleza tafiti za mifugo na uvuvi nchini;

(v) Kujenga uwezo wa wagani **150** katika Halmashauri kwa kupatiwa mafunzo tarajali;

(vi) Kuandaa na kusambaza Mwongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa Vyuo vya Mafunzo vya Mifugo na Uvuvi kwa kuzingatia sheria, kanuni na mahitaji ya taaluma; na

(vii) Kutayarisha na kurusha hewani vipindi **52** vya radio na **6** vya luninga;

**Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (Tanzania Veterinary Laboratory Agency-TVLA)**

**83. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 Wizara kupitia Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania ilitekeleza kazi za utambuzi, uchunguzi na utafiti wa magonjwa ya mifugo, uhakiki wa vyakula vya mifugo na madawa ya kuogeshea mifugo katika maabara zake za Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Tabora, Mpwapwa, Tanga, Kigoma, Iringa na Mtwara. Aidha, Wakala iliendelea kuimarisha kiwanda cha kuzalisha chanjo za mifugo Kibaha na kutekeleza mfumo wa usimamizi wa ubora wa huduma za maabara katika Maabara Kuu ya Mifugo Temeke .

**84. Mheshimiwa spika**, Katika mwaka 2013/2014, TVLA ilipokea jumla ya sampuli **6,860** katika maabara zake nchini na kuzifanyia utambuzi wa magonjwa. Baadhi ya magonjwa yaliyotambuliwa ni pamoja na Ugonjwa wa Kutupa Mimba kwa Ng'ombe, Ndigana kali, Ndigana baridi, Minyoo, Kimeta, Kichaa cha mbwa, Sotoka ya Mbuzi na Kondoo, Homa ya Mapafu ya Mbuzi, kuharisha na kuharisha damu, Mdondo, Gumboro na Homa ya Nguruwe. Aidha, sampuli **760** za Ndegepori wanaosafirishwa nje ya nchi zilifanyiwa uchunguzi wa Mafua makali ya ndege na Mdondo na hazikuonyesha maambukizi ya magonjwa hayo.

**85. Mheshimiwa Spika**, TVLA ilipokea sampuli **679** kwa ajili ya uhakiki wa ubora wa vyakula vya mifugo katika maabara kuu ya mifugo, Dar es Salaam na kuzifanyia uchunguzi ambapo asilimia **40** ya vyakula hivyo vilikuwa na upungufu wa protini, wanga na unyevu uliozidi kiwango kinachokubalika. Wakala iliwaelekeza wazalishaji na watengezaji kutengeneza vyakula vinavyofikia viwango vya virutubisho vinavyotakiwa.

**86. Mheshimiwa Spika**, TVLA iliendelea na utafiti wa kudhibiti mbungó kwa kutumia teknolojia ya vitambaa ili kudhibiti Ugonjwa wa Nagana na Malale. Katika mwaka 2013/2014, TVLA kwa kushirikiana na Hifadhi ya Mbuga ya Selous imetengeneza vitambaa **300** na kuviweka katika maeneo ya Mbuga ya Selous ili kudhibiti mbung'o. Aidha, utafiti huo unaendelea katika maeneo ya Hifadhi za Ngorongoro, Serengeti na maeneo yanayozunguka hifadhi hizo na Wilaya ya Meatu. Aidha, Matokeo ya awali ya utafiti huo yameonyesha asilimia moja (**1%**) ya ngómbe katika maeneo ya Ngorongoro ina maambukizi ya vimelea vya ugonjwa wa Nagana katika ng'ombe **450** waliofanyiwa utafiti.

**87. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2013/2014, Wakala imeimarisha kiwanda cha Kuzalisha Chanjo cha Kibaha kwa kununua mashine za kuchanganya, kujaza, kuweka vizibo na kuweka lebo kwenye chupa na kuweka mfumo wa kuchuja hewa kiwandani na uzalishaji unaendelea.

Katika mwaka 2014/2015, TVLA itaendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuendelea kufanya utambuzi wa magonjwa mbalimbali ya mifugo, kuendeleza tafiti za magonjwa ya mifugo, kuzalisha dozi **100,000,000** za chanjo ya Mdondo, dozi **500,000** za chanjo ya Chambavu, dozi **500,000** za chanjo ya Kimeta na dozi **250,000** za chanjo ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba kwa Ng'ombe na Maabara Kuu ya Mifugo Temeke kukamilisha taratibu za kupata ithibati ya Kimataifa.

### *3.8 USIMAMIZI WA UBORA WA MAZAO NA HUDUMA ZA MIFUGO NA UVUVI*

**88. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia ubora wa mazao ya mifugo na uvuvi pamoja na huduma za kitaalam kupitia Bodi ya Nyama, Bodi ya Maziwa, Baraza la Veterinari na Kitengo cha Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi na Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi- Nyegezi.

**Bodi ya Nyama Tanzania**

**89. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuimarisha Bodi ya Nyama Tanzania kwa kuipatia wataalam na vitendea kazi. Aidha, Bodi imeandaa maelezo ya Sheria ya Nyama Sura 421 katika lugha ya Kiswahili na kutoa elimu kwa wadau kupitia vipindi vya redio **14** na kusambaza nakala **800** za vipeperushi. Vile vile, Bodi imehamasisha wadau wa tasnia ya nyama katika mikoa ya Simiyu, Mwanza, Geita, Dar es Salaam, Arusha, Iringa na Pwani kusajili, ambapo wadau **116** wamesajiliwa na wadau wengine **50** wameunganishwa na soko la mifugo na nyama.

**90. Mheshimiwa Spika,** Bodi kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), Shirika lisilo la kiserikali la CHIGOTO Plus na sekta binafsi imehamasisha ufugaji wa kibiashara katika mikoa ya Simiyu, Mwanza, Geita ambapo vikundi **18** vya ufugaji wa kibiashara vimeundwa kwa lengo la kuingia mkataba wa kibiashara na Kampuni ya Chobo (Mwanza) na Tandan Farms (Mkuranga). Pia, Bodi imeandaa mwongozo na kutoa elimu ya madaraja ya mifugo na nyama ili kusimamia ubora wa mifugo inayochinjwa na nyama inayozalishwa katika Halmashauri za Mwanza, Magu na Hanang. Aidha, Bodi imehamasisha wadau wa tasnia ya nyama na kuwezesha uundwaji wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) kilichosajiliwa mwezi Desemba, 2013.

Katika mwaka 2014/2015, Bodi ya Nyama Tanzania itaendelea kuimarisha Sekretarieti ya Bodi kwa kuajiri watumishi sita **(6)** na kutambua na kusajili wadau **200** wa tasnia ya nyama na vyama vyao. Aidha, itafanya tathmini ya mahitaji ya nyama, uwezo wa kuzalisha, kutafuta masoko na kufuatilia uingizaji na uuzaji wa nyama na bidhaa zake ndani na nje ya nchi. Pia, itaandaa na kuendesha vikao vinne (**4)** vya Bodi na kimoja (**1**) cha Baraza la Wadau wa Nyama. Vilevile, Bodi itaendelea kuimarisha vyama vya wadau vya wafanyabiashara wa Mifugo na Nyama Tanzania (TALIMETA), Wasindikaji wa Nyama Tanzania (TAMEPA) na Wafugaji Tanzania (CCWT) kwa kushauri, kutoa mafunzo na kuratibu maendeleo ya vyama hivyo.

**Bodi ya Maziwa Tanzania**

**91. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kuimarisha Bodi ya Maziwa Tanzania na imeendelea kuratibiwa na Bodi ya Maziwa Tanzania iliyoundwa kwa Sheria ya Maziwa SURA 262. Aidha, Bodi imeelimisha wadau **100** wa maziwa kuhusu Sheria ya Maziwa katika Mkoa wa Njombe; imeeandaa miongozo mitano **(5)** ya ukaguzi wa mashamba, sehemu ya kukusanyia maziwa na vyombo vya usafirishaji, vioski vya maziwa, viwanda vya kusindika maziwa na majukumu ya ukaguzi katika Halmashauri. Pia, Bodi imeandaa taratibu za usafi (code of hygiene) katika uzalishaji, ukusanyaji, usindikaji na uuzaji wa maziwa ghafi kwa ajili ya kutumiwa na wakaguzi. Vilevile, vibali **80** vya kuingiza maziwa lita **13,200,000** kutoka nje ya nchi yenye thamani ya shilingi **4,142,018,414.50** kabla ya kodi **(**FOB*)* vilitolewa.

**92. Mheshimiwa Spika,** kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kusajili wadau wa tasnia ya maziwa **25**, kuratibu programu ya unywaji maziwa shuleni ambapo jumla ya shule **145** zenye

wanafunzi **51,894** katika Halmashauri za Njombe, Hai, Siha, Musoma na Jiji la Tanga zimeshiriki (**Jedwali Na.9**); kuandaa Wiki ya Maziwa iliyofanyika katika Manispaa ya Musoma ikiwa na Kauli mbiu ya **Fuga ng'ombe wa Maziwa, Uboreshe Kipato na Lishe. "Badilika Sasa"** na kufanya vikao vitano (**5**) vya Bodi na mkutano wa dharura kupitia rasimu ya mpango mkakati wa Bodi wa kipindi cha miaka mitano (2013/14 – 2017/2018).

Katika mwaka 2014/2015, Bodi itaendelea kuelimisha wadau wa maziwa kuhusu Sheria ya Maziwa SURA 262 na kuisimamia, kuwajengea uwezo wakaguzi **50** wa maziwa kutoka Halmashauri za mikoa ya Iringa, Njombe na Mara kuhamasisha Halmashauri kutekeleza Mpango wa Unywaji wa Maziwa Shuleni na kuratibu Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa yatakayofanyika kitaifa katika Manispaa ya Babati - Manyara.

**Baraza la Veterinari Tanzania**

**93.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania lililoundwa chini ya Sheria ya Veterinari SURA 319 imeendelea kusimamia viwango vya huduma zinazotolewa na wataalam wa afya ya mifugo nchini. Katika mwaka 2013/2014, Baraza limeimarisha ukaguzi katika ngazi za kanda, mikoa na halmashauri ambapo Wakaguzi wapya **20** wameteuliwa kwa mujibu wa Sheria na kutangazwa katika Gazeti la Serikali G.N.439. Majukumu yao ni pamoja na kukagua huduma zote zinazohusu afya ya mifugo, zinazotolewa na wataalam wa sekta za umma na binafsi.

**94.** **Mheshimiwa Spika**, jumla ya vituo **246** vya huduma ya afya ya mifugo vimekaguliwa katika Halmashauri za mikoa ya Arusha, Dar-es-Salaam, Kilimanjaro, Pwani na Tanga, na vimeelekezwa kurekebisha upungufu uliobanika ili kuboresha huduma wanazozitoa. Aidha, wakaguzi wa nyama na watalaam wa afya ya mifugo **150** katika mkoa wa Dar-es-Salaam walikaguliwa ili kubaini sifa walizonazo kwa lengo la kuboresha huduma. Katika ukaguzi huo **25** walibainika kutokuwa na sifa na waliagizwa kuacha kujihusisha na utoaji wa huduma hiyo. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kusajili madaktari wa mifugo **37** hivyo kufanya idadi ya madaktari waliosajiliwa nchini kufikia **681,** kuandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi wa afya ya mifugo **221** wenye stashahada na astashahada hivyo kufikia **1,661.** Aidha, vituo **106** vya kutolea huduma ya afya ya mifugo vimesajiliwa na kufikia vituo **237** vilivyopo hapa nchini, kutoa leseni kwa wakaguzi wa nyama **40**, wahimilishaji **6** na mafundi sanifu **3** wa maabara za veterinari.
Katika mwaka wa 2014/2015, Baraza la Veterinari litaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Veterinari SURA 319 kwa kusajili madaktari wa mifugo **40,** vituo vya huduma za mifugo **200,** kuorodhesha na kuandikisha wataalamu wasaidizi **700,** kutoa leseni kwa wataalam wasaidizi **110** na kufanya ukaguzi wa maadili kwa kushirikiana na Halmashauri **156** nchini. Aidha, Baraza limepanga kufanya vikao **4** na vikao **8** vya kamati zake na kuhakiki viwango vya taaluma ya Veterinari katika vyuo **5** na makampuni **10** yanayotoa huduma za mifugo.

**Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

**95.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Kitengo cha Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi na Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi-Nyegezi imeendelea kuratibu na kusimamia ubora, viwango na usalama wa mazao ya uvuvi pamoja na huduma za kitaalam ikiwemo kufanya kaguzi mbalimbali za kuhakiki ubora wa mazao ya uvuvi katika

viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, mialo, masoko na kwenye magari na boti zinazobeba mazao ya uvuvi.

### Usimamizi na Ukaguzi wa Viwanda, Maghala, Mialo na Masoko ya Samaki

**96. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2013/2014, Wizara imetoa mafunzo kuhusu taratibu na kanuni za usafirishaji wa samaki hai nje ya nchi na teknolojia ya uhifadhi na utunzaji wa samaki kwa wasafirishaji wadogo **40** wa samaki hai wa mapambo na wafanyabiashara **18** wanaoingiza mazao ya uvuvi nchini. Aidha, Wizara imefanya kaguzi **3,439** ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ambapo kaguzi **1,594** zilifanyika wakati wa kusafirisha mazao ya uvuvi kwenda nje ya nchi, kaguzi **586** kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, kaguzi **220** kwenye maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi na kaguzi **995** kwenye boti na magari ya kubebea mazao ya uvuvi. Matokeo ya kaguzi hizo yalionesha kukidhi viwango vya ubora na hivyo viwanda na maghala hayo kuruhusiwa kuendelea na shughuli za uchakataji na uhifadhi. Vilevile, kaguzi zimefanyika katika masoko **44** ya samaki ya Halmashauri na maelekezo ya kuboresha miundombinu ya masoko na usafi kutolewa.

**97. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi ambapo viwanda vitano (**5**) vya kuchakata mazao ya uvuvi katika ukanda wa Pwani vimejengwa na kufanya idadi ya viwanda kufikia **48** ikilinganishwa na viwanda **43** katika mwaka 2012/2013. Kati ya viwanda hivyo, **11** viko Ukanda wa Ziwa Victoria, **36** Pwani na **1** Ziwa Tanganyika na Viwanda hivi vimeendelea kukidhi viwango vya uzalishaji wa mazao bora ya uvuvi kulingana na mahitaji ya soko la ndani na nje likiwemo soko la Kimataifa la Jumuiya ya Ulaya lenye Sheria na Viwango vya hali ya juu vya ubora.

**98. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imekarabati mialo **25** ya kupokelea samaki katika Ukanda wa Ziwa Victoria na mialo mitatu (**3**) ya Kilindoni-Mafia, Nyamisati-Rufiji na Kilwa-Masoko imejengwa. Aidha, ujenzi wa mialo minne (**4**) ya Kibirizi-Kigoma Ujiji, Muyobozi-Uvinza, Ikola-Mpanda na Kirando-Nkasi upo katika hatua za mwisho.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuratibu usimamizi wa usafi kwenye mialo na masoko ya samaki kwa kufanya kaguzi **100** na kuhimiza uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Pia, itahamasisha wadau kuwekeza zaidi katika ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi ili kuongeza uzalishaji na thamani ya mazao ya uvuvi. Aidha, itafanya kaguzi **3,600** za ubora wa samaki na mazao yake wakati wa kusafirisha nje ya nchi, kwenye mialo, masoko na kaguzi **100** za kina kwenye viwanda vya kuchakata samaki na maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi.

### Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi katika Maabara

**99. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuimarisha vituo nane (**8**) vya Uthibiti Ubora wa mazao ya Uvuvi vya Bukoba, Dar es Salaam, Kigoma, Kilwa, Mafia, Musoma, Mwanza na Tanga, pamoja na Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi-Nyegezi kwa kuvipatia watumishi na vitendea kazi. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya sampuli **1,318** za samaki, maji, vyakula vya samaki na udongo zilifanyiwa uchunguzi kati ya hizo **966** zilichunguzwa kubaini uwepo wa vimelea vya magonjwa na **352** kubaini mabaki ya viuatilifu, madini tembo na kemikali. Matokeo ya uchunguzi wa sampuli hizi ulionyesha kukidhi viwango. Aidha, Wizara imekamilisha Miongozo ya Utendaji (Standard Operating Procedures – SOPs) wa Maabara ya Kemikali ya Uvuvi Nyegezi na kushiriki katika majaribio ya *Proficiency Testing Scheme Providers* wa maji na chakula iliyohusisha maabara 12 kutoka nchi za SADC ikiwa ni maandalizi ya kupata

Ithibati ya uchunguzi wa kemikali (viuatilifu na mabaki ya sumu). Vilevile, Maabara ya Taifa ya Ubora wa Mazao ya Uvuvi Nyegezi imeongeza *parameters* vyenye Ithibati kutoka sita (**6**) mwaka 2012/2013 na kufikia **12** mwaka 2013/2014. Pia, Maabara ya kuchunguza kemikali na vimelea Kurasini imefanyiwa ukarabati.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha vituo vinane (8) vya Ubora na Uthibiti wa Mazao ya Uvuvi na Maabara za Uvuvi – Nyegezi na ya HABs-Temeke (Harmful Algal Blooms) kwa kuzipatia vitendea kazi na mafunzo kwa watalaam wanne **(4).** Aidha, Maabara zitafanya chunguzi za kimaabara kwa sampuli **800** za minofu ya samaki, maji, majitaka na udongo ili kulinda afya ya mlaji

### *3.9 USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UVUVI*

**100. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Halmashauri imeendelea kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi kwa kudhibiti uvuvi haramu na utoroshaji wa samaki na mazao ya uvuvi mipakani.

#### Udhibiti wa Uvuvi Haramu

**101. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeanzisha kituo kimoja cha doria cha Buhingu (Uvinza) na kufanya vituo vya doria kufikia **23.** Aidha, imeimarisha vituo vya doria kwa kununua boti nne (**4**) kwa ajili ya vituo vya doria vya Ikola, Kigoma, Mbamba Bay na Kasanga. Pia, kupitia Programu ya Maendeleo ya Uwiano katika Bonde la Ziwa Tanganyika boti za doria nne (**4**) zimenunuliwa kwa ajili ya vituo vya doria vya Kipili, Kigoma, Buhingu na Kasanga. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo kuhusu Sheria na Kanuni za uvuvi na athari za matumizi ya zana haramu kwa wavuvi **620** kutoka Ukanda wa Ziwa Tanganyika, wafanyabiashara na wasafirishaji wa mazao ya samaki **142** kutoka Ukanda wa Ziwa Victoria. Pia, Wizara kupitia Programu ya SmartFish imetoa mafunzo kwa vitendo kuhusu udhibiti wa uvuvi haramu kwa Maafisa Uvuvi **73** kutoka Ukanda wa Ziwa Victoria (**32**), Ukanda wa Ziwa Tanganyika (**18**) na Ukanda wa Pwani (**23**); na wajumbe wa BMUs **15** kutoka ukanda wa Ziwa Victoria **12**, Ziwa Tanganyika **2** na Pwani **1**.

**102. Mheshimiwa Spika,** jumla ya doria zenye siku kazi (man-days) **6,201** zilifanyika katika maeneo mbalimbali ya uvuvi yakiwemo maziwa, mito, bahari, mipakani na katika masoko kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu, biashara ya samaki wachanga na utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwenda nchi jirani. Uendeshaji wa doria hizo umewezesha kukamatwa kwa zana mbalimbali ikiwemo; nyavu za kokoro **1,342**, kamba za kokoro mita **320,620**, nyavu aina ya Timba (monofilament) **11,952**, nyavu za makila **20,329**, nyavu za dagaa **238**, vyandarua **123**, Katuli **15**, Kimia **5**, mabomu **73**, tambi za kulipulia mabomu **15**, Detoneta **58**, mitungi ya gesi **48**, viatu vya kuzamia jozi **35**, miwani ya kuogelea jozi **11**, mikuki **8**, Kasia **18**, Tanga **2**, mizani **17**, karabai **2**, mitumbwi **194**, injini za boti **10**, magari **12**, pikipiki **2** na baiskeli **1** na kontena **1** la samaki aina ya Migebuka na dagaa.

Aidha, samaki wachanga kilo **30,823** za sangara, **2,478** za sato, **1,112** za samaki aina nyingine na kilo **187** za samaki waliovuliwa kwa mabomu, kilo **682** za dagaa, kilo **57** za Pweza, kilo **5** za majongoo bahari na kilo **210** za nyama ya Kasa zilikamatwa. Nyavu haramu zilizokamatwa ziliteketezwa kwa moto baada ya kupata idhini ya Mahakama na samaki wachanga

waliokamatwa waligawiwa katika vituo vya kulelea watoto yatima, magereza na kwa wananchi kwa idhini ya Mahakama. Aidha, kutokana na makosa hayo, watuhumiwa **319** walikamatwa na kesi **48** zilifunguliwa mahakamani na kati ya hizo kesi mbili (**2)** zimeisha kwa kutolewa hukumu na nyingine bado zinaendelea.

**103. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha vikundi Shirikishi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) kwa kusajili BMUs **13** katika Ukanda wa Pwani (**11**), Ziwa Tanganyika (**1**) na Ziwa Kitangiri (**1**). Aidha, kwa kushirikiana na Mashirika ya WWF na Sea Sense, ilitoa elimu kwa BMUs **20** na wavuvi **10** kuhusu utunzaji wa kasa katika Halmashauri za Temeke na Mafia ambapo jumla ya kasa **22** waliwekewa alama (tags) kwa ajili ya kufuatilia mienendo yao na kufanya tathmini ya utendaji wa BMUs zilizopo katika Ukanda wa Pwani.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuratibu na kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi na kudhibiti biashara haramu ya mazao ya uvuvi kwa kufanya doria zenye siku kazi **6,000** katika maeneo ya maji baridi, Bahari ya Kitaifa (territorial waters) na maeneo ya mipakani. Aidha, itaendelea kuwezesha uanzishwaji wa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) sita (**6**) na kuimarisha vikundi vilivyopo.

**104. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu (Deep Sea Fishing Authority – DSFA) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inaendelea kufanya utafiti kuhusu matumizi sahihi ya vifaa vya kuvutia samaki (Fish Aggregating Devices – FADs*)*. Pia, Mamlaka imeendelea kuandaa mazingira rafiki ambayo yatawawezesha watanzania kuingia ubia na wageni ili waweze kuwekeza kwenye uvuvi katika Bahari Kuu. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na nchi wanachama wa *Indian Ocean Tuna Commission (IOTC)* za Comoro, Madagascar, Seychelles, Reuninon na Mauritius, ilifanya doria za pamoja za siku nane (**8**) kukagua meli nane (**8)** zinazovua katika Bahari Kuu ya Tanzania. Pia, ukaguzi ulifanyika kwa meli **25** za uvuvi wa *purse seine* na *long liner* zenye Bendera ya Hispania, Taiwan na China katika Bandari za Dar es Salaam na Zanzibar, Mombasa, Mahe Victoria (Ushelisheli), Madagascar na Mauritius. Katika ukaguzi huo meli husika zilionekana kukidhi masharti ya leseni. Vilevile, leseni za uvuvi wa Bahari Kuu **68** zenye thamani ya Dola za Kimarekani **1,472,153** sawa na shilingi **bilioni 2.4** zilitolewa kwa meli kutoka mataifa ya Hispania, Ufaransa, Ushelisheli, Taiwan, Japan, Oman na China.

**105. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa kushirikiana na Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi, Kampasi ya Mbegani imetoa mafunzo kwa wavuvi **25** kuhusu uvuvi wa samaki aina ya jodari kwa kutumia zana za *purse seine* na *long lines*; udhibiti na ukaguzi wa meli bandarini; sheria, udhibiti na kuhifadhi vidhibiti; udhibiti na kupambana na uvuvi haramu baharini; kuandaa na kuchambua takwimu za uvuvi kutoka meli za kigeni zinazovua kwenye Bahari Kuu.
Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaiwezesha Mamlaka kukamilisha marekebisho ya Sheria na Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu, kuendesha doria na kufanya tathimini ya utendaji wa FADs. Pia, kuendelea kuhamasisha wavuvi wa Tanzania na wawekezaji wengine kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu na kusindika mazao ya uvuvi. Vilevile, kuendelea kutoa mafunzo ya uvuvi wa Bahari Kuu kwa wavuvi.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu**

**106. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia maendeleo ya rasilimali za uvuvi katika maeneo yaliyohifadhiwa kupitia kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU). Katika mwaka 2013/2014, Kitengo kimefanya doria zenye siku kazi **800** ili kudhibiti uvuvi haramu ambapo mabomu **21** na tambi zake, chupa mbili (**2)** za mbolea ya Urea inayotumika kutengeneza mabomu, makokoro matano (**5**), michinji sita (**6**), mishipi (**14**), kilo kumi (**10**) za samaki waliovuliwa kwa mabomu vilikamatwa na watuhumiwa tisa (**9**) walifikishwa mahakamani.

**107. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kukiimarisha kitengo kwa kuwawezesha watumishi kuhudhuria mafunzo na kukipatia vitendea kazi. Katika mwaka 2013/2014 watumishi nane (**8**) wamewezeshwa kuendelea na mafunzo ya muda mrefu kwenye Shahada za uzamivu (**1**), uzamili (**3**), Shahada ya kwanza (**3**) na Stashahada ya Uhazili (**1**). Pia, watumishi saba (**7**) wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, Kitengo kimeimarishwa kwa kununua Injini mbili (**2)** za boti, trekta mbili **(2)**, Jenereta moja **(1)**, Kompyuta mpakato tatu **(3)**, GPS tano (**5**), maboya ya kujiokolea **(20),** samani za ofisi na kukarabati boti **(1)** kwa ajili ya Hifadhi za Bahari za Mafia, Mnazi Bay na Tanga.

**108. Mheshimiwa Spika,** Kitengo kwa kushirikiana na wadau kimeandaa Mpango Mkakati (Strategic plan) wa miaka mitano (**2014/2015 – 2018/2019**) wa kuendeleza uhifadhi wa rasilimali. Vilevile, Mwongozo wa Ufuatiliaji wa Rasilimali za Bahari umeandaliwa na zoezi la ukusanyaji takwimu za rasilimali mbalimbali ikiwemo; samaki, matumbawe, mikoko, majani bahari, na kasa kwenye Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu linaendelea. Katika kutekeleza mwongozo huo, ufuatiliaji wa mazalia ya Kasa (mnyama aliye katika hatari ya kutoweka) ulifanyika ambapo mayai katika viota **9** vya kasa kati ya **13** vilivyogunduliwa kwenye ufukwe wa Litokoto (Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi) yalianguliwa na mayai katika viota **11** kati ya **15** vilivyogunduliwa kwenye ufukwe wa Ushongo, Tanga yalianguliwa na vifaranga kurudishwa baharini.

Katika mwaka 2014/2015, Kitengo kitafanya doria zenye siku kazi **416** katika eneo la kilomita za mraba **2,000** kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu kwenye Hifadhi za Bahari **(3)** na Maeneo Tengefu **(15)**. Aidha, Kitengo kitaendelea kuwezesha Serikali za vijiji kutekeleza shughuli za uhifadhi; kitaimarisha miundombinu ya kushusha boti baharini katika Hifadhi za Bahari za Tanga na Mnazi bay; kujenga uwezo wa ubadilishanaji taarifa za uhifadhi; kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo yote ya uhifadhi kwa wawekezaji na wadau wengineo. Pia, Kitengo kitaendelea kufuatilia rasilimali za bahari ili kubaini viwango vya uhifadhi wa rasilimali vilivyofikiwa na kuratibu shughuli za utafiti katika Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu.

### *3.10 MASUALA MTAMBUKA*

#### Uendelezaji wa Rasilimali Watu

**109. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia na kuimarisha rasilimali watu ili itumike kutimiza na kufikia malengo yake. Katika mwaka 2013/2014, Wizara imeajiri watumishi **124** wakiwemo **71** wa kada za mifugo, **43** kada za uvuvi na **10** kada mtambuka. Aidha, Maafisa Mifugo na Uvuvi **853** wamepelekwa katika Sekretarieti za Mikoa **17** na Halmashauri **103** nchini kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Vilevile, Watumishi **187** wamepandishwa vyeo, **8** wamebadilishwa kazi baada ya kupata sifa za Miundo ya Utumishi na **57** wamethibitishwa kazini, **161** wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi, **39** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu wakiwemo uzamivu sita (**6**), uzamili **22** na Shahada ya Kwanza **11** na **55** walipatiwa mafunzo elekezi.

**110. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya mapitio ya Miundo ya Utumishi ya Kada za Mifugo na Uvuvi ili kukidhi mahitaji ya wakati; kutoa mafunzo kwa watumishi **458** kuhusu kutumia Mfumo wa Wazi wa Utendaji Kazi (OPRAS); kufanya kikao kimoja cha Baraza la Wafanyakazi; kuchapisha na kutekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja; Kuratibu na kuelimisha watumishi juu ya maadili na uadilifu; na kutoa huduma kwa watumishi nane (**8**) wanaoishi na Virusi vya Ukimwi na wanaougua UKIMWI. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa michezo katika kumjengea mtumishi maisha bora kiafya pamoja na kukuza ushirikiano miongoni mwao, watumishi **50** walishiriki michezo ya SHIMIWI pamoja na mabonanza.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara inatarajia kuajiri watumishi **214** (wakiwemo mifugo **62**, uvuvi **86** na mtambuka **66**), kupandisha vyeo watumishi **223**, kuthibitisha kazini watumishi **125** na watumishi **312** watahudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Aidha, watumishi wataendelea kupatiwa vitendea kazi; kutekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Pia, watumishi **300** watahamasishwa kuhusu umuhimu wa kupima afya zao kwa hiari na kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na VVU na wanaougua UKIMWI na kutoa elimu kwa Waelimisha Rika **10**. Vilevile, watumishi **50** watashiriki katika michezo ya SHIMIWI na bonanza, kufanya vikao **2** vya Baraza la Wafanyakazi na kuwezesha majukumu ya vyama vya Wafanyakazi (TUGHE na RAAWU).

**Mawasiliano na Elimu kwa Umma**

**111. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutayarisha na kusambaza taarifa za matukio mbalimbali kuhusu sekta za mifugo na uvuvi kupitia vyombo vya habari. Katika mwaka 2013/2014, vipindi vitano (**5**) kuhusu mafanikio ya sekta za mifugo na uvuvi na makala moja ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 vilitangazwa kupitia luninga na gazeti. Aidha, vipindi vitatu (**3**) vya luninga na vitatu (**3**) vya redio vya miaka **50** ya Muungano viliandaliwa na nakala **1,000** za kalenda zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau. Pia, Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara umekamilishwa na nakala **100** za Mkakati huo zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau.

**112. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha Maktaba kwa kuweka vitabu, majarida na kompyuta mbili. Aidha, Dawati la Malalamiko la Wizara limeimarishwa kwa kupatiwa mafunzo ya kuliendesha na namna ya watumishi kuleta malalamiko yao. Pia, watumishi wote wa kitengo walishiriki mkutano wa Taaluma ya Habari na Mawasiliano. Vilevile, Kitengo kiliandaa mikutano **7** kati ya Wizara na Waandishi wa Habari na wadau wengine.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha Dawati la Malalamiko, kuimarisha Maktaba na kutoa mafunzo kwa maafisa habari wawili. Aidha, itatoa mafunzo kwa maafisa kutoka vituo vya nje kuhusu mawasiliano kwa umma na kuchapisha na kusambaza kwa wadau nakala 1,000 za kalenda.

**Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

**113. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeunganishwa na mkongo wa Taifa na kuboresha mawasiliano ya intaneti na mifumo ya TEHAMA ambapo watumishi wa Wizara waliopo Makao Makuu wameanza kutumia barua pepe za Wizara baada ya kukamilisha kazi ya kuunda anuani hizo. Pia, Tovuti ya Wizara imeboreshwa na kuhuishwa kwa kuunganishwa na vituo vya TALIRI-Mpwapwa, TAFIRI-Dar es Salaam na FETA- Mwanza. Aidha,

Mfumo wa kompyuta wa kuhifadhi kumbukumbu na kufuatilia mzunguko wa majalada uko katika hatua za mwisho kukamilika. Wizara kwa kushirikiana na wadau imefanya mapitio na kuandaa Rasimu ya mwisho ya Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya TEHAMA. Vilevile, Mtumishi mmoja amewezeshwa kupata mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika Utawala wa Usimamizi wa shughuli za TEHAMA.
Katika mwaka 2014/2015, Wizara itachapisha nakala **1800** za Mkakati wa Wizara wa TEHAMA na kusambaza kwa wadau. Pia, itaendelea kujenga mtandao (LAN na WAN) utakaounganisha mawasiliano kati ya Makao Makuu ya Wizara na vituo vyake. Vilevile, Wizara itaendelea kukamilisha mfumo wa mawasiliano ya mbali na kusimamia mifumo ya mawasiliano ya wizara.

**Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

**114. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) imeendelea kutoa taarifa kuhusu mwenendo wa Hali ya Hewa.Taarifa hizo zimetumika kutoa ushauri kwa wafugaji na wavuvi katika upatikanaji wa maji, malisho, samaki na hali ya bahari na maziwa na kutoa maelekezo stahiki. Aidha, katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Wizara kwa kushirikiana na Asasi za kiraia zikiwemo: *Tanzania Natural Resources Forum* (TNRF); *Tanzania Pastoralists Community Forum* (TPCF) na *Dodoma Environmental Network* (DONET) imeelimisha wafugaji **1,620** kutoka wilaya za Longido, Ngorongoro, Kiteto, Hanang', Meatu, Chamwino na Kondoa kuhusu mabadiliko ya tabianchi na hifadhi ya mazingira.

**115. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya biogas kwa wafugaji wa Halmashauri za Singida, Mpwapwa, Bahi, Iramba, Kondoa, Njombe, Kongwa na Chamwino. Kutokana na elimu hiyo wafugaji wa vijiji **nane (8)** vya Halmashauri ya Njombe wamehamasika na kuweka mitambo ya biogas.

Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia zinazozingatia hifadhi ya mazingira na matumizi ya nishati mbadala. Aidha, itaendelea kuhimiza matumizi ya boti za Fibre glass ili kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya kutengeneza boti za uvuvi.

**4.0 SHUKRANI**

**116. Mheshimiwa Spika***,* Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wafugaji, Wavuvi, Wasindikaji, Wafanyabiashara na wadau wengine kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Wizara inaomba waendeleze juhudi hizo na itaendelea kushirikiana nao kuleta mapinduzi katika sekta za mifugo na uvuvi nchini. Aidha, napenda kuzitambua na kuzishukuru nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Serikali za Australia, Austria, Brazil, Canada, Jamhuri ya Czech, Hispania, Iceland, Ireland, Japan, Jamhuri ya Watu wa China, Israel, Korea Kusini, Marekani, Misri, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *FAO, IAEA, UNICEF, UNDP, UNIDO* na WHO na mifuko ya kimataifa ya GEF na IFAD kwa kuchangia katika maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi.

**117. Mheshimiwa Spika***,* vilevile, nazishukuru taasisi za kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika; Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japan (JICA), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (KOICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Shirika la Misaada la Australia (AUSAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa

Afrika (AU-IBAR), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE)*, Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GTZ), United Nations University (UNU), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA) kwa michango yao katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi. Pia, nayashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *Bill and Melinda Gates Foundation, Association for Agricultural Research in East and Central Africa (ASARECA), The New Partnership for African's Development (NEPAD), International Livestock Research Institute (ILRI), World Wide Fund for Nature (WWF), Indian Ocean Commission (IOC), South West Indian Ocean Fisheries Commission (SWIOFC), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Co-operation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFAM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute for Security Studies (ISS-Africa), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC), International Whaling Commission (IWC), SmartFish na Marine Stewardship Council (MSC)*.

**118. Mheshimiwa Spika**, naomba nimalizie kuwashukuru kwa dhati **Mhe. Kaika Saning'o Ole Telele**, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa msaada wake wa karibu katika kusimamia kazi za Wizara. Aidha, napenda pia nitoe shukurani zangu kwa Katibu Mkuu **Dkt. Charles Nyamrunda**, Naibu Katibu Mkuu **Dkt. Yohana Budeba,** Wakuu wa Idara na Vitengo, Taasisi na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa na kufanikisha maandalizi ya bajeti hii. Vilevile, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Busega kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Pia, naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunitia moyo ninapotekeleza majukumu ya kitaifa.

**5.0 BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

**119. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi **66,142,627,000.00** kama ifuatavyo:-

(i) Shilingi **40,952,022,00.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi **22,968,188,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi *(PE);* na shilingi **17,984,834,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengine *(OC);* na

(ii) Shilingi **25,190,605,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi **23,000,000,000.00** ni fedha za ndani na shilingi **2,190,605,000.00** ni fedha za nje.

**120. Mheshimiwa Spika,** naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani: *www.mifugouvuvi.go.tz.*

**121. Mheshimiwa Spika,** pamoja na hotuba hii nimeambatanisha Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015.

**122. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, umeisoma kwa muda mwafaka na umeisoma kwa weledi mkubwa sana; nakushukuru sana na ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki ni mdogo kwa Wenyeviti pamoja na Kambi ya Upinzani, kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 23 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)*